KOZI YA
WANAMABADILIKO
WA JAMII

Mwongozo wa wawezeshaji kwa warsha tisa
mfululizo za kusaidia jamii kujifunza, kuthamini na kuendeleza
Uhuru wa Dini au Imani kwa wote.

FORB Learning Platform

“Kila mtu ana haki ya uhuru
wa mawazo, dhamiri na dini;
haki hii inajumuisha uhuru wa kubadilisha dini
au imani yake, na uhuru wa kudhihirisha dini au imani yake,
akiwa peke yake au pamoja na wengine katika jamii,
hadharani au faraghani, kupi ia mafundisho,
vitendo, Kuabudu na mienendo.”

Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu,
Kifungu cha 18

YALIYOMO

Mwongozo wa mwezeshaji

Shukurani ... 5
Kwa nini tunahitaji wanamabadiliko wa jamii? ... 6
Ni nani mwanzilishi wa Kozi ya Wanamabadiliko wa Jamii? ... 7
Ujumbe kutoka kwa wabia wetu ... 8

SEHEMU YA A **JINSI YA KUTUMIA NYENZO HIZI**

Utangulizi wa Kozi ya Wanamabadiliko wa Jamii ... 11
Jinsi ya kutumia nyenzo hizi ... 13
Jinsi ya kujiandaa kwa kila kipindi ... 15
Vidokezo vya uwezeshaji ... 17
Kujibu maswali ya mtego ... 21
Mrejesho na ruhusa ... 29

SEHEMU YA B **NYENZO ZA KOZI**

KIPINDI CHA 1 **MAHITAJI YA BINADAMU – HAKI ZA BINADAMU – WAJIBU WA BINADAMU**
Muhtasari wa kipindi ... 32
Mpango wa kina wa kipindi ... 35
Mwongozo wa uwasilishaji na hadithi ya wanamabadiliko ... 41

KIPINDI CHA 2 **UTANGULIZI KUHUSU UHURU WA MAWAZO, DHAMIRI, DINI NA IMANI**
Muhtasari wa kipindi ... 46
Mpango wa kina wa kipindi ... 49
Nyimbo za filimbi na ngoma – hadithi ya FORB ... 56
Mwongozo wa uwasilishaji ... 60
Hadithi ya wanamabadiliko: Hadithi ya Peter, Pakistan ... 64

KIPINDI CHA 3 **NAMNA MBALIMBALI YA UTAMBULISHO WETU**
Muhtasari wa kipindi ... 65
Mpango wa kina wa kipindi ... 68
Mwongozo wa uwasilishaji na hadithi ya Sameh na Hanaa, Misri ... 75

KIPINDI CHA 4 **VIOLATIONS OF FREEDOM OF RELIGION OR BELIEF**
Muhtasari wa kipindi ... 78
Mpango wa kina wa kipindi ... 80
Mwongozo wa uwasilishaji ... 85
Maigizo mafupi ya dakika mbili: toleo lililo na maelezo ... 92
Hadithi ya wanamabadiliko: Hadithi ya Mchungaji James na Imam Ashafa ... 95

KIPINDI CHA 5 **UHURU WA DINI AU IMANI KATIKA JAMII YETU**
Muhtasari wa kipindi ... 96
Mpango wa kina wa kipindi ... 99
Mwongozo wa uwasilishaji ... 107
Hadithi ya wanamabadiliko: Hadithi ya Emina, Bosnia Herzegovina ... 109

KIPINDI CHA 6 **KUCHOCHEWA NA HADITHI – KUWEZESHWA NA MBINU**
Muhtasari wa kipindi 111
Mpango wa kina wa kipindi 114
Mwongozo wa uwasilishaji 121
Hadithi ya wanamabadiliko kutoka India, Uholanzi na Kyrgyzstan 124

KIPINDI CHA 7 **KUZUNGUMZA KUHUSU MBINU**
Muhtasari wa kipindi 126
Mpango wa kina wa kipindi 128

KIPINDI CHA 8 **SAFARI YA MABADILIKO YETU**
Muhtasari wa kipindi 132
Mpango wa kina wa kipindi 135
Mwongozo wa uwasilishaji 140

KIPINDI CHA 9 **SAFARI YA MABADILIKO YETU (INAENDELEA)**
Muhtasari wa kipindi 144
Mpango wa kina wa kipindi 146

SEHEMU YA C **NYENZO ZA REJEA**

Ahadi muhimu za haki za binadamu zinazohusiana na uhuru wa dini au imani 151
Tafuta taarifa kuhusu uhuru wa dini au imani (FORB) katika nchi yako. 153
Endelea kujifunza: nyenzo za ziada na kozi za mtandaoni 155
Orodha ya mazoezi 159

NYENZO ZA ZIADA

Kwenye kiungo kilicho upande wa kulia, unaweza kupata kila kitu unachohitaji ili kuendesha kozi hii, ikiwemo:

- Mwongozo wa slaidi za kila kipindi
- Muhtasari wa uwasilishaji katika mfumo wa maandishi ambayo unaweza kurekebisha na kuhariri ili yaendane na muktadha na hadhira yako
- Vitini
- Kadi za michezo na mabango ya kutumia katika mazoezi

https://www.forb-learning.org/sw/changemakers/course-materials/

Pata hapa
NYENZO ANDAMIZI

NAKALA ZA LUGHA NYINGINEZO

Mwongozo huu wa wawezeshaji na nyenzo zote zinazoambatana nao zinapatikana kwa lugha mbalimbali. Angalia hapa ikiwa Kozi ya Wanamabadiliko wa Jamii inapatikana katika lugha yako.

https://www.forb-learning.org/sw/changemakers/languages/

Pata hapa
NAKALA ZA LUGHA NYINGINEZO.

Shukurani

SHUKURANI ZA PEKEE ziwaendee wanachama wa kundi rejea la Kozi ya Wanamabadiliko wa Jamii, kwa mchango wao mkubwa katika kuandaa nyenzo na mchakato wa majaribio.

- Galina Kolodzinskaia, Baraza la Kidini, Kyrgyzstan
- Hala Farid Faris, Misri
- Hammam Haddad, Taqarob for Civil Society Development, Jordan
- Hidaya Maulidi Dude, Kituo cha Kidini cha Zanzibar, Tanzania
- Irfan Engineer, Kituo cha Utafiti wa Jamii na Usekulari, India
- Mchungaji Jimmy M.I. Sormin, Jumuiya ya Makanisa ya Indonesia
- Melisa Nguyen, Jukwaa la Uhuru wa Dini au Imani, Vietnam
- Mike Gabriel, Muungano wa Kitaifa wa Kikristo wa Kinjili Sri Lanka (NCEASL)
- Tehmina Kazi, Mshauri na Mkufunzi huru wa FORB, Uingereza
- Mchungaji Ukoha Ngwobia, Kanisa la Presbiteria la Nigeria

SHUKURANI pia ziwaendee watu wafuatao kwa mchango na maoni yao: Lisa Winther, Kristine Tveit na Alexander Borello Krosby (Stefanus Alliance International), Kristina Patring na Niklas Eklöv (SMC Faith in Development), Tabitha Schrøder-Knudsen, Ida Schmidt na Filip Buff-Pedersen (CKU), Lan Yu Tan, Gry Zierau na Sidsel-Marie Winther Prague (Fabo), pamoja na Chian Yew Lim na Michael Weiner (UN OHCHR).

SHUKRANI ZA DHATI ziwaendee wote waliotushirikisha hadithi zao kuhusu mabadiliko! Shukurani za pekee zimwendee mfasiri, Shisia Ali Abubakar, na mhakiki wa fasiri, Furaha Dimitrios Caloupis, kwa kazi nzuri ya lugha ya kiswahili ya kozi ya wanamabadiliko wa jamii.

Mwongozo huu umetengenezwa kwa msaada wa kifedha kutoka Norway. Yaliyomo katika mwongozo huu ni kwa ajili ya Jukwaa la Kujifunza kuhusu ya Uhuru wa Dini au Imani na hayana uhusiano na serikali ya Norway kwa namna yoyote ile.

Norway

Kwa nini tunahitaji wanamabadiliko wa jamii

Duniani kote, watu wa dini na imani zote wanakumbwa na ukiukwaji wa haki yao ya binadamu ya Uhuru wa Dini au Imani (FORB), na katika maeneo mengi, ukiukwaji huu unazidi kuwa mbaya. Asili, uzito na kiwango cha matatizo haya vinatofautiana kwa kiasi kikubwa, lakini ubaguzi, matamshi ya chuki, uhalifu wa chuki na ghasia ni mambo ya kawaida kote ulimwenguni.

Vikwazo vya serikali dhidi ya haki ya kuabudu na kutangaza imani kwa amani ni tatizo kubwa, linalohusiana na mwelekeo wa kidunia wa kuminya nafasi kwa asasi za kiraia. Katika muktadha tofauti, mifumo iliyopo ya chuki na vizuizi vya kisheria imezidishwa na janga la COVID-19.

Ukiukwaji wa FORB huwaathiri wanaume na wanawake kwa njia tofauti. Wanawake wako katika hatari zaidi ya kubaguliwa kupitia sheria binafsi zinazotokana na dini na ukatili wa kijinsia.

Ukiukwaji wa uhuru wa dini au imani unasababisha mateso makubwa kwa watu binafsi na kuchangia hali ya kutokuwa na utulivu katika jamii. Kuna uhitaji wa dharura wa mabadiliko, ambayo yanapaswa kuanzia juu Kwenda chini na pia kutoka chini Kwenda juu.

Jamii zinazoongozwa na usawa, amani na haki haziwezi kufikiwa bila juhudi thabiti kutoka kwa watunga sheria na maafisa kubadili sheria na kuhakikisha utekelezaji wa haki bila ubaguzi. Hata hivyo, juhudi hizi za juu hazitawezekana bila msukumo na shinikizo la mabadiliko kutoka kwa raia wa kawaida. Kwa nyongeza, ukiukwaji mwingi wa kila siku unaowakumba watu hufanywa na wanajamii wenzao – katika sehemu za kazi, shuleni na nyumbani. Hivyo basi, mabadiliko pia yanapaswa kuanzia ngazi ya chini.

Watu wengi wanahofia ukiukwaji wa FORB katika jamii zao lakini hawajui jinsi ya kuleta mabadiliko. Wanahisi uhitaji wa maarifa na ujuzi utakaowawezesha kuchukua hatua za vitendo kuleta mabadiliko. Kozi ya Wanamabadiliko wa Jamii inalenga kuchangia uwezeshaji huu, kwa kuzingatia si tu maarifa na mitazamo, bali pia mbinu za kuchukua hatua – iwe katika kuelewana baina ya imani tofauti au kupitia mtazamo unaozingatia haki za binadamu.

Tuna matumaini kuwa utapenda kushiriki katika kuleta mabadiliko katika nafasi yako, na tunatumai kuwa nyenzo za Kozi ya Wanamabadiliko wa Jamii zitakusaidia katika safari hii.

Katherine Cash
Jukwaa la Kujifunza kuhusu Uhuru wa Dini au Imani

Ni nani mwanzilishi wa Kozi ya Wanamabadiliko wa Jamii?

Kozi ya Wanamabadiliko wa Jamii imeandaliwa na Jukwaa la Kujifunza kuhusu Uhuru wa Dini au Imani (Jukwaa la Kujifunza kuhusu FORB), kwa msaada wa watu wengi na mashirika yanayojitolea kutetea Uhuru wa Dini au Imani kwa wote (FORB).

Jukwaa la Kujifunza kuhusu Uhuru was Dini au Imani linatoa nyenzo za mafunzo, kozi, na fursa za kujenga mitandao ili kusaidia watu binafsi, jamii, na watunga sera kuelewa, kutafakari, na kukuza uhuru wa dini au imani.Ni mradi wa Mtandao wa makanisa ya kikristo Kaskazini mwa Ulaya kuhusu Uhuru wa Dini au Imani (NORFORB), ambao unashirikiana na jumuiya mbalimbali za dini na imani, mashirika ya haki za binadamu na maendeleo, pamoja na taasisi za kitaaluma kutoka kote ulimwenguni.

Rasilimali na kozi nyingine kutoka Jukwaa la Kujifunza kuhusu FORB ni pamoja na seti ya filamu nane zinazofafanua maana ya FORB na hali ambazo inaweza kuzuiwa (zinapatikana kwa lugha nyingi); kozi ya mtandaoni ya mafunzo ya wakufunzi wa FORB; kozi ya mtandaoni inayopatikana kwa mahitaji, kuhusu FORB na usawa wa kijinsia, na zana ya mazoezi kwa wawezeshaji wa FORB.

PATA TAARIFA ZAIDI
Katika tovuti yetu:
forb-learning.org

Jinsi kozi ilivyoandaliwa

Kozi ya Wanamabadiliko wa Jamii iliandaliwa kati ya mwaka 2020 na 2021 na timu ya Jukwaa la Kujifunza kuhusu Uhuru wa Dini au Imani kwa kushirikiana na kundi lililojumuisha asasi za kiraia na jumuiya za kidini kutoka nchi kumi barani Afrika, Asia, ukanda wa MENA na Ulaya. Kundi hili lilihusisha watu kutoka asili mbalimbali za kidini, wakiwemo Wakristo, Waislamu, Wabudha, na wale wasio na dini.

Lengo letu lilikuwa kuunda kozi inayofaa, inayoweza kufikiwa kwa urahisi, na inayoweza kutekelezwa katika ngazi ya jamii kwenye mazingira yoyote salama vya kutosha. Hii ilikuwa na maana ya kuandaa kozi inayoweza kuendeshwa na mwezeshaji yeyote mwenye uwezo (bila kujali kiwango chake cha ujuzi wa haki za binadamu) kwa hadhira yoyote (bila kujali kiwango chao cha elimu), kwa hali inayoruhusu muktadha kuzingatiwa kwa njia ya asili.

Kwa hivyo, tulizingatia mambo matatu muhimu:

- Mbinu inayoanzia mahali walipo watu – kwa kutumia kushirikishana, kusimulia hadithi, mafunzo ya kiuzoefu, na mawasiliano ya kuona kama njia za kuanzisha na kuchunguza dhana, badala ya kutumia nadharia na maandishi pekee.
- Njia za vitendo za kuleta mabadiliko katika jamii.
- Kufanya kozi iwe rahisi kuendeshwa – kwa kuandaa kila nyenzo inayohitajika na wawezeshaji.

Baada ya kuandaa na kubuni kozi, wanachama wa kundi rejea kutoka India, Jordan, Nigeria, na Tanzania walijaribu kozi hiyo kwa vikundi vya watu 12-25 kutoka jamii za kienyeji. Walioshiriki walikuwa ni pamoja na madereva wa teksi, wauzaji madukani, mafundi cherehani, walimu, wafanyakazi wa kijamii, walimu wa madrasa, waumini wa makanisa, viongozi wa vikundi vya vijana, na wanafunzi wa vyuo vikuu. Maoni kutoka kwa washiriki na wawezeshaji yalikuwa chanya kwa kiwango kikubwa, na marekebisho yalifanywa kwenye kozi kwa kuzingatia maoni yao.

Nordic Ecumenical Network on Freedom of Religion or Belief
NORFORB

FORB Learning Platform

Ujumbe kutoka kwa wabia wetu

Dibaji kutoka Baraza la Makanisa Ulimwenguni

"Tangu Azimio la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu lilipotangaza haki yetu isiyoweza kuondolewa ya uhuru wa mawazo, dhamiri na dini mwaka 1948, mataifa yamejitahidi kuelewa na kufafanua dhana zilizomo katika haki hii. Sheria, viwango na sera nyingi zimejadiliwa, kupingwa na kupitishwa kote ulimwenguni, ingawa kwa masikitiko mengi, mara nyingi zinashindwa kuhakikisha watu wanafurahia kikamilifu haki hii.

Hata hivyo, sheria zote, mifumo na matamko hayana thamani yoyote ikiwa kanuni zake hazifahamiki wala kueleweka na watu wa kawaida katika jamii. Ulinzi na ukuzaji wa haki zote za binadamu huanzia nyumbani, miongoni mwa familia, majirani, na jamii. Kozi ya Wanamabadiliko wa Jamii inalenga jamii hizo ambazo huenda hazina uelewa wa awali kuhusu haki za binadamu na viwango vya kisheria. Imeundwa kwa namna inayosaidia kubadili mitazamo kwa kutumia usimulizi wa hadithi na mbinu za mawasiliano kwa njia ya picha, ili kusaidia kushinda hofu dhidi ya wale wenye imani tofauti.

Aidha, Kozi hii itawapa uwezo wana mabadiliko wa jamii kuwa watetezi wa haki ya uhuru wa dini au imani. Kozi hii itakuwa nyenzo muhimu kwa makanisa wanachama na wadau wengine wa Baraza la Makanisa Ulimwenguni tunapojitahidi kukuza uelewa na uungwaji mkono wa kanuni ya uhuru wa dini au imani kwa watu wote, bila kujali imani zao."

"Tofauti hazikusudiwi kututenganisha wala kutufanya wageni kwa wengine Tumetofautiana kwa makusudi ili kutambua kuwa tunahitajiana."

Askofu Mkuu Desmond Tutu

JENNIFER PHILPOT-NISSEN, MKUU WA MIPANGO, HAKI ZA BINADAMU NA UTWAAJI WA SILAHA, BARAZA LA MAKANISA ULIMWENGUNI

"Nguvu ya mabadiliko ya Kozi ya Wabunifu wa Mitaa haiwezi kulinganishwa; athari zake zinaibadilisha jamii kote Afrika. Imetengenezwa kuwa rahisi kueleweka na inayohusiana sana na muktadha wa eneo, kozi hii ni kama ufunguo unaofungua mlango wa fursa mpya. Leo, mtandao wa PROCMURA wa wakufunzi wa FORB kusini mwa jangwa la Sahara umeongezeka hadi kufikia takriban wabunifu/walinda FORB 350 wanaochochea mabadiliko, wote wakitumia rasilimali hii yenye thamani kubwa. Hii ni ongezeko la maarifa, mtazamo unabadilika, mienendo inageuka, na ujuzi wa kuhimiza uhuru wa dini unazidi kuwa imara. Tafsiri ya hivi karibuni ya rasilimali hii kwa Kiswahili ni mabadiliko makubwa, ikiahidi kuongeza uelewa wa FORB katika nchi za Afrika Mashariki, hasa kuwapa nguvu wanawake kusimama kwa msimamo. Kwa PROCMURA, kuhimiza uhuru wa dini siyo tu mbinu; ni msingi ambao mshikamano wa amani na maendeleo endelevu yanajengwa juu yake."

ASKOFU (DKT.) NATHAN SAMWINI, MSHAURI MKUU, PROGRAMU YA MAHUSIANO YA KIKRISTO NA KIISLAMU BARANI AFRIKA (PROCMURA)

"Kozi ya Wanamabadiliko wa Jamii ni nyenzo zuri sana katika kuhamasisha uelewa na heshima kuhusu Uhuru wa Dini au Imani (FoRB) kwa jamii za Kiafrika. Ni njia shirikishi inayozingatia muktadha ambayo inawajengea uwezo watendaji wa chini kabisa – wanaharakati, viongozi wa dini na waelemishaji – kushughulikia changamoto wakati inahamasisha ujumuishaji wa kila mwananchi. Kwa kuwapa wawezeshaji nyenzo za vitendo na mikakati ya kuendana na mazingira, kozi inatengeneza nafasi za midahalo, kupata suluhisho kutoka kwa jamii, na kujenga mshikamano wa wa kijamii wa muda mrefu. Kama mkufunzi na mtetezi, nimejionea mwenyewe jinsi ambavyo nyenzo hizi zimechochea mabadiliko kupitia macho ya utu na haki za binadamu"

FRED NYABERA, MKURUGENZI MTENDAJI,
ARIGATOU INTERNATIONAL – KOMESHA UMASIKINI WA MTOTO NA MWEZESHAJI NA MKUFUNZI WA KUFUNZI WA JUKWAA LA MAFUNZO YA IMANI AU DINI (FORB)

“Kwa kushirikiana na wabia 50 kutoka zaidi ya nchi saba kwa lengo la kukuza jamii zenye amani na ujumuishi kupitia Uhuru wa dini au imani, Mpango wa Pamoja wa Hatua za Kimkakati za Kidini (JISRA) unakaribisha kwa moyo mkunjufu Kozi ya Wanamabadiliko wa Jamii. Kozi hii imeleta nyenzo zinazopatikana kwa urahisi kuhusu Uhuru wa dini au imani, ambazo ni rahisi kuziweka katika muktadha wa eneo husika, kubadilika kulingana na mahitaji, na zinapatikana kwa lugha mbalimbali. Kozi hii inawapa wabia wa JISRA zana za nyongeza na lazima ili kuwawezesha wahamasishaji wa mabadiliko na kuwaunga mkono katika kuwezesha mazungumzo ndani na katika jamii za kidini, pamoja na kazi yao ya kuimarisha asasi za kiraia – hususan kwa wanawake, vijana, na wahusika wengine wenye upatikanaji mdogo wa elimu rasmi. Tunashukuru kwa fursa za kujifunza zinazotolewa na Jukwaa la Kujifunza kuhusu Uhuru wa Dini au Imani na tunasubiri kwa hamu kuona kinachofuata!"

CHRISTINA MAASDAM, MRATIBU WA MUUNGANO WA JISRA

“Kwa kuwa tunafanya kazi katika maeneo ambayo washiriki wengi hawana elimu rasmi, kozi hii inatupa fursa za kujifunza na kutekeleza malengo yetu kwa ufanisi zaidi. Maarifa rahisi na yanayoweza kufikiwa kuhusu uhuru wa dini au imani yanachangia uelewa bora na kukubaliana kwa jamii za kidini. Kozi hii inatusaidia kuhamasisha mshikamano wa kijamii kati ya madhehebu mbalimbali, na kuandaa viongozi wa kidini na wadau kuwa wahamasishaji wa amani na maisha ya pamoja kwa utulivu."

JISRA CONSORTIUM MEMBERS, MALI

"Kozi ya Wanamabadiliko wa Jamii ni nyenzo bora kwa wanaharakati, wakufunzi na waelimishaji. Mbinu yake jumuishi, shirikishi na nyumbufu inawaruhusu kuandaa uwasilishaji na mazoezi yanayolingana na muktadha wa eneo lao – kwa njia inayofaa katika kuongeza uelewa, kubaini ukiukwaji wa haki, na kuchunguza mbinu bora zaidi za kushughulikia changamoto. Ikiwalenga watu wa ngazi ya jamii, kozi hii inatoa fursa kwa washiriki kueleza malalamiko yao na wasiwasi wao, huku pia wakipata nafasi ya kugundua suluhisho bunifu na kuanzisha miradi ya kijamii. Inajumuisha zana za kujifunza kwa njia ya burudani na ushirikiano wa hali ya juu, lakini haiepuki masuala tata. Pia, inawapa wawezeshaji mbinu bora za kupanga vipindi vyao kwa ufanisi. Hii ni nyenzo ya kipekee kwa wanachama wa mitandao ya Uhuru wa Dini na Imani katika eneo hili wanaotafuta kukuza uraia jumuishi na kuheshimu uhuru wa dini na imani."

ANA MARIA DAOU, MKUU WA KITENGO CHA UTAFITI NA KOZI, TAASISI YA USIMAMIZI WA URAIA NA UANUWAI – WAKFU WA ADYAN

SEHEMU YA A

Jinsi ya kutumia nyenzo hizi

Utangulizi wa Kozi ya Wanamabadiliko wa Jamii

Kozi ya Wanamabadiliko wa Jamii ni mfululizo wa warsha tisa, kila moja ikichukua saa mbili, na imeandaliwa kusaidia vikundi vya watu wazima na vijana kujifunza, kuthamini, na kuendeleza uhuru wa dini au imani (FoRB) kwa wote katika jamii zao.

Mwongozo huu wa mwezeshaji na nyenzo zote zinazohusiana nao zinapatikana bila malipo kwa matumizi yako, na unaweza kuzibadilisha ili zifae jamii yako. Nyenzo hizi zinapatikana kwa lugha mbalimbali kupitia kiungo hiki.

Pata hapa
NYENZO ANDAMIZI
hapa.

Nini malengo ya kozi hii?

Kozi hii ina malengo makuu manne:

- kutusaidia kutambua na kukubali utofauti wetu na katika jamii
- kutufanya tuelewe na kuzikubali haki zetu za binadamu, ikiwa ni pamoja na haki ya uhuru wa dini au imani
- kutambua matatizo yanayohusiana na uhuru wa dini au imani katika jamii zetu
- na kupata njia za kushughulikia matatizo kwa pamoja.

Kozi hii inawalenga akina nani?

Kozi ya Wanamabadiliko wa Jamii inalenga watu wa ngazi ya jamii – wale wanaohisi kwamba kuna matatizo yanayohusiana na uhuru wa dini au imani katika jamii zao na wanataka kutafuta njia za kufanya mabadiliko.

Kozi hii haihitaji ujuzi wa awali, uzoefu, au hata kukubaliana na haki za binadamu kutoka kwa washiriki. Kinachohitajika ni mtu kuwa muwazi, awe na shauku ya kusaidia kujenga jamii za amani na usawa, na utayari wa kushiriki katika mchakato shirikishi wa kujifunza na kutafakari.

Imetayarishwa kwa ajili ya vikundi vya watu 12-24 lakini inaweza kubadilishwa ili kufaa vikundi vidogo au vikubwa zaidi.

Ingawa kozi hii imeundwa hasa kwa ajili ya jamii za Afrika, Mashariki ya Kati, na Asia, tunaamini kwamba maudhui yake yanafaa katika mazingira yoyote.

"Kitu bora zaidi kuhusu kozi hii ni jinsi ilivyoshirikisha na kuendana na masuala yanayowahusu watu, huku ikiwa rahisi kufanywa kwa furaha tele. Ulikuwa uzoefu mzuri sana!"
HIDAYA DUDE, MWEZESHAJI, TANZANIA

"Kozi hii ilichochea mabadiliko – niliweza kuona mitazamo ikibadilika kadiri vipindi vilivyoendelea. Tutaiendesha tena hivi karibuni."
IRFAN ENGINEER, MWEZESHAJI, INDIA

"Kozi hii ilifungua macho ya washiriki kwa njia mbalimbali walizoweza kuitikia ukiukwaji wa haki za binadamu. Iliwasaidia kuboresha ujuzi wao wa kupanga hatua za kuchukua. Matokeo yake, kutakuwa na wanamabadiliko wenye ufanisi mkubwa katika jamii zao."
HAMMAM HADDAD, MWEZESHAJI, JORDAN

Nani anaweza kuendesha kozi hii?

Kozi ya Wanamabadiliko wa Jamii ni shirikishi – inajumuisha mazoezi ya vikundi, michezo, hadithi, mijadala, na maigizo pamoja na mawasilisho. Yeyote mwenye uzoefu wa kuendesha mafunzo shirikishi kwa watu wazima na vijana anaweza kuendesha kozi hii. Mwongozo wa mwezeshaji na nyenzo zinazoambatana nao zinatoa mwongozo wa kina juu ya jinsi ya kuendesha kila kipindi.

Huhitaji kuwa mtaalamu wa haki za binadamu au uhuru wa dini au imani ili kuendesha kozi hii. Habari zote muhimu zinatolewa, ikiwa ni pamoja na maandishi na mawasilisho kuhusu mada zinazohusika. Jukumu la mwezeshaji si kuwa mtaalamu, bali ni kuwaongoza washiriki kupitia mchakato wa kujifunza kwa pamoja.

Kinachohitajika zaidi kwa mwezeshaji ni uelewa wa muktadha – uwezo wa kutathmini iwapo mada fulani ni nyeti sana au hatari kwa mijadala, na kurekebisha mchakato ipasavyo, pamoja na uwezo wa kushughulikia mienendo ya kundi endapo masuala nyeti au mvutano utatokea.

KIDOKEZO! Pata idokezo vya kukusaidia kujenga ujuzi wako wa uwezeshaji katika kurasa 17-20. Ukurasa wa 15 unatoa mwongozo wa jinsi ya kujiandaa kwa kila kipindi.

Kozi ina mada gani na Muundo wake ukoje?

Kozi hii ina vipindi tisa vya ana kwa ana, kila kimoja kikiwa cha saa mbili. Imegawanywa katika sehemu mbili:

Sehemu ya 1 (Vipindi 1-5), Inalenga kukuza uelewa na mtazamo ili akili na mioyo yetu iwe tayari kuwa wanamabadiliko. Washiriki wanajifunza kuhusu haki za binadamu na uhuru wa dini au imani, kutafakari kuhusu mtazamo wao kwa watu wa imani tofauti, na kupata ujuzi wa kuchambua muktadha wa jamii zao.

Sehemu ya 2 (Vipindi 6-9), washiriki wanajifunza mbinu mbalimbali za kuendeleza FoRB na haki nyingine, na wanaongozwa katika mchakato wa kupanga hatua za kuchukua kwa tatizo la FoRB walilotambua. Vipindi hivi vinaangazia ujuzi na hatua za utekelezaji.

Tazama nyenzo za kozi kwa maelezo zaidi.

"Shughuli zilikuwa za kusisimua, hadithi zilikuwa za kuvutia, na washiriki walikuwa na hamu ya kuzungumza. Nadhani kozi hii inafaa kwa yeyote anayevutiwa na masuala haya, kuanzia ngazi ya jamii hadi wale wenye uelewa wa kati wa haki za binadamu. Ulikuwa uzoefu wa kusisimua kwangu kama mwezeshaji."
UKOHA NGWOBIA, MWEZESHAJI, NIGERIA

"Kozi hii ilikuwa ya kipekee – ilichochea mijadala mingi! Kikundi kilikuwa cha watu wa makabila na imani tofauti – Waislamu, Wakristo, Baha'i na Druze. Haikuwa rahisi kila wakati kupata misimamo ya pamoja, lakini mijadala ilienda vizuri sana."
HAMMAM HADDAD, MWEZESHAJI, JORDAN

Jinsi ya kutumia nyenzo hizi

Kozi ya Wanamabadiliko wa Jamii imeandaliwa kama mchakato wa mafunzo wa vipindi tisa vinavyodumu kwa jumla ya saa 18-20. Vipindi hivi vinaweza kuendeshwa kwa siku tatu, kwenye wikendi mbili, au kwa kwa muda mrefu zaidi, kwa mfano, kipindi kimoja kila wiki.

Kwa kila kipindi, kuna mpango wa kipindi uliotayarishwa pamoja na seti ya nyenzo zinazohusiana, zikiwemo maandishi yaliyoandaliwa awali, mawasilisho, vitini, na vifaa vya mazoezi kama vile kadi na mabango.

Nyenzo nyingi zinapatikana kama nyaraka kwa mfumo wa maandishi ya kawaida, hivyo unaweza kuzipakua, kuzihariri, na kuzioanisha na muktadha wako na mahitaji ya kundi lako. Pia, unaweza kutafsiri maandishi kwenye slaidi za mawasilisho na vitini ikiwa unataka.

Nyenzo nyingi za kozi hii zinapatikana kama nyaraka za maandishi ya kawaida, ambazo unaweza kuzipakua, kuzihariri na kuzifanya zilingane na muktadha wako na mahitaji ya vikundi vyako. Pia, unaweza kutafsiri maandishi kwenye slaidi za mawasilisho na vitini upendavyo.

Pata hapa **NYENZO ZA ZIADA** hapa.

KIDOKEZO! Nyenzo zote za kozi zinapatikana katika lugha mbalimbali! Matoleo ya lugha nyinginezo yanaweza kupatikana hapa.

UZINGATIAJI WA HATARI NA USALAMA

Kwenye muktadha mwingine, kuna hatari ya kujadili masuala ya haki za binadamu na FORB kwa uwazi.Tafadhari kuwa muangalifu kama kufundisha kozi hii kunaweza kukufanya wewe au washiriki kuwa katika hatari au kusababisha vurugu au madhara. Kipi kinaweza kujadiliwa, na nani, wapi na namna gani? Unawezaje kupunguza hatari –kwa mfanokwa kubadilisha au kuzuia maudhui?Kwa mfano kwa kuwashirikisha na kupata msaada kwa walinzi wa eneo husika? Omba ushauri kwa watu na jaribu kuendesha kozi na kundi 'lililosalama' kwanza. Endesha kozi tu kama ni salama kufanya hivyo.

Nitahitaji teknolojia na vifaa gani kuendesha kozi?

NYENZO

- Ili kutumia nyenzo hizi kwa urahisi, ni vyema uwe na printa au mashine ya kunakili. Ikiwa huna, unaweza kutumia bango kitita na kalamu, au hata kijiti kwenye mchanga.
- Kompyuta na projekta kwa ajili ya kuonyesha uwasilishaji ni jambo zuri, lakini si lazima.
- Utahitaji kuandaa vifaa muhimu vya warsha kama vile bango kitita, kalamu na vikaratasi vya kubandika, pamoja na vitu vya kawaida kama mpira laini na mpira wa sufi. Orodha ya vifaa vinavyohitajika inapatikana katika kila mpango wa kipindi na kwenye ukurasa wa 15 (Jinsi ya kujiandaa kwa kila kipindi).

Je, ninaweza kuchagua na kuchanganya shughuli? Lazima nifanye vipindi vyote tisa?

Huenda ungependa kupata mawazo mapya ya kuongeza kwenye mdahalo wa kidini au shughuli za kuongeza uelewa ambazo tayari unashiriki. Unakaribishwa kuchagua na kuchanganya shughuli kutoka kwenye kozi hii na kuzijumuisha katika mchakato wa kujifunza ulioubuni mwenyewe.

Vipindi tisa vya kozi vinajengwa kwa mtiririko wenye mantiki. Hata hivyo, ikiwa hutaki kuendesha kozi nzima, unaweza kuacha baada ya Sehemu ya 1 (kipindi cha 5). Hasara ya kufanya hivi ni kwamba washiriki wanaweza kujisikia kukatishwa tamaa kwa kujifunza kuhusu changamoto za haki za binadamu bila kupewa nyenzo za kuzitatua.

Inawezekana pia kuondoa kipindi cha 3 (Namna mbalimbali ya Utambulisho wetu) bila kuathiri mtiririko wa vipindi vingine vya Sehemu ya 1. Hata hivyo, kipindi cha 3 kinazingatia mitazamo yetu kuhusu 'wengine' – dhana potofu na mambo yanayotuunganisha licha ya tofauti zetu. Usikiondoe isipokuwa una uhakika kuwa washiriki wako wana mtazamo mzuri kuhusu 'wengine'.

Ikiwa una kundi linaloelewa haki za binadamu na linafahamu na kuthamini haki zinazolindwa na FORB, inawezekana kurekebisha mchakato na kuanza moja kwa moja na kipindi cha 5.

"Nyenzo hizi ni rahisi sana kuelewa na matumizi rafiki kwa mwezeshaji na washiriki na zimebuniwa vizuri pia. Mmoja wa washiriki wangu, kiongozi wa vijana wa eneo hilo, anataka kuendesha kozi hii na kikundi chake cha vijana – hilo linaonyesha jinsi kozi hii ilivyo rahisi kufikiwa na kuendeshwa."

HIDAYA DUDE, MWEZESHAJI, TANZANIA

"Unaweza kupata kila kitu unachohitaji kwenye nyenzo – ni rahisi kutumia. Lakini ushauri mzuri ni kuwa na mwezeshaji mwenza. Mmoja wenu anaweza kuongoza kikundi katika mchakato wa mafunzo, huku mwingine akishughulikia teknolojia na kuwasaidia washiriki binafsi wanaohitaji msaada wa ziada."

IRFAN ENGINEER, MWEZESHAJI, INDIA

Jinsi ya kujiandaa kwa kila kipindi

Ratiba za vipindi zinaeleza kwa kina jinsi ya kuendesha vipindi. Chukua hatua zifuatazo ili kujiandaa kwa kila kipindi:

1. Tafuta nyenzo zinazoambatana na kipindi

Katika kila mpango wa kipindi, utapata kiungo cha moja kwa moja kwa nyenzo zinazohusiana na kipindi hicho, zikiwemo:

- Slaidi za mawasilisho ya kipindi
- Muhtasari wa mawasilisho au hadithi,
- Nyenzo za mafunzo zinazoweza kuchapishwa kwa ajili ya mazoezi, kama vile kadi, mabango, na vitini.

Pata hapa
NYENZO ANDAMIZI
hapa.

2. Soma, Fikiri, Badilisha!

SOMA kwa makini mpango wa kipindi.

FIKIRI jinsi mazoezi ya kipindi hiki yatakavyofanya kazi na kikundi chako. Je, kuna kitu unachohitaji kurekebisha?

BADILISHA mpango wa kipindi, mazoezi, na hata slaidi za uwasilishaji kulingana na mahitaji yako.

KIDOKEZO! kupendelea kubadilisha maandishi ya Kiingereza kwenye slaidi za uwasilishaji na vitini kwa lugha ya washiriki wako.

3. Andaa na ufanye mazoezi ya uwasilishaji!

Vipindi saba vina uwasilishaji. Umepewa maandishi na slaidi kwa ajili ya uwasilishaji huu. (Ikiwa una ujuzi wa kutosha kuhusu haki za binadamu na uhuru wa dini au imani, unaweza kuandaa uwasilishaji wako mwenyewe – lakini hakikisha unajumuisha hoja kuu kutoka kwenye maandishi yaliyotolewa!)

Hatua za kujiandaa kwa uwasilishaji:

SOMA NA UHARIRI MAANDISHI
Soma maandishi mara kadhaa na tafakari yaliyomo. Je, kuna kitu unachotaka kubadilisha au kuongeza, kama vile mifano inayohusiana na nchi yako? Fanya marekebisho yako. (Toleo linaloweza kuhaririwa la maandishi linapatikana katika nyenzo za ziada.)

HARIRI POWERPOINT AU ANDAA MICHORO YA BANGO-KITITA
Badilisha PowerPoint kulingana na mabadiliko yoyote uliyofanya kwenye maandishi. Ikiwa hutumii slaidi, unaweza kuandaa mabango yenye hoja kuu kutoka kwenye slaidi.

FANYA MAZOEZI YA UWASILISHAJI WAKO
Fanya mazoezi ya kutumia teknolojia inayohitajika na uwasilishe mada yako ukitumia slaidi au michoro ya bango-kitita.

FIKIRIA JINSI WASHIRIKI WATAKAVYOITIKIA
Washiriki wanaweza kuwa na maswali au maoni gani? Utayajibu vipi? Soma sehemu ya “Kujibu Maswali Magumu” kwenye ukurasa wa 21 ili kusaidia maandalizi yako. Kumbuka kuwa ni sawa kusema “Sijui” ikiwa huna jibu la moja kwa moja! Huhitajiki kuwa mtaalam – ni sawa pia kuwa na maswali kama washiriki wako.

CHAGUO LA ZIADA: JENGA KUJIAMINI
Baadhi ya mipango ya vipindi inajumuisha viungo vya filamu fupi au makala za kusoma ambazo zinaweza kukusaidia kujiamini na kujiandaa vizuri zaidi.

4. Jiandae na vifaa vyako!

Tayarisha na ukusanye nyenzo zote utakazohitaji kuendesha kipindi. Orodha ya nyenzo za kawaida zinazotumika katika vipindi vyote inapatikana hapa chini. Katika sehemu ya "Jiandae" ya kila mpango wa kipindi, utapata orodha ya nyenzo za mafunzo za ziada zinazohitajika kwa kipindi hicho, kama vile vitini au vifaa vya michezo – kwa mfano, chungu cha supu au mpira wa sufi.

NYENZO ZA MSINGI ZA KUFUNDISHIA

Utahitaji vifaa vifuatavyo kwa vipindi:

- Bango kitita na kalamu zake
- Kalamu za kawaida na karatasi za kuandika
- Vikaratasi vya kubandika
- Gundi au njia nyingine za kubandika mabango, karatasi za bango-kitita n.k
- Kompyuta na projekta kwa ajili ya kuonyesha slaidi za uwasilishaji (hiari)

5. Andaa ukumbi!

Maelekezo ya jinsi ya kupangilia chumba (mfano, mpangilio wa viti, vitu gani vya kubandikwa ukutani) yanapatikana katika sehemu ya "Jiandae" ya kila mpango wa kipindi.

ZINGATIA

Mipango ya vipindi imetayarishwa kwa kipindi cha kawaida cha saa mbili. Katika majaribio, baadhi ya vikundi viliona saa mbili zinatosha, huku vingine vikihitaji muda mrefu kwa ajili ya mjadala zaidi. Unaweza kupanga muda wa ziada ili kuruhusu mijadala kuendelea inapohitajika.

"Inachukua muda kujiandaa kwa kozi. Kuna nyenzo nyingi za kupitia, lakini ni rahisi kuendesha kozi hii ukifanya maandalizi. Kila kitu kimeelezwa wazi. Na mara ya pili unapofundisha, haitachukua muda mrefu kujiandaa."
HAMMAM HADDAD, MWEZESHAJI, JORDAN

"Unapaswa kwanza kusoma mwongozo wa wawezeshaji kwa ujumla, kisha utumie muda wako kuandaa kila kipindi. Ni wazo zuri kuwaza kwa kina juu ya kila kipindi na jinsi mazoezi yatakavyofanyika. Ikiwa hujui jinsi kipindi kitakavyoenda, jaribu kufanya mazoezi na mwezeshaji mwenza."
UKOHA NGWOBIA, MWEZESHAJI, NIGERIA

Vidokezo vya uwezeshaji

Uwezeshaji ni nini?

TAFSIRI

Kuwezesha: ni kufanya kitendo au mchakato kuwa rahisi, kurahisishwa, au kuwezekana. Mwezeshaji husaidia kufanya mchakato wa kujifunza, kuchunguza mitazamo, na kupata ujuzi mpya kuwa rahisi kwa washiriki.

MWEZESHAJI:

- hutumia mbinu shirikishi kusaidia washiriki kushiriki na kushirikiana kwa njia ya kufurahisha, yenye umakini na ya kusisimua.
- hutengeneza mazingira ya kuaminiana, uwazi, na kujifunza kwa pamoja, ambapo maoni tofauti yanaheshimiwa.
- hutambua na kushughulikia tofauti za mamlaka ndani ya kikundi, kuhakikisha kila mmoja anajihisi kujumuishwa na ana nafasi ya kushiriki.
- hutoa muundo wa kujifunza na kuwaongoza washiriki katika mchakato huo.
- huhakikisha masuala ya maandalizi yamekamilika – ikiwa ni pamoja na kupanga vipindi, kuweka chumba tayari, na kuwajulisha washiriki.

Nyenzo katika mwongozo huu zimeundwa kukusaidia kutekeleza majukumu haya. Mipango ya vipindi inajumuisha mazoezi mengi shirikishi, muundo unaoeleweka wa mchakato wa kujifunza, na mwongozo unaoeleweka wa namna ya kufanya maandalizi ya vipindi.

MWEZESHAJI SI:

- mwalimu au mhadhiri – katika mchakato shirikishi wa kujifunza, mwezeshaji ni mwenza wa washiriki na huongoza mchakato wa kujifunza unaohusisha kila mtu kuchangia jambo.
- mtaalam wa kila kitu – Ingawa mwezeshaji hujiandaa kwa kila kipindi, baadhi ya washiriki wanaweza kuwa na maarifa zaidi kuhusu mada fulani kuliko mwezeshaji! Maarifa ya kila mmoja hufanyiwa kazi pamoja.
- kitovu cha umakini – Mwezeshaji mzuri huzungumza kidogo kuliko washiriki, akiwahamasisha kushiriki katika mjadala.

JE, UNATAKA KUJIFUNZA ZAIDI kuhusu uwezeshaji wa elimu ya haki za binadamu kuhusu Uhuru wa dini au imani? Jisajili kwa kozi yetu ya bure ya Mafunzo ya Wakufunzi wa FORB. Kipaumbele kinatolewa kwa wale wanaohusika moja kwa moja katika kutoa elimu ya haki za binadamu kuhusu uhuru wa imani katika mazingira yenye ukiukwaji mkubwa wa haki hizi.

KOZI YA AKUFUNZI
Soma kozi hii mtandaoni kwa kubofya hapa TOT

Maelekezo ya jumla kwa mwezeshaji

ANDAA VIPINDI VIZURI NA UWE MNYUMBUFU!

Kadiri unavyojiandaa vizuri zaidi, ndivyo unavyojiamini zaidi. Badilisha shughuli mapema kulingana na mahitaji ya kikundi chako, na uwe tayari wakati wa vipindi kujua shughuli gani inahitaji muda zaidi au muda kidogo.

ANDAA JUKWAA LA MAONI HURU

Mitazamo hubadilika kupitia michakato inayowapa washiriki nafasi ya kusikiliza sauti mbalimbali, kutafakari, na kuendeleza mawazo yao bila kulazimishwa kuchukua msimamo ambao hawako tayari kuuchukua. Toa fursa kwa washiriki kutokubaliana na kufikia misimamo tofauti na yako. Epuka mijadala inayolenga kutengeneza hali ya kushinda au kushindwa.

EPUKA MAJIBU RAHISI KWA MASWALI MAGUMU
Sababu za ukiukwaji wa haki mara nyingi huwa ngumu na zinahusisha mambo mengi kama vile mila na mifumo ya mamlaka. Kuwa makini na urahisishaji kupita kiasi, hasa unapopunguza uwajibikaji wa kunyimwa haki kwa sababu moja au mbili, kama vile utambulisho wa kidini. Wahimize washiriki kuchambua sababu mbalimbali zinazochangia hali zao.

JITAHIDI KUTUMIA LUGHA KWA USAHIHI NA PUUZA MAWAZO FINYU
Epuka kishawishi cha mitizamo ya jumla na saidia washiriki kuepuka mitizamo ya jumla kama vile "Waislamu ni…", "Wahindu hufikiri…" au "Wanawake hawawezi…". Wakumbushe washiriki kuwa hata kama wapo katika kundi lenye uzoefu au Imani inayofanana, mitizamo ya jumla lazima itafutiwe usahihi (mfano, "wakati mwingine", "katika visa vingi").

EPUKA KULINGANISHA MAUMIVU
Himiza mshikamano na ushirikeli kati ya watu binafsi na makundi badala ya kulinganisha, kushindana, au kubishana kuhusu nani anayeteseka zaidi.

USISITE KUSEMA "SIJUI"
Kumbuka kuwa mwezeshaji pia ni mwanafunzi! Ikiwa huwezi kujibu swali, uliza ikiwa kuna mtu mwingine anaweza. Epuka kishawishi cha kujibu kila swali mwenyewe, hasa ikiwa swali linahusisha maoni (mfano, "Njia bora ya kukabiliana na hotuba ya chuki ni ipi?"). Badala yake, uliza kundi jinsi wanavyoweza kujibu swali hilo na waruhusu mawazo tofauti.

FANYA KAZI KATIKA TIMU NA TUNZA KUMBUKUMBU
Wawezeshaji hujifunza kutokana na uzoefu na kutoka kwa wenzao! Jaribu kufanya kazi katika timu ya wawezeshaji 2-3 ambao hupanga, kuendesha, na kutathmini kozi pamoja. Weka kumbukumbu ya kila kikao, ikiwa ni pamoja na marekebisho ya mpango, mawazo mapya, mafanikio na changamoto. Hili litakusaidia kupanga warsha zijazo.

Changamoto kuu zinazowakabili wawezeshaji

CHANGAMOTO YA UWEZESHAJI: MIFUMO YA MAMLAKA
Katika jamii, kuna hali za kutokuwepo kwa usawa wa mamlaka – kati ya wanaume na wanawake, makundi ya rangi, kikabila au kidini, watu wazima na watoto/vijana, watu wenye ulemavu na wasio na ulemavu, watu waliosoma na wasio na elimu. Hali hizi huathiri jinsi washiriki wanavyohusiana wao kwa wao na na mwezeshaji. Uwepo wa viongozi wa kidini kwenye mafunzo ya FORB huathiri mienendo ya kundi, kama vile mijadala juu ya masuala ambayo wanawake, kulingana na tamaduni za jamii, hawatarajiwi kuwa na maoni, kama vile Theolojia. Mienendo ya mamlaka mara nyingi huwa fiche, na wawezeshaji wanapaswa kuiangalia na kuidhibiti ili kuhakikisha kuna mazingira mazuri ya ujifunzaji.

Vidokezo vya kudhibiti hali za mamlaka:

- Kuwa makini! Angalia ni washiriki gani wanatawala mijadala au wako kimya, wanakaa wapi, lugha yao ya mwili, na jinsi wanavyohusiana na wenzao na wewe.
- Tumia mamlaka yako kama mwezeshaji kubadilisha hali hasi za mamlaka, kwa mfano kwa kurejelea kanuni za msingi au kusisitiza kuwa unathamini maoni na mawazo ya kila mshiriki.
- Tumia mazoezi shirikishi na vikundi vidogo ili kuhakikisha ushiriki wa kila mtu. Jaribu kuhakikisha kuwa watu walewale hawafanyi kazi pamoja.

- Simamia mijadala kwa kuhakikisha kila mtu anapata nafasi ya kuzungumza na kusikilizwa.
- Wahimize washiriki waoga kuzungumza kwa kutumia lugha ya mwili, kama vile kuwakaribia au kuwahimiza kupitia mawasiliano ya macho.
- Tumia pongezi kwa ukarimu lakini epuka kuwa na mshangao wa dhihaka.
- Wape majukumu washiriki wasiosikika sana, kama vile kuwa wasemaji wa vikundi vidogo.
- Usiruhusu kauli zinazodhalilisha wengine, zinazomaanisha ubabe au kiburi au ambazo zinamadhara, ukatili au ubaguzi ziendelee bila kushughulikiwa, hasa kama zimekusudiwa kuwalenga washiriki moja kwa moja au kwa namna nyingine. Rejea kanuni zilizopo au waombe washiriki "wapingaji" kuelezea kwa nini walisema hicho walichokifanya na waalike washiriki wengine kutoa maoni yao kuhusu hali hiyo.
- Katika mazingira fulani, inaweza kuwa rahisi au muhimu kwa wanawake na wanaume, au makundi ya umri, dini, au tamaduni tofauti kujadili masuala kivyao kabla ya kushiriki na kundi lote.

CHANGAMOTO YA UWEZESHAJI: MASUALA NYETI

Haki za binadamu zinahusisha maadili, hisia na maoni, na zinaweza kupingana na mitazamo na dhana za awali za washiriki. Baadhi yao wanaweza kuhisi kuwa mada hii inapingana au inatishia maadili, imani na desturi zao, na wale waliopitia ukiukwaji wa haki za binadamu huenda wakachochewa na hali zao za kiwewe katika kutoa majibu yao.

Iwapo washiriki wataanza kuwa na hasira, kujitenga, kuhujumu mijadala au kuwa na tabia za fujo, hii inaweza kuwa ishara kwamba wanahisi kutishiwa na masuala nyeti.

Kama mwezeshaji, jukumu lako ni kusimamia mjadala na mienendo ya kikundi kwa kuhakikisha mazingira salama kwa kila mmoja, ukiwemo wewe mwenyewe, kutoa jukwaa lisilo la kuhukumu kwa ajili ya kujifunza kwa pamoja, na kuweka mjadala katika muktadha wa haki za binadamu/FORB.

Hapa kuna vidokezo vya jumla vya kushughulikia masuala nyeti:

- Fikiria kwa kina kuhusu kipindi kabla ya kuanza, tambua masuala nyeti, na tafakari jinsi ya kushughulikia hali zinazoweza kutokea.
- Usivamie tu mjadala ili kuepuka utata. Ruhusu washiriki kuuliza maswali magumu.
- Usikubali kushiriki kwenye mabishano. Wewe ni mwezeshaji, si mshindani wa mdahalo.
- Kumbuka kuwa elimu ya haki za binadamu inahusisha kujenga ujuzi wa kujadili masuala ambayo hatuafikiani. Kikundi hakihitaji kukubaliana juu ya kila jambo!
- Andaa mazingira vizuri – tumia muda kuunda kanuni za msingi na kufanya mazoezi yanayojenga ushirikeli na kuaminiana.
- Tumia uzoefu wako binafsi kuchochea washiriki kufunguka na kushiriki kikamilifu.
- Rejea kanuni za msingi wakati mvutano unapotokea na wakumbushe washiriki umuhimu wa kusikiliza na kuheshimu mitazamo tofauti.
- Tambua pingamizi dhidi ya haki za binadamu. Eleza kuwa sote tunafaidika kwa kuelewa na kushughulikia migongano ya maadili na mawazo.

- Kubali upinzani! Tumia kama nyenzo ya kuwezesha mazungumzo kwa kuwaomba washiriki washirikishe mawazo, hisia au hofu zao kuhusu suala husika. Mitazamo hasi inapaswa kujadiliwa kwa uwazi katika mazingira ya kikundi ili kuwezesha kujifunza na kubadilika.
- Tambua na shughulikia mvutano. Simamisha mjadala kwa muda, taja kuwa unahisi mvutano ndani ya chumba, waombe washiriki watambue mitazamo tofauti na waulize ikiwa ni sawa kutokubaliana. Uliza maoni ya kikundi kuhusu jinsi wanavyotaka kushughulikia mada husika. Huenda wakapendelea kujadili katika makundi madogo, katika kikao kingine, au kusitisha mjadala. Eleza hofu zozote binafsi ulizonazo, kwa mfano, unaweza kupendekeza kuahirisha mada fulani hadi washiriki wawe wamefahamiana vizuri na kujenga uaminifu wa pamoja.
- Ikiwa kutokubaliana kunahatarisha kuharibu kipindi na mahusiano, basi "hifadhi" mjadala huo kwa muda na elekeza tena mjadala kwenye masuala yanayoweza kuleta makubaliano. Kozi hii si jukwaa la mdahalo wa ushindani.
- Usiwen a matarajio makubwa sana! Fanya kazi kwa utaratibu kujenga mazungumzo juu ya masuala yanayoleta hitilafu. Watu hawawezi kubadili fikra zao hadharani kwa haraka zilizojengwa kwa Mawazo finyu na desturi kwa muda mrefu. Hata hivyo, kukutana na mitazamo mbadala na kujenga mahusiano ya kishirikeli huwafanya washiriki kufikiria upya mitazamo yao kwa muda.

UWEZESHAJI: WASHIRIKI WENYE UTATA

Baadhi ya washiriki wanaweza, kwa makusudi au bila kujua, kuvuruga mshikamano wa kundi, kama vile kutawala mazungumzo au kutoshiriki kabisa (Mf. Muda wote kuchezea simu). Suluhisho ya hawa hutofautiana kma vile watu na mazingira wanavyotofautina, lakini mikakati ifuatayo inaweza kusaidia.

- Tumia busara na ucheshi wakati mshiriki amezungumza kwa muda mrefu sana. Kwa mfano, mkatishe haraka kati ya hoja zake kwa kusema: "Hiyo ni hoja nzuri, asante! Wengine wana maoni gani?" au elekeza kidole kwenye saa yako kisha utabasamu.
- Mpe mshiriki anayependa kuzungumza sana jukumu fulani, kwa mfano, aandike mawazo ya kikundi kwenye bango-kitita Hii inaweza kupunguza hitaji lake la kutawala wengine.
- Tambua wakati mienendo ya kikundi haifanyi kazi vizuri na wakumbushe washiriki kuhusu kanuni za msingi. Hakikisha kuwa mambo kama kutokatiza wengine, mijadala kuwa ya siri, kutotumia simu, na kuheshimu maoni ya kila mtu yamejumuishwa kwenye kanuni hizo. Eleza kuwa utekelezaji wa kanuni za msingi ni jukumu la kila mtu na ruhusu shinikizo la kikundi kusaidia kutatua tatizo.
- Ikiwa ni lazima, zungumza na mshiriki anayetawala sana darasa au asiyeheshimu wengine hata katika mazingira ya ana kwa ana, kwa mfano wakati wa mapumziko. Mweleze kuwa unathamini ushiriki wake, taja changamoto zilizopo, muulize suluhisho na jadilini njia anazoweza kutumia kuboresha mazingira ya kujifunza.
- Uamuzi wa mwisho, mshiriki anaweza kuombwa kuondoka kwenye kikundi. Hisia mbaya zitakazotokana na hatua hiyo zinapaswa kupimwa dhidi ya athari mbaya ambazo mshiriki huyo anasababisha katika kikundi.

Chanzo: Sehemu ya 'Vidokezo vya Uwezeshaji' imetoka kwa 'The Human Rights Education Handbook', kilichoandikwa na Nancy Flowers na wenzake, kilichochapishwa na The Human Rights Resources Center na The Stanley Foundation. Kimetumiwa kwa ruhusa yao.

Kujibu maswali ya mtego

Unapoendesha kozi ya wanamabadiliko wa jamii, huenda ukakutana na maswali magumu kuhusu haki za binadamu kutoka kwa washiriki. Hapa tumekusanya baadhi ya maswali na vikwazo unavyoweza kukumbana navyo pamoja na mawazo ya jinsi ya kuyajibu. Kila hadhira na muktadha ni tofauti, hivyo si kila pingamizi au jibu litakuwa linafaa kwako. Hata hivyo, tunatumaini mkusanyiko huu utakusaidia kujiandaa kwa mazungumzo yenye utata.

Unapojibu pingamizi, kumbuka kuthibitisha ukweli wowote unaoweza kupatikana katika pingamizi hiyo na uzoefu binafsi unavyoakisi jibu. Pia, kumbuka kwamba ni sawa kusema hujui na kwamba kozi hii itawasaidia nyote kuchunguza majibu kwa pamoja! Mabadiliko ya mitazamo huchukua muda na hutokea hatua kwa hatua. Lengo lako linapaswa kuwa kupanda na kumwagilia mbegu za mabadiliko kwa upole badala ya kutarajia mabadiliko ya haraka ya maoni.

Kwa maswali kuhusu FORB na jinsi inavyoweza kuendeshwa, tafadhali tazama mfululizo wetu wa filamu fupi kuhusu mada hii.

Maswali mengi magumu yanahusiana na JINSI ya kushughulikia tatizo fulani kuhusu FORB na kufanya mabadiliko. Tafadhali tumia nyenzo za vipindi vya 6-9 (vinavyoangazia mbinu na upangaji wa hatua) ili kusaidia vikundi kusaka majibu ya maswali hayo.

TAZAMA
FILAMU HIZI
ili zikusaidie kujibu maswali kuhusu FORB.

–––– UZINGATIAJI WA HATARI NA USALAMA ––––

Pingamizi kali dhidi ya haki za binadamu, hasa zile zinazotokana na imani za kidini, zinaweza kuwa ishara ya hatari inayoweza kutokea. Katika mazingira magumu, mjadala wa wazi kuhusu haki na ukiukwaji wa haki unaweza kuzidisha mvutano uliopo ndani ya kundi au hata kuhatarisha usalama wako au wa washiriki wako. Iwapo mjadala utaendelea katika mwelekeo unaoweza kusababisha hatari, yafaa kusitisha kwa kutambua unyeti wa mada husika. Badala yake, elekeza mjadala katika maeneo ya makubaliano ya pamoja na tumia muda kufanya mazoezi ya kujenga uhusiano na kuimarisha uaminifu ndani ya kundi.

ZINGATIA

Kukosoa au kusikiliza?

Huenda ukashawishika kupinga watu moja kwa moja kwa kuwaambia, 'mwelekeo wako ni mbaya' au "Umeelewa vibaya" unapokabiliana na kauli fulani. Huenda pia ikawa muhimu kukomesha majadiliano na kuwakumbusha washiriki sheria za msingi, hasa iwapo wengine ndani ya kundi wanajihisi kushambuliwa au kudharauliwa. Hata hivyo, kubadilisha mitazamo kunahitaji zaidi kusikiliza na kutumia hoja za kushawishi kwa njia ya uelewa – mazungumzo nyeti ambayo mwezeshaji na mtu anayetoa pingamizi wanajaribu kutafuta msingi wa makubaliano, hata ikiwa mdogo. Mazungumzo ya ana kwa ana wakati wa mapumziko au baada ya vipindi yanaweza kuwa mbinu bora, hasa ikiwa mtu mwenye pingamizi anatawala majadiliano au anachangia hali hasi ndani ya kundi.

Mada – Wengi dhidi ya wachache

PINGAMIZI: Wengi wanapaswa kuwa na haki zaidi! Wana haki ya kuamua katika demokrasia.
PINGAMIZI: Wachache wanapaswa kuzingatia imani na mtindo wa maisha wa wengi ikiwa wanaztaka kuishi hapa, hii ni nchi yetu.

MAJIBU AMBAYO YANAWEZA KUTOLEWA:

- Katika demokrasia, chama cha siasa kinachopata kura nyingi zaidi ndicho huunda serikali. Lakini ili demokrasia iwe yenye afya na endelevu, serikali hiyo inatakiwa kulinda masilahi ya kila mmoja. Demokrasia yaweza kugeuka kuwa udharimu wa waliowengi kama hakutakuwa na haki sawa kwa wananchi wote – ni kama mbwea wawili na kondoo mmoja wanaopiga kura kuhusu aina ya chakula kitakachowafaa kwa usiku!
- Ikiwa serikali yako inaweza kuwanyima haki walio wachache na ikiwa wachache hapa wanalazimika kufuata imani na mtindo wa maisha wa walio wengi, hii inamaanisha nini kwa watu waliowachache wa imani yako wanaoishi katika nchi nyingine? Je, ni sawa kwa serikali zao kuwafanyia hivyo hivyo na kuwanyima haki?
- Demokrasia inategemea haki za binadamu. Uchaguzi huru na wa haki hauwezekani bila haki kama vile uhuru wa kujieleza, uhuru wa kupata taarifa, uhuru wa kukusanyika na kushirikiana, uhuru wa vyombo vya habari, na haki ya msingi ya kupiga kura. Bila haki hizi, raia hawawezi kuunda vyama vya siasa, kuwa na maoni sahihi kuhusu nani wa kumpigia kura, au kupiga kura kwa usalama.
- Utofauti wa tamaduni na mila huleta utajiri mkubwa kwa jamii kwa njia nyingi, kwa mfano kupitia sanaa na vyakula.

PINGAMIZI: Haki za binadamu ni muhimu tu kwa wachache.

MAJIBU AMBAYO YANAWEZA KUTOLEWA:

- Haki za binadamu ni muhimu kwa watu wa makundi yote madogo kwa sababu mara nyingi wanakabiliwa na hatari kubwa zaidi, kama vile ubaguzi. Hata hivyo, haki za binadamu ni kwa kila mtu. Haki hizi zinalenga kulinda kila mmoja dhidi ya matumizi mabaya ya mamlaka na kuhakikisha ustawi wa wote. Hakuna mtu anayetaka kukamatwa bila sababu, kuteswa, kubaguliwa, au kunyimwa elimu kwa watoto wao. Bila kujali ikiwa tupo kwenye kundi la waliowengi au wachache, sote tunataka kuishi katika jamii ambapo tunalindwa dhidi ya hatari hizi – jamii ambayo utu wetu unalindwa kwa haki.
- Kila mtu ana utambulisho mbalimbali. Huenda nikawa sehemu ya kundi la kidini au kabila kubwa, lakini pia nikawa sehemu ya kundi dogo katika muktadha mwingine – kwa mfano, ikiwa nina ulemavu.

Mada – Msimamo na njama za magharibi

PINGAMIZI: Mataifa ya Magharibi hutumia haki za binadamu kudhoofisha na kuathiri msimamo wa nchi nyingine, ilhali wao wenyewe hawaheshimu viwango hivyo. Haki za binadamu ni nyenzo za propaganda za mamlaka ya kisiasa.

MAJIBU AMBAYO YANAWEZA KUTOLEWA:

- Chombo chochote, hata kiwe kizuri vipi, kinaweza kutumiwa vibaya. Ni kweli kwamba haki za binadamu wakati mwingine hutumiwa kisiasa. Pia ni kweli kwamba hakuna nchi iliyo na rekodi kamilifu ya kuheshimu haki za binadamu (ingawa baadhi zinafanya vizuri zaidi kuliko nyingine). Baadhi ya serikali hudai kutetea haki huku zenyewe zikizivunja waziwazi. Hata hivyo, hilo halifanyi haki za binadamu kuwa zisizo na maana kwetu – kwa sisi waliostahili haki hizo. Haki hizi zinahusu uhuru wetu, usalama wetu na ustawi wetu.
- Ukiukwaji mwingi wa haki za binadamu hutokea katika jamii – kupitia ubaguzi na uhalifu wa chuki, kwa mfano. Hata kama serikali zinashindwa kutekeleza haki hizi, sisi kama raia tunaweza kuchangia kuzifanya haki za binadamu kuwa uhalisia katika jamii zetu. Tunaweza pia kushirikiana kutetea haki za kila mmoja na kukabiliana na mapungufu ya serikali. Swali si kama serikali zinacheza michezo ya kisiasa, bali ni nini tunaweza kufanya kuhakikisha.

PINGAMIZI: Haki za binadamu ni za kigeni, ni maadili ya Magharibi na utamaduni wa kibeberu.

MAJIBU AMBAYO YANAWEZA KUTOLEWA:

- Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu liliandikwa na wawakilishi kutoka sehemu nyingi za dunia zenye dini na imani tofauti. Wawakilishi hao walisisitiza kuwa haki za binadamu zinahusu heshima ya binadamu na mahitaji yetu sote katika maisha ya kila siku. Karibu nchi zote duniani zimesaini makubaliano ya haki za binadamu – zikikubali kuziheshimu, kuzilinda na kuzikuza.
- Haki za binadamu zinahusu jinsi tunavyopaswa kutendewa na jinsi tunavyopaswa kuwatendea wengine katika shule zetu, mashamba yetu, sehemu za kazi, nyumbani na majirani. Zinawalinda watu dhidi ya unyanyasaji unaoweza kufanywa na wale walio na mamlaka juu ya maisha yao – wawe ni wamiliki wa nyumba, waajiri, walimu au hata wanafamilia, na dhidi ya dhuluma zinazoweza kufanywa na mamlaka za serikali. Hili linawahusu watu wote.
- Tazama haki zilizoainishwa katika Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu kisha jiulize: Je, kuna yoyote kati ya hizi ambayo haihusiani na mahitaji ya msingi ya binadamu? Ni haki zipi hasa ambazo zinaonekana kuwa za kigeni? Je, kuna haki yoyote ambayo hatuitaki sisi wenyewe?

PINGAMIZI: Haki za binadamu zinahimiza ubinafsi. Katika utamaduni wetu, wajibu wa kijamii na mahusiano ni muhimu zaidi kuliko haki za mtu binafsi. Jamii yetu itaporomoka ikiwa kila mtu atadai haki zake bila kuzingatia majukumu yake.

MAJIBU AMBAYO YANAWEZA KUTOLEWA:

- Ni kweli kwamba haki za binadamu zinaanzia katika kutambua haki za mtu binafsi. Ni muhimu kwa mtu binafsi kuwa na haki, kwa sababu watu binafsi wanaweza kuwa waathirika wa unyanyasaji, kwa mfano kutoka kwa maafisa wala rushwa au wanafamilia wakandamizaji. Mtu anapokumbwa na hali kama hiyo, anapaswa kupata msaada na haki.

- Hata kama haki za binadamu zinaanzia katika ngazi ya mtu binafsi, nyingi kati ya haki hizi zinalinda shughuli tunazofanya kwa pamoja. Kwa mfano, tuna haki ya kuunda familia, uhuru wa kukusanyika unatupa haki ya kukutana kwa vikundi, na uhuru wa dini au imani unalinda haki yetu ya kustahili jumuiya ya waumini, kuunda mashirika ya kidini na kuabudu kwa pamoja. Kuna pia haki za vikundi zinazolinda jamii za wenyeji na wachache wa kikabila.
- Haki za binadamu pia zinahusisha majukumu. Kila mtu ana jukumu la kuheshimu haki za wengine – kuwatendea watu haki na kufanya kazi kwa ajili ya jamii ambapo hakuna mtu anayenyanyaswa kwa matumizi mabaya ya mamlaka. Jamii ingekuwa imara zaidi ikiwa kila mmoja wetu angechukua jukumu hili kwa dhati.

Mada – Nyenzo haina meno na haiendani

PINGAMIZI: Serikali zinavunja haki za binadamu mara kwa mara na hakuna anayewazuia. Zinamaana gani? Haki za binadamu ni maneno tu kwenye karatasi.
PINGAMIZI: Haki za binadamu zinaweza kufanya kazi kwa watu wa Magharibi au wa mijini, lakini hazina maana kwa wale wanaoishi vijijini.

MAJIBU AMBAYO YANAWEZA KUTOLEWA:

- Hakuna jeshi la kimataifa la kusimamisha serikali zinazovunja haki za binadamu. Jamii ya kimataifa mara nyingi inashindwa kuzuia ukiukwaji mkubwa wa haki. Na hata pale ambapo serikali zinatunga sheria na sera za kutekeleza haki za binadamu, mara nyingine sheria hizo hazina athari kubwa kwa wananchi wa kawaida. Hata hivyo, hiyo haimaanishi kuwa haki za binadamu hazina maana.
- Haki za binadamu haziwezi kufikiwa kutoka nje. Kuzifanya haki hizi kuwa uhalisia kwa watu wa kawaida ni mchakato tunaouanzisha ndani ya jamii na mataifa yetu. Mchakato huu mara nyingi huwa wa polepole, unahitaji uvumilivu, ujasiri na mikakati mizuri – hasa pale ambapo wenye mamlaka hawataki mabadiliko. Njia ya kuelekea mabadiliko mara nyingi ni ndefu na hujengwa na hatua ndogo ndogo. Kuna mambo mengi ambayo yanaweza kuwa magumu kufanikisha kwa muda mfupi, lakini safari yenyewe ina thamani kubwa.
- Sheria, kanuni na sera nzuri ni muhimu katika ngazi ya kimataifa, kitaifa na ya mtaa, lakini hatua inayofuata ni muhimu pia – kujenga taasisi zinazofanya kazi. Hii inamaanisha kuhakikisha kuwa sheria zinajulikana na kufuatwa na kila mmoja mwenye wajibu wa kuzitekeleza. Inajumuisha kuongeza uelewa, ujuzi na mifumo ya uwajibikaji katika kila ngazi – kutoka kijijini hadi mahakama kuu.
- Ukiukwaji mwingi wa haki hutokea katika jamii. Kufanikisha haki za binadamu kunategemea kuongeza uelewa na kubadilisha mitazamo, maadili na tabia za watu wa kawaida katika ngazi ya chini.
- Kumekuwa na mafanikio mengi! Harakati za kumaliza utumwa, kupigania haki ya kupiga kura kwa wote, kutunga sheria za kulinda wanawake dhidi ya unyanyasaji wa majumbani, au kuhakikisha kaya katika maeneo yaliyotengwa zinapata huduma za umma kama vile huduma za afya na umeme – haya ni baadhi tu ya mifano ya jinsi kazi ya haki za binadamu imeboresha maisha ya watu wa kawaida kote duniani. Ni rahisi kusahau ni haki ngapi tumepata kupitia mapambano ya vizazi vilivyopita.

Mada – Pingamizi za kidini kuhusu haki za binadamu

ZINGATIA

Pingamizi za kidini hugusa masuala tata na nyeti, na tafsiri za kidini pamoja na hoja zake hubadilika sana kulingana na muktadha. Majibu yaliyopendekezwa hapa chini yanatoa ushauri wa kimsingi na wa jumla, na hayajumuishi mijadala ya mafundisho maalum ya kidini. Ikiwa unatarajia kwamba masuala haya yanaweza kuwa magumu kushughulikia katika kundi lako, fikiria kumwalika mtaalamu ambaye ana imani sawa na wale wenye pingamizi ili kukusaidia kuendesha kipindi. Je, kuna mashirika ya kidini au viongozi wanaofanya kazi kwa haki za binadamu katika mazingira yako ambao unaweza kuwasiliana nao? Motisha ya mtu anayeuliza maswali/anayepinga pia ni muhimu kuzingatia ili kutathmini hatari – je, wana udadisi wa kweli, wakitaka kujua ikiwa wanaweza kuwa waaminifu kwa imani yao na kufanya kazi kwa haki za binadamu, au wanajaribu kwa makusudi kugawanya? Kumbuka kwamba ni sawa kusema hujui na kupendekeza kwamba washiriki waendelee kufikiria jinsi imani yao inavyohusiana na mada zinazojadiliwa katika kozi nzima.

FORB NA THEOLOJIA
Pata nyenzo za dini mbalimbali hapa.

PINGAMIZI: Haki za binadamu ni jambo lililobuniwa na wanadamu. Sisi tunafuata mapenzi na sheria za Mungu. Dini yetu inatoa majibu yote tunayohitaji – hatuhitaji haki za binadamu!

MAJIBU AMBAYO YANAWEZA KUTOLEWA:

- Haki za binadamu ni jambo lililobuniwa na wanadamu. Hata hivyo, ndani ya kila dini kuna wasomi, viongozi na waumini wengi wanaoamini kuwa maudhui ya haki za binadamu kwa kiasi kikubwa yanadhihirisha mafundisho ya msingi ya dini zao kuhusu heshima ya utu wa binadamu, haki na wajibu. Huenda tunapochunguza haki za binadamu pamoja, tutagundua mambo yanayofanana na imani zetu.
- Haki za binadamu zina jukumu tofauti na mafundisho ya dini. Katika dunia ambayo watu wa imani mbalimbali na wasio na imani yoyote wanaishi pamoja, haki za binadamu hutupatia lugha ya pamoja ya kujadili aina ya jamii tunayotaka kujenga. Pia, zinatoa mfumo wa kisheria wa kuwawajibisha serikali – kuhakikisha zinaheshimu utu wa binadamu na haki.
- Wawakilishi wa dini na imani nyingi walishiriki katika kuandaa Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu, na rasimu zake zilijadiliwa kwa kina na nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa. Baadhi ya mijadala hiyo ilihusu uhusiano wa haki hizo na maadili ya kidini na kibinadamu. Lengo lilikuwa kuunda tamko ambalo ni la kweli la kiulimwengu – kufafanua haki ambazo kila mtu anaweza kukubaliana nazo, bila kujali dini au itikadi.

PINGAMIZI: Siwezi kufanya kazi kwa ajili ya haki za binadamu na/au FORB kwa sababu hazikubaliki katika dini yangu.

Vipindi vinaweza kuvurugwa kwa urahisi na mijadala ya haki maalum au njia za kutekeleza haki ambazo watu hawakubaliani nazo. Uliza haki zipi maalum ambazo mpingaji ana wasiwasi nazo. Isipokuwa makubaliano juu ya haki hiyo maalum ni muhimu kufikia malengo ya kozi, jaribu kuelekeza tena kwenye maeneo ya makubaliano na kupanua eneo la makubaliano hatua kwa hatua.

MAJIBU AMBAYO YANAWEZA KUTOLEWA:

- Uliza ikiwa kuna haki za binadamu/vipengee vya FORB vinavyoakisi maadili ya dini ya anayeleta pingamizi na ikiwa kuna matatizo ya haki za binadamu ambayo angependa yashughulikiwe. Eleza kuwa madhumuni ya kozi si kwamba tukubaliane kwa kila jambo bali kuwa wakala wa mabadiliko wenye nguvu, tukishughulikia matatizo katika jamii zetu.

- Toa mifano ya athari halisi za ukiukwaji wa haki husika kwa watu binafsi, makundi na jamii. Madhara hayo yanahusianaje na ujumbe wa heshima ya utu wa binadamu na upendo unaopatikana katika dini zetu?
- Huenda kupunguza haki kupitia sheria si njia bora ya kukuza maadili na mafunzo ya kiroho.
- Uliza kikundi dini yao inasema nini kuhusu haki wanayopinga na ni nini kinapaswa kutokea kwa watu wanaoitekeleza. Je, kuna andiko moja tu au tafsiri moja tu inayohusika? Je, kuna maandiko, maadili au tafsiri zinazounga mkono haki hiyo kwa namna yoyote? Je, mafundisho yamebadilika kadri muda unavyosonga?
- Nchi zilizo na aina moja ya dini waliowengi hushushughulikia haki za binadamu na FORB kwa njia tofauti. Hakuna njia moja pekee ya Kiislamu, Kibuddha au Kikristo ya kutunga sheria kuhusu haki za binadamu.

KIDOKEZO! Mwombe kiongozi wa dini au mwanateolojia anayejishughulisha na haki za binadamu aongoze mjadala huu.

SWALI: Je, kukubali haki sawa kwa dini nyingine kunamaanisha kwamba ninadhani dini zote ni sawa? Je, ni lazima niache kuamini kwamba dini yangu pekee ndiyo kweli ili kufanya kazi kwa ajili ya Uhuru wa dini au imani kwa wote?
PINGAMIZI: Kwa nini tuwape haki sawa wakati dini yetu inanguvu zaidi?

MAJIBU AMBAYO YANAWEZA KUTOLEWA:

- Uhuru wa dini au imani unalinda haki yako ya kuamini kwamba dini yako pekee ndiyo njia ya kweli. Pia unalinda haki ya wengine kuamini kwamba dini au imani yao pekee ndiyo ya kweli. Haki za binadamu na sheria za kimataifa si mahali pa kutoa maamuzi kuhusu ukweli wa dini. Haki za binadamu zinalenga watu, kwa msingi wa maadili ya utu wa binadamu. Zinaunda nafasi salama ya kuishi pamoja na tofauti zetu zote kwa kuweka viwango vya chini vya jinsi tunavyopaswa kutendeana kwa heshima na utu.
- Dini nyingi zinahimiza heshima ya utu wa binadamu na zinajumuisha toleo fulani la sheria kuu – kwamba tunapaswa kuwatendea wengine kama tunavyotaka kutendewa sisi wenyewe. Waulize washiriki ikiwa dini yao ina kanuni hiyo na wawasilishe mafundisho yanayohusiana nayo. Je, inawezekana kuishi kulingana na kanuni hiyo ikiwa watu hawana haki sawa?
- Kuwatendea watu kwa usawa kwa mujibu wa viwango vya chini vya haki za binadamu si sawa na kusema kuwa tunakubaliana na imani zao. Tunaweza kutofautiana kabisa na imani za watu wengine bila kutumia ubaguzi, vurugu au kunyima haki. Vikwazo vya haki ya kutekeleza dini vinakubalika tu ikiwa vitendo hivyo vinahatarisha haki na uhuru wa watu wengine, afya ya umma, n.k.
- Je, kuna haki tunazotaka sisi wenyewe, lakini tunadhani zinapaswa kunyimwa kwa wengine? Ikiwa tunawanyima watu wengine haki hizi, tunawezaje kuwa na hakika kwamba hapatakuja wakati ambapo serikali itaona ni sawa kutunyima haki zetu pia? Isipokuwa kila mtu ana haki, hakuna mtu mwenye haki – kinachobaki ni upendeleo wa kisheria ambao serikali inaweza kuondoa inapoona imekidhi matakwa yake.
- Haki za binadamu ndizo zinazowalinda watu wa imani yetu ambao ni wachache katika nchi nyingine. Ikiwa tunasema kuwa walio wengi au serikali katika nchi yetu inaweza kuamua nani ana haki na nani hana, basi tunasema pia kuwa ni sawa kwa mataifa mengine/idadi kubwa ya watu kumnyima mtu wa imani yetu haki zake.

Mada: Uhuru na udhibiti

SWALI: Watu hao wanaitekeleza dini kwa njia isiyolingana na utamaduni wetu. Si kila mtu wa dini hiyo anafanya hivyo, kwa hiyo si lazima. Ikiwa si lazima, basi tunapaswa kuwa na uwezo wa kuizima.
SWALI: Ikiwa viongozi wa kidini wanasema kuwa dini inapaswa kutekelezwa kwa namna moja, kwa nini tuwaruhusu watu kuitekeleza kwa njia tofauti?

MAJIBU AMBAYO YANAWEZA KUTOLEWA:

- Dini zina utofauti mkubwa wa ndani. Kuna njia tofauti za kufanya mambo ndani ya dini yoyote, na mara chache kuna mamlaka moja ya kidini inayokubalika na waumini wote. Katika dunia inayozidi kuwa na uhamaji mkubwa wa binadamu, watu wenye mitazamo mbalimbali wanaishi pamoja.
- Fikiria ikiwa ungelazimika kukimbilia nchi nyingine. Ungejisikiaje ikiwa jamii hiyo ingekunyima haki ya kutekeleza imani yako kwa njia unayoithamini au kukulazimisha kufuata njia inayokwenda kinyume na dhamiri yako?
- Watu hawapaswi kuthibitisha kuwa matendo yao ni sehemu muhimu ya dini yao ili kuruhusiwa kuitekeleza. Tunapaswa kuwa na uhuru. Ili kuzuia uhuru wa kidini, serikali lazima ithibitishe kuwa kizuizi kinachopendekezwa ni cha lazima – kwa mfano, ili kulinda afya ya umma au haki za wengine. Kuondoa uhuru kwa vizuizi visivyo vya lazima kunasababisha kinyongo, mvutano wa kijamii na hutoa mamlaka makubwa na ya kiholela kwa serikali, jambo ambalo hutoa jamii kwenye demokrasia kuelekea udikteta.

Mada: Kosa na maelewano

SWALI: Je, kuna haki ya kulindwa dhidi ya kukosewa?
PINGAMIZI: Kuwaruhusu wachache/wanafikra huru kuzungumzia au kuendesha dini zao kwa uhuru kunahatarisha maadili yetu na mshikamano wa kijamii.
PINGAMIZI: Hakuna mtu anayepaswa kuudhi hisia za kidini za wengine. Tunapaswa kupiga marufuku kufuru na aina nyingine za mazungumzo na tabia za kukera. Hivi ndivyo tunaweza kudumisha maelewano na kulinda vitu vitakatifu.
PINGAMIZI: Tunapaswa kulindwa dhidi ya dini yetu kutazamwa kwa njia hasi – jambo hili husababisha ubaguzi.

MAJIBU AMBAYO YANAWEZA KUTOLEWA:

- Kulingana na sheria za kimataifa, kila mtu ana haki ya kuamini, kutekeleza na kuonyesha imani yake kwa uhuru, ilimradi mazoea hayo hayadhuru haki na uhuru wa wengine. Sheria za kimataifa hazitupi haki ya kulindwa dhidi ya kuona na kusikia mambo tunayoyapinga au dhidi ya ukosoaji wa mambo tunayoyathamini. Hakuna haki ya kibinadamu ya kulindwa dhidi ya kuhisi kukosewa.
- Inaweza kuonekana kuwa jambo la busara na la kimaadili kupiga marufuku hotuba na tabia za kukera ili kulinda mshikamano wa kijamii. Hata hivyo, haiwezekani kufafanua kikamilifu ni nini hasa kinachochukuliwa kuwa ni kosa. Watu wengine huudhika hata kwa kuwepo kwa mawazo tofauti na yao. Kulingana na sheria za kimataifa, hotuba inayopaswa kupigwa marufuku ni hotuba ya chuki inayochochea uhasama na ghasia. Sheria kuhusu kufuru, uasi wa dini na 'kulinda maelewano ya kijamii' mara nyingi huwa na upana mkubwa kuliko inavyotakiwa. Sheria hizo zina mwelekeo wa:
  - kuwa tata kiasi kwamba ni vigumu kujua ni nini kinachozingatiwa kuwa kinyume cha sheria.

- kufafanua kosa kwa mtazamo wa walio wengi (kwa vitendo, hata kama si kwa nadharia).
- kuwa rahisi kutumiwa vibaya na kusababisha shutuma za uongo – ni vigumu kuthibitisha kwamba hukusema jambo fulani.
- kutia moyo ghasia kwa kuunga mkono wazo kwamba tunapaswa kuwaadhibu wanaoonyesha imani zao kwa amani ikiwa haziwafurahishi walio wengi.
- kufanya watu wanaoonyesha imani zao kwa amani wabebeshwe lawama kwa mvutano wa kijamii, badala ya watu wanaojibu maoni hayo kwa chuki na ghasia kuwajibika.

• Inaweza kuonekana kuwa sahihi kupiga marufuku mzaha au ukosoaji wa dini na taasisi za kidini ili kulinda vitu vitakatifu. Hata hivyo, ukosoaji wa nje na wa ndani una mchango mkubwa katika kuzifanya taasisi za kidini ziwe imara zaidi na ziwe na uaminifu zaidi. Taasisi za kidini zinaendeshwa na watu, na mara nyingine watu hufanya makosa. Ni kwa kuzungumzia matatizo bila hofu ndipo tunaweza kuyashughulikia. Kesi za hivi karibuni za unyanyasaji wa watoto katika taasisi za kidini zinaonyesha umuhimu wa uhuru huu.

• Je, 'maelewano' yanayojengwa juu ya wachache na wanafikra huru kunyamaza kuhusu imani na utambulisho wao siyo unafiki ambao unahisiwa kama maelewano tu na walio wengi? Je, tutakuwa na jamii thabiti na yenye amani ya kudumu ikiwa ni walio wengi pekee wanaohisi kuwa kuna maelewano na mshikamano?

• Hakuna haki ya kibinadamu ya kulindwa dhidi ya kuhisi kukosewa. Kwa hakika, ukosoaji na uvumilivu wa maoni mbalimbali na yanayokinzana ni muhimu kwa jamii bora. Hata hivyo, wakati serikali, vyombo vya habari, na/au jamii za walio wengi zinaposhiriki katika uonyeshaji wa kimfumo wa dini za wachache kwa mtazamo hasi na wa uhasama, matokeo yake ni ubaguzi na ghasia dhidi ya wafuasi wa dini hizo. Hii hutokea hata pale ambapo matamko binafsi yanayotolewa hayafikii kiwango cha hotuba ya chuki au uchochezi wa ghasia. Heshima kwa haki za binadamu na uthabiti wa jamii vinategemea serikali na vyombo vya habari kutenda kwa maadili na kwa haki. Jitihada za kukuza maadili katika siasa, vyombo vya habari, na mijadala ya umma, pamoja na mwitikio wa haraka dhidi ya hotuba za chuki na uchochezi, ni za umuhimu mkubwa.

Mrejesho na ruhusa

Tueleze **HADITHI NA MAONI** yako **hapa.**

TUELEZE HADITHI ZAKO ZA UANAMABADILIKO NA TUPE MREJESHO NA MAPENDEKEZO!
Tungethamini sana kusikia jinsi unavyotumia nyenzo hizi na ikiwa, na jinsi gani, zinachangia watu kuchukua hatua za mabadiliko! Nini kinafanya kazi vizuri na nini tunapaswa kuboresha?

Tafadhali tupe mrejesho wako na hadithi zako nasi hapa: https://www.forb-learning.org/feedback-form/

JE, NINAHITAJI KUOMBA RUHUSA AU KUMFAHAMISHA MTU KABLA YA KUTUMIA NYENZO HIZI?
Hapana. Yaliyomo katika mwongozo huu wa wawezeshaji na rasilimali zote zinazohusiana yanapatikana bure kwa yeyote kuyarekebisha na kutumia kwa madhumuni ya kuwaelimisha wengine na kukuza uhuru wa dini au imani kwa wote.

Unapotumia nyenzo hizi, tafadhali watambue na kuwaeleza watu kuhusu Jukwaa la Kujifunza kuhusu Uhuru wa Dini au Imani kupitia; www.forb-learning.org, ambapo wanaweza kupata taarifa zaidi, rasilimali za kujifunza, na kozi za mtandaoni.

JE, NAHITAJI KUOMBA RUHUSA ILI KUJUMUISHA MAZOEZI MAALUMU KUTOKA KATIKA MWONGOZO HUU KWENYE MACHAPISHO MENGINE?
Hapana. Unaweza kujumuisha maandishi ya mazoezi haya au toleo lake lililorekebishwa au kutafsiriwa katika machapisho mengine. Hata hivyo, huwezi kutumia vielelezo bila ruhusa. Unapotumia maandishi, tafadhali watambue na kuwaeleza watu kuhusu Jukwaa la Kujifunza Uhuru wa Dini au Imani na uweke kiungo cha nyenzo chanzo kama ifuatavyo:

Chanzo: Kozi ya Wanamabadiliko wa Jamii, Jukwaa la Kujifunza kuhusu Uhuru wa Dini au Imani, (FORB learning platform). www.forb-learning.org/changemakers

Tungependa kusikia kuhusu machapisho yako! Tafadhali tumia fomu ya maoni kushiriki taarifa.

JE, NINAWEZA KUTAFSIRI NA KUCHAPISHA MWONGOZO WA WAWEZESHAJI NA NYENZO ANDAMIZI ZINAZOHUSIANA KATIKA LUGHA YANGU?
Tunaamini umuhimu wa kuhakikisha kwamba nyenzo za kujifunza kuhusu Uhuru wa Dini au Imani zinapatikana kwa watu wasiozungumza Kiingereza. Unaweza kutafsiri na kutumia sehemu za yaliyomo bila vikwazo. Ikiwa unataka kutafsiri kozi nzima na mwongozo wa wawezeshaji, tafadhali wasiliana nasi kupitia barua pepe: info@forb-learning.org

HAKI MILIKI
Maandishi ya chapisho hili yanalindwa chini ya Haki Miliki ya Creative Commons CC BY-SA. Hii inamaanisha kuwa uko huru kurekebisha na kutumia nyenzo kwa njia yoyote mradi tu utaje chanzo chake kuwa Jukwaa la Kujifunza kuhusu Uhuru wa Dini au Imani na kushiriki matoleo yako yaliyorekebishwa nasi na wengine kwa kutumia masharti yaya haya ya Haki Miliki.

Vielelezo kutoka kwenye mwongozo wa wawezeshaji na maandishi na vielelezo vya hadithi ya 'Nyimbo za Filimbi na Ngoma' vinalindwa na haki miliki na haviwezi kuchapishwa au kuboreshwa bila idhini. Tafadhali wasiliana nasi.

Haki miliki zote zinashikiliwa na SMC Faith in Development, 2021, kwa niaba ya NORFORB, mtandao ulioandaa Jukwaa la Kujifunza kuhusu Uhuru wa Dini au Imani.

SEHEMU YA B

Nyenzo za kozi

Vipindi vya 1-5

Sehemu ya 1: Kuandaa mifuko yetu ya safari

Kozi ya Wanamabadiliko wa Jamii inalenga kuwaandaa washiriki kuwa watetezi wa Uhuru wa Dini au Imani (FORB) katika jamii zao. Mchakato wa kuleta mabadiliko kwa ajili ya uhuru wa dini au imani ni safari ndefu na mara nyingine yenye changamoto. Ni muhimu kuwa tayari!

Sehemu ya 1 ya kozi hii inajikita katika 'kuandaa mifuko yetu ya safari' – kujenga maarifa na mitazamo ili akili na mioyo yetu iwe tayari kwa safari ya mabadiliko. Inawapa washiriki fursa ya kujifunza kuhusu haki za binadamu kwa ujumla, kuchunguza mitazamo yao kuhusu FORB, na kutafakari jinsi wanavyowaona watu wenye utambulisho tofauti na wao. Pia, inatoa ujuzi wa kufanya uchambuzi wa muktadha.

Vipindi vya 1-5 vinaunda mchakato wa hatua kwa hatua, ambapo kila kipindi hujengwa juu ya maarifa na tafakari ya kipindi kilichopita:

- Kipindi cha 1 kinatambulisha haki za binadamu kwa ujumla.
- Kipindi cha 2 kinatambulisha Uhuru wa Dini au Imani kwa kina.
- Kipindi cha 3 kinahusu uchunguzi wa utambulisho wetu na masuala ya upendeleo na madhila.
- Kipindi cha 4 kinachunguza ukiukwaji wa FORB na kuwapa washiriki fursa ya kufanya mazoezi ya kutambua ukiukwaji huo.
- Kipindi cha 5 kinawawezesha washiriki kuandaa uchambuzi wa muktadha wa FORB katika jamii zao kwa kutambua changamoto zinazohusiana na FORB

Maarifa na tafakari kutoka vipindi hivi yanaweka msingi muhimu kwa Sehemu ya 2 ya kozi, ambayo inahusu kupanga safari za mabadiliko katika jamii zetu – kwa kutumia mbinu za kutetea haki za binadamu na kupanga hatua za utekelezaji. Uchambuzi wa muktadha uliotengenezwa katika Kipindi cha 5 utatumika kama nyenzo ya rejea katika vipindi vyote vya Sehemu ya 2.

KIPINDI CHA 1

Mahitaji ya binadamu – haki za binadamu – wajibu wa binadamu

Muhtasari wa kipindi

Katika mktadha mbalimbali, watu huona haki za binadamu kama jambo lililo mbali na maisha ya kila siku, lisilohusiana na tamaduni za kiasili, au kama sehemu ya ajenda mpya ya ukoloni wa Magharibi. Kwa bahati mbaya, mtazamo huu hasi kuhusu haki za binadamu unaweza kuwafanya watu wakose kutumia zana muhimu inayoweza kuboresha maisha katika jamii zao. Ikiwa watu hawajui haki zao na haki za wengine kulingana na sheria za kimataifa na kitaifa, inakuwa rahisi kwa ukiukwaji wa haki za binadamu kuendelea bila kupingwa.

KIDOKEZO! Katika muhtasari wa kipindi, unaweza kuona malengo ya mafunzo, maudhui, muda wa kipindi, pamoja na orodha ya nyenzo na maandalizi yanayohitajik.

Kipindi hiki kina sehemu mbili:

SEHEMU YA 1: UTANGULIZI
Sehemu hii inajumuisha utangulizi wa muundo na malengo ya kozi, pamoja na kuwapa washiriki nafasi ya kufahamiana. Pia, inajumuisha mjadala kuhusu kanuni za msingi za mijadala. Hili ni muhimu sana hasa katika makundi yenye changamoto za kuaminiana au yanayojadili mada nyeti.

SEHEMU YA 2: MAHITAJI YA BINADAMU – HAKI ZA BINADAMU – WAJIBU WA BINADAMU
Sehemu hii inalenga kujenga maarifa ya washiriki kuhusu haki za binadamu na kuwafanya waone thamani yake, kwa kuzihusisha haki na mahitaji wanayopitia katika maisha yao na jamii zao. Hili linatoa msingi muhimu kwa vipindi vyote vitakavyofuata.

Malengo ya mafunzo

Kipindi hiki kinajikita katika kujenga maarifa ya washiriki kuhusu haki zao za binadamu na mtazamo chanya kuelekea haki hizo.

KIDOKEZO! Unaweza kupata mwongozo wa kukusaidia kujibu maswali magumu kuhusu haki za binadamu kwenye kurasa 21–28.

Kufikia mwisho wa kipindi, washiriki wataweza:

- Kutaja angalau haki sita za binadamu zilizo muhimu kwa maisha yao ya kila siku na kutambua angalau haki moja inayokiukwa katika jamii zao.
- Kueleza kwamba haki za binadamu ni muhimu na zinahusiana moja kwa moja na maisha yao ya kila siku, na kwamba kila mtu anaweza kuchangia katika kujenga jamii inayoheshimu na kulinda haki za binadamu.

ZINGATIA

Malengo ya mafunzo ni kumsaidia mwezeshaji kutathimini namna mchakato unavyoenda, kwa kuonyesha maeneo maeneo ambayo unaweza kuyazingatia kuyaendeleza kama vile uelewa wa washiriki, mitazamo na maarifa yao. Hayatarajiwi kuchukuliwa kama taarifa za washiriki – orodha ya vitu ambavyo washiriki wanatarajia 'kufanikiwa).

Uhalisia wa malengo ya kila kipindi utategemea namna ambavyo washiriki walivyo wakati wa kuanza kipindi – kwa mfano, mitazamo waliyonayo kuhusu haki za binadamu. Mchakato wa kufikia malengo katika kozi unaweza kuwa wa taratibu kuliko ukilinganisha na katika kipindi kimoja.

Yaliyomo katika kipindi na muda

Ukaribisho na utangulizi Ukaribisho, utambulisho wa washiriki, kozi na zoezi la kuweka kanuni.	Dakika 30
Mazoezi ya pamoja: Supu ya maisha Huchunguza mahitaji ya binadamu kwa kutumia taswira ya viungo katika sufuria ya supu.	Dakika 35
Mazoezi ya kutembea na kuzungumza: Matunzio ya haki za binadamu Husaidia washiriki kuunganisha mahitaji ya binadamu na haki za binadamu.	Dakika 25
Uwasilishaji: Mahitaji ya binadamu – Haki za binadamu – Wajibu wa binadamu Utangulizi wa haki za binadamu unaoangazia makubaliano muhimu, wajibu wa mataifa, na nafasi ya watu wa kawaida katika kufanya haki ziwe jambo la uhalisia.	Dakika 15
Kufunga mjadala Huwapa washiriki fursa ya kutafakari juu ya maudhui yaliyowasilishwa na kufunga kipindi.	Dakika 15
JUMLA YA MUDA	**Saa 2**

Jiandae

Jiandae kwa kipindi kulingana na mwongozo katika ukurasa wa 15, 'Jinsi ya kujiandaa kwa kila kipindi.' Kumbuka – unawajua washiriki wako! Unakaribishwa kurekebisha na kubadilisha vipengele vyovyote vya kikao ili kivutie na kukidhi mahitaji ya kundi lako.

NYENZO ZA KIPINDI HIKI

Mbali na nyenzo za kawaida kwa kila kipindi zilizoainishwa kwenye ukurasa wa 16, utahitaji vifaa vifuatavyo ili kuendesha kipindi hiki kwa ufanisi:

- Kikapu kidogo.
- Vipande vidogo vya karatasi.
- Chungu cha supu (aina yoyote inayojulikana katika tamaduni yako) chenye lebo 'supu ya maisha'.
- Nakala moja ya 'Kadi za mahitaji ya binadamu' - ikatwe vipande kabla ya kipindi.
- Nakala moja ya 'Mabango ya jumba la maonyesho ya haki za binadamu'.
- Ikiwa utaendesha zoezi la nyongeza la 'Kubadilishana mawazo,' utahitaji mawe 10, sarafu, au vipande vya karatasi kwa **KILA** mshiriki.

NYENZO ANDAMIZI za kipindi hiki zinaweza kupatikana hapa.

CHAGUO LA ZIADA: JENGA KUJIAMINI!

Kama sehemu ya maandalizi yako, tazama filamu fupi kuhusu haki za binadamu. Hii itakusaidia kujiamini zaidi na kuongeza uwezo wa kujibu maswali. Lakini usiwe na wasiwasi – kama mwezeshaji, jukumu lako si kuwa mtaalamu bali kuongoza mchakato wa kujifunza kwa pamoja.

FILAMU

ANDAA UKUMBI

Kwa kipindi hiki, ni wazo zuri kuanza na viti katika umbo la nusu duara vikielekea mbele. Kundi linapaswa kuwa na nafasi ya kutembea kwa uhuru. Ukumbi mkubwa usio na meza utafaa zaidi!

'Supu ya maisha'

"Mazoezi ya 'Supu ya maisha' na 'Matunzio ya haki za binadamu' yalikuwa na mafunzo mengi. Baadhi ya washiriki waligundua kwa mara ya kwanza kuwa haki za binadamu zina maana katika maisha yao ya kila siku. Walitambua haki za binadamu walizokuwa hawajui kuwa wanazo."

UKOHA NGWOBIA, MWEZESHAJI, NIGERIA

Mpango wa kina wa kipindi

SEHEMU YA 1: UTANGULIZI Dakika 30

Kwa kuwa hiki ni kipindi cha kwanza, ni muhimu kutumia kidogo muda kusaidia kujenga umoja wa kundi, kuweka kanuni na kutambulisha malengo na muundo wa kozi.

ZINGATIA

Mnaweza kufupisha zoezi hili kama washiriki wote tayari mnafahamiana vizuri. Kama kunauwezakano wa kuwepo masuala ya kutoaminiana katika kundi, basi unaweza kutumia muda kidogo kujenga uhusiano kwanza.Kama ni hivyo, fikiria kuanza na kipindi cha kwanza kirefu cha kozi. Pendekeza kazi za ziada za vikundi kwa wale wanapenda kutumia muda mwingi zaidi katika hili

1. Ukaribisho Dakika 3

Karibisha kila mtu kwa njia inayofaa kikundi chako, kwa mfano, kwa kutoa maneno machache ya shukurani kwa mahudhurio yao, kuimba ubeti wa wimbo au kusema dua.

2. Zoezi la ufunguzi: Kamilisha senstensi Dakika 12

ZOEZI LA PAMOJA

LENGO
Zoezi hili linawapa washiriki fursa ya kujitambulisha na linakusaidia kuelewa sababu zao za kuhudhuria kozi hii.

JINSI YA KUENDESHA ZOEZI
Zunguka duara kisha umwombe kila mshiriki amalizie sentensi ifuatayo (Sentensi moja kwa kila mshiriki – si majibu marefu!).
"Jina langu ni… na nimejiunga na kozi hii kwa sababu…"

JINSI YA KUHITIMISHA ZOEZI
Baada ya kila mtu kuzungumza, taja kwa ufupi mada zilizojitokeza mara kwa mara katika majibu yao. Washukuru washiriki kwa maoni yao na waambie kuwa unatarajia angalau baadhi ya matarajio yao kwa kozi yatatimizwa. Kisha, utawasilisha malengo na muundo wa kozi.

KIDOKEZO! Kuwa makini kulinda muda katika Sehemu ya 1: Utangulizi. Unahitaji kulinda muda kwa ajili ya Sehemu ya 2!

3. Utangulizi wa kozi Dakika 5

GUMZO FUPI

LENGO
Mazungumzo haya mafupi yanawaletea washiriki muhtasari wa malengo ya kozi, mbinu za ufundishaji, mada zitakazojadiliwa, na mambo ya kiutendaji.

NINI CHA KUSEMA
Pitisha yaliyomo kwenye slaidi za uwasilishaji 3-6 au maandishi hayo hayo kwenye karatasi la bango kitita. Kuna maelezo kwa wawezeshaji kwenye slaidi ya uwasilishaji unayoweza kutumia (hata ikiwa unatumia karatasi za bango kitita.

ZINGATIA

Kama haki za binadamu zinaleta kutoelewana katika kundi, unaweza kuamua kutumia maneno mengine ya mada za kozi katika slaidi ya 5 ili kutumia dhana zinazokubalika kiasilia na zinazohusiana.

4. Zoezi la kuweka kanuni: Pitisha kapu Dakika 10

ZOEZI LA PAMOJA

LENGO

Kanununi ni muhimu sana katika kusaidia kujenga mazingira salama yenye matarajio yanayofanana kuhusu namna tutakavyoongea na kusikilizana.

NYENZO

- Kapu.
- Vipande vidogo vya karatasi.
- Peni.

JINSI YA KUANZA ZOEZI

Eleza yafuatayo:

Katika kozi hii tunataka kila mtu ajisikie salama na aheshimiwe – awe na fursa ya kuzungumza na kushiriki mawazo, mitazamo na uzoefu wake kwa usawa. Ili kusaidia kuunda mazingira haya, ni muhimu kuwa na kanuni za msingi ambazo sote tunakubaliana nazo na tunawajibika nazo. Kanuni hizi zinaweza kuwa za kiutendaji (kama vile kufika kwa wakati au kuweka simu kimya), au kuhusu jinsi tunavyohusiana (kama vile kusikiliza kwa heshima au kumpa kila mtu nafasi ya kuzungumza).

JINSI YA KUENDESHA ZOEZI

Weka kikapu katikati ya mduara. Mpe kila mshiriki kipande kidogo cha karatasi na kalamu. Mwambie kila mmoja aandike kanuni mbili wanazoona zinapaswa kuwa mwongozo wa kikundi, kisha waweke karatasi zao kwenye kikapu.

Soma maoni yote kutoka kwenye kikapu na uyaandike kwenye bango-kitita. Ikiwa kanuni zifuatazo hazijatajwa, ongeza:

- Sikiliza kwa makini – heshimu wengine wanapozungumza.
- Zungumza kwa kutumia uzoefu wako badala ya ujumlishaji (sema 'mimi' badala ya 'wao', 'sisi', na 'nyinyi').
- Usisite kuuliza maswali kwa heshima lakini jiepushe na mashambulizi ya kibinafsi – zingatia mawazo.

Waulize wanakikundi ikiwa wanakubaliana na kanuni hizi.

5. Zoezi la chaguo la ziada: Kubadilishana mawazo Dakika 15

ZOEZI LA KIKUNDI

Ikiwa kikundi chako kinahitaji muda zaidi wa kufahamiana, unaweza kuongeza dakika 15 kwenye kipindi na kujumuisha zoezi hili

LENGO

Husaidia washiriki kuungana na kuonesha mambo mengi wanayoshabihiana.

JINSI YA KUENDESHA ZOEZI

- Gawanya washiriki katika makundi ya watu 4-6.
- Wape kila mshiriki sarafu 10/vijiwe vidogo/karatasi ndogo n.k.
- Kila mshiriki atazunguka na kutaja jambo analopenda (kwa mfano, kusoma). Wale wanaopenda jambo hilo pia wataweka sarafu moja katikati ya duara.
- Mshiriki wa pili atasema kitu kingine anachopenda, na kila anayependa pia ataweka sarafu moja.
- Endelea hadi mshiriki mmoja atakapomaliza sarafu zake zote.

SEHEMU YA 2: UTANGULIZI KUHUSU HAKI ZA BINADAMU

1. Zoezi la pamoja: Supu ya maisha Dakika 35

ZOEZI LA PAMOJA

MAELEZO

Zoezi hili linatumia taswira ya viungo katika chungu cha supu kusaidia washiriki kuchunguza mahitaji ambayo sisi (na wanadamu wote) tunayo. Kwa kutumia kadi zilizotayarishwa tayari pamoja na mawazo yao binafsi, washiriki huchagua viungo vinavyopaswa kuwemo kwenye 'supu' ili maisha yao yawe na hadhi.

LENGO

Zoezi hili linafuatwa na zoezi la 'Matunzio ya Haki za Binadamu', ambalo linaunganisha mahitaji yaliyotambuliwa katika zoezi hili na haki zilizobainishwa katika Azimio la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu. Mazoezi haya mawili yanahusiana na yanapaswa kufanywa pamoja. Kwa pamoja, yanalenga kusaidia washiriki kugundua jinsi haki za binadamu zinavyohusiana na maisha yao ya kila siku na jinsi zinavyoakisi mahitaji wanayoyatambua wao wenyewe—badala ya kuonekana kuwa ya kigeni au ya mbali.

NYENZO NA MAANDALIZI YA AWALI

Utahitaji:

- Chungu cha jadi cha kupikia supu au sufuria kubwa, kikiwa na lebo iliyoandikwa 'supu ya maisha' iliyobandikwa pembeni.
- 'Kadi za mahitaji ya binadamu', zilizochapishwa na kukatwa. Ikiwa ni lazima, hariri kadi hizo kwa kubadilisha maandishi ya Kiingereza na tafsiri katika lugha ya washiriki.
- Kalamu chache.

KIDOKEZO! Kumbuka kuwa nyenzo za kozi zinapatikana katika lugha mbalimbali kwenye klungo.

JINSI YA KUANZA ZOEZI DAKIKA 4

Weka chungu cha supu katikati ya chumba kisha sambaza 'kadi za mahitaji ya binadamu' sakafuni kuzunguka chungu hicho, pamoja na kalamu chache. Waombe kila mtu asimame katika duara kuzunguka kadi hizo.

Eleza yafuatayo:

- Maisha ni sawa na chungu cha supu chenye viungo vingi—kama ilivyo kwa supu, maisha yanahitaji viungo mbalimbali ili yawe na ladha nzuri.
- Baadhi ya viungo vya maisha, kama vile (taja kitu cha anasa kinachojulikana katika tamaduni husika), vinaweza kufanya maisha yawe matamu zaidi. Lakini kuna viungo vingine, kama makazi, chakula au huduma za afya, ambavyo ni mahitaji ya msingi. Ikiwa viungo hivyo havipo, maisha yanakuwa magumu na tunateseka kimwili, kisaikolojia, kijamii au kiroho. Tunapoteza hadhi yetu.
- Katika zoezi hili, tutafakari kuhusu viungo vya msingi katika maisha yetu. Tutapika supu ya maisha—haswa maisha yenye hadhi!
- Kila moja ya kadi zilizo sakafuni kuzunguka chungu cha supu inawakilisha kitu ambacho kinaweza kuwa muhimu kwa maisha yenye hadhi. Pia kuna kadi tupu ambazo tunaweza kutumia kuandika au kuchora mawazo yetu wenyewe kuhusu tunachokihitaji kwa maisha yenye hadhi.

JINSI YA KUENDESHA ZOEZI DAKIKA 30

- Waambie wanakundi kwamba wana dakika 2 kutazama kadi na kufikiria ni zipi zilizo muhimu zaidi kwao.

KIDOKEZO! Kuwa makini na muda hapa – unahitaji kuhifadhi muda kwa ajili ya majadiliano yanayofuata!

- Kisha, wakizunguka mduara, mwombe kila mtu achukue kadi moja inayoakisi kitu wanachoona kuwa muhimu kwa maisha yenye hadhi, aseme sentensi moja tu kuhusu kwa nini ni muhimu, kisha aiweke kwenye chungu cha kupikia.
- Endelea kuzunguka mduara hadi watu wahisi kwamba hakuna kadi nyingine iliyobaki ambayo ni muhimu kwao. Pia wanaweza kuchukua kadi tupu, kueleza inawakilisha nini, na kuiweka kwenye kikapu. Watu hawapaswi kutoa maoni kuhusu chaguo za wenzao wakati huu.
- Mara tu kadi zote ambazo watu wanataka kuongeza zimeongezwa kwenye kikapu, waambie kundi kwamba sasa tumetengeneza "supu ya maisha". Waombe wajadili maswali yafuatayo:
  - Je, kuna viungo tulivyoongeza ambavyo si vya lazima kwa maisha yenye hadhi?
  - Je, kuna viungo (kadi) tulivyoacha na tukaviacha chini? Kwa nini?
  - Ni athari gani tunazopata tunapokosa "Viungo vya msingi" katika maisha yetu? Shiriki mawazo yako.
  - Ikiwa kundi lingine katika sehemu tofauti ya dunia lingefanya zoezi hili, unadhani wangekuwa na mahitaji tofauti sana au kuna mahitaji ya msingi yanayotakiwa na wanadamu wote?

JINSI YA KUHITIMISHA ZOEZI DAKIKA 1
Malizia mjadala kwa kusema kwamba binadamu duniani kote wana mambo mengi yanayofanana – kwa sababu sisi sote ni wanadamu na tuna mahitaji sawa.

2. Zoezi la kutembea na kuzungumza: Matunzio ya haki za binadamu Dakika 25

ZOEZI LA PAMOJA

MAELEZO
Washiriki wanatembea ukumbini wakilinganisha "kadi za mahitaji ya binadamu" kutoka zoezi lililopita na mabango ya haki za binadamu yanayoonyesha haki zinazotambuliwa katika Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu.

LENGO
Pamoja na zoezi lililotangulia, hili linasaidia washiriki kuelewa uhusiano kati ya haki za binadamu na maisha yao ya kila siku, na kutambua kuwa haki hizo zinahusiana moja kwa moja na mahitaji wanayoyatambua – badala ya kuziona kama dhana za 'kigeni' au 'zisizo na uhalisia.'

NYENZO NA MAANDALIZI YA AWALI

- Chapisha mabango 30 ya 'matunzio ya haki za binadamu' na yabandike ukutani kote chumbani. Ikiwa ni lazima, hariri maandishi ya mabango kwanza kwa kutafsiri maandishi yake katika lugha ya washiriki.
- Soma mabango hayo na fikiria ikiwa haki zozote zilizoelezwa zinakiukwa katika muktadha wenu. Kufikiria haya mapema kutakusaidia kuongoza mjadala vizuri.

JINSI YA KUANZA ZOEZI DAKIKA 1
Chukua 'kadi zote za mahitaji ya binadamu' kutoka zoezi lililopita na wagawie washiriki.

Waulize washiriki kama wamewahi kusikia kuhusu haki za binadamu. Waeleze kuwa mabango yaliyobandikwa ukutani yanaelezea haki za binadamu ambazo kila mwanamume, mwanamke, na mtoto duniani anazo, kulingana na mikataba ya kimataifa ya haki za binadamu iliyosainiwa na karibu serikali zote duniani.

JINSI YA KUENDESHA ZOEZI DAKIKA 23

- **MATEMBEZI KWENYE MATUNZIO** (DAKIKA 15)
  Tembelea matunzio' kuzunguka chumba, ukitembelea kila bango. Unapofika kwenye kila bango, soma maandishi ya bango kwa sauti. Uliza kama mtu yeyote ana "kadi ya mahitaji ya binadamu" inayohusiana na haki hiyo ya binadamu, na uwaombe wale wanaojibu ndiyo waseme hitaji hilo ni nini. (Bango na kadi zinazolingana zina utambulisho sawa, hivyo hii inapaswa kuwa rahisi!). Endelea mara moja kwenye bango linalofuata bila mjadala – unahitaji kulinganisha mabango mawili kwa dakika!
  Usijali ikiwa hakuna mtu anayependekeza kadi kwa bango fulani, endelea kuzunguka mabango na unapofika mwisho, linganisha kadi zozote zilizosalia ambazo watu hawajataja, ukitumia utambulisho kama mwongozo.

- **MASWALI YA KUJADILI** (DAKIKA 8)
  Baada ya kusoma mabango yote na kuyalinganisha na kadi za mahitaji, waulize washiriki:
  – Je, haki hizi zinaakisi mahitaji mliyonayo kwa maisha yenye hadhi – kwa maneno mengine, zina uhusiano na maisha yetu
  – Ni haki zipi kati ya hizi zinaheshimiwa na kulindwa katika nchi/jamii yetu na zipi haziheshimiwi? Ikiwa washiriki wanapata ugumu kujibu, taja baadhi ya haki za binadamu unazojua ambazo zinakiukwa kisheria au kivitendo.

KIDOKEZO! Kama unaweza kupata kipindi kirefu zaidi, unaweza kuongeza muda wa mjadala hapa.

JINSI YA KUHITIMISHA ZOEZI DAKIKA 1

Hitimisha mjadala kwa kusema kwamba mazoezi tuliyofanya hadi sasa yametusaidia kuchunguza mahitaji tuliyonayo, maana ya haki za binadamu, na jinsi mahitaji yetu yanavyohusiana na haki za binadamu. Tunaweza kusema kwa muhtasari kwamba haki za binadamu zina uhusiano wa karibu na mahitaji yetu ya msingi pamoja na aina ya jamii tunayotaka kuishi ndani yake. Sasa tunakwenda kujifunza zaidi kuhusu haki za binadamu kupitia uwasilishaji.

Waombe washiriki wote warudishe kadi zao kwenye chungu cha supu. Tutahitaji chungu na kadi hizo katika kikao kijacho.

3. Uwasilishaji: Mahitaji ya binadamu – Haki za binadamu – Wajibu wa binadamu Dakika 15

WASILISHO

MAELEZO NA LENGO

Wasilisho hili linawatambulisha washiriki kwenye misingi ya haki za binadamu kwa mtazamo wa mahitaji ya binadamu, haki za binadamu, na majukumu ya binadamu. Linaeleza mikataba muhimu ya kimataifa, majukumu ya serikali, na wajibu wa kimaadili wa wanajamii. Hili ni jambo la msingi kwa mwendelezo wa mafunzo haya.

NYENZO

- Mwongozo wa uwasilishaji unapatikana ukurasa wa 41 wa mwongozo huu.
- Maandishi haya yanahusiana na slaidi 7-28 za kipindi na yamejumuishwa katika maelezo ya mzungumzaji kwa kila slaidi.
- Toleo linaloweza kuhaririwa la maandishi haya linapatikana miongoni mwa nyenzo za kipindi hiki.

MAANDALIZI YA AWALI

Andaa kwa kufuata mwongozo uliotolewa katika ukurasa wa 15 'Jinsi ya kuandaa kila kipindi.

Soma na rekebisha maandishi na slaidi za PowerPoint (au tengeneza karatasi za maandishi kwa hoja kuu kutoka kwa slaidi). Soma sehemu ya maswali magumu katika kurasa za 21-28 na fikiria ikiwa unahitaji kuongeza hoja nyingine, kulingana na pingamizi inayoweza kutolewa na washiriki. Fanya mazoezi ya kuwasilisha mada ukitumia slaidi au karatasi za maandishi.

KIDOKEZO! Waombe washiriki wahifadhi maswali na maoni yao hadi mwisho wa wasilisho lako.

4. Kufunga mjadala   Dakika 15

MJADALA WA PAMOJA

LENGO

Mjadala huu unawapa washiriki nafasi ya kutafakari juu ya yale waliyosikia kwenye wasilisho na kuhitimisha kipindi.

JINSI YA KUENDESHA MJADALA

Karibisha maoni na maswali kuhusu wasilisho lililopita, kisha waulize maswali haya:

- Haki za binadamu zinatokana na misingi ya usawa, utu, na uwajibikaji kwa kila mmoja wetu. Ni dhana gani, hadithi, au methali kutoka katika tamaduni, mila na lugha zetu zinazoakisi mawazo haya?
- Je, tunataka haki za binadamu ziwe halisi katika jamii zetu? Je, tunaweza, kama Zaliha na Magdalena, kuchangia hilo kutimia?

KIDOKEZO! Tafuta msaada wa kujibu maswali magumu katika kurasa za 21-28.

Hitimisha mjadala kwa kusema kuwa katika kipindi kijacho, tutazingatia haki ya binadamu ya uhuru wa mawazo, dhamiri, dini au imani. Katika kipindi chote cha mafunzo haya, tutaendelea kufikiria ikiwa na jinsi gani tunaweza kuleta mabadiliko katika jamii zetu.

KIDOKEZO! Usitupe kadi za haki za binadamu – utazihitaji katika kipindi kijacho!

Chanzo

Kubadilishana mawazo: Imetoholewa kutoka zoezi la 'Me too', katika kuwezesha Ujitambulishaji wa Kundi, Lions Club International. https://temp.lionsclubs.org/EN/pdfs/icebreakers.pdf

Mwongozo wa uwasilishaji

Mahitaji ya binadamu – Haki za binadamu – Wajibu wa binadamu

Nakala hii ya uwasilishaji wa kipindi cha 1 inaonyeshwa kwenye slaidi za 7-28 za PowerPoint ya kipindi.

UTANGULIZI: HAKI ZA BINADAMU

Haijalishi sisi ni nani, tuna dini gani, kabila gani, jinsia gani au umri gani, na haijalishi tunaishi wapi – kuna mahitaji ya msingi ambayo sote tunashiriki. Hakuna mtu anayetaka kukamatwa bila sababu, kuteswa au kubaguliwa, na hakuna mtu anayetaka watoto wake wafe kwa njaa. Sote tunataka kuishi katika jamii ambako tunalindwa dhidi ya mambo haya.

Binadamu wote wana mahitaji sawa ya msingi na ya ulimwengu mzima. Ikiwa mahitaji haya hayatatimizwa, ustawi wetu wa kimwili, kihisia na kiroho utaathirika.

HAKI ZA BINADAMU

Serikali za dunia zimekubali kwamba kila mtu kila mahali ana mahitaji haya na kwamba serikali zina jukumu – kwa hakika, zina wajibu – wa kuheshimu mahitaji haya na kufanya kila liwezekanalo kuhakikisha yanatimizwa.



Ili kuhakikisha hili linakuwa uhalisia, serikali za dunia zilikubaliana juu ya haki za binadamu za ulimwengu mzima – haki ambazo kila mtu anazo, na wajibu wa kila serikali kuheshimu, kulinda na kuendeleza haki hizo.

Makpokubaliano matatu muhimu zaidi ya haki za binadamu ni:

- azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu, ambalo tumelichunguza kwa kutumia mabango,

na makubaliano mawili yenye maelezo ya kina zaidi kuhusu haki zetu:

- mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa (ICCPR)
- mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kitamaduni (ICESCR)

Mikataba hii miwili ni ya kisheria kwa nchi zinazoiridhia.



Nchi nyingi duniani zimejitolea kutekeleza makubaliano haya – nchi zote zilizo kwenye rangi ya kijani kwenye ramani hizi! Serikali za nchi hizi zote zimekubali kuwa na wajibu wa kisheria chini ya sheria za kimataifa kufanya mambo matatu:



- Kuheshimu haki za binadamu katika sheria wanazotunga na hatua zinazochukuliwa na maafisa wa serikali. Kwa mfano, hakupaswi kuwa na sheria za kibaguzi, na hakuna mtu anayepaswa kuteswa.
- Kulinda haki za binadamu kwa kuhakikisha kila mtu anaweza kutafuta haki pale haki zake zinapokiukwa na serikali au mtu mwingine yeyote.
- Na kukuza haki za binadamu kwa kufanya kila juhudi kuhakikisha kila mtu anapata haki zake. Kwa mfano, kuhakikisha kila mtu anaweza kupata huduma za afya na elimu. Bila shaka, si serikali zote zina nyenzo sawa, hivyo kutimiza haki hizi za kijamii na kiuchumi ni mchakato wa hatua kwa hatua.

Serikali zimekubaliana kuwa kila binadamu ana haki hizi kwa usawa. Kifungu cha kwanza cha Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu kinasema, "Watu wote huzaliwa huru na sawa katika utu na haki."

Kwa bahati mbaya, serikali nyingi hazitimizi ahadi hizi – watu wengi wanakumbwa na ukiukwaji wa haki zao. Wanawake, wasichana, makundi ya wachache, watu wenye ulemavu na wahamiaji wako katika hatari zaidi ya kukumbwa na ukiukwaji wa haki zao. Ukatili wa kijinsia ni mfano wa kawaida unaotokea katika kila nchi duniani.

UKOSOAJI WA HAKI ZA BINADAMU

Wakati serikali zinapokiuka haki au kushindwa kuwalinda watu dhidi ya ukiukwaji wa haki, hakuna jeshi la polisi la kimataifa linaloweza kuja na kuiadhibu serikali husika. Ikiwa hakuna polisi wa kimataifa wa kulazimisha serikali kufuata haki za binadamu – je, haki za binadamu ni dhaifu, maneno tu kwenye karatasi badala ya kuwa chombo chenye nguvu cha mabadiliko?

Kuna ukweli fulani katika hoja hiyo – baadhi ya serikali ni ngumu kushawishi. Lakini katika nchi nyingi, ukosoaji wa ndani na wa kimataifa kuhusu ukiukwaji wa haki za binadamu umesababisha mabadiliko chanya. Kuna njia nyingi za kuhamasisha haki za binadamu bila kuwa na jeshi la polisi la kimataifa.

Pia, kuna sababu nyingine zinazofanya watu wakosoe haki za binadamu. Huenda nawe umewahi kuwa na mawazo haya:

- Pengine unahisi haki za binadamu ni jambo la kiufundi – ni mada kwa wanasheria na wanasiasa badala ya kitu unachoweza kushiriki moja kwa moja.
- Au labda unadhani haki za binadamu ni jambo lililo mbali na maisha yako ya kila siku – kitu ambacho wasomi mijini wanaweza kujishughulisha nacho.
- Au pengine haki za binadamu zinaonekana kama silaha katika mchezo wa kisiasa wa kimataifa, ambapo serikali zinazitumia kwa unafiki, zikiwakosoa maadui wao huku nazo zikikiuka haki hizo hizo.

Haki za binadamu zinahusiana na sheria, wanasiasa hutunga sheria, na wanasheria wanaweza kupigania haki za binadamu kupitia mahakama. Na ndiyo, mara nyingine neno hili hutumiwa vibaya kwa malengo ya kisiasa. Lakini haki za binadamu ni zaidi ya hayo!

HAKI ZA BINADAMU NA SISI

Kama tulivyoona, haki za binadamu zinahusiana na mahitaji tunayokuwa nayo katika maisha yetu ya kila siku. Zinahusu kile kinachotokea katika shule zetu, mashamba yetu, maeneo yetu ya kazi, nyumba zetu na majirani zetu. Zinahusu jinsi tunavyopaswa kutendeana na kutendewa. Zinahusu kutulinda dhidi ya unyanyasaji kutoka kwa wale walio na mamlaka juu ya maisha yetu – kama vile wamiliki wa nyumba, waajiri, walimu au hata wanafamilia. Na bila shaka, zinahusiana na mamlaka kama vile polisi, mahakama, jeshi na serikali.

Tunaweza kusema kwa ufupi kwamba haki za binadamu zinahusu aina ya jamii tunayotaka kuishi ndani yake na jamii tunayotaka kuijenga.

Ikiwa haki za binadamu zinapaswa kuwa uhalisia katika jamii zetu, basi kila mmoja wetu ana jukumu la kuchangia hilo. Ukiukwaji mwingi wa haki za binadamu hutokea kwa sababu watu wa kawaida hawaheshimu haki za wengine – kwa mfano, tunapowatendea baadhi ya watu kana kwamba hawana usawa na sisi. Zaidi ya hayo, serikali, wafanyabiashara na watu binafsi wanaendelea kukiuka haki za binadamu kwa sababu watu hawasimamii haki za wenzao wala hawajitahidi kubadili hali hiyo. Mara nyingi, tunabaki kimya.



Sisi si serikali – hatujatia saini mikataba ya kimataifa ya haki za binadamu. Hatuna wajibu wa kisheria wa kuhakikisha haki za binadamu zinafuatwa. Lakini sisi ni wanadamu wenye akili na dhamiri, na tuna wajibu wa kimaadili kwa kila mmoja wetu. Kama Tamko la Ulimwengu la Haki za Binadamu linavyosema:

> "Watu wote huzaliwa wakiwa huru na sawa katika hadhi na haki. Wamepewa akili na dhamiri na wanapaswa kutendeana kwa moyo wa undugu."
>
> "... kila mtu na kila taasisi katika jamii [...] inapaswa kujitahidi, kwa njia ya elimu na mafunzo, kukuza heshima kwa haki hizi na uhuru huu."

Kila mara tunapokuwa na uwezo wa kufanya jambo jema au baya kwa maisha ya watu wengine, tunakuwa na wajibu wa kimaadili wa kuzingatia haki za binadamu. Hatutaweza kufanya kila kitu – mara nyingine ni vigumu hata kufikiria la kufanya – lakini tunapoona ukosefu wa haki ukitendeka, na TUNAWEZA kufanya jambo kusaidia, basi huenda tunalo jukumu la kimaadili la kujaribu.

Kufanya jambo inaweza kuwa rahisi tu kama vile kuwa jirani mwema.

HADITHI ZA WANAMABADILIKO

Shafaq Hassan ni mwanamke Mwislamu kutoka London Kusini, Uingereza. Katika miaka ya hivi karibuni, kumekuwa na ongezeko kubwa la uhalifu wa chuki nchini Uingereza. Waislamu, hasa wanawake Waislamu wanaovaa hijabu kama Shafaq, mara nyingi hulengwa – iwe mtandaoni au mitaani. Katika mazingira haya, vitendo vya urafiki na ukarimu kati ya watu wa dini tofauti vinaweza kuwa na maana kubwa sana.

Shafaq anasema kuwa imani yake kwa ubinadamu ilirejeshwa pale ambapo jirani yake asiye Mwislamu alimpa yeye na mwanawe Ayaan, mwenye umri wa miaka 14, zawadi kwa ajili ya kusherehekea Sikukuu ya Eid.

Shafaq aliweka picha ya zawadi hizo kwenye Twitter, akisema:

> "Jirani yetu asiye Mwislamu alitushangaza kabisa kwa kutuletea tende kutoka Algeria na mswala wa maombi kwa ajili ya mwanangu wa miaka 14, ambaye alikuwa amefunga mwezi mzima. Tumekuwa majirani kwa zaidi ya miaka 20, lakini hakika alinistajabisha kwa zawadi za Eid."
>
> "Sikutambua kwamba alikuwa ameona Ayaan akifunga. Mwanangu alihisi upekee fulani. Ni majirani wa kupendeza; wanapenda sana biriani ya mama yangu, kwa hivyo huwa tunawapelekea bakuli kila mara. Sisi ni jamii yenye watu wa tamaduni mbalimbali, na ni jambo la kufurahisha kuona jinsi jirani yetu alivyokuwa na moyo wa upendo na alivyomhimiza Ayaan kuhusu imani yake ya kidini."



Zaliha na Magdalena nao wanajitahidi kuleta mabadiliko katika mazingira tofauti kabisa. Zaliha ni bibi mwenye imani thabiti ya Kiislamu kutoka kisiwa cha Pemba, Zanzibar, ambako anafundisha katika madrasa ya jamii yao.

Zaliha anasema,

> “Nina hofu sana kuhusu hali ya vurugu katika jamii zetu. Vijana wetu hawana imani na viongozi wetu wa kisiasa, na hawana fursa za maisha.

Anaendelea kusema:

> "Wakazi wengi kutoka bara wanaokuja hapa kufanya kazi katika sekta ya utalii ni Wakristo. Waislamu wengi ninaowajua wanawalaumu Wakristo kwa kuchukua nafasi zao za kazi. Nimepitia vipindi vingi vya misukosuko ya kisiasa na mvutano wa kidini. Nimeona makanisa yakichomwa moto, vipeperushi vyenye maneno ya chuki vikisambazwa, na Wakristo wakinyanyaswa njiani wakielekea kanisani. Naona vijana wetu wakizidi kuwa na misimamo mikali, jambo ambalo linanitia hofu. Ndiyo maana niliamua kujiunga na Kamati ya Wanawake ya dini mbalimbali."

> "Nataka kukusaidia kuzuia ghasia za kidini kwenye kisiwa chetu. Katika madrasa, ninawafundisha watoto kwamba uvumilivu na upendo ni sehemu ya msingi wa dini yetu. Mustakabali upo mikononi mwa watoto wetu, na ni jukumu letu kuwaonyesha njia."

Magdalena, Mkristo kutoka bara aliyehamia Zanzibar, pia anajihusisha na kazi za maelewano ya kidini. Amekumbana na ubaguzi kutokana na mavazi yake na dini yake, lakini amejizatiti kuleta mshikamano kati ya Wakristo na Waislamu. Alijiunga na Baraza la Wanawake wa Mkoa wa Ungoya, linaloingia katika jamii kujadili changamoto za uhusiano wa kidini na haki za wanawake.

> “Nilijiunga na kamati ili kujifunza zaidi kuhusu Uislamu na kuelewa jinsi Waislamu wanavyoishi,” anaeleza. “Sisi sote ni wanawake, na sote

tunakumbana na ubaguzi kwa sababu hiyo – lazima tusimame pamoja na kuungana kusaidiana."

Kuna watu wengi kama jirani wa Shafaq, kama Zaliha na Magdalena. Watu wa kawaida kama sisi, ambao kwa njia zao ndogo wanajitahidi kuhakikisha kwamba haki za binadamu zinakuwa uhalisia katika jamii zao – wanamabadiliko wa jamii!

Haijalishi sisi ni nani, kila mmoja wetu anaweza kufanya jambo ili haki za binadamu zitimie!

Vyanzo
Faith Matters www.faith-matters.org
https://www.faith-matters.org/family-surprised-by-presents-from-non-muslim-neighbour-to-celebrate-eid/

Zanzibar Inter-faith Centre (ZANZIC)
https://www.facebook.com/ZanzicMeansPeace/
https://english.danmission.dk/project/zanzibar-peacebuilding-through-interfaith-dialogue/

KIPINDI CHA 2

Utangulizi kuhusu uhuru wa mawazo, dhamiri, dini na imani

Muhtasari wa kipindi

Kwa urahisi, uhuru wa mawazo, dhamiri, dini na imani mara nyingi hufupishwa kama Uhuru wa Dini au Imani. Katika mwongozo huu, tutatumia jina hili na kifupi hiki mara kwa mara – lakini tusisahau kuwa Mawazo na dhamiri pia zinalindwa!

Haki ya binadamu ya kuwa na uhuru wa fikra, dhamiri, dini au imani ni suala lenye utata karibu kila mahali. Watu wengi huona imani zao na mawazo yao kuhusu jinsi watu wanavyopaswa kufikiri na kuishi kuwa ndio ya kawaida, sahihi na ya kweli. Bila uhusiano mzuri wa kibinafsi na watu wenye imani na mawazo tofauti, ni rahisi kuwaona wengine kama watu duni kwa namna fulani, au kama tishio kwa maadili na utamaduni wetu, au hata kwa umoja na usalama wa taifa. Hali hii inaweza kutokea katika jamii zenye dini ya kina na pia katika jamii zilizo za kidunia zaidi.

Kama ilivyo kwa vipengele vingine vya utamaduni wa binadamu, dini na imani vinaweza kuwa na athari chanya na hasi. Wakati mwingine, imani, desturi, viongozi na taasisi zinazohusiana nazo zinaweza kusababisha changamoto kubwa katika jamii. Hata hivyo, mara nyingi dini na imani hujitokeza kwa namna inayowawezesha waumini na kunufaisha jamii kwa ujumla.

Kwa hiyo, haki za kimataifa za binadamu zinasemaje kuhusu fikra, dhamiri, dini na imani? Tunazo haki gani, na ni lini serikali inaruhusiwa kuweka mipaka katika utekelezaji wa dini au imani?

Kipindi hiki kinatambulisha haki ya Uhuru wa Dini au Imani na kuchunguza iwapo, lini na vipi mamlaka zinaruhusiwa kuidhibiti. Pia kinawapa washiriki fursa ya kujifunza kuhusu haki hii na kutafakari jinsi.

Malengo ya mafunzo

Kipindi hiki kinazingatia kukuza uelewa wa washiriki na kuthamini thamani ya haki ya binadamu ya uhuru wa mawazo, dhamiri, dini na imani.

Kufikia mwisho wa kipindi, washiriki wataweza:

- kueleza kiini cha Uhuru wa Dini au Imani: haki ya kuwa na, kuchagua/kubadili na kutekeleza mafundisho ya dini au imani bila ubaguzi, kulazimishwa au kufanyiwa vurugu.
- kueleza jinsi Uhuru wa Dini au Imani inavyohusika na maisha yao ya kila siku.
- kueleza kwa njia ya msingi kuhusu mipaka ya haki hii, yaani Uhuru wa Dini au Imani haiwezi kutumiwa kama kisingizio cha kuwadhuru watu wengine.

Yaliyomo katika kipindi na muda

Zoezi la ufunguzi: Eleza kila kitu! Linawakumbusha washiriki kile walichojifunza katika kipindi kilichopita.	Dakika 10
Zoezi la hadithi na mjadala: Hapo zamani za kale Hadithi hii inawasaidia washiriki kutafakari ikiwa wanathamini mambo ambayo uhuru wa dini au imani inashughulikia.	Dakika 45
Uwasilishaji: Utangulizi kuhusu uhuru wa dini au imani Uwasilishaji muhimu wa kozi unaoeleza kile ambacho uhuru wa dini au imani inashughulikia na wakati haki hii inaweza kuwekewa mipaka.	Dakika 15
Mjadala wa pamoja: Uhuru wa dini au imani Mjadala kuhusu yaliyomo katika uwasilishaji uliotangulia.	Dakika 10
Zoezi la pamoja: Uhuru wa dini au imani katika maisha yangu ya kila siku Linawasaidia washiriki kutambua jinsi wanavyotumia haki yao ya uhuru wa dini au imani katika maisha ya kila siku.	Dakika 35
Maoni ya kuhitimisha na hadithi ya wanamabadiliko Hadithi zimejumuishwa katika kozi nzima ili kuwahamasisha washiriki.	Dakika 5
JUMLA YA MUDA	**Saa 2**

Jiandae

Tayari unawajua washiriki wako! Tumia mwongozo uliopo ukurasa wa 15, Jinsi ya kuandaa kila kipindi, na urekebishe vipengele vya kipindi kulingana na mahitaji yao.

NYENZO ZA KIPINDI HIKI

Tayari unawajua washiriki wako! Tumia mwongozo uliopo ukurasa wa 16, Jinsi ya kuandaa kila kipindi, na urekebishe vipengele vya kipindi kulingana na mahitaji yao

- Mpira laini.
- Chungu cha supu na kadi za mahitaji ya binadamu zilizotumika katika kipindi kilichopita.
- Vitini au karatasi za bango kitita zenye maswali ya mjadala wa kikundi kwa zoezi 'Hapo zamani za kale'.
- Vitini au karatasi za bango kitita zenye maswali ya majadiliano ya kikundi kwa zoezi 'Uhuru wa dini au imani katika maisha yangu ya kila siku'.
- Iwapo HUTEGEMEI kutumia slaidi/filamu, unaweza kuandaa:
  - Hapo zamani za kale: Chapisho la mabango yanayoonyesha hadithi.
  - Karatasi kubwa ya mawasilisho yenye maudhui muhimu kutoka kwenye slaidi za wasilisho.
  - FORB katika maisha yangu ya kila siku: Chapisho la slaidi 47-59 za wasilisho la kipindi.

NYENZO ANDAMIZI
za kipindi hiki zinaweza kupatikana hapa.

CHAGUO LA ZIADA – JENGA KUJIAMINI

Kama sehemu ya maandalizi yako, kwa nini usitazame filamu hizi fupi ili kujifunza zaidi kuhusu uhuru wa dini au imani? Hii itakusaidia ujiamini na uwezo wa kujibu maswali. Kuna filamu nane kwenye orodha hii ya kutazamwa, kila moja ikiwa na urefu wa takribani dakika 5-10. Ikiwa huna muda wa kuzitazama zote, zingatia filamu namba 2 (haki ya kuwa na au kuchagua imani), 3 (haki ya kuabudu), na filamu namba 8, ambayo ni ndefu kidogo, inayozungumzia mipaka ya haki hii.

FILAMU

ANDAA UKUMBI

Kwa kipindi hiki, ni vyema kuanza na viti vikiwa katika nusu mduara vikielekea mbele, huku sehemu kubwa ya katikati ikiwa wazi ili kuruhusu harakati huru za washiriki. Ukumbi mkubwa usio na meza utakuwa bora zaidi kwa mjadala na shughuli mbalimbali!

'Hapo zamani za kale'

"Zoezi la 'Hapo zamani za kale' lilichochea mijadala ya kina. Lilifungua milango mingi ya fikra kwa washiriki. Walianza kutafakari kuhusu jamii zao – kutoka kwa miundo ya kijinsia hadi iwapo ni sawa kuvunja taratibu zilizopo."

HAMMAM HADDAD, MWEZESHAJI, JORDAN

Mpango wa kina wa kipindi

1. Zoezi la ufunguzi: Eleza kila kitu! Dakika 10

ZOEZI LA PAMOJA

MAELEZO

Washiriki wanatupiana mpira, kila mmoja akisema jambo analokumbuka kutoka kwenye kipindi kilichopita kabla ya kutupa mpira kwa mshiriki mwingine.

LENGO

Zoezi hili linaanzisha kipindi kwa njia ya kufurahisha na shirikishi. Lengo lake ni kusaidia kundi kukumbuka walichojifunza, walivyohisi, na walivyotafakari katika kipindi kilichopita, huku wakishirikishana kumbukumbu hizo. Pia, linawasaidia washiriki wapya kupata mtazamo wa yale yaliyojadiliwa awali.

NYENZO

- Mpira laini.
- Chungu cha supu kilichojaa kadi za ‘mahitaji ya binadamu’ (zilizotumika katika kipindi kilichopita).

JINSI YA KUANZA ZOEZI

Weka chungu cha supu kilicho na kadi za mahitaji ya binadamu katikati ya duara la washiriki. Hakikisha kadi tatu zinazohusiana na uhuru wa dini au imani ziko juu ili ziwe rahisi kufikiwa mwisho wa zoezi.

Karibisha kila mtu na eleza kuwa kipindi kitaanza kwa kuangalia haraka yaliyofanyika katika kipindi kilichopita. Waombe washiriki wasimame katika duara linalozunguka chungu cha supu, wakiwa na nafasi ya kutosha kati yao.

Eleza kuwa watajitupia mpira kwa mfuatano wa kubahatisha. Yeyote anayepokea mpira anapaswa kusema sentensi moja kuhusu jambo analokumbuka kutoka kwenye kipindi kilichopita—iwe ni hadithi, somo alilojifunza, au hisia/takwimu aliyopata. Baada ya kushiriki, anapaswa kutupa mpira kwa mshiriki mwingine kwa nasibu, kuhakikisha kila mtu anapata nafasi ya kuzungumza. Yeyote ambaye hakuwepo kipindi kilichopita, anapopokea mpira, anapaswa kusema ‘Eleza kila kitu’ kabla ya kutupa mpira kwa mshiriki mwingine.

JINSI YA KUENDESHA ZOEZI

Anza mwenyewe kwa kushiriki jambo moja unalokumbuka kutoka kwenye kipindi kilichopita kisha mtupie mpira mshiriki mwingine. Toa maneno ya kuhamasisha kama ‘asante’ na ‘vizuri sana’ kwa michango ya washiriki! Endeleza zoezi hadi kila mtu awe amepokea mpira angalau mara moja.

JINSI YA KUHITIMISHA ZOEZI

Pongeza kundi kwa jinsi wanavyokumbuka mambo mengi na kisha, kwa kifupi, ongezea hoja zozote muhimu ambazo huenda walikosa. Kisha, chukua kadi tatu kutoka kwenye chungu cha supu zinazohusiana na uhuru wa dini au imani. Zionyeshe kwa washiriki kisha uwaeleze kuwa kipindi cha leo kitachunguza haki ya uhuru wa mawazo, dhamiri, dini, na imani.

2. Zoezi la hadithi na mjadala: Hapo zamani za kale   Dakika 45

MAELEZO
Zoezi hili linahusiana na hadithi 'Nyimbo za Filimbi na Ngoma'. Lina sehemu nne: usimuliaji wa hadithi – mjadala wa pamoja – mjadala wa vikundi – mrejesho/hitimisho.

LENGO
Zoezi hili linanuia kusaidia kikundi kutafakari iwapo wanathamini mambo ambayo FORB inalinda, na ikiwa/kama mambo hayo yanathaminiwa katika tamaduni na desturi zao. Hadithi hii inaangazia maneno saba muhimu yanayohusiana na Uhuru wa Dini au Imani: fikiri, amini, kuwa sehemu ya, tenda, hoji, badili, na kataa.

HADITHI

NYENZO

- Nakala ya hadithi (angalia ukurasa wa 56).
- Slaidi 3-23 za PowerPoint ya kipindi inayoonyesha hadithi AU nakala zilizochapishwa za mabango yenye picha hizo hizo. (Inawezekana kufanya zoezi hili bila hizi ikiwa ni lazima.)
- Karatasi ya maswali ya kazi ya kikundi 'Hapo zamani za kale' (moja kwa kila washiriki 3-4) AU karatasi ya bango-kitita iliyoandaliwa mapema yenye maswali ya kazi ya kikundi.

Pata **HADITHI, MABANGO NA VIPEPERUSHI** hapa.

MAANDALIZI YA AWALI
Fanya mazoezi ya kusoma hadithi kwa sauti au kuielezea kwa maneno yako mwenyewe, ili uweze kuwa msimulizi wa hadithi anayevutia na uwe na uhakika kuhusu slaidi ipi ya PowerPoint au bango lipi la kuonyesha wakati gani. Ikiwa unatumia mabango, fikiria kuyabandika kwa mpangilio kwenye ukuta mapema. Hii itafanya iwe rahisi kuonyesha bango sahihi wakati unaofaa.

JINSI YA KUENDESHA ZOEZI DAKIKA 35

- **USIMULIAJI WA HADITHI** (DAKIKA 15)
  Eleza kwamba utasoma hadithi ambayo itajadiliwa kwa pamoja na katika vikundi vidogo.
  Simulia hadithi na uonyeshe slaidi za wasilisho/mabango. Jaribu kusoma kwa hisia nyingi!

- **MJADALA WA HARAKA WA PAMOJA** (DAKIKA 5)
  Waombe washiriki kuinua mikono kujibu maswali yafuatayo – pokea jibu moja au mawili kwa kila swali.
  – Unadhani ujumbe au mafunzo ya hadithi ni yapi?
  – Je, kulikuwa na jambo lolote ulilothamini kuhusu tabia za wahusika?

KIDOKEZO! Kuwa makini na muda ili kuhakikisha vikundi vidogo vinapata muda wa mjadala.

(Ikiwa watu wanapata ugumu kuelewa umuhimu wa ngoma na filimbi, eleza kuwa zinawakilisha mfumo wa imani na desturi za kidini za wanakijiji.)

- **MJADALA KATIKA KUNDI DOGO** (DAKIKA 15)
  Gawanya washiriki katika vikundi vya watu 3-4, ukitoa nakala ya maswali ya kazi ya kikundi kwa kila kikundi.
  Onyesha slaidi ya PowerPoint namba 24 iliyo na maneno saba muhimu, au tumia karatasi kubwa yenye orodha ya maneno haya. Eleza kuwa maneno haya yote yanahusiana na hadithi kwa namna fulani. (Maneno muhimu: Fikiri, Amini, Kuwa Sehemu ya, Tenda, Hoji, Badili.)

- Waulize wanakundi kujadili maswali haya:
  - Maneno fikiria, amini, kuwa sehemu ya, tenda, hoji, badili na kataa yanahusianaje na yaliyotokea katika hadithi? Yanahusianaje na mambo unayopenda au usiyopenda kuhusu wahusika?
  - Je, unaweza kufikiria hadithi kutoka katika utamaduni wako au imani yako zinazozungumzia kwa njia chanya kuhusu watu wanaofikiria, kuamini, kuwa sehemu ya, kutenda, kuhoji, kubadili au kukataa?
  - Jamii inanufaika au inatishiwa watu wakiruhusiwa kufanya mambo haya? Au ni mambo yote mawili?
  - Je, mabadiliko chanya yanaweza kutokea bila watu wanaofikiria, kuamini, kuwa sehemu ya, kutenda, kuhoji, kubadili au kukataa?

JINSI YA KUHITIMISHA ZOEZI DAKIKA 10
Omba kila kikundi kushiriki jambo moja walilopata kuwa la kuvutia, muhimu au gumu katika mjadala wao.

Hitimisha kwa kusema jambo lifuatalo:

- Tumekuwa tukitafakari hadithi hii kama njia ya kuanza kuchunguza maadili na haki zinazohusiana na haki ya binadamu ya uhuru wa dini au imani.

- Maadili na haki hizi si rahisi wala si jambo lisilo na utata. Huenda zikatusababisha wasiwasi. Kwa mfano, unaweza kujiuliza:
  - Ikiwa watu wako huru kufikiri kwa uhuru na kuchagua jinsi wanavyoishi maisha yao, je, si tamaduni, desturi na imani zetu zitakuwa hatarini?
  - Tuna hakikisho gani kwamba watu watatumia uhuru huu kwa njia nzuri? Wapo watu wenye mawazo au nia mbaya. Sio kila mtu ni kama Ziana aliyekuwa na nia njema kwa rafiki zake. Wakati mwingine watu hutumia imani zao kuhalalisha vitendo vinavyowaumiza wengine – kama vile mwenye duka la chai aliyemnyanyasa Ono na kupanga kundi la watu kubomoa mabango ya "karibu wote".

- Haya ni maswali muhimu ambayo tutaendelea kuchunguza! Lakini, mabadiliko chanya hayawezi kutokea ikiwa watu hawaruhusiwi kufikiri, kuamini na kuhoji mambo wanayoyaona kuwa mabaya – kama vile ubaguzi sokoni.

- Kwa hivyo, ni haki gani watu wanapaswa kuwa nazo na ni lini serikali inapaswa kuwa na uwezo wa kuzuia haki hizo? Sasa tutajifunza kuhusu sheria za kimataifa za haki za binadamu kuhusu hili.

3. Uwasilishaji: Utangulizi kuhusu uhuru wa dini au imani Dakika 15

WASILISHO

MAELEZO NA LENGO
Uwasilishaji huu unaleta utangulizi wa haki ya uhuru wa dini au imani na wakati inaweza kuzuiliwa. Ni sehemu muhimu ya maarifa katika kozi hii.

NYENZO

- Mwongozo wa uwasilishaji unaweza kupatikana katika ukurasa wa 60 wa mwogozo huu.
- Nakala hiyo inalingana na slaidi 25-46 za wasilisho la kipindi na imejumuishwa katika maelezo ya spika kwa slaidi hizi.
- Toleo la mwongozo huu linapatikana katika mfumo wa kompyuta la Word ambalo linaweza kuhaririwa.

MAANDALIZI YA AWALI

Jitayarishe kulingana na mwongozo uliotolewa katika ukurasa wa 15, "Jinsi ya kuandaa kila kipindi". Soma na rekebisha maandishi na slaidi za wasilisho (au andaa karatasi la bango kitita kwa ajili ya hoja kuu zilizo kwenye slaidi) na fanya mazoezi ya kutoa uwasilishaji huu pamoja na slaidi/karatasi za maandishi.

KIDOKEZO! Waombe watu wahifadhi maswali/maoni yao hadi mwisho wa wasilisho lako.

ZINGATIA

Unaweza kutaka kuongeza dakika chache kwenye uwasilishaji huu – kwa kuongeza taarifa kuhusu sheria muhimu zinazohusiana na FORB katika nchi yako na jinsi zinavyohusiana na viwango vya kimataifa. Ushauri na viungo vya kupata taarifa hizi vinapatikana kwenye kurasa za 153-154 za mwongozo wa wakufunzi. Usiongee kwa muda mrefu sana kwani watu hawawezi kuzingatia kwa muda mrefu! Tumia mchezo wa kuhamasisha (energiser) baada ya uwasilishaji ikiwa ni lazima. Punguza muda wa shughuli nyingine ili kuruhusu hili (kwa mfano, kata zoezi la ufunguzi) au fanya kipindi kiwe cha muda mrefu zaidi.

4. Mjadala wa pamoja: Uhuru wa Dini au Imani Dakika 10

MJADALA WA PAMOJA

MAELEZO NA LENGO

Mjadala kuhusu uwasilishaji uliopita ili kuwawezesha washiriki kuchakata kile walichojifunza.

JINSI YA KUENDESHA MJADALA

Waombe washiriki kutoa maoni na maswali yao kuhusu mada hii, kisha waulize maswali yafuatayo:

- Ni haki gani kati ya zile zilizoelezwa unazoziona kuwa muhimu kwako?
- Je, kulikuwa na jambo lolote ulilopata kuwa gumu kukubali au lililokuchanganya?

KIDOKEZO! Tazama mwongozo wa kukusaidia namna ya kujibu maswali tata kuhusu uhuru wa dini au Imani katika ukurasa wa 21-28.

Baada ya dakika 10, funga mjadala wa pamoja. Eleza kuwa sasa kikundi kitaendelea kujadili na kuchunguza masuala haya kwa njia ya zoezi.

KUMBUKA: Wewe ni mwezeshaji, si mtaalamu! Ikiwa washiriki watauliza swali ambalo unajua jibu lake, jibu, lakini usijisikie kuwa unashinikizwa kujua majibu yote! Eleza kuwa huu ni mchakato wa uchunguzi wa pamoja, na jukumu lako ni kuwezesha mazungumzo, si kuwa mtaalamu.

5. Zeozi la pamoja: Uhuru wa Dini au Imani katika siku yangu
Dakika 30

ZOEZI LA PAMOJA

MAELEZO

Zoezi la kufikiri-kuwa pamoja-kushirikishana ambapo watu wanatafakari namna wanavyofikiri, amini, kuwa sehemu ya, kutenda, kubadili, kuhoji na kukataa katika maisha yao ya kila siku.

LENGO

Lengo la zoezi hili ni kusaidia watu kutambua kwamba tunatumia haki yetu ya uhuru wa mawazo, dhamiri, dini na imani kila siku. Hii inaonyesha kuwa haki hii ni muhimu kwetu kwa vitendo, si kwa nadharia tu.

NYENZO NA MAANDALIZI YA AWALI

- Slaidi za 48-60 za PowerPoint ya kipindi AU nakala za slaidi hizi, zilizobandikwa ukutani kabla ya kipindi.
- Nakala moja ya maswali ya kazi ya kikundi kwa kila washiriki 3-4 AU karatasi iliyoandaliwa mapema yenye maswali ya kazi ya kikundi.

JINSI YA KUANZA ZOEZI DAKIKA 4

Waombe washiriki wajipange wawili wawili. Eleza yafuatayo:

"Sasa tutatafakari maana ya uhuru wa dini au imani katika maisha yetu ya kila siku. Kwanza, kila mtu atafikiria kimyakimya, kisha tutashirikiana mawazo yetu wawili wawili, kabla ya kuja pamoja tena kwa mjadala wa pamoja."

Soma maandishi yafuatayo (au eleza jambo kama hili). Pitia slaidi za wasilisho 47-59 au uonyeshe nakala za slidi hizi huku unasoma:

"Fikiria siku yako ya kawaida. Ni lini na vipi unaonyesha mawazo yako, imani zako, maswali yako na utambulisho wako wa kidini au usio wa kidini? Inaweza kuwa:

- *Katika vyakula unavyokula au unavyokataa kula,*
- *Katika mavazi unayovaa au usiyovaa,*
- *Katika sala, matambiko au sherehe za nyakati muhimu za maisha,*
- *Katika mambo unayosoma,*
- *Katika mazungumzo unayofanya na familia, marafiki au wenzako na jinsi unavyowalea watoto wako,*
- *Katika huduma unayotoa kwa jamii au kushiriki katika masuala yanayokuhusu katika jamii."*

JINSI YA KUENDESHA ZOEZI DAKIKA 30

FIKIRI (DAKIKA 5)

Waombe washiriki wachukue dakika tano kufikiria kimyakimya kuhusu siku yao ya kawaida. Ni lini na vipi wanavyoonyesha mawazo, imani, maswali na utambulisho wao wa kidini au usio wa kidini katika maisha yao ya kila siku?

KUWA PAMOJA (DAKIKA 10)

Waombe washiriki washirikiane wawili wawili na wajadili maswali yafuatayo kulingana na yale wanayohisi vizuri kuyajadili:

- Simulia hadithi ya wakati ambapo ulitoa mawazo yako au ulihoji jambo fulani. Nini kilitokea, na ulijisikiaje?
- Simulia hadithi ya wakati ambapo hukuweza kutoa mawazo yako, kuhoji jambo ulilohisi ni makosa, au kuwa wazi kuhusu utambulisho wako. Ilikuwaje kihisia?
- Je, ni muhimu kwako kuwa na uwezo wa kueleza mawazo yako na utambulisho wako katika maisha yako ya kila siku? Je, ni muhimu kuwa na uhuru wa kuhoji mawazo au desturi unazoamini kuwa si sahihi?
- Ungejisikiaje ikiwa ungelazimishwa kuishi kwa mujibu wa mawazo na imani za watu wengine badala ya imani yako mwenyewe?

SHIRIKISHA (DAKIKA 15)

Waombe washiriki warudi kwenye mjadala wa pamoja. Eleza kuwa maswali tuliyojadili wawili wawili yanahusiana na maswali haya mapana:

- Je, haki zinazolindwa na uhuru wa mawazo, dhamiri, dini na imani ni muhimu kwetu?
- Tunajisikiaje tunaponyimwa haki hizi?

KIDOKEZO! Uwe tayari kutoa tafakari zako kuhusu FORB katika maisha yako binafsi ikiwa mazungumzo yatachelewa kuanza.

Waulize ikiwa kuna yeyote anayetaka kushirikisha mawazo, hisia au uzoefu wao kutokana na mjadala wao wawili wawili. Kushiriki kunapaswa kuwa kwa hiari! Baada ya muda, waulize wanakundi ikiwa hali yetu ya kibinadamu inamaanisha kuwa kila mtu ana mahitaji sawa kuhusu haki za kufikiri – kuamini – kuwa sehemu ya – kutenda – kuhoji – kubadili na kukataa? Je, haki hizi ni muhimu kwa watu wa dini au imani yoyote?

JINSI YA KUHITIMISHA ZOEZI DAKIKA 1

Hitimisha zoezi kwa kuwashukuru wote kwa mawazo na ushiriki wao katika mjadala.

6. Hitimisho na hadithi ya wanamabadiliko Dakika 5

GUMZO FUPI

MAELEZO

Mazungumzo haya mafupi yanahitimisha kipindi, yakihusianisha na mabadiliko kupitia hadithi ya mtu wa kawaida aliyesimama kutetea haki yake ya Uhuru wa dini au imani. Pia inawafahamisha washiriki kile cha kutarajia katika vipindi vijavyo.

NINI CHA KUSEMA

Onyesha hoja zifuatazo. Tumia slaidi 61-63 za wasilisho la kipindi ikiwa inawezekana ili kuonyesha hadithi ya Peter.

- Leo tumechunguza haki ya uhuru wa dini au imani na tumejifunza kuhusu haki tunazopaswa kuwa nazo kulingana na sheria za kimataifa.
- Hii ni haki tata ya kibinadamu, na kunaweza kuwa na mambo ambayo hatuelewi au hatukubaliani nayo. Lakini bila shaka kuna mambo tunayoyelewa na tunayokubaliana nayo. Hapo ndipo wanamabadiliko wanapoanzia!
- Watu wa kawaida kama sisi wanaweza kuleta mabadiliko na Suluhu kwa matatizo ya jamii yetu.
- Soma hadithi ya Peter kwenye ukurasa wa 64 (pia inapatikana katika nyenzo zinazoweza kupakuliwa kwa ajili ya kipindi).
- Katika kipindi chetu kijacho, tutachunguza masuala ya utambulisho, upendeleo na unyanyasaji. Pia, katika vipindi vijavyo, tutajifunza zaidi kuhusu ukiukwaji wa haki ya uhuru wa dini au imani na njia tunazoweza kutumia kuleta mabadiliko.

'Nyimbo za filimbi na ngoma'

> “Washiriki walipenda sana hadithi – ilikuwa sehemu bora zaidi ya kipindi. Wahusika, michoro, matukio – iliwasisimua.”
> **HIDAYA DUDE**, MWEZESHAJI, TANZANIA

Nyimbo za filimbi na ngoma

Zimeandikwa na Katherine Cash na Sidsel-Marie Winther Prag
Michoro na Toby NewsomeNewsome

Hadithi hii ndiyo msingi wa zoezi la 'Hapo zamani za kale' na imeonyeshwa katika slaidi za 3-23 za kipindi cha 2 cha wasilisho.

NYIMBO ZA FILIMBI NA NGOMA

Hapo zamani za kale, kulikuwa na vijiji viwili.

Watu wa kijiji kilichokuwa msituni walijulikana kwa umahiri wao wa kupiga ngoma na kucheza. Mara tu mtoto alipoanza kukaa wima, alipewa ngoma. Kulikuwa na ngoma ndogo zilizosikika kama manyunyu ya mvua tulivu na ngoma kubwa zenye mtikisiko mkali zilizohitaji watu wawili kubeba. Kupiga ngoma kulifuatana na maisha yao – kusherehekea, kuomboleza, na kila jambo kati ya hayo – na waliamini kuwa ngoma zilihifadhi maisha yao katika mwafaka na roho za msitu.

Watu wa kijiji kilichokuwa bondeni hawakuwahi kuelewa wapigaji wa ngoma. Waliona kupiga ngoma kuwa kelele zisizovutia na wakadharau midundo hiyo kwa kuiona kama vurugu ya kawaida. Kila mvulana alipozaliwa katika kijiji hiki, baba yake alimchongea filimbi kwa kutumia kuni au mfupa, na mvulana huyo aliivaa shingoni kwa kamba hadi mwisho wa maisha yake. Ilihitaji miaka mingi kuweza kumudu sauti zao za muziki wa kitamaduni, na heshima kubwa kabisa ilitolewa kwa wanaume walioweza kupuliza filimbi kwa ustadi mkubwa kiasi kwamba Mungu wa mbinguni alivutiwa na kuwapa mvua na jua kwa ajili ya mashamba.

Ingawa wakazi wa Kijiji cha Ngoma walikwenda sokoni kila wiki katika Kijiji cha Filimbi kuuza bidhaa zao, watu wa vijiji hivyo viwili hawakuchangamana. Kupiga ngoma kulikatazwa sokoni. Wauzaji wengi wa Kijiji cha Filimbi walikataa kuwauzia wapiga ngoma, nao wapiga ngoma walikuwa na kinyongo dhidi ya wenyeji wa Kijiji cha Filimbi.

Msichana mmoja mdogo, mtoto wa pekee aitwaye Ziana, aliishi katika Kijiji cha Filimbi. Alipendwa na wote kwa sababu ya udadisi wake na wema wake. Alipofikisha umri wa miaka kumi, baba yake aliugua sana. Siku moja, alimwita na kumwambia, "Binti yangu mpenzi, sitadumu kwa muda mrefu. Chukua filimbi yangu na uivae ili tuwe pamoja daima." Ziana alihisi uchungu mkubwa; haikuwa desturi kwa wasichana kubeba filimbi, lakini baadaye akajiuliza, "Kwa nini nisiruhusiwe kuipiga?" Usiku ule baba yake alipofariki, Ziana alichukua filimbi na kujivika shingoni.

Kadiri Ziana alivyokua, alifanya kazi kwa bidii akimsaidia mama yake kulima mboga za kuuza katika kibanda chao sokoni. Ingawa alikuwa mchapakazi na mwenye upole, mara nyingi watu wa kijiji cha Ziana walimdhihaki kwa sababu ya kuvaa filimbi. Wakati mwingine walijaribu kumshawishi aivue, lakini alikataa. Kila alipopata nafasi, Ziana alitorokea msituni na kupiga filimbi ya baba yake.

Siku moja alipokuwa akicheza filimbi msituni, alisikia sauti hafifu ya ngoma. Akiwa na hamu ya kujua zaidi, alifuata midundo hiyo hadi kwenye uwazi kati ya miti, ambako kijana mmoja alikuwa akipiga ngoma na kuimba, huku dada yake akivuna matunda kutoka kwenye mti. Ziana aliwatambua mara moja – walikuwa ndugu waliitwa Ono na Iris, ambao mara kwa mara aliona sokoni.

Akiwa amejificha nyuma ya miti, Ziana alianza kupuliza filimbi yake kwa kufuata mpigo wa ngoma. Wimbo wa filimbi na midundo ya ngoma vilichanganyika kwa uzuri na kuunda muziki wa kuvutia. Wimbo ulipomalizika, Ziana alijitokeza kwa tahadhari kwenye uwazi huo. Ono na Iris walishangazwa na kumuona msichana na filimbi, lakini wakatabasamu walipotambua kuwa, kama wao, Ziana pia hakuruhusiwa kupiga ala yake katika kijiji cha Filimbi. Iris alimpatia Ziana tunda, na watatu hao wakaanza kuzungumza na kucheza muziki hadi jioni ilipoingia.

Siku iliyofuata ya soko, Ziana aliwaona marafiki zake wapya mbele ya kibanda cha chai. Mmiliki wa kibanda alikuwa akiwafokea kwa hasira, “Tokeni hapa, ninyi wapiga ngoma wachafu!” Ono alikasirika, lakini Iris akamvuta mbali. Mtoto wa mmiliki wa kibanda hicho, ambaye alikuwa akimiminia Ono chai, alionekana mwenye aibu.

Ziana hakuwahi kufikiria kuhusu mabango yaliyoandikwa ‘Hakuna Wapiga Ngoma’ hapo awali. Moyo wake ulilemewa alipotambua kuwa yeye na mama yake hawakuwahi kununua chochote kutoka kwa vibanda vya wapiga ngoma.

Usiku huo, Ziana alizungumza na mama yake na kumuuliza kwa nini hawakuwahi kwenda kwenye vibanda vya wapiga ngoma. Mama yake alijibu, “Ni bora kushikamana na kile unachokifahamu.” Lakini Ziana hakuweza kuelewa na akaendelea kuuliza kwa nini kila mtu asikaribishwe kila mahali, huku akimsimulia mama yake kuhusu matunda matamu ambayo Ono na Iris waliuza katika kibanda chao. Hatimaye, mama yake alikubali kujaribu baadhi ya matunda yao katika siku inayofuata ya soko.

Wakati huohuo, katika nyumba ya mmiliki wa kibanda cha chai, kulizuka ugomvi mkali baada ya mwanawe, Brone, kumhoji baba yake kuhusu jinsi alivyowatendea wapiga ngoma. Mmiliki wa kibanda hicho alikuwa mmoja wa wapulizaji filimbi mashuhuri katika kijiji na mtu mwenye kiburi. Baba yake na babu yake walikuwa wanamuziki hodari, lakini kwake, mwanawe alikuwa fedheha kubwa. Haijalishi Brone alijitahidi kiasi gani, hakuweza hata kumudu sauti ya muziki rahisi kabisa. Baada ya miaka mingi ya mazoezi ya kulazimishwa na maneno makali ya kudhalilisha, Brone alipoteza kabisa mapenzi yake kwa filimbi. Badala yake, alihisi kuvutiwa na midundo ya ngoma iliyo mbali na akaota maisha tofauti.

Kadiri muda ulivyopita, Ziana, Iris, na Ono waliendelea kukutana msituni na kupiga muziki pamoja. Waliota ndoto – ndoto ya wakati ambapo kila mtu atakaribishwa, ambapo ngoma na filimbi zingeweza kupigwa waziwazi, na ambapo wangeweza kucheza muziki wao mzuri sokoni bila hofu.

Kila wiki, Ono na Iris walimtembelea Ziana na mama yake katika kibanda chao cha mboga, na mama yake Ziana alinunua matunda na karanga kutoka kwao. Siku moja, Ono aliona mama yake Ziana akitazama kwa udadisi ngoma aliyobeba kiunoni mwake.

"Hii ni ngoma ya kicheko," Ono alisema. "Sauti yake huleta furaha, na watoto hucheza na kucheka ninapopiga." Mama yake Ziana alivutiwa sana.

Wapiga ngoma wengine walianza kukusanyika, na Ziana pamoja na mama yake wakauliza maswali kuhusu ngoma zao pia. Siku hiyo, mama yake Ziana aliuza mboga zake haraka sana. Wafanyabiashara jirani walikasirika kwa sababu alikuwa amewakaribisha wapiga ngoma kwenye sehemu yao ya soko, lakini mama yake Ziana alisisitiza kuwa ikiwa kila mtu angenunua kutoka kwa kila mmoja, basi wote wangenufaika.

Karibu na kibanda chao, kulikuwa na mzee aliyekuwa akiuza viungo, lakini biashara yake ilikuwa duni. Ono alipendekeza waweke bango lililosema, "Kila mtu anakaribishwa" ili kuvutia wateja zaidi. Akaichora alama hiyo kwa mkono wake, picha ya ngoma na filimbi.

Mauzo ya mzee huyo yaliongezeka, na polepole wafanyabiashara wengine wakashawishika. Bango la "Kila mtu anakaribishwa" likaanza kuonekana kwenye vibanda vya wapiga ngoma na wapulizaji filimbi vilevile. Soko likastawi.

Lakini mambo hayakuwa shwari. Baba yake Brone alihuzunika sana kuona wapiga ngoma wakiingia sehemu yake ya soko. Aliwaona kama tishio kwa desturi za zamani, hivyo akakusanya watu waliokuwa na mawazo sawa naye ili kung'oa mabango na kuwahangaisha wapiga ngoma.

Hofu ikazidi kuongezeka sokoni, na baraza la soko likaanza kuwa na wasiwasi.

Brone alikataa kushiriki njama ya baba yake. Badala yake, yeye na yule mzee muuzaji wa viungo walizungumza na baraza la soko na kuwashawishi waandae tamasha la muziki kwa kila mtu sokoni. Labda baba yake Brone na wengine wangeweza kujifunza kuwakubali wapiga ngoma ikiwa wangesikiliza hadithi zao na nyimbo zao.

Habari kuhusu tamasha hilo zilienea, na watu wakaja kutoka maeneo ya mbali. Siku hiyo, wafanyabiashara waliuza zaidi ya kawaida.

Hatimaye, wakati wa tamasha ukafika. Mzee muuzaji wa viungo alipiga melodi maridadi kwenye filimbi yake ya mbao, huku binti yake akiimba wimbo wa shukrani kwa Mungu wa mbinguni kwa mavuno mazuri. Akasimulia jinsi wimbo huo ulivyokuwa na maana kubwa kwake baada ya miaka ya shida katika ujana wake.

Baba yake Brone alinyanyua nyusi kwa mshangao alipoona tabasamu na nyuso za kuridhika za baadhi ya wapiga ngoma waliokuwa miongoni mwa umati.

Yule mzee alimwalika Ono na Iris jukwaani. Wakawaambia hadhira kuhusu ngoma zao, wakisimulia hekaya za sauti zao za kipekee. Walipiga midundo yenye uchangamfu kumheshimu roho mcheza dansi wa kijito cha msituni, kisha wakapiga nyimbo za radi kwa shukrani kwa roho wa dhoruba aliyelinda miti yao ya matunda. Kwa mara ya kwanza, wanakijiji wa filimbi wakaanza kuelewa maana ya ngoma kwa wapiga ngoma. Lakini baba yake Brone alikunja uso kwa dharau.

Hatimaye, Ziana aliungana na Ono na Iris jukwaani. Alimkumbuka baba yake, akashika filimbi yake kwa ujasiri, akaileta mdomoni, na wakaanza kupiga muziki pamoja. Ukimya mzito ukashuka. Hakukuwa kumewahi kusikika sauti za filimbi na ngoma pamoja, wala msichana hakuwa amewahi kuonekana akipiga filimbi.

Sauti ya mziki wa shukrani kwa jua na mvua kutoka kwa filimbi ya Ziana ilielea angani, ikilingana kikamilifu na midundo ya kijito kinachocheza kutoka kwa ngoma ya Ono.

Wimbo ulipomalizika, umati ulitazamana. Wengine walipiga makofi kwa kusita, huku wengine wakigeuza nyuso zao kwa aibu. Ghafla, baba yake Brone aliripuka kwa hasira. "Msaliti!" alipiga kelele, kisha akaondoka kwa ghadhabu.

Brone alimtazama baba yake kwa huzuni. Akitingisha kichwa, aliondoa filimbi aliyovaa shingoni, akaweka juu ya kibanda cha baba yake, na kuondoka kijijini milele.

Baada ya tamasha, mijadala mingi ilizuka katika vijiji vyote viwili. Je, kila mtu anapaswa kuhudumiwa katika vibanda vyote vya soko? Je, wasichana waruhusiwe kupiga filimbi? Je, filimbi na ngoma zinaweza kuchezwa pamoja?

Baada ya miezi mingi ya mabishano, baraza la soko likatoa uamuzi:

"Watu wote watatendewa vyema sokoni!"

Marufuku ya ngoma iliondolewa, na mabango yote yaliyosema "Hakuna Wapiga Ngoma" yakatolewa. Lakini kuhusu masuala ya kupiga ala za muziki, baraza lilikaa kando. Badala yake, waliamua kwamba kila mtu ataheshimiwa kulingana na imani yake na kuachwa huru kufuata njia yake.

Ilichukua miaka mingi kabla ya wapiga ngoma kuhisi kukaribishwa katika vibanda vyote vya soko. Lakini kila wiki, Ziana, Ono na Iris walionekana pamoja, wakicheza nyimbo za filimbi na ngoma, hadi vidole vyao vilipolegea na nywele zao zikawa nyeupe.

Mwongozo wa uwasilishaji

Utangulizi kuhusu Uhuru wa Mawazo, Dhamiri, Dini na Imani

Nakala hii ya uwasilishaji wa kipindi cha 2 inaonyeshwa kwenye slaidi za 25-46 za PowerPoint ya kipindi.

Zingatia: Uwasilishaji huu unarejelea hadithi "Nyimbo za Filimbi na Ngoma".
Iwapo hutakusudia kutumia hadithi hii na kikundi chako, utahitaji kuhariri nakala hii. Unaweza kuipata hadithi hiyo kwenye ukurasa wa 55 wa mwongozo wa wakufunzi na pia katika nyenzo zinazofuatana nayo

UTANGULIZI

Kwa hiyo, uhuru wa dini au imani unamlinda nani au nini?

Huenda ukadhani jibu la moja kwa moja ni dini na imani. Lakini kwa kweli, uhuru wa dini au imani haulindi dini au imani zenyewe. Haulindi Mungu au vitu vitakatifu. Kama haki nyingine yoyote ya binadamu, unawalinda watu.

Kwa jina lake kamili, uhuru wa mawazo, dhamiri, dini na imani ni haki ya kila binadamu – bila kujali yeye ni nani, anaamini nini, au dini yake ni ipi.

Uhuru wa dini au imani unategemea wazo kwamba binadamu wote wana mahitaji ya msingi:

- Kuruhusiwa kufikiri na kuamua wenyewe kuhusu yaliyo mema na ya kweli
- Kustahili makundi yenye imani, desturi, na utambulisho wa pamoja
- Kuhoji mawazo na desturi, kubadilisha mtazamo wao kuhusu kile wanachoamini, na kukataa kufanya mambo yanayokiuka dhamiri zao.

Kwa hivyo, mtu anapaswa kuwa na uhuru wa Kufikiri, Kuamini, Kuwa sehemu ya, Kutenda, Kuhoji, Kubadili mawazo, na Kukataa.

TUNA HAKI ZIPI?

Kwa hiyo, tuna haki zipi? Hebu tuangalie yaliyoandikwa katika mikataba ya kimataifa. Uhuru wa dini au imani unalindwa na Kifungu cha 18 cha Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa (ICCPR). Huu ni mkataba wa kisheria unaofungamanisha nchi zilizouridhia, na mataifa 173 yamejitolea kuufuata. [*Waambie washiriki ikiwa nchi yako imekubali ICCPR*.]

Sentensi ya kwanza ya Kifungu cha 18 inasema:
"Kila mtu atakuwa na haki ya uhuru wa mawazo, dhamiri na dini."

Kila mtu ana haki ya kufikiri kwa uhuru – kama Ziana katika hadithi, aliyefikiri kuwa alipaswa kuruhusiwa kupiga filimbi hata kama alikuwa msichana.

Tuna haki ya kusikiliza dhamiri zetu – kama Brone, ambaye alikataa kumsaidia baba yake kwa sababu aliamini kuwa matendo ya baba yake hayakuwa sahihi.



Pia, tuna haki ya kushikilia imani za kidini au zisizo za kidini na kuwa na utambulisho wa kidini au wa imani – haki ya **kuamini na kuwa sehemu** ya jamii. Kama wanakijiji wa filimbi na ngoma, wengi wetu tunashikilia imani zetu kwa dhati. Imani zetu na jumuiya tunazoshiriki nazo zinaweza kuwa na maana kubwa kwetu.



Lakini bila kujali jamii tunayoishi au ukweli wa imani zetu, daima kutakuwa na watu ambao, kwa sababu yoyote ile, wanapoteza imani katika imani zao au katika jumuiya zao – kama Brone aliyekataa kupiga filimbi na kuondoka katika jamii yake.



Katika sheria za kimataifa za haki za binadamu, haki ya kuacha na kubadilisha dini au imani inalindwa kwa kiwango sawa na haki ya kuwa na dini au imani.

Haki hizi za kufikiri, kuamini, kuhoji na kubadilisha imani mara nyingi huitwa **uhuru wa ndani**. Zinahusiana na kinachotendeka katika akili na roho zetu, na hivyo kuathiri utambulisho wetu – hisia ya sisi ni nani.

Kwa sababu hii, hizi ni haki zisizoweza kuvunjwa. Kulingana na sheria za kimataifa, hakuna mtu wala serikali inayoruhusiwa kuweka mipaka kwenye haki hizi, kamwe.

Lakini bila shaka, dini na imani ni zaidi ya kile kinachotokea katika akili na roho zetu! Zinahusu matendo yetu – jinsi tunavyoonyesha imani zetu kupitia maneno na vitendo.

Katika hadithi yetu, maisha ya wanakijiji yalijaa matendo yaliyoonyesha imani zao na utambulisho wao! Kuanzia uvaaji wa filimbi hadi upigaji wa ngoma katika maisha yao ya kila siku. Uhuru wa dini au imani unalinda pia haki hizi. Hebu turejee kwenye Mkataba wa Kimataifa tena:



Kifungu cha 18 kinasema:

> "Haki hii itajumuisha... uhuru wa mtu binafsi, au akiwa katika jamii na wengine, hadharani au faraghani, kuonyesha dini au imani yake kwa ibada, kushika desturi, matendo na mafundisho."

Tuna haki ya kuomba kwa faragha na kuonyesha dini au imani yetu kama sehemu ya jamii, kupitia ibada na desturi za pamoja. Na jamii hiyo nayo ina haki – lakini si haki ya kuwatawala wanachama wake, bali haki zinazohusiana na serikali. Kwa mfano, serikali inapaswa kuhakikisha kuwa jumuiya za kidini na za imani zinaweza kupata utambulisho wa kisheria iwapo zinataka, ili ziweze kumiliki akaunti za benki, kuajiri watu na kumiliki majengo.

Kuna njia nyingi tofauti kwa watu binafsi na vikundi kutekeleza dini au imani, na wataalamu wa Umoja wa Mataifa wameelezea mifano mingi ya shughuli zinazolindwa. Kwa mfano, tuna haki zifuatazo:



- Kukusanyika kwa ajili ya ibada, kusherehekea sikukuu za kidini na kuheshimu siku za mapumziko.
- Kuvaa mavazi ya kidini na kufuata taratibu maalum za chakula.
- Kuwa na maeneo ya ibada, makaburi na kuonyesha alama za kidini.
- Kushiriki katika jamii, kwa mfano kwa kuanzisha mashirika ya hisani.
- Kuzungumza kuhusu na kufundisha dini au imani, na pia kufunza au kuteua viongozi wa kidini.

Kwa wakati huu, huenda unawaza, "Vizuri – hizi ni haki ninazotaka kwa jamii yangu!" Au pengine unaanza kuwa na wasiwasi!

KUJITOLEA NA USAWA – USIWADHURU WENGINE!

Vipi kuhusu watu au vikundi vinavyotumia dini au imani yao kueneza chuki au vurugu dhidi ya wengine, kubagua wengine, au kuwanyanyasa na kuwatawala watu ndani ya kundi lao? Je, uhuru wa dini au imani unamaanisha kwamba wanaweza kufanya haya yote – bila kujali athari kwa watu wengine?

Kwa bahati nzuri, sivyo!



Mikataba ya haki za binadamu inatuambia siyo tu haki zetu ni zipi, bali pia mipaka ya haki zetu ni ipi. Kwa maneno mengine – inatuonyesha wajibu wetu tunapotekeleza haki zetu. Tunaweza kusema kwa kifupi kuwa hakuna mtu anayepaswa kutumia haki na uhuru wake kwa namna inayowadhuru wengine.

Hili ni jukumu la kimaadili kwa kila mtu kulingana na mikataba ya haki za binadamu. Na serikali ina jukumu la kisheria la kuheshimu haki za kila mtu na kuwalinda wote dhidi ya madhara. Hebu tuangalie kwa undani zaidi JINSI tunavyopaswa kulindwa dhidi ya madhara.

Kwanza: Hakuna Kulazimishwa!
Kulazimishwa hakuruhusiwi katika masuala ya dini au imani. Kuamini na kuwa sehemu ya dini ni jambo la hiari. Mamlaka, jumuiya za kidini na hata familia HAZIRUHUSIWI kutumia vitisho, vitisho vya adhabu au vurugu ili kumlazimisha mtu yeyote kuamini au kutokuamini, kufuata au kutofuatilia dini, kuwa sehemu ya dini fulani au kutokuwa sehemu ya dini.

Pili: Hakuna Ubaguzi!
Kifungu cha 2 cha Mkataba kimepiga marufuku ubaguzi wa aina yoyote – iwe ni kwa misingi ya dini, rangi, jinsia au lugha, kwa mfano. Mataifa yaliyotia saini mikataba ya haki za binadamu yamekubali kuwatendea watu wote kwa usawa na kufanya kazi kwa bidii ili kumaliza ubaguzi katika jamii – kama vile baraza la soko lilivyofanyaka.



Tatu: Hakuna Kuangamiza Haki!
Kifungu cha 5 kinasema kuwa hakuna serikali, kikundi au mtu anayepaswa kufasiri haki moja ya binadamu kwa namna inayompa ruhusa ya kuvuruga haki nyingine za binadamu.Na Kifungu cha 20 kinapiga marufuku uchochezi wa chuki za kidini kupitia uchochezi wa ubaguzi, uhasama au vurugu.

Haijalishi serikali au mtu binafsi anafikiria dini inamtaka afanye nini, hakuna anayeweza kusema kwamba uhuru wa dini au imani unampa haki ya kukiuka haki

za wengine. Hivyo basi, baba yake Brone hakuwa na haki ya kuwanyanyasa wapigaji ngoma, hata kama alidhani anafanya jambo sahihi.tika hadithi yetu.

Nina uhakika kwamba unaweza kufikiria mifano mingi ambapo dini imetumika kuhalalisha au kuchochea vurugu, au ambapo matendo ya kidini yameleta madhara kwa watu. Pia, unaweza kufikiria nyakati ambapo watu wamezuiwa isivyo haki kutekeleza dini au imani yao kwa amani.

MIPAKA YA UHURU WA DINI AU IMANI

Basi, ni sheria zipi zinahusika? Ni lini serikali inaruhusiwa kuweka mipaka kwa uhuru wa dini au imani? Hebu tuangalie kanuni hizo kwa ufupi.

Kwanza kabisa, haki ya kufikiri na kuamini (uhuru wa ndani) haiwezi kamwe kuwekwa mipaka. Pili, matendo ya kidini au imani yanaweza kuwekwa mipaka – lakini NI PALE TU masharti manne yafuatayo yanapofuatwa:



1. Lazima kuwe na SHERIA inayofafanua kikomo hicho. Kwa maneno mengine, polisi hawawezi kufanya watakavyo bila msingi wa kisheria.
2. Kikomo kinapaswa kuwa SAWA KULINGANA NA SHIDA inayoshughulikiwa. Kwa mfano, ikiwa mfumo wa sauti wa jumuiya ya kidini ni wa sauti kubwa kupita kiasi, wanaweza kuamriwa kuupunguza au kulipa faini. Lakini kuwapiga marufuku kukutana kabisa haitakuwa sawa na tatizo hilo.
3. Kikomo lazima kisiwe CHA UBAGUZI – lazima kitumike kwa kila mtu sawa.
4. Kikomo lazima kiwe CHA LAZIMA kwa ajili ya kulinda moja ya mambo haya: usalama wa umma, utulivu wa jamii, afya ya umma, maadili ya umma, au haki na uhuru wa watu wengine.

Neno lazima ni muhimu sana hapa. Haitoshi kwa serikali au idadi kubwa ya watu kuamini kwamba kikomo fulani kinapendelewa kwa ajili ya kufanikisha malengo haya. Lazima kiwe cha lazima. Kwa maneno mengine, hakuna njia nyingine ya kutatua tatizo hilo bila kuweka kikomo kwa haki hiyo. Kuweka mipaka kwa haki kunapaswa kuwa hatua ya mwisho kabisa. Hata hivyo, wakati mwingine ni jambo lisiloepukika.

Kwa mfano, inaweza kuwa hatari kujaa watu kupita kiasi ndani ya sehemu ya ibada. Kwa hivyo, inaweza kuwa lazima kwa mamlaka kupunguza idadi ya watu wanaoruhusiwa kuingia kwa sababu za usalama wa umma. Pia, vizuizi vya kiafya kuhusu mikusanyiko ya ibada vilikuwa vya kawaida wakati wa janga la virusi vya Korona – wakati mwingine vizuizi hivyo vilikuwa vya lazima, sawa na visivyo vya kibaguzi. Lakini mara nyingine vilikuwa vya kibaguzi na visivyo vya haki.

Marufuku dhidi ya ukeketaji wa wasichana ni mfano wa kikomo kinacholinda haki na uhuru wa wengine – katika hali hii, haki za wasichana. Haijalishi ikiwa jambo hili linachukuliwa kama desturi ya kitamaduni au ya kidini, ukweli ni kwamba linahatarisha afya ya wasichana na haliwezi kuhalalishwa kwa kutumia hoja ya uhuru wa dini au imani.



Kanuni hizi ni muhimu sana. Bila kuzifuata, serikali zinaweza kuweka mipaka kwa kundi lolote au desturi yoyote zisizopenda tu. Mipaka ya haki inapaswa kuwa suluhisho la mwisho, siyo chombo cha serikali cha kudhibiti watu. Katika vipindi vijavyo, tutachunguza kwa kina ukiukwaji wa uhuru wa dini au imani unaotokea sehemu mbalimbali duniani.

Hadithi ya mwanamabadiliko

Hadithi ifuatayo inasomwa kama sehemu ya maoni ya hitimisho ya kipindi cha pili. Inaonyeshwa kwa slaidi 61-63 za washilisho la kipindi hicho.

Hadithi ya Peter, Pakistan

HADITHI

Peter ni kijana aliyesaidia kuleta mabadiliko kwa jamii ya Wakristo katika eneo la Kot Lakhpat, eneo lenye Waislamu wengi katika jiji la Lahore, Pakistan.Kila asubuhi, Peter huanza siku yake kwa kutazama ibada inayowasilishwa na mchungaji kwenye kituo cha luninga cha Kikristo cha eneo hilo. "Sina muda mwingi wa kusoma maandiko au kushiriki katika vikundi vya masomo ya Biblia, lakini kutazama ibada hii ni njia nzuri sana kwangu ya kuanza siku yangu," anasema.

Siku moja, kituo cha luninga cha Kikristo kilikatika hewani. Kwa mara ya kwanza, Peter alidhani ni tatizo la kiufundi. Lakini baada ya wiki moja bila matangazo, yeye na kundi la watazamaji wa kawaida walimfuata mchungaji wa kituo hicho ili kuuliza kilichotokea. Mchungaji aliwaambia kwamba kituo kilikuwa kinafanya kazi vizuri katika maeneo mengine.

Baada ya kuchunguza, waligundua kuwa imam wa msikiti wa eneo hilo aliomba fundi wa nyaya za televisheni kukata matangazo ya kituo hicho kwa sababu mwanazuoni wa Kiislamu wa eneo hilo aliona kuwa matangazo hayo ni uinjilisti wa Kikristo.

"Unaweza kufikiria jinsi tulivyoshangaa. Tunaishi kwa ushirikiano mzuri na majirani zetu Waislamu, na hatujawahi kuwa na matatizo nao," alisema Peter.

Kundi lilijua kwamba hali hiyo ilikuwa nyeti, hivyo walitafuta ushauri na maelezo kutoka kwa shirika la kiekumeni la kitaifa. Kwa kufuata ushauri huo, walikutana kwanza na fundi wa nyaya za televisheni. Fundi huyo hakuwa na tatizo kurejesha matangazo, lakini alisema hawezi kwenda kinyume na imam. Kundi liliamua kwamba lilipaswa kuwa na mazungumzo na mwanazuoni huyo wa Kiislamu.

Mwakilishi wa kundi hilo alitumia zaidi ya saa tatu kumshawishi mwanazuoni huyo kuwaruhusu kurusha matangazo hayo tena, lakini hakufanikiwa. Siku iliyofuata, mwakilishi alijaribu tena, akimweleza kuhusu haki za binadamu, uhuru wa dini na imani, na haki zinazotolewa kwa kila raia katika Katiba ya Pakistan. Baada ya siku nzima ya kujadiliana, mwanazuoni huyo alikubali kuruhusu kituo cha Kikristo kurudi hewani, lakini aliomba Wakristo wa eneo hilo wapunguze sauti ya televisheni wakati wa sala za Waislamu ili wasiwakere majirani zao.

"Tulifurahi sana!" anasema Peter. "Hata kama kwa wengine ni matangazo ya televisheni tu, kwetu sisi ni sehemu muhimu sana ya maisha yetu kama Wakristo."

Chanzo
Tume ya Kiekumeni ya Maendeleo ya Binadamu (ECHD), Pakistan.
Jina la Peter limebadilishwa kwa sababu za kiusalama.

KIPINDI CHA 3

Namna mbalimbali ya utambulisho wetu

Muhtasari wa kipindi

Kipindi hiki kinachunguza vipengele vingi vinavyojenga utambulisho wetu na jinsi vipengele hivyo vinavyohusiana na fursa au changamoto katika jamii. Kinachunguza changamoto nyingi ambazo watu hukumbana nazo kutokana na namna mbalimbali za utambulisho wao — mathalani, kuwa sehemu ya kundi fulani la kidini au kuwa sehemu ya kikundi cha watu wachache, ama jinsia, umri au daraja fulani katika kijamii.

Katika jamii nyingi, utambulisho wa kidini huchukuliwa kama kitu kinachowagawa watu, hata hivyo sote tuna namna zinazofanana za utambulisho, pamoja na uzoefu mwingi wa maisha. Mazoezi katika kipindi hiki yanaonyesha dhana hii.

Kipindi hiki kinaleta washiriki pamoja na kuwawezesha kuchangamana ili kuondoa hali ya kujifunza kwa kuchangia tu maarifa; bali kinalenga katika kuwawezesha washiriki kujifunza kutokana na uzoefu, kwa kutumia mazoezi mbalimbali, ili kuwafanya waweze kutafakari na kujifunza kutoka kwa kila mmoja.

Malengo ya mafunzo

Kipindi hiki kinalenga kukuza mtazamo chanya kuelekea wale wanaoonekana kuwa "tofauti" na kukuza uwezo wa kutambua fursa na changamoto zinazotokana na utambulisho wa mtu.

Mpaka kufikia mwisho wa kipindi, washiriki waweze:

- Kutambua kuwa utambulisho wa kidini ni sehemu moja tu ya utambulisho wao na kwamba wana utambulisho na uzoefu wa maisha unaowaunganisha na wengine hata katika jamii zenye tofauti za kidini.
- Kutambua kuwa vipengele tofauti vya utambulisho wetu vinaweza kuleta fursa au changamoto, na kwamba baadhi ya watu wanakumbana na changamoto nyingi au fursa nyingi kutokana na vipengele hivyo.
- Kuonyesha mshikamano na wale wanaokumbana na changamoto kwa sababu ya vipengele vya utambulisho wao, na kuelewa umuhimu wa kushirikiana kuvuka tofauti ili kuleta mabadiliko.

ZINGATIA

KUMBUKA kuwa uhalisia wa kufanikisha malengo haya utategemea kiwango ambacho washiriki wanaanzia — kwa mfano, ikiwa kuna mitazamo hasi iliyokita mizizi dhidi ya makundi mengine. Madhumuni ya malengo ya mafunzo ni kuonyesha maeneo ambayo wawezeshaji wanaweza kufuatilia maendeleo ya washiriki katika maarifa, mitazamo, na stadi za kuchukua hatua. Maendeleo yanaweza kufikiwa hatua kwa hatua wakati wa mafunzo, badala ya kutarajia kufikiwa ndani ya kipindi kimoja tu.

Yaliyomo katika kipindi na muda

Ukaribisho	Dakika 2
Zoezi la ufunguzi: Chungu cha bahati Husaidia washiriki kufikiria kuhusu masuala ya ukosefu wa usawa na mshikamano.	Dakika 15
Zoezi la pamoja: Hatua moja mbele Husaidia washiriki kufikiria kuhusu nani anaathiriwa na ubaguzi na ukiukwaji mwingine wa haki katika muktadha wao.	Dakika 45
Zoezi la kuchangamsha: Kila mtu abadilishane viti Zoezi la kimwili ambapo watu wanaokubaliana na kauli fulani hubadilishana viti.	Dakika 10
Zoezi la mjadala: Utambulisho wetu kijamii Husaidia washiriki kutafakari vipengele mbalimbali vya utambulisho wao na jinsi wanavyokuwa na utambulisho sawa na watu wa imani tofauti.	Dakika 40
Maoni ya hitimisho: Utambulisho na mtazamo potofu Maoni haya yanahitimisha ujumbe wa mazoezi yaliyotangulia.	Dakika 8
JUMLA YA MUDA	**Saa 2**

Jiandae

Andaa kipindi kwa mujibu wa mwongozo uliopo ukurasa wa 15, 'Jinsi ya kuandaa kila kipindi'. Kumbuka – unawajua wanakikundi wako! Unakaribishwa kurekebisha na kubadilisha vipengele vyovyote vya kipindi, ili kivutie mahitaji ya kikundi chako.

NYENZO ZA KIPINDI HIKI

Mbali na nyenzo za kawaida kwa kila kipindi zilizoainishwa kwenye ukurasa wa 16, utahitaji nyenzo zifuatazo ili kuendesha kipindi hiki:

- Eneo la nje au chumba kikubwa cha kutosha kwa washiriki kusimama wakiwa kila mmoja kando ya mwingine katika mstari mmoja ambapo wanaweza kuchukua kumi kuelekea upande mwingine wa chumba.
- Vipeperushi kwa ajili ya zoezi la Chungu cha bahati.
- Jozi moja ya mkasi kwa kila washiriki wanane, kwa mfano, jozi tatu kwa kikundi cha washiriki kumi na saba hadi ishirini na wanne.
- Kadi za wahusika zilizochapishwa na kukatwa kwa ajili ya zoezi la Hatua Moja Mbele.
- Orodha ya kauli za kusomwa kwa sauti kwa ajili ya zoezi la Hatua Moja Mbele.
- Orodha ya kauli za kusomwa kwa sauti kwa ajili ya zoezi la Kila mtu abadilishane viti.

NYENZO ANDAMIZI za kipindi hiki zinaweza kupatikana hapa.

ANDAA UKUMBI

Hiki ni kipindi kilichochangamka sana, hivyo nafasi kubwa inahitajika pamoja na viti ambavyo ni rahisi kuvisogeza – kwa mfano kuvisukumia upande wa ukutani. Anza zoezi kwa kusogeza viti ili kupata nafasi kwa ajili ya washiriki kutembea kwa uhuru ndani ya chumba.

‘Hatua moja mbele'

“Hatua moja mbele ni zoezi bora kabisa! Lilionyesha wazi jinsi watu wanavyobaki nyuma na jinsi kutambulika kwa majina na unyanyapaa vinavyoathiri maisha ya watu. Tulihitaji muda mwingi wa majadiliano baada ya zoezi hili.”
HAMMAM HADDAD, MWEZESHAJI, JORDAN

“Zoezi la Hatua moja mbele liliwasaidia washiriki kuelewa kwa nini baadhi ya watu wanabaki nyuma, hata kama wote wana akili, uwezo, na bidii sawa. Pengo lililoongezeka lilidhihirisha jinsi gani jamii inavyojengwa kutoa nafasi kwa watu waliopendelewa wa tabaka fulani na jinsia fulani, ingawa wote huzaliwa sawa.”
IRFAN ENGINEER, MWEZESHAJI, INDIA

Mpango wa kina wa kipindi

1. Ukaribisho   Dakika 2

GUMZO FUPI

NINI CHA KUSEMA
Mada ya kipindi hiki ni 'Namna Mbalimbali za Utambulisho Wetu', na lengo lake ni kutufanya tuangalie si tu vitu mbalimbali vinavyotugawa katika jamii zetu, bali pia mambo yanayotufanya kuwa wamoja. Kipindi kitakuwa cha kushirikiana kwa kiwango kikubwa, chenye mijadala mingi na mazungumzo ya pamoja.

2. Zoezi la ufunguzi: Chungu cha bahati   Dakika 15

ZOEZI LA PAMOJA

MAELEZO
Washiriki wana dakika moja kukata au kurarua picha, lakini ni washiriki wachache tu walio na mkasi.

LENGO
Zoezi hili ni la kufurahisha, na shirikishi ili kuwafanya washiriki kufikiria kuhusu tofauti za fursa walizonazo watu maishani na umuhimu wa mshikamano. (Ili kuwakumbusha kipindi cha kwanza, chungu cha supu inawakilisha haki za binadamu.)

NYENZO

- Nakala moja ya kipeperushi cha chungu cha supu kwa kila mshiriki.
- Jozi moja ya mkasi kwa kila washiriki wanane.

JINSI YA KUANZA ZOEZI   DAKIKA 3
Mpe kila mshiriki nakala ya kipeperushi cha chungu cha supu (au mchoro wake ikiwa hakuna mashine ya kunakili). Wape mikasi washiriki wachache (mmoja tu kati ya wanane). Eleza kazi yao bila kufafanua madhumuni ya zoezi, kwa mfano:

> *"Nitakaposema 'Anzeni!', kazi yenu ni kutoa picha ya chungu cha supu kutoka kwenye karatasi ndani ya dakika moja kwa njia yoyote mnayoweza. Tumieni ubunifu wenu kupata njia ya kufanya hivyo. Wachache kati yenu mmekuwa na bahati na kupewa mkasi."*

JINSI YA KUENDESHA ZOEZI   DAKIKA 11
Sema 'Anzeni!' kisha weka kipima muda kwa dakika moja. Wakati muda ukifika, waambie kila mtu asimamishe kazi na kushikilia picha yao ya chungu cha supu ili kila mmoja aone matokeo.aged.

Wapongeze kwa juhudi zao na uwaulize:

- Ulitatua kazi hii kwa njia gani?
- Ulihisi vipi kutokuwa na mkasi?
- Ilikuwaje kuwa miongoni mwa wachache waliopata mkasi?
- Je, mtu yeyote alifikiria kuazima au kukopesha mkasi? Kwa nini au kwa nini hapana?

Eleza yafuatayo:

- Zoezi linaonyesha kuwa ulimwenguni pote na kwenye jamii zetu watu huzaliwa wakiwa na mazingira tofauti ya kuanzia maishani. Hali nyingi huamua mustakabali wao, hasa hali ya kijamii na kiuchumi ya wazazi wao. Wengine wana bahati ya kuzaliwa na fursa mbalimbali, kama vile kuwa na 'mkasi'. Wengine hawana.
- Wakati mwingine, watu wasio na fursa hudhani kwamba ni lazima kubaki walipo na kukubali nafasi waliyowekwa bila hata kuazima mkasi ama kubadili hali waliyonayo. Vivyo hivyo, wale walio na fursa hawafikirii kila mara kuwasaidia wengine kupata 'mkasi'.
- Haki za binadamu zinahusu maisha utu wa mtu. Kuzifahamu zaidi kunaweza kutusaidia kufikiria kwa njia tofauti. Hatupaswi kukubali dhuluma au kushindwa kwa sababu hatuna 'mkasi'. Tunaweza kuomba 'mkasi'! Haki za binadamu pia zinaweza kuwahamasisha watu wenye fursa kusaidia kusimama kwa ajili ya haki za wale wasio na fursa.

JINSI YA KUHITIMISHA ZOEZI DAKIKA 1

Hitimisha kwa kusema kuwa katika kipindi hiki tutafikiria ni nani ana fursa na ni nani anakabiliwa na dhuluma katika jamii yetu. Tunatumani kuwa hili litatufanya tufikirie jinsi tunavyoweza kuhakikisha kila mtu anaweza kuishi maisha yenye heshima na kuwa na 'chungu cha supu' – haki zetu za binadamu.

ZINGATIA

Ikiwa kipindi kina muda mrefu zaidi, unaweza kurudia zoezi hili kwa kuwapa washiriki nafasi ya pili. Mara hii, waruhusu wajadili kwa dakika moja kuhusu jinsi ya kushirikiana kabla ya kufanya zoezi tena. Kisha uwaulize walivyojisikia waliposhirikiana. Eleza kuwa kwa kuwa wazi kushirikiana, tunaweza kuunda fursa za pili kwa jamii na sisi wenyewe. Hakikisha una nakala za kutosha za kipeperushi ikiwa utafanya zoezi hili mara mbili.

3. Zoezi la pamoja: Hatua moja mbele Dakika 45

ZOEZI LA PAMOJA

MAELEZO

Katika zoezi hili rahisi la kuigiza majukumu, washiriki huchukua nafasi za wahusika waliopewa na wanapiga hatua moja mbele ikiwa mhusika wao angekubali kauli inayosomwa na mwezeshaji. Kadri pengo kati ya washiriki linavyoongezeka, inadhihirisha wazi jinsi makundi mbalimbali katika jamii yanavyokuwa na fursa au changamoto tofauti.

LENGO

- Kuwasaidia washiriki kuelewa umuhimu wa haki za binadamu na uhuru wa dini au imani kwa watu wa dini zote na wale wasio na dini, kwa kujifikiria katika nafasi za watu wa asili tofauti.
- Kuongeza uelewa kuhusu changamoto wanazokabiliana nazo watu wa dini au imani tofauti katika maisha ya kila siku.
- Kuonyesha jinsi dini au imani inavyoingiliana na vipengele vingine kama vile jinsia na tabaka, na jinsi baadhi ya watu wanavyokumbana na changamoto nyingi zaidi na ukosefu wa fursa.

NYENZO

- Chumba chenye nafasi ya kutosha kwa washiriki kusimama kila mmoja kando ya mwingine kuelekea ukutani, na kuchukua hatua ndogo kumi na tano kuelekea upande mwingine wa chumba.
- Kadi za wahusika ili kuwapa washiriki.
- Orodha ya kauli za kusomwa kwa sauti.

Pata **WAHUSIKA NA KAULI** za eneo lako hapa.

MAANDALIZI YA AWALI

Andaa kadi za wahusika na kauli kama ifuatavyo:

- Chagua seti sanifu ya kadi za wahusika na kauli kama sehemu ya kuanzia. Kuna seti za wahusika na kauli kwa muktadha mbalimbali wa kijiografia. Chagua ile inayolingana zaidi na mazingira yako.

Kisha:

- Chagua wahusika wa kutumia. Kila seti sanifu inajumuisha takribani kadi 30 za wahusika ambazo unaweza kuhariri na kuchapisha. Utahitaji kadi moja ya mhusika kwa kila mshiriki. Chagua kadi za kutumia kwa kuzingatia umuhimu na utofauti mkubwa wa wahusika. Mwongozo kamili wa jinsi ya kuchagua na kurekebisha wahusika unapatikana kwenye nyaraka.
- Chagua kauli za kutumia. Unahitaji kauli 12-15 za kusoma kwa sauti. Chagua kauli kutoka kwenye orodha sanifu kwa kuzingatia umuhimu wake katika muktadha wa nchi yako.

JINSI YA KUANZA ZOEZI DAKIKA 8

- Eleza kwamba sasa tunaenda kufikiria kuhusu ni nani ana fursa na nani ana changamoto katika jamii zetu na jinsi hali hiyo inavyoathiri maisha yao.
- Eleza kuwa kundi litafanya mazoezi rahisi ya uigizaji kwa pamoja. Kila mshiriki atapewa mhusika. Wote wanapaswa kusimama wakiwa wameelekeza migongo yao upande mmoja wa chumba. Jambo pekee watakalofanya ni kupiga hatua moja mbele ikiwa wanadhani mhusika wao angekubaliana na kauli utakayosoma.
- Sambaza wahusika kwa njia ya bahati nasibu huku ukiwaomba washiriki wasifichue wahusika wao. Haijalishi ikiwa mwanaume atapata mhusika wa mwanamke au kinyume chake.
- Tumia dakika chache kuwasaidia washiriki kuingia katika nafasi ya wahusika wao kwa kuwauliza wafikirie maswali yafuatayo:Chukulia kwamba wewe ndiye mhusika uliye kwenye kadi yako:
  - Utotoni mwako ulikuwaje?
  - Maisha yako ya kila siku yaoje – unafanya nini katika siku ya kawaida, unashirikiana na nani, mapato yako na mtindo wako wa maisha ukoje?
  - Unaogopa nini na unatarajia nini?

JINSI YA KUENDESHA ZOEZI DAKIKA 35

- **KUIGIZA MAJUKUMU** (DAKIKA 15)
  Waombe washiriki wasimame bega kwa bega katika mstari ulionyooka upande mmoja wa chumba. Waambie kwamba utasoma kauli kadhaa. Ikiwa wanadhani mhusika wao angekubaliana na kauli hiyo, wanapaswa kupiga hatua moja mbele. Ikiwa mhusika wao hangekubaliana, wanapaswa kusimama pale walipo bila kusogea.

Lengo la mchezo huu si kuchukua hatua mbele, bali kuwa wa kweli kwa hali halisi ya maisha ya mhusika wako. Washiriki hawaruhusiwi kuzungumza wakati wa mazoezi haya.
Soma kwa sauti kauli moja baada ya nyingine. Baada ya kila kauli, simama kidogo ili kuruhusu washiriki kufikiria ikiwa mhusika wao anaweza kusonga mbele. Baada ya kusoma kauli zote, wape washiriki muda wa kutazama nafasi zao katika chumba ikilinganishwa na wengine, bila kusema walikuwa nani.

- **MJADALA WA PAMOJA** (DAKIKA 20)
  Waulize washiriki maswali ya wazi kama ifuatavyo (chukua jibu moja au mawili kwa kila swali ili kuhakikisha kuwa kuna muda wa mjadala wa mwisho):
  – Nini kilitokea wakati wa zoezi?
  – Ulijisikiaje uliposonga mbele au kushindwa kusonga mbele?
  – Ulijisikiaje ulipoona kuna tofauti zinazozidi baina ya watu?
  – Ilikuwa rahisi au ngumu kiasi gani kuigiza nafasi yako – kuweka nafasi yako katika maisha ya mhusika?
  – Je, kuna nyakati ambapo ulijihisi kuwa haki za msingi za binadamu za mhusika wako zilipuuzwa, ikiwemo na uhuru wao wa kidini au imani? Ni wakati gani?

  Omba kila mmoja aseme aliigiza mhusika gani.
  – Je, nafasi zetu katika chumba zinaakisi uhalisia wa ukosefu wa usawa katika jamii yetu? Ni nani anayeachwa nyuma – wanawake, jamii ya watu wachache, watu maskini?
  – Hali hii ina athari gani kwa maisha ya watu?

JINSI YA KUHITIMISHA ZOEZI DAKIKA 2
Malizia kwa kusema kwamba mikataba ya haki za binadamu inasema kuwa tunazaliwa tukiwa sawa kwa haki na hadhi – kwamba tunaanza kwenye mstari mmoja. Lakini kukiukwa kwa usawa wetu, kwa mfano, kwa misingi ya dini zetu, imani, hali yetu ya kijamii, ama hali ya kuwa mwanaume au mwanamke, inaathiri sana maisha yetu tangu kuzaliwa. Watu wengi huishia kuachwa nyuma.

4. Zoezi la kuchangamsha: Kila mtu abadilishane viti Dakika 10

ZOEZI LA PAMOJA

MAELEZO
Washiriki hubadilishana viti iwapo wanakubaliana na kauli zinazosomwa na mwezeshaji.

LENGO
Kuinua ari ya washiriki huku tukigundua kwamba tuna mambo yanayotufanya tufanane licha ya tofauti zetu.

MAANDALIZI YA AWALI
Tayarisha orodha ya kauli za kusoma, ukizirekebisha ili ziendane na kikundi chako.

JINSI YA KUANZA ZOEZI
Waombe washirki wote wakae kwenye duara. Eleza kwamba, kabla ya kuendelea na mjadala mkubwa, tutaanza na zoezi fupi na la kufurahisha. Eleza kwamba utasoma kauli na kila anayekubaliana nayo anapaswa kubadilisha kiti.

JINSI YA KUENDESHA ZOEZI

Soma kauli zifuatazo:

- Wote wanaopenda kula (*chakula cha kienyeji kinachopendwa na jamii zote)* badilisheni viti.
- Wote wanaopenda *(msanii maarufu kwa jamii zote)* badilisheni viti.
- Wote wanaopenda *(timu ya michezo maarufu kwa jamii zote)* badilisheni viti.
- Wote wanaotazama *(kipindi cha televisheni maarufu kwa jamii zote)* badilisheni viti.
- Wote wanaofurahia jua badilisheni viti.
- Wote wanaofurahi mvua inaponyesha badilisheni viti.
- Wote wanaotamani kuishi katika jamii yenye amani na mshikamano badilisheni viti.

JINSI YA KUHITIMISHA ZOEZI

Washukuru wote kwa kushiriki na waambie kwamba inaonekana tuna mambo mengi yanayotufanya tufanane – ikiwa ni pamoja na ndoto zetu zinazofanana.

5. Zoezi la mjadala: Utambulisho wetu kijamii   Dakika 40

MJADALA WA PAMOJA

LENGO

Kuwasaidia washiriki kugundua mambo yanayowafananisha na watu wa imani au mitazamo mingine na kutafakari jinsi utambulisho unavyohusiana na udhaifu wa kijamii.

NYENZO

- Bango-kitita yenye orodha ya 'utambulisho' 10.
- Slaidi ya 3 ya kipindi cha PowerPoint, au yaliyomo yakiwa yameandikwa kwenye bango kitita.

MAANDALIZI YA AWALI

- **CHAGUA AINA 10 MBALIMBALI ZA UTAMBULISHO KISHA ANDAA BANGO-KITITA NA UZIORODHESHE**

  Orodha ifuatayo inajumuisha 'aina 15 za utambulisho' ambao tunaweza kuwa nao. Chagua 10 kati ya hizi kwa ajili ya washiriki wako kujadili, kulingana na yale yaliyo muhimu zaidi kwa kundi hili kutafakari. Hakikisha unajumuisha baadhi ya utambulisho wa 'kufurahisha' kama michezo na muziki ili kufanya mjadala uwe mwepesi na kutoa mbadala 'salama' kwa watu kuzungumzia endapo wataona maswali ya mjadala ni nyeti sana. Usijumuishe utambulisho wowote ambao unaweza kupotosha mchakato na kusababisha mijadala mikali – lengo la zoezi hili si kubishana.

  UTAMBULISHO

  – Dini au imani
  – Jinsia
  – Klabu ya mpira au michezo unayoiunga mkono
  – Kabila/ukoo
  – Uraia
  – Ladha ya muziki
  – Hali ya kifamilia
  – Kiwango cha elimu
  – Burudani
  – Daraja/hali ya kiuchumi
  – Kundi la kijamii
  – Umri
  – Lugha ya kwanza
  – Utambulisho wa kijinsi
  – Uwezo/ulemavu

- **ANDAA NYENZO ZA KUNDISHIA KWA KUTAZAMA**
  Andika kwenye bango kitita aina 10 mbalimbali za utambulisho. Kama hautumii slaidi, andaa bango kitita ingine yenye wasilisho la slaidi ya 3.

JINSI YA KUANZA ZOEZI DAKIKA 4

- Waombe washiriki wakae katika vikundi vya watu wawili na wajitenge mbali kidogo na wengine.
- Tambulisha zoezi hili kwa kueleza yafuatayo:
  Mara nyingi, tunajikita zaidi kwenye mambo yanayotutofautisha. Kwa mfano, tunapozungumzia dini, huwa tunafikiria kuhusu wao – watu wa dini nyingine, na sisi – watu tulio na imani na tamaduni zetu. Utambulisho wa kidini unaweza kuwa na nguvu sana. Lakini kila mmoja wetu ana utambulisho mwingi unaotufanya kuwa namna tulivyo – kwa mfano, kuzungumza lugha ya asili (lugha ya kienyeji), kutoka sehemu moja (mkoa/wilaya), au kuwa shabiki mkubwa wa (klabu ya mpira wa miguu)! Sasa tutafanya zoezi litakalotusaidia kufikiria kuhusu utambulisho wetu tofauti na jinsi unavyohusiana na utambulisho wa wengine.
  Soma aina mbalimbali 10 za utambulisho pamoja na maswali ya mjadala kutoka kwenye bango-kitita au slaidi ya PowerPoint ya 3.

  MASWALI YA KUJADILI
  - Ni aina gani ya utambulisho wako ambayo ina nguvu zaidi kwa jinsi unavyojiona?
  - Ni aina gani ya utambulisho wako zinazoathiri jinsi watu wengine wanavyokuona?
  - Ni aina gani ya utambulisho wako unazohisi hukupatia faida au hukufanya upate changamoto zaidi?

JINSI YA KUENDESHA ZOEZI DAKIKA 35

- **FIKIRI** (DAKIKA 5)
  Waombe washiriki watumie dakika 5 kufikiria binafsi kuhusu utambulisho wao na jinsi ambavyo wangeyajibu maswali yaliyo kwenye bango-kitita au skrini.
- **KUWA PAMOJA** (DAKIKA 10)
  Waombe washiriki wajadili maswali haya wawili wawili kwa dakika 10. Sisitiza kwamba hakuna mtu anayelazimika kusema jambo lolote analohisi kuwa la faragha – wanapaswa kushirikisha tu yale wanayojihisi vizuri kuyasema.
- **SHIRIKISHA** (DAKIKA 20)
  Walete walete washiriki kwenye mjadala wa pamoja. Waombe watoe mawazo yao kwenye kundi kubwa. Sisitiza kwamba, kushiriki ni kwa hiari! Hakikisha unadumisha mtazamo wa usikivu katika mjadala huu wa kibinafsi. Japokuwa ni sawa kwa watu kuuuliza maswali, kutoa maoni au kueleza uzoefu wao kwenye hadithi za wenzao, lakini hairuhusiwi mtu yeyote kumkosoa mwingine.

JINSI YA KUHITIMISHA ZOEZI DAKIKA 1

Washukuru wote kwa kushiriki na useme unatumai wamepata fursa ya kufikiria kuhusu pande nyingi za utambulisho wao.

6. Maoni ya hitimisho: Utambulisho na mtazamo potufu Dakika 8

WASILISHO

MAELEZO

Maoni ya hitimisho kwa kipindi hiki yanawasilishwa kwa njia ya uwasilishaji mfupi unayojumuisha vipengele mbalimbali vya mafunzo tuliyofanya katika kipindi hiki. Uwasilishaji huu unahusisha nadharia pamoja na hadithi ya mwanamabadiliko katika jamii yake.

LENGO

Lengo ni kusisitiza masuala muhimu ya kipindi hiki: kwamba kila mtu ana utambulisho mwingi na anaweza kukumbana na fursa au changamoto kulingana na utambulisho wake. Ni muhimu pia kutoangalia mtu mwingine kwa utambulisho mmoja tu unaomwakilisha, bali kumwona kama mtu mwenye utambulisho anuai.

NYENZO

- Nakala ya mwongozo wa maoni ya hitimisho inapatikana kwenye ukurasa wa 75 wa Kiongozi hiki.
- Mwongozo unaendana na slaidi ya 4 ya PowerPoint na kuendelea na inajumuisha maelezo ya msemaji kwenye slaidi hizo.
- Toleo la mwongozo huu katika mfumo wa kompyuta la Word ambalo linaweza kuhaririwa, pia linapatikana katika nyenzo.

MAANDALIZI YA AWALI

Soma na, ikiwezekana, rekebisha mwongozo na slaidi za PowerPoint (au tengeneza bango-kitita zenye hoja kuu kutoka kwenye slaidi). Fanya mazoezi ya kuwasilisha mada hii ukitumia slaidi au bango-kitita.

Vyanzo

Chungu cha Bahati Imetolewa kutoka kwenye Star Exercise kutoka kwenye kitabu Facilitating Group Learning cha George Lakey, Uk. 109.

Hatua Moja Mbele: Kutoka kwenye Compass Manual ya Tume ya Ulaya na nyenzo za mafunzo ya Elimu kwa Amani. http://www.educationforpeace.com/english/forb.php

Utambulisho wa Kijamii: Kutoka The Social Identity Wheel ya programu ya ujumuishi ya kufundisha katika Chuo Kikuu cha Michigan. https://sites.lsa.umich.edu/inclusive-teaching/social-identity-wheel/)

Mwongozo wa uwasilishaji

Utambulisho na mtazamo potofu

Nakala hii ya mwongozo wa hitimisho kwa kipindi cha 3 inaonyeshwa katika slaidi za 4-13 za PowerPoint ya kipindi.

Katika kipindi hiki, tumetafakari jinsi utambulisho wetu tofauti unavyoathiri namna tunavyojiona sisi wenyewe, tunavyowaona wengine, na tunavyotendeana. Pia tumechunguza utambulisho mbalimbali tulionao na jinsi mara nyingi utambulisho huu unavyovuka mipaka ya kidini. Wanawake wa Kihindu, Kiislamu, na wasio na dini wanakabiliwa na changamoto nyingi zinazofanana katika jamii, kama vile Wabuddha, Wakristo, na Wayahudi wenye ulemavu, au watu wa imani yoyote wasiopata fursa ya elimu ya kutosha. Tuna mambo yanayotufanya kuwa tofauti, lakini pia tuna mengi yanayotufanya tufanane.



Mara nyingi, utambulisho wa kidini hutumiwa kama chombo cha kutugawa. Hii inaweza kusababisha tuwaone watu kutoka jamii nyingine kana kwamba wana utambulisho mmoja tu – Myahudi, Mwislamu, Mbuddha, na kadhalika – na kudhani kwamba kila mtu mwenye utambulisho huo hufikiri, kuhisi, na kutenda kwa njia ile ile.

Ni kawaida kwa watu kuwekeana dhana potofu. Mara nyingi, kwa kujua au bila kujua, tunadhani kwamba watu wenye imani fulani wanafanana kimsingi, bila kujali umri, jinsia, tabaka la kiuchumi, utaifa, au mtazamo wao wa kisiasa – na bila kuzingatia iwapo wanafuata kwa dhati mafundisho na desturi za imani yao au la.



Ni kawaida pia kuona watu wengine wanatambulika kutokana na dini zao - tukidhani kwamba kila kitu kuhusu wao ni kwa sababu ya wanachoamini. Kwa hiyo, kama mwanakikundi mmoja wapo akifanya jambo baya, basi lazima watu waamini dini yao inahimiza mambo mabaya au ina maadili mabaya.



Wakati watu wa jamii tofauti hawana mahusiano ya karibu, ni rahisi kudhani kuwa 'wale' ni tofauti kabisa na 'sisi' – kwamba 'wao' wana maslahi, mahitaji, maadili na hisia tofauti na 'sisi.' Kutokana na dhana hiyo, tunaweza kufikiri kuwa hawana maarifa yoyote tunayoweza kujifunza kutoka kwao au hata kuwaona kuwa wako chini kimaadili au kitamaduni.

Lakini badala ya kufanya hivyo, tukianza kuwaona watu wa makundi mengine kama watu kamili – wenye utambulisho mwingi na uzoefu wa maisha tofauti (ambazo nyingi tunashirikiana nazo) – basi huenda tukaweza kuthamini, kuelewa na kufungamana wao kwa wao kwa njia mpya, tukivuka mipaka na kujenga mahusiano.

Baadhi ya utambulisho huleta changamoto na ubaguzi katika jamii, huku mingine ikitupatia fursa na upendeleo. Kutambua upendeleo tulionao kunaweza kutusaidia kuelewa jinsi tunavyoweza kuwa sehemu ya tatizo linalowasababishia wengine changamoto. Vilevile, kutambua utambulisho wetu mwingi kunaweza kutufungulia fursa na njia za kupinga ukosefu wa haki na ubaguzi, na kusimama pamoja na wale wanaokumbana na kutengwa.

HADITHI YA WANAMABADILIKO



Sameh, kijana Mkristo, na Hanaa, kijana Mwislamu, wanatoka kijiji cha Hijaza katika mkoa wa Qana, Misri. Wanafanya kazi pamoja kuvunja vizuizi baina ya jamii za Waislamu na Wakristo katika kijiji chao.

Hanaa anasema:

> "Niliona watoto wakikataa kukaa au kushirikiana pamoja kwa sababu walitoka dini tofauti."

Sameh anasema:

> "Nilihisi kuwa ingekuwa rahisi zaidi kushughulikia hili kwa pamoja na kujaribu kubadili mitazamo yao. Tulitaka watoto wa eneo hili wawe chachu za mabadiliko."

Waligundua kuwa watoto walitaka kucheza mpira wa miguu, lakini eneo bora la kuchezea lilikuwa kwenye uwanja nje ya kanisa Katoliki. Waliwasiliana na kasisi wa eneo hilo, Padre Francis, ambaye alikubali kusaidia.

Anasema:

> "Tunahitaji sana kile ambacho Sameh na Hanaa wanafanya katika kijiji hiki na tunatumaini kuwa kitapanuka hadi vijiji vyote."

Watoto Waislamu walikataa kwenda kwenye uwanja huo, lakini hatimaye walimfuata Hanaa.

Hanaa anasema:

> "Polepole, nilijaribu kuwachanganya watoto pamoja. Mwanzoni walikataa, lakini hatua kwa hatua, wao wenyewe walianza kuunda makundi mchanganyiko."

Hanaa na Sameh waliwaalika wazazi wa watoto kushuhudia shughuli za vikundi hivyo. Mara nyingi, akina mama walikuwa wa kwanza kuitikia kwa njia chanya.

Sameh alisema:

> "Tunapaswa kubadilika, na mabadiliko huanza kwa imani katika wazo."

Hanaa aliongeza:

> "Sisi wawili ni mfano hai. Tunafanya kazi pamoja ingawa tunatoka dini tofauti. Tunakamilishana na tunashiriki lengo moja. Lengo letu ni watoto."

HITIMISHO

Mwisho wa siku, sote tunataka "supu ya maisha" iwe na utamu na ladha! Sisi sote ni sehemu ya familia moja ya kibinadamu na tunashiriki mahitaji na haki sawa. Tunapokuja pamoja kutetea haki za kila mtu, tutakuwa na ufanisi mkubwa zaidi.

Katika vipindi viwili vijavyo, tutajifunza zaidi kuhusu ukiukwaji wa uhuru wa dini au imani na kujaribu kuonyesha hali halisi katika jamii yetu. Tunatumai kuwa maarifa hayo yatatusaidia kuchukua hatua kuwa wanamabadiliko wa mabadiliko katika jamii zetu.

Vyanzo

Taadudiya, www.taadudiya.com

Unaweza kupata filamu ya YouTube ya Hanaa na Sameh wakisimulia hadithi yao kwa Kiarabu ikiwa na manukuu ya Kiingereza hapa: What is your story? Egypt.

Kwa bahati mbaya, Hanaa alifariki katika ajali ya barabarani mwaka 2019.

KIPINDI CHA 4

Ukiukwaji wa Uhuru wa Dini au Imani

Muhtasari wa kipindi

Kipindi hiki kinawatambulisha washiriki aina mbalimbali za ukiukwaji wa uhuru wa Dini au Imani, na jinsi watu wa dini zote na wasio na dini, katika sehemu tofauti za dunia, wanavyoathiriwa. Pia kinawaimarisha washiriki katika uwezo wa kutambua Ukiukwaji wa Uhuru wa Dini au Imani, wanaoweza kukutana nao.

Kipindi kinaanza kwa uwasilishaji wa dakika-20 kuhusu ukiukwaji. Sehemu za uwasilishaji huu zinaweza kuwa tata katika muktadha wako. Utahitaji kurekebisha uwasilishaji huu kulingana na tathmini yako ya kile ambacho ni salama na kinawezekana kujadiliwa kwa njia ya kujenga na washiriki wako.

Baada ya uwasilishaji, kipindi kinakuwa cha mwingiliano wa hali ya juu, kikijumuisha zoezi la maigizo la dakika 75 linaloshirikisha washiriki wote. Kipindi kinakamilika kwa hadithi kuhusu wanaharakati wawili wa mabadiliko nchini Nigeria.

Malengo ya mafunzo

Kipindi hiki kinajikita katika kujenga uelewa kuhusu aina mbalimbali za ukiukwaji wa Uhuru wa Dini au Imani, na hali ya Uhuru wa Dini au Imani kimataifa, pamoja na kuimarisha ujuzi wa kutambua ukiukwaji huo.

Mpaka mwisho wa kipindi, washiriki waweze:

- Kuelezea aina tofauti za ukiukwaji wa Uhuru wa Dini au Imani,
- Kutambua ukiukwaji wa kawaida wa Uhuru wa Dini au Imani, katika mazingira tata,
- Kukiri kwamba watu wa imani zote na wasio na imani wanaathiriwa na ukiukwaji wa Uhuru wa Dini au Imani, na kuelewa mateso yao na kujenga hali ya ushirikeli.

Yaliyomo katika kipindi na muda

Ukaribisho na utangulizi Kukumbusha watu maana ya Uhuru wa Dini au Imani, na kutambulisha kipindi	Dakika 5
Uwasilishaji: Kuelewa ukiukwaji wa uhuru wa dini na imani Maelezo yanayofafanua aina mbalimbali za ukiukwaji wa Uhuru wa Dini au Imani, yakijumuisha mifano kutoka sehemu tofauti za dunia.	Dakika 20
Mjadala wa pamoja Nafasi ya kutafakari na kujadili uwasilishaji.	Dakika 10
Zoezi la maigizo: Maigizo mafupi ya dakika mbili ya Uhuru wa Dini Washiriki wanapata fursa ya kutambua ukiukwaji wa Uhuru wa Dini au Imani kwa njia ya kufurahisha na shirikishi.	Dakika 80
Maoni ya hitimisho na hadithi ya wanamabadiliko Kuunganisha maudhui ya kipindi na kujadili changamoto na suluhisho	Dakika 5
JUMLA YA MUDA	**Saa 2**

Jiandae

iandae kwa kipindi hiki kwa kufuata mwongozo uliopo ukurasa wa 15, Jinsi ya Kujiandaa kwa Kila Kipindi. Kumbuka – unawajua washiriki wako! Unaweza kurekebisha na kubadilisha vipengele vyovyote vya kipindi ili kiendane na mahitaji ya kundi lako.

NYENZO ZA KIPINDI HIKI

Mbali na nyenzo za kawaida kwa kila kipindi zilizoorodheshwa kwenye ukurasa wa 16, utahitaji pia:

- Nakala za kutosha za matukio ya maigizo mafupi. Hakikisha kila kundi la takribani washiriki sita lina nakala mbili za tukio lao maalum.

NYENZO ANDAMIZI za kipindi hiki zinaweza kupatikana hapa.

CHAGUO LA ZIADA – JENGA KUJIAMINI

Kama sehemu ya maandalizi yako, unaweza kutazama filamu hii fupi ili kupata uelewa zaidi kuhusu ukiukwaji wa uhuru wa dini au imani?

FILAMU

ANDAA UKUMBI

Panga viti kwa umbo la nusu duara vikielekea mbele kwa ajili ya utangulizi na mjadala. Hakikisha chumba ni kikubwa kiasi cha kutosha au kuna vyumba vya ziada ili vikundi viweze kufanya mazoezi ya maigizo yao bila kusumbuliwa.

‘Uwasilishaji'

Mpango wa kina wa kipindi

1. Ukaribisho na utangulizi   Dakika 5

GUMZO FUPI

MAELEZO NA LENGO

Utangulizi huu mfupi unasaidia washiriki kuelewa mchakato wa mafunzo. Unawakumbusha yale waliyosoma kuhusu uhuru wa dini au imani katika Kipindi cha 2 na kutambulisha mada kuu za vipindi vya 4 na 5 – ukiukwaji wa haki.

NYENZO

- Bango-kitita yenye kanuni za msingi kutoka Kipindi cha 1.
- PowerPoint ya Kipindi cha 4, slaidi ya 3 au bango-kitita iliyoandikwa maneno 'FIKIRI – AMINI – KUWA SEHEMU YA - TENDA – HOJI – BADILI – KATAA'.

NINI CHA KUSEMA

Karibisha washiriki wote kwenye kipindi na toa hoja zifuatazo, ukizirekebisha ili ziendane na kikundi chako:

- Katika kipindi cha pili, tulichunguza maana ya uhuru wa dini au imani. Je, mnakumbuka maneno muhimu tuliyotumia kuelezea Uhuru wa Dini au Imani? (Waulize washiriki waorodheshe maneno haya: FIKIRI – AMINI – KUWA SEHEMU YA – TENDA – HOJI – BADILI – KATAA, kisha waonyeshe slaidi ya 3 na uyasome kwa sauti.)

- Tulijifunza pia kuhusu wakati ambapo uhuru wa dini au imani inaweza kuwa na mipaka. Tulielewa kuwa uhuru wa ndani – kufikiri, kuamini, na kubadili imani – haviwezi kudhibitiwa, lakini kile TUNACHOFANYA – yaani, matendo yetu ya kidini au kiimani – yanaweza kuzuiwa IKIWA yanadhuru watu wengine kwa njia maalum. Tulijifunza pia kuwa ubaguzi, kulazimisha imani, na uchochezi wa vurugu haviruhusiwi.

- Vipindi viwili vijavyo vitazingatia ukiukwaji wa uhuru wa dini au imani. Katika kipindi hiki, tutaangalia aina za ukiukwaji na mifano kutoka sehemu mbalimbali za dunia. Hii itatusaidia kuelewa jinsi watu wa dini zote na wasio na dini wanavyoathirika katika mazingira tofauti. Katika kipindi kijacho, tutajaribu kutathmini ukiukwaji wa uhuru wa dini au imani katika jamii yetu.

- Vipindi hivi vinaweza kuwa vigumu – kwa sababu simulizi tutakazosikia zinaweza kutufanya tukumbuke uzoefu binafsi ambao ni mgumu, na kwa sababu masuala yatakayoibuliwa yanaweza kujaribu mitazamo yetu kuhusu kile kinachopaswa au kisichopaswa kuruhusiwa katika jamii. Huenda tusiwe na maoni sawa kuhusu kila jambo. Kwa hiyo, katika kipindi hiki, tuheshimiane na tusikilize kwa makini, tukizingatia kanuni tulizokubaliana! *(Tumia bango-kitita yenye kanuni za msingi kuwaonyesha washiriki.)*

- Kusikiliza simulizi za ukiukwaji kunaweza kutufanya tuhisi kukatishwa tamaa au hata kukosa matumaini. Lakini, ili tuweze kufanya jambo lolote kuhusu matatizo haya na kuleta mabadiliko, tunahitaji kuvitambua na kuvielewa kwanza.

2. Uwasilishaji: Kuelewa ukiukwaji wa uhuru wa dini au imani
Dakika 20

WASILISHO

MAELEZO NA LENGO

Uwasilishaji huu unalenga kuongeza maarifa ya washiriki kuhusu aina mbalimbali za ukiukwaji wa uhuru wa dini au imani na hali ya uhuru wa dini au imani duniani kote. Maarifa haya yatakuwa msingi wa kipindi hiki na kijacho, ambacho kitasaidia washiriki kukuza ujuzi wa kuchanganua muktadha wa uhuru wa dini au imani.

NYENZO

- Nakala ya uwasilishaji inapatikana kwenye ukurasa wa 85 wa Kiongozi hiki.
- Uwasilishaji huu unahusiana na slaidi 4-39 za PowerPoint ya kipindi na maelezo yake yanapatikana kwenye maelezo ya mwezeshaji ya slaidi hizo.
- Toleo la mwongozo huu katika mfumo wa kompyuta la Word ambalo linaweza kuhaririwa, pia linapatikana katika nyenzo zilizojumuishwa za kipindi hiki.

MAANDALIZI YA AWALI

Andaa kipindi kulingana na mwongozo wa ukurasa wa 15, 'Jinsi ya kuandaa kila kipindi'. Soma na rekebisha mwongozo wa uwasilishaji na PowerPoint (au bango-kitita yenye hoja kuu). Fanya mazoezi ya kuwasilisha huku ukitumia slaidi au bango-kitita.

KIDOKEZO! Waombe watu waweke maswali/maoni yao hadi mwisho wa uwasilishaji wako.

ZINGATIA

Uaasilishaji huu unaweza kuwa mrefu na unajumuisha mifano mingi. Huenda ukataka kuondoa mifano inayoonekana kuwa si muhimu sana kwa kikundi chako. Pia, unaweza kubadilisha baadhi ya mifano na hadithi kutokana muktadha wako mwenyewe. Ujumbe muhimu katika mwongozo umetajwa kwa herufi nzito. Tafadhali hakikis ha unajumuisha hoja hizi katika mazungumzo yako!

3. Mjadala wa pamoja   Dakika 10

MJADALA WA PAMOJA

MAELEZO NA LENGO

Mjadala kuhusu uwasilishaji ulilotangulia unaowawezesha washiriki kuchakata na kuelewa mafunzo.

JINSI YA KUENDESHA MJADALA

Waombe washiriki kutoa maoni na kuuliza maswali kuhusu yaliyowasilishwa, kisha uliza maswali yafuatayo:

- Je, kulikuwa na jambo lolote ambalo hukulijua au lililokushangaza katika tulichosikia?
- Ni hadithi gani katika uwasilishaji iliyokuvutia zaidi?
- Ni aina gani za ukiukwaji unaofikiri ni changamoto kubwa zaidi katika muktadha wetu?

Baada ya dakika 15, funga mjadala wa pamoja. Eleza kuwa kikundi sasa kitaendelea kujadili na kuchunguza masuala haya kupitia zoezi.

ZINGATIA

Msitishe mtu yeyote anayeanza 'kuhubiri' au 'kuchochea' kwa njia isiyokuwa na tija. Mshukuru kwa maoni yake na thibitisha hisia zake, hasa ikiwa zinatokana na uzoefu wa kiwewe au udhaifu. Ikiwa ni lazima, wakumbushe washiriki kanuni za msingi za mazung-umzo. Jaribu kurejesha mazungumzo mahali ambapo watu wanahisi salama – kwa mfano, kwa kuuliza swali linalolenga mambo ya msingi yanayoweza kuungwa mkono na wengi.

4.Zoezi la magizio: Maigizo mafupi ya dakika mbili ya uhuru wa dini 80 min

ZOEZI LA KIKUNDI

MAELEZO

Katika zoezi hili, vikundi huunda na kuandaa igizo la dakika mbili kwa kutumia matukio rahisi waliyopewa. Matukio haya yanaonyesha hali mbalimbali ambapo ukiukwaji wa uhuru wa dini au imani unafanyika kwa njia tofauti. Baada ya hapo, maigizo hayo hujadiliwa kwa pamoja, huku washiriki wakitambua ukiukwaji wa uhuru wa dini au imani uliopo katika matukio hiyo.

LENGO

Zoezi hili linasaidia kubadilisha maarifa ya nadharia kutoka kwa uwasilishaji kuwa ujuzi wa vitendo katika kutambua ukiukwaji wa uhuru wa dini au imani, na kuwawezesha washiriki kutafakari kuhusu ukiukwaji katika muktadha wao.

NYENZO NA MAANDALIZI YA AWALI

- Amua idadi ya vikundi: Vikundi 2-3 yenye watu 6-10 ni bora zaidi, kwani matukio mengi yanahitaji angalau wahusika sita. Muda wa zoezi umewekwa kwa vikundi visiyozidi vitatu (washiriki wasiozidi 30). Usiweke vikundi vya ziada isipokuwa kama unaweza kuongeza muda wa kipindi!
- Chagua matukio matano ya maigizo ya kutumia, kulingana na umuhimu wake kwa kikundi chako na idadi ya vikundi vitakavyohusika. Kila kikundi kinapaswa kuwa na matukio tofauti. Matukio haya yanapatikana katika ukurasa wa 92-94 wa Kiongozi hiki na kwenye kiungo cha nyenzo za kipindi.
- Chapisha nakala mbili za kila matukio uliyochagua ili kuyagawa kwa vikundi husika.
- Andaa slaidi ya 40 ya PowerPoint ya kipindi au bango-kitita yenye maneno yafuatayo: ubaguzi, vizuizi vya serikali, kushindwa kwa serikali, na vurugu.

Pata nakala ya **TUKIO LA IGIZO** hapa.

JINSI YA KUANZA ZOEZI DAKIKA 5

Eleza kwa njia ifuatayo:

- Tutafanya zoezi la kuigiza ili kutusaidia kutambua ukiukwaji wa uhuru wa dini au imani tunaoweza kukutana nao.
- Tutajigawa katika vikundi. Kila kikundi kitapokea mkasa – wenye matukio yanayofuatana baina ya wahusika wachache. Kazi yenu ni kuigiza matukio haya kwa muda usiozidi dakika mbili!
- Mtakuwa na dakika 15 za kuunda na kufanya mazoezi ya maigizo yenu. Muda huo si mwingi, kwa hivyo mgawanye majukumu haraka na muanze kuigiza papo hapo!
- Baada ya dakika 15, kila kundi litaonyesha igizo lake mbele ya kundi zima.
- Ikiwa mnataka kuongeza maelezo kwenye hadithi, fanyeni hivyo – lakini hakikisheni igizo haizidi dakika mbili.
- Msijali! Tunatafuta uigizaji mwepesi tu – si uigizaji wa kitaalamu. Mradi hadithi inaeleweka, igizo lenu ni mafanikio!

Gawa katika vikundi na kuwapa kitini cha tukio.

JINSI YA KUENDESHA ZOEZI DAKIKA 75

- **KUCHEZA MAIGIZO** (DAKIKA 15)
  Waambie wanakikundi waanze kufanya mazoezi yao! Tembea vikundi kutoa msaada na kuhakikisha wanaanza vizuri.

ZINGATIA

Kulinda muda ni muhimu sana katika zoezi hili! Usiruhusu muda wa mazoezi kupita dakika 15, kwani hii itapunguza muda wa sehemu muhimu ya uwasilishaji na majadiliano. Pia, hakikisha muda unasimamiwa vyema wakati wa uwasilishaji na majadiliano ili vikundi ya mwanzo yasitumie muda wa vikundi wa baadaye.

- **UIGIZAJI NA MJADALA** (DAKIKA 50)
  Timing: Dakika 15 per group for WASILISHO plus Dakika 5utes flexibility.Mpangilio wa muda: Dakika 15 kwa kila kikundi kwa ajili ya uwasilishaji na dakika 5 za ziada kwa unyumbufu.
  Kila kikundi kitawasilisha igizo lao la dakika mbili mara mbili. Mara ya kwanza, wataigiza bila kusimamishwa. Mara ya pili, watazamaji watapiga kelele "Simama!" pindi wanapoona ukiukwaji wa uhuru wa dini au imani unafanyika. Igizo litasimama papo hapo (wahusika wabaki kama walivyo). Onyesha slaidi ya 40 kwenye PowerPoint na waulize wale waliopiga kelele "Simama!" wajibu kwa ufupi swali hili:
  - Huu ni mfano wa ukiukwaji wa aina gani na nani anahusika? (Kwa mfano: uhasama wa kijamii kama ubaguzi au vurugu, vizuizi vya serikali, au kushindwa kwa serikali kuwalinda watu?)

  Endeleza igizo hadi mtu mwingine atakaposema "Simama!" na mchakato huo utarudiwa. Kila igizo lina ukiukwaji wa aina tatu. Unaweza kuona maelezo haya katika toleo la mwongozo wa mwezeshaji kwenye kurasa za 92-94.

  Ikiwa muda utaruhusu baada ya uwasilishaji mara mbili, anza majadiliano mapana kwa kutumia maswali haya:
  - Nini kingepaswa kuwa tofauti katika hali hii? Ni taasisi gani au watu gani walipaswa kuchukua hatua tofauti? Je, sheria au kanuni zinapaswa kubadilika vipi?
  - Nani angeweza kuingilia kati kwa njia chanya ili kubadilisha hali hii? Je, mwanajamii, mwanaharakati?

  Tenga dakika 15 kwa kila kikundi kwa mchakato wa uwasilishaji na mjadala, na kuwa mkali katika kufuatilia muda! (Ikiwa una vikundi viwili tu, unaweza kuongeza muda huu.) Ikiwa italazimu kukatiza kikundi kikiwa katikati, eleza kwa upole kuwa ni muhimu kila mtu apate fursa ya kuwasilisha. Kumbuka kupongeza kila kikundi kwa kupiga makofi mwishoni mwa muda wao!

- **MUDA WA KUSHIRIKI KWA PAMOJA** (DAKIKA 10)
  Baada ya vikundi yote kuwasilisha na kujadili hali zao, wapongeze tena kwa juhudi zao. Kisha anzisha mjadala mpana kwa kutumia maswali haya:
  - Je, ukiukwaji kama tuliouona kwenye maigizo hutokea katika jamii yetu?
  - Hali hizi huwaathiri watu na jamii kwa ujumla kwa njia gani? Himiza watu kusimulia hadithi au uzoefu wao ikiwa wako tayari kufanya hivyo. Wakati watu wakifanya hivyo, jaribu kuuliza maswali ya jumla:
  - Uzoefu kama huu unamaanisha nini kwa jamii kwa ujumla?

  Elekeza mjadala kuhusu uelewa kwamba ukiukwaji wa haki una madhara kwa kila mtu kwa sababu unaleta mvutano na hatari kwa jamii nzima.

5.Maoni ya hitimisho na hadithi ya mwanamabadiliko Dakika 5

GUMZO FUPI

MAELEZO NA LENGO

Maoni ya hitimisho yanakusudia kuwahamasisha washiriki waamini kuwa mabadiliko yanawezekana.

NYENZO

Slaidi 41-44 za wasilisho ya kipindi cha 4 au nakala ya slaidi ya 41.

NINI CHA KUSEMA

- Ingawa ni rahisi kukata tamaa tunaposikia matatizo ya jamii yetu, mabadiliko yanawezekana hata katika mazingira yenye chuki na vurugu! Tumalizia na hadithi moja ya matumaini.
- Soma hadithi ya Mchungaji James na Imam Ashafa kwenye ukurasa wa 95. (pia inapatikana kwenye nyenzo zinazoweza kupakuliwa kwa ajili ya kipindi hiki).
- Mabadiliko hufanyika taratibu lakini ni mchakato muhimu sana. Mabadiliko huanza tunapofahamu hali ya uhuru wa dini au imani si kwa ajili yetu tu, bali kwa kila mtu katika nchi na jamii yetu.

Mwongozo wa uwasilishaji

Kuelewa ukiukwaji wa uhuru wa dini au imani

Nakala hii ya uwasilishaji wa kipindi cha 4 inaonyeshwa kwenye slaidi za 4-39 za PowerPoint ya kipindi.

ZINGATIA: Uwasilishaji huu ni mrefu (chini ya dakika 20) na unajumuisha mifano mingi. Huenda ungependa kuondoa mifano inayokosa umuhimu kwa kikundi lako. Pia, unaweza kuchukua nafasi ya mifano mingine kwa hadithi kutoka katika muktadha wako. Ujumbe muhimu katika sehemu za ‘Hadithi za…’ umetiliwa mkazo kwa maandishi yenye herufi nzito. Tafadhali hakikisha unajumuisha hoja hizi katika mazungumzo yako! Tumia PowerPoint, machapisho ya slaidi muhimu za PowerPoint au vielelezo vya bango-kitita kusaidia washiriki wako kuelewa maudhui.

UTANGULIZI

Watu wa kila aina katika nchi mbalimbali hukumbwa na matatizo yanayotokana na ukosefu wa uhuru wa dini au imani. Kinachotofautiana ni nani anayeathirika, ukali wa ukiukwaji huo, na ni nani anayefanya ukiukwaji huo.



Katika uwasilishaji huu, tutasikia hadithi halisi kuhusu ubaguzi, vizuizi vya haki, na ghasia.

Ukiukwaji huu hufanywa na serikali na pia na watu wa jamii. Mara nyingi, tunafanya tunarejea ya haya kama ukiukwaji wa serikali na uhasama wa kijamii. Hata hivyo, ukiukwaji pia unaweza kufanyika ndani ya familia na ndani ya jamii za waumini.

Kuna aina ya nne ya ukiukwaji: Kushindwa kwa serikali kulinda watu dhidi ya ukiukwaji katika jamii. Serikali ina jukumu la kulinda kila binadamu ndani ya mipaka yake dhidi ya ubaguzi, vizuizi visivyo na msingi vya haki zao, na ghasia. Serikali nyingi zinashindwa kufanya hivyo.



Ubaguzi, vizuizi vya haki, na ghasia mara nyingi huingiliana na kushirikiana. Kizuizi kinaweza kuwa cha kibaguzi na pia kuchangia ghasia. Aidha, ukiukwaji wa serikali na uhasama wa kijamii mara nyingi huchocheana, na kuunda mzunguko unaoendelea.

Sheria za nchi zilizotungwa ambazo zinabagua makundi madogo huendeleza hali ya kutovumiliana katika jamii, na kusababisha ubaguzi, unyanyasaji, na ghasia. Ikiwa mamlaka hazichukui hatua dhidi ya ukiukwaji katika jamii, watu huhisi kuwa wanaweza kufanya ukatili bila madhara yoyote, na hali inazidi kuwa mbaya.

Tuangalie mifano halisi ya ubaguzi, vizuizi, na ghasia katika sehemu mbalimbali za dunia. Pengine baadhi ya mifano hii inahusiana na yale uliyoshuhudia au kuyapitia wewe mwenyewe.

HADITHI ZA UBAGUZI



Ubaguzi ni jambo la kawaida na huathiri nyanja zote za maisha
Mchungaji Kumar ni kiongozi wa Kikristo katika eneo la vijijini Sri Lanka. Yeye na familia yake wamekumbwa na ubaguzi kutoka kwa jamii ya Wabudha walio wengi kijijini mwao. Watoto wake wameteswa na kudhalilishwa na walimu pamoja na wanafunzi wenzao. Isitoshe, mamlaka zilikatiza huduma za umeme na maji kwa madai kuwa nyumba yao ni sehemu haramu ya ibada.[1]



Serikali zingine hubagua katika ugawaji wa fedha za umma – kwa mfano, kuwekeza rasilimali chache sana katika miundombinu, afya au elimu katika maeneo ya jamii za watu walio wachache. Hali hii inaweza kuleta hatari za muda mrefu za mvutano wa kijamii na machafuko ya kisiasa.

Ubaguzi pia unaweza kujidhihirisha katika utendaji wa taasisi. Kwa mfano, watoto wa shule wanaweza kubaguliwa, kulazimishwa kushiriki shughuli za kidini zinazokinzana na imani zao, au kufundishwa kupitia vitabu vya kiada vinavyosema mabaya kuhusu jamii zao. Katika baadhi ya matukio nadra, makundi fulani huzuiwa kabisa kupata elimu. Kwa mfano, waumini wa dini ya Kibaha'i hawaruhusiwi kujiunga na vyuo vikuu nchini Iran.[2]

HADITHI ZA VIKWAZO NA UBAGUZI

Sheria nyingi huweka vikwazo vinavyosababisha ubaguzi kwa njia moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja. Kanuni za upangaji miji, ambazo huonekana kuwa za kawaida, mara nyingi hutumika kuwazuia wachache kujenga maeneo ya ibada.

Katika Urusi, makundi mbalimbali ya jamii za watu wachache yamekumbwa na changamoto kama vile kunyimwa vibali vya manispaa vya ujenzi wa nyumba za ibada au kuvunjwa mikataba ya upangishaji mara baada ya ujenzi kuanza ama majengo yanapovunjwa.begun,[3]



Sheria zinazosimamia usajili wa jumuiya za kidini pia zinaweza kuwa kandamizi na zenye ubaguzi. Kwa mfano, serikali ya Algeria inawataka makundi yote – ya kidini au vinginevyo – kujisajili kama vyama rasmi kabla ya kuendesha shughuli zao. Hata hivyo, jamii ndogo ya Ahmadi haijapewa usajili huo. Kufikia mwisho wa mwaka 2020, kulikuwa na kesi 220 za kisheria dhidi ya wanachama wa jumuiya hii waliokuwa wakishtakiwa kwa makosa kama vile kufanya ibada katika maeneo yasiyoruhusiwa.[4]

Baadhi ya serikali pia huweka vikwazo kwa waumini wa dini inayotawala katika nchi zao. Mwaka 2020, maafisa katika mkoa wa Lebap nchini Turkmenistan waliamuru wafanyakazi wa serikali – wakiwemo walimu na wauguzi – kutohudhuria sala za Ijumaa misikitini. Wale waliopatikana wakihudhuria walitishiwa kufukuzwa kazi.[5]

[1] Nyenzo zilizopo
[2] The Guardian, https://www.theguardian.com/world/2013/feb/27/bahai-student-expelled-iranian-university
[3] Forum 18, https://www.forum18.org/archive.php?article_id=2508
[4] US State Dept., https://www.state.gov/reports/2020-report-on-international-religious-freedom/algeria/
[5] Forum 18, https://www.forum18.org/archive.php?article_id=2555

Hebu tuzingatie aina mbili zaidi za sheria zinazoweza kuleta vikwazo: Sheria za Familia na sheria za Kufuru au Uasi wa imani.

SHERIA ZA FAMILIA

Sheria zote za kidunia na za kidini zinazosimamia ndoa, talaka, urithi, na malezi ya watoto zinaweza kukiuka haki na kusababisha ubaguzi.

Nchini India, Sheria Maalum ya Ndoa inawataka wanandoa wa dini tofauti kutoa taarifa kwa hakimu siku 30 kabla ya ndoa. Hakimu huchunguza maombi hayo na kutuma taarifa kwa familia za wanandoa. Hili huweka wanandoa wengi katika hatari ya kushambuliwa kwa misingi ya heshima ya familia.[6]

Revathi Massosai ni raia wa Malaysia. Alizaliwa na wazazi Waislamu lakini alilelewa kama Mhindu na bibi yake wa upande wa mama. Mahakama ya kidini ilimpeleka Revathi katika kituo cha elimu ya Kiislamu kwa miezi sita kwa sababu alimuoa Mhindu na alikataa kurudi katika Uislamu.[7]



Mara nyingine, sheria za familia za kidini na zile za sheria za uasi wa imani huyaweka makundi madogo katika hatari ya kushambuliwa kijinai.
Kila mwaka, mamia ya wasichana Wahindu na Wakristo nchini Pakistan hukumbwa na utekaji nyara, ubadilishwaji wa imani kwa lazima, na ndoa za kulazimishwa. Hili lilimtokea Maira Shahbaz alipokuwa na umri wa miaka 14. Wazazi wake walienda mahakamani kudai arudishwe, lakini kwa kuwa kuacha Uislamu kunakatazwa Pakistan, na wazazi Wakristo hawawezi kuwa na haki ya malezi ya mtoto Mwislamu, mahakama Kuu iliamua Maira arudishwe kwa mtu aliyemteka. Wiki mbili baadaye, Maira alitoroka. Sasa anaishi mafichoni na anapambana kupata ndoa yake ibatilishwe na hadhi yake ya kisheria irejeshwe kuwa Mkristo.[8]

SHERIA ZA MAKUFURU NA UKENGEUFU WA IMANI

Sheria zinazohusu kufuru na uasi wa imani (kuacha dini yako) mara nyingi hutetewa kwa hoja ya kudumisha amani ya jamii. Hata hivyo, sheria hizi zinaweza kuwa na athari tofauti. Katika baadhi ya nchi, hutumiwa vibaya kwa mashitaka ya uongo kwa madhumuni ya kulipiza kisasi. Sheria hizi mara nyingi hudhibiti uhuru wa kujieleza na tabia kwa namna inayozuia uhuru wa dini au imani, hasa kwa watu wanaoshikilia imani tofauti na zile zinazopendelewa na serikali au jamii kubwa.

Waahmadiya, ambao wanaamini katika nabii baada ya Muhammad, pamoja na wasioamini katika Mungu na watu wanaokosoa serikali au viongozi wa kidini, mara nyingi wako hatarini. Hata hivyo, yeyote anaweza kuwa mwathirika wa sheria hizi.

---

[6] The Leaflet, https://www.theleaflet.in/india-needs-to-overhaul-laws-on-interfaith-marriage-and-religious-conversion/
[7] Forum Asia, https://www.forum-asia.org/?p=7086
[8] UK Parliament, https://edm.parliament.uk/early-day-motion/57474/maira-shahbaz-and-child-abduction-forced-conversion-and-marriage-in-pakistan

Mnamo mwaka wa 2020, mahakama ya kidini kaskazini mwa Nigeria ilimhukumu mtoto wa Kiislamu mwenye umri wa miaka 12 kifungo cha miaka 10 gerezani baada ya kushutumiwa kwa kumtukana Mtume. Hukumu hiyo ilibatilishwa na mahakama ya rufaa ya sheria za kiulimwengu mwaka wa 2021, lakini hatari ya mashambulizi ya kulipiza kisasi imeifanya familia yake isiwe salama kuishi katika eneo hilo. [9]



Kwa mujibu wa sheria za kimataifa, aina ya hotuba inayopaswa kupigwa marufuku ni ile inayochochea vurugu. Badala ya kuzuia ghasia, sheria za kufuru na uasi wa imani mara nyingi huchochea machafuko kwa kuendeleza dhana kwamba watu wanaoeleza kwa amani imani ambazo hazikubaliki na wengi basi wanapaswa kuadhibiwa.



UFUATILIAJI NA UDHIBITI WA SERIKALI

Eneo jingine ambapo serikali huweka vikwazo ni kupitia ufuatiliaji, uchunguzi na udhibiti wa shughuli na fedha za jumuiya za kidini. Kwa mfano, baadhi ya makanisa nchini Sri Lanka yanaripoti kuwa yanachunguzwa na mamlaka za serikali.[10] **Hii ni sehemu ya mpango mpana wa kubana uhuru wa asasi za kiraia.**

Hakuna mahali ambapo ufuatiliaji ni mkali zaidi kuliko magharibi mwa China, ambako teknolojia ya utambuzi wa nyuso imetengenezwa ili kuwezesha kamera za ulinzi kuwatambua watu jamii ndogo ya Waislam ya Uighur, na kuwajulisha polisi kuhusu mahali walipo.[11]

VIKWAZO VYA KIJAMII

Haki pia zinaweza kubanwa ndani ya familia, makundi ya kidini, au jamii kwa ujumla. Hili mara nyingi huathiri wanaume na wanawake kwa njia tofauti. Wanawake mara nyingi hukosa fursa – kwa mfano, fursa ya kusomea teolojia – na tabia zao pamoja na ibada zao za kidini zinaweza kudhibitiwa na familia au jamii kwa misingi ya dini.

Jamii zinazotawaliwa na dini fulani mara nyingi pia huweka vikwazo kwa wanawake wa makundi madogo ya kidini, kwa mfano kwa kuwalazimisha kuficha utambulisho wao wa kidini ili wapate ajira.



Maria ni msichana Mkristo anayeishi Misri. Baada ya kuhitimu chuo kikuu, alipewa kazi katika benki lakini akaambiwa kwamba endapo angeikubali, angehitajika kuvaa hijabu. Maria hakufikiri kuwa ni haki kujifanya kuwa wa dini tofauti ili apate kazi, hivyo akakataa nafasi hiyo. [12]

[9] BBC news, https://www.bbc.com/news/world-africa-55756834
[10] Nyenzo zilizopo
[11] New York Times, https://www.nytimes.com/2019/04/14/technology/china-surveillance-artificial-intelligence-racial-profiling.html
[12] Chanzo: Maria, ambaye jina lake limebadilishwa kwa sababu za kiusalama.

HADITHI ZA UKATILI

Sasa hebu tuangalie ukatili. **Matamshi ya chuki na uhalifu wa chuki ni miongoni mwa aina za ukatili zinazopatikana kwa wingi. Maeneo ya ibada na waumini wanaohudhuria huwa katika hatari kubwa ya kushambuliwa kwa misingi ya chuki.**

Nchini Brazil, wafuasi wa dini za jadi za Kiafro-Brazil wanakumbwa na mashambulizi ya kikatili kutoka kwa majirani zao Wakristo wa dhehebu la Pentekoste-mpya, ambao wanaamini kuwa dini hizo ni za kishetani. Kasisi Marcio, kuhani wa dini ya Candomblé, ameripoti zaidi ya mashambulizi 20 dhidi ya hekalu lake. Polisi hawajachukua hatua yoyote.[13]



Kwa mara nyingine tena, athari za ukatili huu zinawatofautisha wanaume na wanawake.
Wanawake Waislamu nchini Uswidi, hasa wale wanaovaa mavazi ya kidini kama hijabu, wana uwezekano mkubwa wa kushambuliwa kwa uhalifu wa chuki na watu wasiojulikana katika maeneo ya umma. Kwa upande mwingine, wanaume Waislamu wanakumbwa na uhalifu wa chuki kutoka kwa majirani au wenzao wa makazini.[14]



Katika maeneo mengi, janga la virusi vya korona lilizidisha mifumo iliyokuwepo ya ubaguzi na chuki. Waislamu nchini India walilaumiwa kwa kufanya *jihad* ya korona baada ya mlipuko wa virusi kutokea kufuatia tamasha la kidini la Kiislamu. Ahmed Shaikh ni mfanyabiashara mdogo wa Kiislamu anayepambana kujikimu. Mnamo Aprili 2020, kundi la wanaharakati wa Kihindu wenye msimamo mkali lilimwamuru afunge biashara yake na kuondoka kwa madai kwamba Waislamu walikuwa wakieneza virusi vya korona kimakusudi. Ahmed aliomba msamaha, lakini alishambuliwa vibaya kwa kupigwa kwa marungu. Alijaribu kuripoti tukio hilo kwa polisi, lakini walikataa kulisajili wakidai kuwa biashara ya mitaani ni haramu.[15]

Aina mbaya zaidi za ukatili ndani ya jamii ni ghasia za kijamii na mashambulizi ya kigaidi.
Mchungaji Samuel anatoka kaskazini mwa Burkina Faso. Taifa hili limekuwa na historia ya kuvumiliana kwa dini mbalimbali, lakini makundi ya kigaidi yameanza kuharibu utamaduni huo. Mnamo 2019, mashambulizi dhidi ya makanisa yakawa sehemu ya mkakati wa magaidi hao. Hivi sasa, Mchungaji Samuel anaishi katika kambi ya wakimbizi wa ndani baada ya kukosa makazi.

> "Mashambulizi haya yameharibu maisha ya watu wetu. Tumejawa na maumivu," anasema.

Mashambulizi ya kigaidi yameongezeka tangu mwaka wa 2019, yakiwaathiri watu wote, huku zaidi ya watu milioni moja wakilazimika kuhama makazi yao.[16]

---

[13] RioOnWatch, https://rioonwatch.org/?p=40117
[14] The Swedish National Council for Crime Prevention, https://www.bra.se/om-bra/nytt-fran-bra/arkiv/press/2021-03-31-islamofobiska-hatbrott-yttrar-sig-i-manga-olika-former.html
[15] Sabrang India, https://sabrangindia.in/article/stop-targeting-discriminating-against-and-attacking-vendors-and-hawkers-national-hawker
[16] Open Doors UK, https://www.opendoorsuk.org/persecution/world-watch-list/burkina-faso

Ingawa takwimu za kimataifa zinaonyesha kuwa makundi yenye uhusiano na Uislamu yanahusika sana na ugaidi, kuna maeneo mengi ambapo makundi mengine yanatoa tishio kubwa zaidi. Katika baadhi ya nchi za Magharibi, vyombo vya usalama vinaona kuwa wazungu wenye msimamo mkali na wafuasi wa itikadi kali za mrengo wa kulia ndio tishio kubwa zaidi la ugaidi wa ndani. [17] Makundi haya hulenga jamii za watu wachache. Mnamo 2018, watu kumi na moja waliuawa katika sinagogi moja huko Pittsburgh, Marekani, na mnamo 2019, watu hamsini na moja waliuawa katika msikiti wa Christchurch, New Zealand mwaka 2019.

Ukatili unaotekelezwa na polisi, vikosi vya usalama, wanajeshi, au hata makundi yanayoajiriwa na serikali unaweza kulenga watu binafsi au jamii nzima. Hali ya Wauighur katika magharibi mwa China inaonyesha jinsi ghasia za serikali zinavyoweza kufikia kiwango cha juu cha ukatili. Wanawake wa Kiuighur wamelazimishwa kufanyiwa upasuaji wa kuzuia uzazi na kutumia njia za uzazi wa mpango kwa lazima, hali ambayo imesababisha kushuka kwa idadi ya watoto wanaozaliwa. Zaidi ya watu milioni 1.8 wa jamii hiyo wamepelekwa katika kambi za "marekebisho ya tabia" kwa sababu kama za kuvaa hijabu au kuwa na ndevu. Kuna ripoti za mateso na ubakaji ndani ya kambi hizo, ambako wafungwa hunyimwa kutumia lugha yao na dini yao, na badala yake hulazimishwa kuamini itikadi ya serikali. Serikali ya China inadai kuwa kambi hizi ni vituo vya elimu ya hiari.[18]

WAJIBU NA UZEMBE WA SERIKALI



Mwishowe tuchunguze kushindwa kwa serikali kuwalinda watu. **Serikali zina jukumu la kulinda haki za binadamu. Zinaposhindwa kufanya hivyo, ubaguzi na ghasia huongezeka. Hata hivyo, hatua madhubuti za polisi katika kesi za kibinafsi zinaweza kusaidia kuzuia ukiukwaji wa haki.**

Mnamo mwaka 2017, mwanamke mzee aliyebadili dini kutoka Uislamu kwenda Ukristo alifariki huko kusini mwa Kyrgyzstan. Binti yake alipomzika katika makaburi ya manispaa, kundi la watu likiongozwa na imamu wa eneo hilo lilipinga vikali. Mwili wake ulifukuliwa mara kadhaa hadi jamii ilipocharuka na mamlaka za serikali kuingilia kati. Waliotekeleza kitendo hicho walifunguliwa mashtaka, na baada ya tukio hilo, kauli kali dhidi ya watu waliobadili dini zilipungua kwa kiasi kikubwa.[19]



Mara nyingi, mamlaka hushindwa kuingilia kati ili kuzuia ukiukwaji wa haki unaofanyika ndani ya familia au jumuiya za kidini. Nadia, mwanafunzi wa Kikristo mwenye umri wa miaka 22 nchini Jordan, alipendana na mwanafunzi mwenzake Muislamu. Wazazi wake walipogundua, walimzuia kutoka nje na wakamtesa. Nadia alifanikiwa kutoroka, lakini miezi miwili baadaye baba yake alimtafuta na kumuua. **Mahakama iliona kuwa aliua kwa sababu ya 'heshima ya familia,' na ikazingatia hiyo kama sababu ya kumpunguzia adhabu, hivyo hakufungwa jela.**[20]

[17] United States Congress, https://www.congress.gov/116/bills/s894/BILLS-116s894is.xml
[18] The Guardian, https://www.theguardian.com/world/2020/sep/04/muslim-minority-teacher-50-tells-of-forced-sterilisation-in-xinjiang-china
[19] Forum 18, https://www.forum18.org/archive.php?article_id=2248
[20] Nyenzo zilizopo

HITIMISHO



Katika mada hii, tumechunguza ubaguzi, vikwazo, na ghasia zinazofanywa na serikali na wanajamii. Pia tumeangalia kushindwa kwa serikali kuwalinda watu.

Kutokana na simulizi tulizosikia, tunaweza kufikia hitimisho kadhaa:

- Ukiukwaji wa haki hutokea katika nchi zote na huathiri watu wa dini au imani zote. Kinachotofautiana ni nani anaathirika, kiwango cha ukiukwaji, mara ngapi hutokea, na iwapo serikali inahusika moja kwa moja katika uvunjaji huo.

- Sheria na sera mbalimbali za serikali zinaweza kuchangia ukiukwaji wa haki.

- Mara nyingi, jamii za watu wachache huathirika zaidi, pamoja na wale wanaotofautiana nao kimaoni ndani ya jamii kubwa. Hata hivyo, hata jamii kuu huathirika, hususan kupitia mashambulizi ya kigaidi.

- Hadithi tulizosikia zinaonyesha jinsi ukiukwaji wa uhuru wa dini au imani mara nyingi huambatana na ukiukwaji wa haki zingine, kama vile haki ya kupata elimu, haki ya ndoa, au hata haki ya kuishi. Aidha, kuna tofauti kubwa kwa jinsi wanaume na wanawake wanavyoathirika – iwe ni kwa uhalifu wa chuki, ndoa za kulazimishwa, mauaji ya "heshima," au hata upasuaji wa kulazimishwa wa uzazi.



- Baadhi ya hadithi tulizosikia zinadhihirisha jinsi ukiukwaji wa haki ndani ya jamii, kushindwa kwa serikali kuchukua hatua, na ukiukwaji wa haki unaofanywa na serikali vinavyoweza kushabihiana na kuunda mzunguko usioisha wa unyanyasaji.

Ukiukwaji wa uhuru wa dini au imani husababisha mateso makubwa kwa watu wa kawaida. Pia huchangia katika hali ya kutokuwa na utulivu wa kijamii, kiuchumi na kisiasa. Hatimaye, kila mtu huathirika kutokana na hali hii.

Haijalishi sisi ni nani au tunatoka katika jumuiya gani ya kidini, sote tunanufaika wakati haki za kidini na imani zinaheshimiwa kwa watu wote katika nchi yetu. Vile vile, waumini wenzetu wanaoishi kama jamii ya watu wachache katika mataifa mengine wanatamani kuona haki sawa kwa wote. Haki sawa kwa kila mtu, kila mahali, ingewaletea wanadamu wote dunia iliyo na amani na usalama zaidi.

Matukio ya maigizo mafupi ya dakika mbili

Toleo lenye maelezo kwa wawezeshaji

Katika kurasa hizi, utapata hali za maigizo zilizopendekezwa kwa ajili ya kipindi cha nne, zoezi la "Hali za maigizo mafupi ya dakika mbili kuhusu uhuru wa dini au imani". Kila mfano unaelezea ukiukwaji tatu wa uhuru wa dini au imani, na kuna hali tano tofauti ambazo unaweza kuchagua.

Tukio: Mtaani na kazini

Mwanamke anaelekea kazini. Amevaa nguo zinazoonyesha utambulisho wake wa kidini wa jamii ya watu wachache. Mpita njia anaanza kumdhalilisha kwa sababu ya mavazi yake. Hakuna anayemsaidia. Anamuona ofisa wa polisi na anaomba msaada. Mdhalilishaji anakimbia lakini ofisa wa polisi hamsaidii kwa njia yoyote. Anafika ofisini kwake na anakutana na mfanyakazi mwenzake mdogo ambaye anasherehekea kupandishwa cheo. Kwa mara nyingine, yeye hakupewa nafasi ya kupandishwa cheo.

WAHUSIKA
Wahusika muhimu: mwanamke, mdhalilishaji, ofisa wa polisi, mpita njia, mfanyakazi mwenzake.
Wahusika wa ziada: Wafanyakazi wenzake na wapita njia.

UKIUKWAJI KATIKA TUKIO HILI

Hali hii inawakilisha udhalilishaji na ubaguzi kulingana na utambulisho wa kidini wa mtu na kushindwa kwa mamlaka kuchukua hatua yoyote.

- Uadui wa kijamii: udhalilishaji/uhalifu wa chuki.
- Kushindwa kwa serikali kulinda: ofisa wa polisi asiyesaidia.
- Uhasama wa kijamii: ubaguzi - kikwazo kwa watu wachache kazini.

Tukio: Maeneo ya ibada

Kundi dogo la kidini limepata ardhi na limepewa kibali cha kujenga mahali pa ibada. Wanaanza ujenzi, lakini eneo la ujenzi linaharibiwa mara kwa mara. Wanawasiliana na polisi na mamlaka za mitaa, lakini wanadai kuwa hawawezi kufanya lolote. Hatimaye, wanakamilisha ujenzi, lakini kila mara watu wanapokwenda kuabudu, wanakumbana na matusi na vurugu kutoka kwa wanajamii walio wengi.

WAHUSIKA
Wahusika muhimu: Wawakilishi wawili kutoka kundi la watu wachache, afisa wa polisi, mwakilishi wa kiongozi wa mtaa, wawakilishi wawili kutoka kundi la watu wengi.
Wahusika wa ziada: Wawakilishi kutoka kundi la watu wachache na kundi la watu wengi.

UKIUKWAJI KATIKA TUKIO HILI

Hali hii inaangazia uadui wa kijamii kulingana na dini na kushindwa kwa mamlaka kuchukua hatua yoyote kuhusu hilo.

- Uadui wa kijamii: uharibifu wa eneo la ujenzi.
- Kushindwa kwa serikali kulinda: mamlaka hazichukui hatua.
- Uadui wa kijamii: udhalilishaji nje ya eneo la ibada.

Tukio: FORB shuleni

Mvulana wa miaka 12 kutoka jamii ya kidini ya jamii ya watu wachache anasoma katika shule ya msingi inayomilikiwa na serikali, na leo ni siku ya kawaida ya masomo. Siku inaanza kwa maombi yanayofanywa kwa mujibu wa dini ya jamii ya watu walio wengi, ambayo anahitajika kushiriki. Baada ya maombi, anaingia darasani kusomea historia, ambapo mwalimu anasoma kutoka katika kitabu cha kiada kinachozungumzia jamii ya kidini ya mvulana kwa maneno ya dharau. Wakati wa mapumziko baada ya somo, wanafunzi wenzake wanamnyanyasa na kumtenga kutoka kwenye michezo yao.

WAHUSIKA

Wahusika muhimu: mtoto wa kiume, mwalimu wa kuongoza maombi/somo la historia, wanafunzi wenzake wawili

Wahusika wa ziada: walimu wa ziada na wanafunzi wenzake

UKIUKWAJI KATIKA TUKIO HILI

Kisa hiki kinajikita katika ukiukwaji wa uhuru wa dini au imani uliohalalishwa na taasisi za serikali (mfumo wa elimu unaoidhinisha vitabu vya kiada, shule, na walimu) na jinsi unavyochangia uadui wa kijamii.

- Ukiukwaji wa serikali: Kumlazimisha mwanafunzi kushiriki maombi ya dini ya kundi la jamii ya watu walio wengi.
- Ukiukwaji wa serikali: Matumizi ya vitabu vya kiada vyenye lugha ya kibaguzi.

Tukio: FORB katika familia

Msichana wa miaka 17 anataka kwenda chuo kikuu kusomea ualimu. Wazazi wake wanagoma kumruhusu. Badala yake, wanataka aolewe ili kulinda heshima ya familia. Wanadai kuwa dini yao haihimizi elimu kwa wasichana, kwa kuwa jukumu la wake ni kubaki nyumbani. Msichana anakataa imani hizo na anataka kufanya maamuzi yake mwenyewe. Akihofia ndoa ya kulazimishwa, anakimbilia kwa rafiki yake mkubwa katika mji mwingine. Familia yake inaripoti kupotea kwake kwa polisi. Polisi wanapompata, wanamrudisha kwa wazazi wake bila ridhaa yake. Siku inayofuata, anaolewa na mwanamume asiyemfahamu na hapewi ruhusa ya kutoka nje ya nyumba yake.

WAHUSIKA

Wahusika muhimu: msichana, mama na baba yake, rafiki, afisa polisi, mume wa msichana.

Wahusika wa ziada: wanafamilia wa ziada, watu wanaohudhuria harusi, maafisa polisi wa ziada.

UKIUKWAJI KATIKA TUKIO HILI

Igizo hili linaangazia muingiliano kati ya haki za wanawake na FORB.

- Uadui wa kijamii (ukiukwaji ndani ya familia): Kukataa kuruhusu elimu ya msichana.
  Hii ni kinyume na haki yake ya elimu na haki yake ya kuamua anachoamini (k.m kuhusu maoni ya Mungu juu ya elimu ya wasichana) na kutenda ipasavyo. Kwa njia hii, ni ukiukwaji wa haki yake ya elimu na haki yake ya FORB.

UKIUKWAJI KATIKA TUKIO HILI

- Kushindwa kwa serikali kulinda: Polisi wanamrudisha msichana kwa wazazi wake licha ya kuwa yuko hatarini kuolew a kwa kulazimishwa.
- Uadui wa kijamii (ukiukwaji ndani ya familia): Ndoa ya kulazimishwa na kunyimwa uhuru wa kutembea.

ZINGATIA

Kulingana na sheria za kimataifa, wazazi wana haki ya kuwalea watoto wao kwa mujibu wa imani zao, lakini wanapaswa pia kuheshimu uwezo wa mtoto unaokua wa kufanya maamuzi binafsi kuhusu dini au imani (na mambo mengine ya maisha).

Tukio: Kupaza sauti – ufisadi na vurugu

Mwanafunzi wa chuo kikuu cha serikali anaripoti ukatili wa kijinsia unaofanywa na mhadhiri kwa gazeti la wanafunzi. Mwandishi wa habari wa chuo anamhoji mkuu wa chuo kuhusu suala hilo. Uongozi wa chuo unataka kuficha habari hiyo, hivyo wanazusha uvumi mitandaoni kwamba mwandishi wa habari amekashifu imani za kidini na viongozi wa dini. Kundi la watu wenye hasira linakusanyika chuoni likidai kwamba mwandishi na gazeti la wanafunzi wamefanya kufuru. Chuo kinatumia hali hii kama kisingizio cha kufunga gazeti hilo. Polisi wanamkamata mwandishi wa habari kwa tuhuma za kukufuru.

WAHUSIKA
Wahusika muhimu: mwanafunzi, mwandishi wa habari, mkuu wa chuo, wanachama wawili wa kundi lenye hasira, ofisa wa polisi.
Wahusika wa ziada: wanachama wa kundi lenye hasira.

UKIUKWAJI KATIKA TUKIO HILI

Kisa hiki kinaonyesha mwingiliano kati ya uhuru wa kujieleza, kujiunga na makundi, na uhuru wa dini au imani , pamoja na uhusiano kati ya ukiukwaji wa haki za binadamu na ufisadi.

- Ukiukwaji wa serikali: c huo kinatumia madai ya kidini kuficha uhalifu.
- Uadui wa kijamii: k undi lenye hasira linafanya vurugu.
- Ukiukwaji wa serikali: p olisi wanamkamata mwandishi wa habari na kufunga gazeti la wanafunzi, kinyume na haki za uhuru wa kujieleza na kujiunga na makundi.

Hadithi ya wanamabadiliko

Hadithi ifuatayo inasomwa kama sehemu ya Maoni ya hitimisho kipindi cha 4. Inaonyeshwa kwenye slaidi 41-44 za uwasilishaji wa PowerPoint ya kipindi hicho.

HADITHI

Hadithi ya Mchungaji James na Imam Ashafa

Huyu ni Mchungaji James na Imam Ashafa. Mnamo mwaka wa 1992, walikuwa vijana wakiongoza makundi hasimu ya wanamgambo waliopigana vikali dhidi ya wao kwa wao wakati wa mgogoro wa kidini kaskazini mwa Nigeria. Mchungaji James alipoteza mkono wake katika mapambano hayo ya ghasia, huku Imam Ashafa akimpoteza mwalimu wake wa kiroho pamoja na jamaa zake wawili wa karibu. Wawili hawa wakawa maadui wakubwa na wakaapa kulipiza kisasi.

Miaka michache baadaye, mkutano wa bahati mbaya ulibadilisha kila kitu. Wakati wa mkutano wa viongozi wa jamii kuhusu chanjo ya watoto dhidi ya polio, viongozi hawa wa kidini walikutanishwa na rafiki yao wa pamoja. Rafiki huyo alishika mikono yao na kuwaambia, "Ninajua kuwa mna uwezo wa kudumisha amani katika jimbo hili. Nataka mzungumze."

Ingawa hakuna hata mmoja aliyekuwa na nia ya kuzungumza na mwenzake, waligundua kuwa walishirikiana katika mapenzi yao kwa Nigeria na kujitolea kwa maendeleo ya nchi yao.

"Chuki yangu dhidi ya Waislamu wakati huo haikuwa na mipaka," anakumbuka Mchungaji James. "Tunamshukuru Mungu kwamba tumejifunza uwezo huu wa kusikilizana na kuunda mazingira salama ya mazungumzo, kwani bila hilo, daima tutakuwa tukihisi mambo kutoka mbali," anaendelea. "Tumepata funzo gumu."

Imam Ashafa anakumbuka kuwa baada ya ghasia za Kaduna mwaka wa 1992, yeye na kundi lake la wanamgambo walipanga kulipiza kisasi. Lakini siku moja, alipokuwa akisali msikitini, alitafakari na kugundua kuwa, "Qur'an inafundisha kwamba ni bora kutumia wema kubadili uovu. Kwa hivyo, ikiwa wewe ni Mwislamu na unakataa kuwasamehe wale waliokudhuru, utawezaje kuwa mfano halisi wa Muhammad?"

Viongozi hawa wawili wa kidini walipambana na tamaa yao ya kulipiza kisasi. Lakini pia walitambua kuwa hawawezi kuwa viongozi wa kweli ikiwa mioyo yao imejaa chuki.

Uaminifu kati ya Imam Ashafa na Mchungaji James ulianza kukua taratibu lakini kwa uthabiti. Mahusiano yao yakageuka kuwa urafiki, uliosababisha kuanzishwa kwa Kituo cha Upatanisho cha Kiimani kati ya Waislamu na Wakristo.

Kituo hiki kinahamasisha kuishi kwa amani na kina lengo la kuzuia kurejea kwa migogoro ya kidini yenye ghasia katika eneo hilo. Kimechangia kupatikana kwa makubaliano ya amani baada ya machafuko nchini Nigeria na kwingineko, na kinafundisha mashirika ya kidini ya kijamii jinsi ya kushiriki katika utetezi wa kuishi kwa amani miongoni mwa watu wa imani zote.

Chanzo
Tanenbaum. https://tanenbaum.org/peacemakers-in-action-network/meet-the-peacemakers/imam-muhammad-ashafa-pastor-james-wuye/

KIPINDI CHA 5

Uhuru wa dini au imani katika jamii yetu

Muhtasari wa kipindi

Vipindi vitatu vilivyopita vimetumiwa kujifunza kuhusu haki za binadamu ya uhuru wa dini au imani na ukiukwaji wa haki hiyo, kutafakari mitazamo yetu kuhusu haki hiyo, pamoja na kuchunguza masuala ya utambulisho, upendeleo na changamoto zinazoyakumba makundi mbalimbali. Kwa msingi wa mafunzo hayo, kipindi cha tano kinawaongoza washiriki kupitia mchakato shirikishi wa kuandaa uchambuzi wa muktadha wa uhuru wa dini au imani katika maeneo yao au nchi zao.

Hiki ni kipindi cha mwisho cha Sehemu ya Kwanza ya mafunzo haya. Uchambuzi wa muktadha unaoandaliwa utatumika kama sehemu ya marejeo katika Sehemu ya Pili ya mafunzo.

Malengo ya mafunzo

Kipindi hiki kinazingatia kukuza ujuzi wa uchambuzi wa muktadha.

Mpaka kufikia mwisho wa kipindi, washiriki wataweza:

- Kufafanua matatizo na ukiukwaji wa uhuru wa dini au imani unaowakumba watu na makundi mbalimbali katika jamii yao.
- Kubainisha jinsi ukiukwaji wa uhuru wa dini au imani unavyoathiri wanawake na wasichana kwa njia tofauti na wanaume na wavulana katika jamii.
- Kuhisi na kuelewa changamoto zinazowakumba watu wa jamii nyingine wanaoathiriwa na ukiukwaji wa uhuru wa dini au imani.

Yaliyomo katika kipindi na muda

Ukaribisho na utangulizi	Dakika 3
Zoezi la ufunguzi: Mtandao wa mazuri Washiriki wanatambua mambo mazuri kuhusu jamii yetu.	Dakika 12
Uwasilishaji: Mambo yanavyokuwa mabaya zaidi (mazuri zaidi) Utangulizi wa zana ya uchambuzi wa muktadha inayoitwa hatua tatu za mateso.	Dakika 10
Zoezi la ramani: Ramani ya uhuru wa dini au imani ya mji wetu, sehemu ya 1 Washiriki wanaunda msingi wa uchambuzi wa muktadha wa uhuru wa dini au imani kupitia zoezi shirikishi.	Dakika 60
Zoezi la kuchangamsha: Tembea kisha simama Zoezi la kimwili la kufurahisha ambapo washiriki hufanya kinyume cha wanachoambiwa.	Dakika 5
Mjadala wa pamoja: Ramani ya uhuru wa dini au imani ya mji wetu, sehemu ya 2 Washiriki wanachambua yale waliyoandaa katika sehemu ya kwanza ya zoezi.	Dakika 25
Maoni ya hitimisho na hadithi ya wanamabadiliko Kipindi kinahitimishwa kwa mtazamo wa matumaini baada ya kujadili changamoto.	Dakika 5
JUMLA YA MUDA	**Saa 2**

IWAPO UNAHITIMISHA MAFUNZO BAADA YA KIPINDI CHA 5

Ikiwa huna nia ya kuendesha 'Sehemu ya 2: Safari kuelekea mabadiliko' au ikiwa baadhi ya washiriki hawatashiriki katika Sehemu ya 2, huenda ukahitaji kuongeza shughuli zifuatazo mwishoni mwa kipindi hiki. Unaweza kutenga muda kwa kufanya mabadiliko, kama vile kuacha zoezi la 'Mtandao wa mazuri' na kufupisha zoezi la ramani kwa dakika 10, au kuendesha kipindi kirefu zaidi.

Zoezi la tathmini: Kichwa, moyo, mikono Linasaidia washiriki kutafakari kile wanachopata kutoka kwenye mafunzo haya	Dakika 15
Shukrani na kuaga Usisahau kusherehekea mafanikio!	Dakika 5

Jiandae

Jiandae kwa kipindi kwa kufuata mwongozo uliopo kwenye ukurasa wa 15, Jinsi ya kujiandaa kwa kila kipindi. Kumbuka – unawafahamu vyema washiriki wako! Unaruhusiwa kurekebisha na kubadilisha vipengele vyovyote vya kipindi ili kivutie na kuendana na mahitaji yao.

USOMAJI WA ZIADA

Mbali na kusoma nyenzo za kipindi, ni muhimu sana kujiandaa kwa kusoma hali ya uhuru wa dini au imani (kwa watu wa imani zote na wasio na imani) katika nchi yako. Mara nyingi, tunajua tu changamoto zinazowakumba kikundi chetu au vikundi vikubwa zaidi katika jamii. Kusoma kidogo kuhusu hali hii kutakuwezesha kusaidia washiriki wako zaidi!

Unaweza kupata vidokezo vya mahali pa kupata taarifa hizi katika kurasa za 153-154.

NYENZO ZA KIPINDI HIKI

Mbali na nyenzo za kawaida kwa kila kipindi zilizoorodheshwa kwenye ukurasa wa 16, utahitaji nyenzo zifuatazo kwa ajili ya kipindi hiki:

- Mpira laini wa uzi au kamba kwa ajili ya zoezi la Mtandao wa mazuri.
- Karatasi kubwa ya mawasilisho iliyotayarishwa awali kwa ajili ya zoezi la Ramani ya uhuru wa dini au imani ya mji wetu.
- Ikiwa unafanya zoezi la tathmini 'Kichwa, moyo, mikono', unahitaji nakala moja ya kijitabu cha zoezi kwa kila mshiriki.

NYENZO ANDAMIZI za kipindi hiki zinaweza kupatikana hapa.

ANDAA UKUMBI

Kwa kipindi hiki, ni vyema kupanga viti katika nusu duara vikielekea mbele, huku kukiwa na nafasi kubwa katikati. Kikundi kinapaswa kuwa na nafasi ya kusogea kwa urahisi. Chumba kikubwa kisicho na madawati kitakuwa bora zaidi!

‘Ramani ya uhuru wa dini au imani ya mji wetu’

“Washiriki walifurahia zoezi la uhuru wa dini au imani katika mji wetu – lilifanya kazi vizuri kabisa. Liliwapa fursa ya kutafakari ukiukwaji wanaokutana nao katika maisha ya kila siku na kuchochea mazungumzo ya kina. Ni zoezi bora kwa kukuza ubunifu, uchambuzi, fikra yakinifu, na ujuzi wa kazi ya pamoja.”

HAMMAM HADDAD, MWEZESHAJI, JORDAN

Mpango wa kina wa kipindi

1. **Ukaribisho** Dakika 3

GUMZO FUPI

NINI CHA KUSEMA

Karibisha kila mmoja kwenye kipindi hiki. Anzisha kipindi kwa kueleza yafuatayo:

- Katika vipindi vitatu vilivyopita, tulitazama haki za binadamu ya uhuru wa dini au imani. Tumeelewa haki tulizonazo na aina mbalimbali za ukiukwaji zinazoweza kutokea. Pia, tumetafakari juu ya maana ya haki hii kwetu na kuchunguza masuala ya utambulisho, fursa, na changamoto.
- Katika kipindi hiki, tutazingatia kuchambua muktadha wetu ili kutambua matatizo wanayoweza kukumbana nayo watu au makundi mbalimbali. Tutafanya hivyo kwa kuchora 'ramani' inayoonyesha hali ya uhuru wa dini au imani katika eneo letu. Lakini kabla ya kuangalia changamoto, tuanze na mazuri!

2. **Zoezi la kufunguzi: Mtandao wa mazuri** Dakika 12

ZOEZI LA PAMOJA

ZINGATIA

Zoezi hili ni la kufurahisha na linaonyesha hoja fulani, lakini si la lazima katika mchakato wa kipindi. Huenda ukapendelea kuliondoa ili kutoa muda zaidi kwa mjadala wa pamoja kuhusu "ramani ya uhuru wa dini au imani ya mji wetu", ambao una muda mfupi.

MAELEZO NA LENGO

Zoezi hili ni njia ya kufurahisha na ya kuonyesha kwa taswira mambo mazuri tunayoyathamini katika jamii yetu kabla ya kuanza kuangalia matatizo.

NYENZO

- Kibunda cha sufu (au uzi).

JINSI YA KUANZA ZOEZI

Omba kikundi kisimame kwenye duara. (Duara liwe na ukubwa unaoruhusu washiriki kutupiana mpira wa uzi kwa urahisi.)

Eleza yafuatayo:

- Tutakuwa tunatupiana kibunda cha uzi kutoka mtu mmoja kwenda kwa mwingine.
- Kabla ya kutupa kibunda, kila mtu anapaswa kukamilisha sentensi hii: "Jambo jema kuhusu kuishi katika mji wangu ni..." Mfano: "Jambo jema kuhusu kuishi katika mji wangu ni kuwa karibu na familia yangu" au timu ya mpira, au shule ya mtaa wetu. Huwezi kurudia jambo ambalo mtu mwingine tayari amesema, hivyo itakuwa changamoto zaidi kadri tunavyoendelea!
- Unapotupa mpira, shikilia sehemu ya uzi kwa mkono mmoja kisha utupe sehemu iliyobaki kwa mtu mwingine. Hii itaunda mtandao unaokuunganisha na mtu uliyemtupia na mtu aliyekutupia. Endelea kushikilia uzi kwa muda wote wa zoezi.

JINSI YA KUENDESHA ZOEZI
Anza zoezi mwenyewe kwa kukamilisha sentensi na kisha kumrushia mtu mwingine kibunda cha sufu upande wa pili wa mduara. Kumbuka kushikilia mwisho wa sufu! Taratibu, mtandao utaanza kuundwa kati ya washiriki.

JINSI YA KUHITIMISHA ZOEZI
Baada ya kila mshiriki kupokea sufu mara moja, simamisha zoezi lakini waombe waendelee kushikilia nyuzi.

Kamilisha kwa tafakari hizi:

- Angalieni nafasi kati yetu sasa inaonekanaje? Kama mtandao wa buibui au nyavu?
- Hata kama kipindi hiki kinahusu matatizo yanayokumba jamii yetu, kuna watu wazuri na mambo mazuri yanayotokea pia. Kuna mambo yanayofanya kazi!
- Ni muhimu kuyakumbuka haya tunapojaribu kushughulikia matatizo. Kwa sehemu, yanaweza kutupa nguvu na matumaini. Pia, mitandao ya watu wazuri na mambo mazuri inaweza kuwa rasilimali muhimu kutusaidia kushughulikia matatizo.

3. Uwasilishaji: Mambo yanavyokuwa mabaya zaidi (mazuri zaidi) Dakika 10

WASILISHO

MAELEZO NA LENGO
Uwasilishaji huu mfupi unalenga kuimarisha uelewa wa washiriki kuhusu jinsi ukiukwaji wa haki unavyoweza kuenea katika jamii. Pia, unawapa zana ya kuchambua muktadha wao, ambayo itatumika katika zoezi linalofuata la 'Ramani ya uhuru wa dini au imani ya mji wetu'.

NYENZO

- Nakala ya mwongozo inapatikana ukurasa wa 107 wa Kiongozi hiki.
- Nakala hiyo inahusiana na slaidi za 3-13 za PowerPoint ya kipindi na imejumuishwa kwenye maelezo ya wasemaji kwa slaidi hizi.
- Toleo linaloweza kuhaririwa la nakala linapatikana kati ya nyenzo zinazoambatanishwa na kipindi.

KIDOKEZO! Waombe watu waweke maswali/maoni yao hadi mwisho wa uwasilishaji wako.

MAANDALIZI YA AWALI
Jitayarishe kwa kufuata mwongozo uliotolewa kwenye ukurasa wa 15, "Jinsi ya kujiandaa kwa kila kipindi." Soma na kurekebisha nakala na slaidi za PowerPoint (au andaa bango-kitita kwa ajili ya hoja kuu kwenye slaidi) kisha fanya mazoezi ya kuwasilisha mada pamoja na slaidi/karatasi za maandishi.

4. Zoezi la ramani: Ramani ya uhuru wa dini au imani ya mji wetu, sehemu ya kwanza Dakika 60

ZOEZI LA PAMOJA

MAELEZO

Zoezi hili linatumia ramani iliyochorwa kwenye bango la mji kuonyesha na kuchambua ukiukwaji wa uhuru wa dini au imani katika muktadha wa washiriki. Wanatumia uzoefu wao binafsi pamoja na maarifa unayowaletea kama mwezeshaji. Zoezi hili lina sehemu mbili, na katikati yake kuna kichangamshi.

LENGO

Linawasaidia washiriki kuelewa jinsi masuala ya uhuru wa dini au imani yanavyowaathiri watu tofauti katika jamii yao na kuwapa ujuzi wa kuchora ramani ya ukiukwaji wa haki za binadamu kwa kutumia modeli rahisi ya taswira.

NYENZO

- Bango-kitita iliyotayarishwa awali yenye 'ramani' (angalia maelekezo hapa chini)
- Kalamu za kuandikia kwenye bango-kitita

MAANDALIZI YA AWALI

Ili kuchangia zaidi katika zoezi hili, soma taarifa kuhusu hali ya uhuru wa dini au imani nchini mwako. Angalia kurasa za 153-154 kwa nyenzo za kusoma.

Fanya maandalizi yafuatayo ya kivitendo kabla ya kipindi:

- **CHORA RAMANI YA UHURU WA DINI AU IMANI YA MJI WAKO**
  Panga pamoja karatasi nne za bango-kitita na kuziunganisha. Chora ramani ya kijiji au mji kwenye karatasi hizo. Ongeza michoro ya jumla au andika majina ya maeneo 10 tofauti ambapo watu wanaweza kukumbana na changamoto zinazohusiana na dini au imani. (Angalia mchoro kwenye ukurasa wa 98).
  Hapa chini kuna orodha ya maeneo yanayopendekezwa kujumuishwa kwenye ramani yako. Ondoa yale yasiyo husika katika muktadha wako na badala yake, jumuisha mengine yanayofaa zaidi. Hakikisha unajumuisha nyumba za watu, maeneo ya ibada, maeneo ya umma kama maduka, maeneo ya rasmi kama kituo cha polisi.
  Unapochora ramani, acha nafasi ya kutosha kati ya maeneo, lakini weka pamoja yale yanayohusiana kwa karibu, kwa mfano, ofisi mbalimbali za serikali. Usijaribu kubana kila kitu kwenye karatasi moja ya bango-kitita — utahitaji nafasi ya kuandika kati ya michoro wakati wa zoezi.
  Maeneo yanayopendekezwa kwa ramani: Nyumba, shule, hospitali, maeneo ya ibada, soko, kiwanda, shamba, basi, kituo cha polisi na mahakama, ofisi ya serikali ya mipango miji inayotoa idhini ua ujenzi, ofisi ya serikali inayoshughulikia masuala ya dini, ofisi ya serikali ya usajili wa vizazi, vifo, na ndoa.

(Toleo mbadala: Gawa washiriki katika vikundi na waombe kila kikundi kitengeneze ramani yake. Malizia kwa mjadala wa pamoja. Hili litaongeza muda wa dakika 20.)

- **ANDAA KARATASI ZENYE WAHUSIKA**
  Tayarisha karatasi 1-2 za bango-kitita zenye orodha ya wahusika waliotajwa hapa chini, ukibadilisha majina yaliyopigiwa mstari na dini zinazofaa katika muktadha wa nchi yako. Kwa mfano, badala ya kuandika “mwanamke wa jamii ya watu wachache zaidi”, unaweza kuandika “mwanamke wa Kibarbaig”. Maandishi yanapaswa kuwa makubwa na yanayoonekana ili kila mtu aweze kuyasoma kwa umbali fulani.

WAHUSIKA
- Mvulana/mwanaume kutoka **jamii ya watu walio wengi**
- Msichana/mwanamke kutoka **jamii ya watu walio wengi**
- Kiongozi wa kidini kutoka **jamii ya watu walio wengi**
- Mvulana/mwanaume kutoka **jamii kuu ya watu wachache**
- Msichana/mwanamke kutoka **jamii kuu ya watu wachache**
- Kiongozi wa kidini kutoka **jamii kuu ya watu wachache**
- Mvulana/mwanaume kutoka **jamii ndogo ya watu wachache**
- Msichana/mwanamke kutoka **jamii ndogo ya watu wachache**
- Kiongozi wa kidini kutoka **jamii ndogo ya watu wachache**
- Mwanamke aliyebadili **dini ya walio wengi** kwenda **dini ya wachache**
- Mwanaume aliyebadili kutoka **dini ya wachache** kwenda **dini ya walio wengi**
- Mwanaume asiyeamini Mungu ambaye maoni yake yameonekana kupitia chapisho la mitandao ya kijamii
- Wanandoa wa dini tofauti (eleza dini ya mwanaume na mwanamke)
- Mwenye changamoto: mwanamke kutoka jamii ya watu walio wengi ambaye tabia/mawazo yake yanapingana na kanuni za kitamaduni za **walio wengi**
- Mkosoaji: mtu anayekosoa mawazo au matendo ya kidini, au tabia ya kiongozi wa dini, au jinsi serikali inavyoshughulikia masuala ya dini

Weka bango-kitita ya ramani na karatasi nyingine kubwa ya wahusika ukutani kabla ya kipindi.

JINSI YA KUANZA ZOEZI DAKIKA 10

- **WASILISHA BANGO-KITITA YA 'RAMANI'**
  Waombe washiriki wasimame katika nusu duara kuzunguka bango-kitita ya ramani. Eleza yafuatayo:
  - Watu hukumbana na matatizo ya uhuru wa dini au imani katika hali na maeneo halisi.
  - Wanaweza kukumbana na matamshi ya chuki kwenye basi au mitandao ya kijamii, ubaguzi kazini au matatizo katika kukutana kwao na serikali – na sera na sheria, maafisa wa mitaa au jeshi la polisi. Baadhi ya maeneo au hali hizi zinaweza kuonekana kwenye 'ramani' hii. (Orodhesha maeneo uliyochora/kuandika kwenye ramani).
  - Ramani hii inawakilisha mji wetu au eneo letu, lakini tunaweza pia kufikiria kuhusu nchi yetu kwa upana zaidi. Tutapanga matatizo yanayohusiana na uhuru wa mawazo, dhamiri, dini au imani kwenye ramani.

- **WASILISHA WAHUSIKA**
  Eleza kuwa zoezi la kuchora ramani litaanzia kwa wahusika mbalimbali ambao huenda wakakumbana na changamoto zinazohusiana na uhuru wa dini au imani katika sehemu moja au zaidi zilizo kwenye ramani yetu.
  Soma orodha ya wahusika waliopo kwenye bango-kitita. Uliza washiriki ikiwa kuna wahusika wowote wanaoweza kukumbana na changamoto lakini hawajajumuishwa. Ongeza wahusika kulingana na mapendekezo ya kundi.

JINSI YA KUENDESHA ZOEZI DAKIKA 50

- **TAFAKARI** (DAKIKA 5)
  Omba kila mshiriki achague kimyakimya mhusika mmoja ambaye anaweza kukumbana na matatizo yanayohusiana na uhuru wa mawazo, dhamira, dini, au imani katika nchi au jamii yao. Waombe watazame ramani na kutumia dakika 3 kutafakari maswali haya: Katika sehemu zipi kwenye ramani mhusika wako angekumbana na matatizo kwa sababu ya mawazo, utambulisho wa kidini, ibada, au imani zake? Ni matatizo gani angekumbana nayo?

Hakikisha washiriki wanaelewa kuwa lengo ni kuchunguza uzoefu wa wahanga wa ukiukwaji wa haki badala ya kujikita kwa wale wanaosababisha ukiukwaji huo?

- **SHIRIKI NA UTUNZE KUMBUKUMBU** (DAKIKA 45)
  1. Mwombe mshiriki mmoja aseme ni mhusika gani alichagua na, kwa ufupi sana, aeleze ni maeneo gani kwenye ramani mhusika huyo anaweza kukumbana na matatizo na matatizo hayo ni yapi. Andika kwa ufupi jina la mhusika na aina ya matatizo anayotaja karibu na kila sehemu husika kwenye bango-kitita. Kwa mfano, unaweza kuandika "Wanandoa wa dini tofauti – unyanyasaji" kando ya basi. Msimamishe mshiriki anayeongea baada ya dakika mbili, hata kama hajamaliza kutaja sehemu zote, ili kuhakikisha kila mtu anapata nafasi ya kuchangia.
  2. Uliza ikiwa kuna mtu mwingine aliyemchagua mhusika huyo huyo na kama ana mambo ya ziada ya kuongeza kuhusu mhusika huyo. Himiza mjadala na hadithi za uzoefu kuhusu mhusika huyu.
  3. Uliza ikiwa kuna wahusika wengine ambao wangepitia matatizo yale yale katika sehemu hizo. Andika wahusika hao karibu na matatizo husika.

Rudia hatua hizo kwa mhusika mwingine. Endelea hadi dakika kumi za mwisho za kipindi hiki. Katika dakika kumi za mwisho, waombe wale ambao bado wana matatizo ambayo hayajajadiliwa waje mbele na kuyaandika kwenye sehemu husika za ramani, wakibainisha mhusika anayekumbana na tatizo hilo. Tumia dakika chache za mwisho kwa washiriki kusoma na kutafakari maongezi yaliyoandikwa na wenzao.

Zoezi hili litaendelea na majadiliano wa pamoja baada ya kipindi cha kuchangamsha mwili.

5. Zoezi la kuchangamsha: Tembea kisha simama   Dakika 5

ZOEZI LA PAMOJA

MAELEZO
Washiriki wanafuata maelekezo kwa kufanya kinyume na kile kilichosemwa.

LENGO
Kuongeza ari ya kikundi na kuleta hali ya furaha katika kipindi kinacholenga matatizo.

JINSI YA KUENDESHA ZOEZI
Fuata hatua zifuatazo:

- Waombe washiriki wasambae ndani ya chumba.
- Waelekeze watembee unapotamka "TEMBEA" na wasimame unapotamka "SIMAMA". Toa maagizo haya kwa mpangilio wowote kwa sekunde 20 hadi 30.
- Tangaza kuwa maana ya amri hizo zimebadilishwa – sasa "TEMBEA" inamaanisha wasimame na "SIMAMA" inamaanisha waendelee kutembea. Endelea kutoa maagizo haya kwa sekunde 30 nyingine.
- Tangaza amri mbili mpya: Wanaposikia "JINA", kila mtu anapaswa kutamka jina lake kwa sauti; na wanaposikia "PIGA MAKOFI", wanapaswa kupiga makofi mara moja. Wanaendelea kusimama au kutembea wakati wakifanya hivyo.
- Fanya mazoezi ya amri hizi mpya pamoja na "TEMBEA" na "SIMAMA" (ambazo bado zina maana zilizobadilishwa).
- Hatimaye, tangaza kuwa maana ya amri mbili za mwisho zimebadilishwa – sasa "JINA" inamaanisha kupiga makofi na "PIGA MAKOFI" inamaanisha kutamka jina.
- Endelea kucheza hadi dakika tano ziishe.

Tazama **VIDEO YA MAFUNZO** kwa zoezi hili hapa.

6. Zoezi la Uchambuzi: Ramani ya uhuru wa dini au imani ya mji wetu, sehemu ya 2 Dakika 25

MJADALA WA PAMOJA

MAELEZO

Huu ni muendelezo wa zoezi lililotangulia kabla ya zoezi la kuchangamsha mwili. Katika sehemu hii, washiriki wanachambua uchunguzi walioufanya katika zoezi la kutengeneza ramani kwa kutumia muundo wa hatua tatu ulioanzishwa kwenye mada iliyowasilishwa.

JINSI YA KUANZA ZOEZI DAKIKA 5

Waombe washiriki wakae kwenye nusu duara mbele ya ramani.

- Waambie kuwa watachambua matokeo ya zoezi lao kwa kutumia muundo walioujifunza kwenye mada iliyopita.
- Uwaulize ikiwa kuna yeyote anayekumbuka hatua tatu za muundo huo. Wakijibu, waonyeshe tena slaidi ya PowerPoint namba 13 au karatasi yenye maneno sawa yaliyoandikwa juu yake.
- Waulize kama wanakumbuka maana ya upotoshaji wa habari na wakihitaji, wakumbushe.

JINSI YA KUENDESHA ZOEZI DAKIKA 20

Uliza maswali yafuatayo na andika hoja kuu kutoka kwenye mjadala kwenye bango-kitita. Ikiwa matatizo au wahusika wapya watajitokeza katika mjadala, waandike pia kwenye ramani.

- Je, kuna mifano ya upotoshaji wa habari, ubaguzi, au vurugu kwenye ramani yetu?
- Nani anaathiriwa na matatizo tuliyotambua?
  - Ni nani aliye hatarini zaidi katika jamii yetu?
  - Je, wanawake na wasichana wanakabiliwa na matatizo na changamoto tofauti na wanaume na wavulana?
- Matatizo haya yanaathari gani kulingana na yanavyotokea mara kwa mara, kiwango na athari zake?
  - Mara yanavyotokea: Je, matatizo tuliyotambua hutokea mara kwa mara au ni nadra? Je, kuna matatizo ambayo yamejengeka ndani ya mfumo wa jamii?
  - Kiwango: Je, ni watu wachache au wengi wanaoathiriwa na matatizo haya? Ni matatizo yapi yanayowaathiri watu wengi zaidi?
  - Athari: Ni matatizo yapi yanayoathiri wahusika kwa njia mbaya zaidi? Wakumbushe kuwa hata kama tatizo linaathiri watu wachache, ikiwa lina madhara makubwa kwao, basi ni tatizo zito.
- Ni nani anachangia matatizo haya?
  - Je, serikali inahusika moja kwa moja katika ukiukwaji wa haki, inakaa kimya kuhusu matatizo yanayosababishwa na wengine, au inajihusisha kikamilifu katika kulinda uhuru wa dini au imani?
  - Je, sisi wakati mwingine tunakuwa sehemu ya tatizo, iwe kwa kujua au kutokujua?
- Je, kuna wahusika – watu binafsi au jumuiya za kidini – ambao hatujui vizuri matatizo yao? Je, tunaweza kuyachunguza zaidi na kuongeza maarifa haya kwenye ramani yetu na uchambuzi wetu?
- Kugundua matatizo haya kunakufanya ujisikie vipi?

KIDOKEZO! Hifadhi ramani ya uhuru wa dini au imani ya mji wetu kwenye karatasi za maandishi, na ikiwa inawezekana, ziache ukutani. Utahitaji ramani hizi kwa vipindi vyote vijavyo.

Wakati wa mjadala, jaribu kusisitiza jinsi mifano inayotolewa na washiriki inaonyesha kwamba ukiukwaji wa uhuru wa dini au imani mara nyingi huambatana na ukiukwaji wa haki nyingine pia, kama vile haki za wanawake, haki ya elimu, au haki ya ajira. Wafanye waelewe kuwa haki za binadamu zote zina uhusiano wa karibu – tunazihitaji zote!

ZINGATIA

Unaweza kutumia zaidi ya dakika 20 kwa hili kwa urahisi. Usitumie muda mwingi kujadili swali moja ili kufanikisha majadiliano ya maswali mengi kadri inavyowezekana. Unaweza kupanga muda zaidi kwa mjadala huu kwa kuondoa zoezi la 'Mtandao wa mazuri.

GUMZO FUPI

7. Maoni ya hitimisho na hadithi ya wanamabadiliko wa jamii Dakika 5

MAELEZO

Huu ni muendelezo wa zoezi lililotangulia kabla ya zoezi la kuchangamsha mwili. Katika sehemu hii, washiriki wanachambua uchunguzi walioufanya katika zoezi la kutengeneza ramani kwa kutumia muundo wa hatua tatu ulioanzishwa kwenye mada iliyowasilishwa.

NINI CHA KUSEMA

Toa hoja zifuatazo. Tumia slaidi za 14-19 za PowerPoint ya kipindi kuonesha hadithi ya Emina iwapo itawezekana (au toa nakala ya slaidi hizi ili kuzionesha).

- Sasa tumefikia mwisho wa vipindi vitano vinavyounda Sehemu ya 1 ya mafunzo ya Wanamabadiliko wa Jamii.
- Katika vipindi hivi, tumetazama haki za binadamu, uhuru wa dini au imani, utambulisho, fursa na changamoto, pamoja na hali ya uhuru wa dini au imani katika nchi yetu na jamii yetu. Katika kipindi cha leo, haswa tumelenga matatizo ambayo watu hukabiliana nayo.
- Huenda hatukukubaliana kila wakati kuhusu matatizo ni yapi au ni mabadiliko gani yanahitajika. Lakini kuna mambo tunayokubaliana juu yake na mabadiliko ambayo sote tunataka kuyaona.
- Mbali ya matatizo yote tuliyotambua, tuna chaguzi mbili: kujihisi tumekata tamaa na hatuna nguvu, au kutambua jambo moja la msingi, hata kama ni dogo, ambalo tunaweza kulibadilisha. Nalo ni kuwa wanamabadiliko katika jamii zetu.
- Soma hadithi ya Emina kutoka ukurasa wa 109 na onyesha slaidi za PowerPoint 14-19 (au machapisho ya slaidi hizo).
- Tumshangilie Emina kwa kazi yake nzuri, na pia tujishangilie kwa kukamilisha Sehemu ya 1 ya mafunzo haya! Katika Sehemu ya 2 ya mafunzo, tutazingatia jinsi tunavyoweza kuleta mabadiliko – ni mbinu gani tunaweza kutumia na jinsi ya kuandaa mipango ya utekelezaji.

Maudhui ya ziada kwa makundi yanayofanya vipindi 1 – 5 pekee vya mafunzo.

Ikiwa mnaendesha Sehemu ya 1 pekee ya mafunzo, tafadhali jumuisha vipengele vifuatavyo mwishoni mwa kipindi cha 5. Aidha, panga kipindi kiwe na dakika 20 za ziada AU ondoa Zoezi la 1: Mtandao wa wema na upunguze dakika 5 kutoka kwenye zoezi la ramani.

8. Zoezi la tathmini: Kichwa, moyo, mikono   Dakika 15

ZOEZI LA KILA MTU

Zoezi hili rahisi la tathmini ya kibinafsi linawasaidia washiriki kutafakari juu ya kile wanachobeba kutoka kwenye mafunzo hii.

NYENZO

- Karatasi moja ya 'Kichwa-moyo-mikono' kwa kila mshiriki.
- Kalamu moja kwa kila mshiriki.

JINSI YA KUANZA ZOEZI   DAKIKA 2

Mpe kila mshiriki karatasi ya Kichwa-Moyo-Mikono. Eleza kuwa watafanya zoezi la tathmini ili kutafakari kile watakachopata binafsi kutoka kwenye mafunzo haya. Eleza wazi ikiwa karatasi zitakusanywa ili kusaidia katika tathmini ya mafunzo au ikiwa wanaweza kwenda nazo nyumbani kama kumbukumbu. Ikiwa karatasi zitakusanywa, hakikisha washiriki hawaandiki tafakari za kibinafsi sana!

JINSI YA KUENDESHA ZOEZI   DAKIKA 13

Waombe washiriki kutafakari yafuatayo:

- Fikiria kile ulichopata kwa mtazamo wa maarifa na mawazo mapya, kisha andika mawazo yako katika sehemu ya kichwa.
- Fikiria hisia zako, ugunduzi wako binafsi au mitazamo mipya uliyo nayo, kisha andika haya katika sehemu ya moyo.
- Fikiria mawazo yoyote uliyonayo kuhusu kuchukua hatua au kufanya jambo tofauti, kisha andika haya katika sehemu ya mkono.
- Jaribu kuwa mahususi kadri iwezekanavyo. Wape dakika 5 kufanya hivi.

Kulingana na ukubwa wa kikundi, ama zunguka kwenye duara na kuwaomba kila mshiriki kutaja kitu kimoja, ama wagawe wawili wawili waweze kushirikishana na kutafakari. (Dakika 8)

(Njia mbadala: Chora kichwa, moyo, na mkono kwenye karatasi tatu tofauti za bango-kitita. Waombe washiriki wajibu maswali hayo kwa kuandika kwenye karatasi ndogo za kunata na kuzibandika kwenye bango-kitita. Jadili matokeo kwenye mjadala wa pamoja.)

9. Shukrani na kuaga   Dakika 5

Wakati wa mafunzo, washiriki wamefahamiana vizuri zaidi na wamejitolea muda na nguvu zao kwa mchakato huu. Sasa ni wakati wa kusema asante na kusherehekea mawazo mapya, maarifa, ujuzi na mahusiano waliyounda katika kipindi cha mafunzo!

Andaa sherehe fupi sana ya kuwapongeza na kuwashukuru. Unaweza kuimba wimbo, kusema machache, kuomba, kucheza n.k. Ikiwa unaweza kuchapisha cheti cheti na kukitoa kwa washiriki.

Chanzo

Walk and stop: Mark Collard, Playmeo. www.playmeo.com/activities/energizer-warm-up-games/walk-stop/

Mwongozo wa uwasilishaji

Mambo yanavyokuwa mabaya zaidi (mazuri zaidi)

Nakala hii ya uwasilishaji wa kipindi cha 5 inaonyeshwa kwenye slaidi za 3-13 za PowerPoint ya kipindi.

UTANGULIZI

Katika kipindi kilichopita:

- Tulizingatia jinsi ukiukwaji wa uhuru wa dini au imani unavyoonekana na athari zake kwa maisha ya watu,
- Tulitafakari kuhusu nani anayehusika na ukiukwaji huu – ikiwa ni serikali kupitia sheria na vitendo au kutochukua hatua kwa maofisa wake, au watu katika jamii,
- Na tulitumia maigizo kama nyenzo ya kuchunguza jinsi ukiukwaji huu unavyoweza kuonekana na kufanya mazoezi ya kuutambua.



Sasa, tutafikiria jinsi ukiukwaji unavyoweza kuanzia hali ya wastani na kuzidi kuwa mbaya – kutoka matukio ya hapa na pale yanayowaathiri watu binafsi hadi mashambulizi ya kimfumo, yaliyoenea na makali dhidi ya haki za watu. Njia moja ya kufikiria jinsi mambo yanavyozidi kuwa mabaya ni kwa kuchunguza hatua tatu kuu: Upotoshaji wa taarifa, Ubaguzi na Ukatili.

HATUA TATU ZA MATESO

Hatua ya kwanza ni upotoshaji wa taarifa. Katika hatua hii, chuki, dhana potofu na uongo huenezwa kuhusu watu binafsi au makundi fulani ya watu – kwa mfano, jamii za watu wachache wa kidini. Upotoshaji huu unafanyika kwa njia nyingi – kupitia yale ambayo wazazi, walimu na vitabu vya shule huwafundisha watoto, redio, mitandao ya kijamii, hotuba za wanasiasa au mahubiri ya viongozi wa kidini.

Hakuna jamii isiyo na chuki au dhana potofu, lakini zinapoachwa bila kupingwa, na hasa zinapopigiwa debe na viongozi wa kisiasa na kidini, huchochea utamaduni wa kutovumiliana na kusababisha mvutano kati ya makundi ya watu. Hali hii inapotokea, huwa rahisi au hata jambo la kawaida kwa watu wa kawaida, maafisa wa serikali za mitaa na hata serikali yenyewe si tu kufikiria na kusema, bali pia kutenda kwa njia za kibaguzi dhidi ya wengine.

Upotoshaji wa taarifa hufanya ubaguzi uonekane kuwa jambo la kawaida. Katika hali yake mbaya zaidi, upotoshaji wa taarifa hutumiwa kuwashawishi watu waamini kuwa si tu ubaguzi bali hata ukatili ni jambo linalokubalika au hata lenye haki.



Ubaguzi huathiri watu katika kila nyanja ya maisha. Katika kipindi kilichopita, tuliona mifano ya ubaguzi wa kiserikali – kwa mfano, sheria za familia na utambulisho wa kibinafsi zinazobagua, ubaguzi katika utekelezaji wa sheria na vyombo vya usalama kama vile polisi na mahakama, na ubaguzi katika upatikanaji wa huduma kama vile elimu. Pia, tuliona mifano ya ubaguzi katika sekta binafsi unaoathiri fursa za watu kupata ajira.

Hakuna jamii isiyo na ubaguzi, lakini ubaguzi ulioenea na wa kimfumo unaweza tu kuendelea pale unapojengwa juu ya utamaduni wa ujinga na kutovumiliana. Ubaguzi usingeendelea kuwepo kama watu wengi wasingeukubali.



Na kama vile upotoshaji wa taarifa unavyoweka msingi wa ubaguzi, kwa pamoja upotoshaji wa taarifa na ubaguzi huunda msingi wa ukatili. Ukatili ndani ya jamii unaweza kujitokeza kwa njia nyingi – kutoka uharibifu wa mali, unyanyasaji na vitisho hadi ukatili wa moja kwa moja wa kimwili. Ukatili wa kiserikali unaweza kujumuisha kifungo cha kiholela, mateso na ukatili wa kijinsia.

WIGO, KIASI NA ATHARI



Aina zote tatu za matatizo – upotoshaji wa taarifa, ubaguzi na ukatili – zinaweza kutokea kwa viwango tofauti vya wigo na kiasi, na kwa athari tofauti. Ukiukwaji unaweza kuathiri watu wachache au makundi makubwa. Unaweza kuwa wa nadra, wa mara kwa mara au wa kimfumo – yaani, umejengeka ndani ya mifumo na miundo ya jamii. Na unaweza kuwa na athari ndogo au madhara makubwa kwa watu wanaoathirika.



Uzoefu katika mataifa mengi unaonyesha kuwa kadri chuki na upotoshaji wa taarifa unavyokuwa mkubwa na mkali, ndivyo ubaguzi unavyozidi kuwa mkubwa na mkali. Na kadri upotoshaji wa taarifa na ubaguzi vinavyoenea, ndivyo uwezekano wa ukatili mkubwa na mkali unavyoongezeka. Jambo moja husababisha jingine. Hili linaweza kuonekana kama jambo la kukatisha tamaa, lakini kuelewa jinsi mambo yanavyokuwa kuwa mabaya hutusaidia pia kufikiria jinsi yanavyoweza kuwa bora.

HITIMISHO

Kila kitu huanza na jinsi tunavyofikiria, tunavyosema na tunavyotendeana. Na hili ni jambo ambalo kila mmoja wetu anaweza kufanya kuhusu lolote – ndani ya familia zetu na katika mitandao yetu ya kijamii. Pia kuna uwezekano wa kuchukua hatua katika jamii zetu – kwa mfano, ndani ya jumuiya za kidini, mashuleni na mahali pa kazi.

Bila shaka, haya pekee hayatoshi. Tunahitaji pia kubadili mifumo rasmi inayobagua na kudhuru watu – kutoka kwenye sheria mbaya hadi tabia za maofisa kama walimu wa shule au maofisa wa polisi.

Ili kuleta mabadiliko haya, tunahitaji watu wachache wanaojua haki zao na walio tayari kuzitetea, wengi waliotayari kusimama nao, na viongozi wa kisiasa na kidini wanaoelewa wajibu wao wa kuheshimu, kulinda na kuendeleza haki za binadamu.



Kufanikisha haya ni mchakato mgumu na wa polepole. Lakini mchakato huo huanza kwa kuchanganua mazingira yetu na kubaini matatizo yaliyopo. Tunaweza kutumia muundo huu wa hatua tatu – upotoshaji wa taarifa, ubaguzi na ukatili – kama nyenzo ya kutusaidia kufanya hivyo.

Shukurani
Nakala hii inatokana na mfano wa 'Hatua Tatu za Mateso' ulioandaliwa na Johan Candelin.

Hadithi ya wanamabadiliko

Hadithi ifuatayo inasomwa kama sehemu ya Maoni ya hitimisho kipindi cha 5. Inaonyeshwa kwenye slaidi 14-19 za uwasilishaji wa PowerPoint ya kipindi hicho.

Hadithi ya Emina, Bosnia Herzegovina

HADITHI

Mwishoni mwa vita vya Bosnia mnamo 1995, mandhari ya kidini ya Bosnia na Herzegovina yalibadilika kwa kiasi kikubwa. Baadhi ya maeneo yaliyokuwa na Waislamu wengi yakawa na Wakristo wengi, na kinyume chake. Tangu wakati huo, mvutano wa kikabila na kidini bado upo, na watu wanaorejea katika maeneo yao ya asili wako katika hatari kubwa zaidi.

Huyu ni Emina. Emina alitaka kuchangia mabadiliko chanya, hivyo akajiunga na mafunzo mafupi ya haki za binadamu yaliyoendeshwa na shirika lisilo la kiserikali la Bosnia liitwalo Nahla.

“Nimejifunza mengi kupitia mafunzo haya. Nilielewa maana ya uhuru wa dini au imani na nikaanza kutambua ukiukwaji katika mazingira yangu. Nilianza kuripoti hotuba za chuki kwenye mitandao ya kijamii.”

Baada ya mafunzo hayo, Nahla alimjulisha Emina kwa kikundi cha vijana wa kujitolea wanaotumia ripoti kutoka kwa vyombo vya habari vya kuaminika vya kitaifa na vya ndani ili kuweka kumbukumbu za ukiukwaji wa uhuru wa dini au imani nchini humo. Wanakusanya orodha ya matukio yote yanayotokea kila mwaka.

Emina anasema, “Tunatumia seti ya maswali ili kuainisha matukio – kwa mfano, ni jamii gani iliyoathiriwa na aina ya ukiukwaji – kama vitisho, mashambulizi dhidi ya mali, au mashambulizi dhidi ya watu, na kadhalika.”

Kikundi hiki hutuma ripoti zake kwa mamlaka na vyombo vya habari vya Bosnia, pamoja na mashirika ya kimataifa kama Shirika la Usalama na Ushirikiano Barani Ulaya (OSCE), ambalo mara nyingi hujumuisha taarifa kutoka kwa vijana wa kujitolea katika ripoti yake ya kila mwaka.

Emina anasema, “Ninaamini kuwa kila hatua tunayochukua ina athari, haijalishi inaonekana ndogo kiasi gani. Kuweka kumbukumbu na kuleta umakini wa kimataifa kuhusu ukiukwaji huu kunaweza kusaidia kushinikiza mamlaka zichukue masuala haya kwa uzito. Kuongeza uelewa kuhusu ukiukwaji wa haki za binadamu pia hutusaidia kutambua upendeleo wetu binafsi.”

Chanzo
Emina Frljak, PRVI na Kituo cha Nahla cha Elimu na Utafiti

Vipindi vya 6-9

Sehemu ya 2: Safari kuelekea kwenye mabadiliko

Mafunzo ya Wanamabadiliko wa Jamii inalenga kuwaandaa washiriki kuwa wawezeshaji wa mabadiliko katika jamii zao kwa kuhimiza Uhuru wa Dini au Imani. Mchakato wa kuleta mabadiliko ni safari ndefu na wakati mwingine mgumu. Kama safari nyingine yoyote, ni muhimu kuwa na ramani na kuelewa jinsi ya kusafiri kutoka hatua A hadi B!

Sehemu ya 2 ya mafunzo haya inasaidia washiriki kupanga 'safari ya mabadiliko yao'. Washiriki wanajifunza mbinu mbalimbali ambazo zinaweza kutumika kuhimiza uhuru wa dini au imani na haki nyinginezo, na wanaongozwa katika mchakato wa kupanga hatua za kuchukua kuhusu tatizo la uhuru wa dini au imani walilobaini. Vipindi hivi vinazingatia ujuzi na hatua – kuwaandaa washiriki kutekeleza wanachojifunza!

Sehemu ya 2 inajumuisha vipindi vinne, vilivyogawanywa katika sehemu mbili. Kila sehemu ina malengo ya pamoja ya kujifunza na mchakato mmoja wa kujifunza unaoendelea katika vipindi vyote viwili.

- Vipindi vya 6 na 7 vinazingatia kujifunza kuhusu mbinu, kuchunguza jinsi washiriki wanavyoweza kuzitumia kuhimiza haki za binadamu, na kupata msukumo kutoka kwa hadithi za watu wanaotumia mbinu hizo kuleta mabadiliko.
- Vipindi vya 8 na 9 vinazingatia upangaji wa hatua – kubuni mawazo madhubuti ya kuleta mabadiliko katika jamii. Washiriki wanajifunza ujuzi wa kupanga hatua na kufanya mazoezi ya kutumia zana za upangaji wa hatua. Kulingana na aina ya kikundi chako, mipango ya hatua inaweza kuwa mipango halisi ya kutekelezwa baada ya mafunzo au mipango ya majaribio.

KIPINDI CHA 6

Kuchochewa na hadithi – kuwezeshwa na mbinu

Muhtasari wa kipindi

Vipindi vya 6 na 7 'vimeunganishwa' – vina malengo ya pamoja ya kujifunza na mchakato mmoja wa kujifunza.

Kuna mbinu nyingi za kufanya kazi ili kuhimiza haki za binadamu, ambazo zinaweza kufupishwa katika mbinu 15. Vipindi vya 6 na 7 vinawatambulisha washiriki kwenye mbinu hizi kwa kiwango cha msingi. Ingawa kipindi cha 6 kinajumuisha uwasilishaji, lengo kuu ni kujifunza na kupata msukumo kupitia hadithi na tafakari za pamoja, badala ya nadharia pekee.

Badala ya kutoa ujuzi wa kina kuhusu mbinu moja au mbili, vipindi hivi vinafungua macho ya washiriki kwa njia mbalimbali wanazoweza kutumia kuleta mabadiliko. Katika kurasa za 155-158, kuna vidokezo vya nyenzo za ziada kwa wale wanaotaka kujifunza zaidi kuhusu baadhi ya mbinu hizi.

MUHTASARI WA MBINU 15

MBINU ZA DHARURA: Kuzuia; Kusimamisha na kuokoa; Kuomba msaada na kuonya.
MBINU ZA MABADILIKO: Kufanya kampeni; Utetezi; Kutoa motisha; Kukaidi.
MBINU ZA KUJENGA: Kujenga uelewa; Kujenga ushirikishwaji; Kujenga ujuzi; Kujenga mahusiano na mitandao.
MBINU ZA UPONYAJI: Msaada wa vitu na kisaikolojia; Kutunza kumbukumbu za ukiukwaji wa haki; Kuelimisha na kukumbuka; Kutafuta haki na fidia.

ZINGATIA

Yaliyomo katika vipindi vya 6-7 yanatumia toleo lililorekebishwa la mfumo wa mbinu ulioandaliwa na Mradi wa Mbinu Mpya za Haki za Binadamu unaoendeshwa na Center for Victims of Torture. www.newtactics.org Tovuti hii inaweza kukupa msukumo zaidi.

Malengo ya mafunzo

Vipindi vya 6 na 7 vinazingatia kukuza uelewa kuhusu mbinu za kuhimiza haki za binadamu.

Ifikapo mwisho wa vipindi hivi, washiriki watakuwa na uwezo wa:

- kutoa maelezo rahisi ya makundi manne tofauti ya mbinu zinazoweza kutumiwa kuhamasisha haki za binadamu na kutoa mifano ya hatua kwa kila aina.
- kuonyesha hamu ya kuhamasisha haki za binadamu katika jamii yao.
- kutambua kwa pamoja angalau hatua tano ambazo wanaweza kuchukua kama watu binafsi na hatua tano ambazo vikundi/taasisi wanazoshirikiana nazo zinaweza kuchukua ili kuhamasisha uhuru wa dini au imani katika jamii yao.

ZINGATIA

Kumbuka kuwa uhalisia wa malengo haya ya kujifunza utategemea kiwango cha kuanzia cha kikundi chako. Kusudi la malengo ya kujifunza ni kuonyesha maeneo ambayo wawezeshaji wanaweza kufuatilia maendeleo ya washiriki katika ujuzi, mtazamo na uwezo wa kuchukua hatua. Maendeleo yanaweza kufanyika hatua kwa hatua wakati wa kozi badala ya kutimizwa ndani ya kipindi kimoja pekee

Yaliyomo katika kipindi na muda

Zoezi la ufunguzi: Makundi ya kujadili hadithi za wanamabadiliko Kipindi kinaanza kwa msukumo kutoka kwa hadithi za wengine.	Dakika 20
Zoezi la tafakari: Washuhudiaji na waponyaji Huwasaidia washiriki kutafakari kwa nini wakati mwingine tunachukua hatua kukomesha dhuluma na wakati mwingine hatufanyi hivyo.	Dakika 25
Zoezi la kila mtu: Mimi ni nani? Zoezi la kuchora linalowasaidia washiriki kutafakari kuhusu muktadha mbalimbali ambamo wanaweza kuleta mabadiliko.	Dakika 15
Uwasilishaji: Mbinu za utangulizi Uwasilishaji muhimu linalotumia taswira ya moto kuanzisha vikundi vinne vya mbinu za kuhamasisha haki (Mbinu za Dharura, Mabadiliko, Kujenga na Uponyaji).	Dakika 10
Zoezi ka kikundi na mjadala wa pamoja: Kuzungumzia mbinu za dharura Washiriki wanajadili mbinu za dharura na kutafakari jinsi ya kuzitumia.	Dakika 45
Maoni ya hitimisho Kuunganisha vipengele tofauti vya kipindi.	Dakika 5
JUMLA YA MUDA	**Saa 2**

Jiandae

Jitayarishe kwa kipindi kulingana na mwongozo uliopo kwenye ukurasa wa 15, 'Jinsi ya kujiandaa kwa kila kipindi'. Kumbuka – unawajua washiriki wako! Una uhuru wa kurekebisha na kubadilisha vipengele vyovyote vya kipindi ili kiendane na mahitaji ya kikundi chako.

NYENZO ZA KIPINDI HIKI

Mbali na nyenzo za kawaida zilizoorodheshwa kwa kila kipindi kwenye ukurasa wa 16, utahitaji nyenzo zifuatazo kwa kipindi hiki:

- Bango-kitita za kutosha na kalamu za rangi ili kila mshiriki awe na moja.
- Bango-kitita za 'Ramani ya uhuru wa dini au imani ya mji wetu' zilizotengenezwa katika kipindi kilichopita.
- Bango-kitita iliyo na kichwa 'Mawazo ya utekelezaji: Mbinu za Dharura' na idadi kubwa ya karatasi za kunata (post-it notes).
- Nakala iliyochapishwa ya bango la muhtasari wa mbinu na mabango yote ya Mbinu za Dharura.
- (Hiari) Ikiwa hutumii PowerPoint, unaweza kuchapisha picha za hadithi za wabunifu wa mabadiliko kutoka slaidi za 3-10 za PowerPoint.

NYENZO ANDAMIZI za kipindi hiki zinaweza kupatikana hapa.

ANDAA UKUMBI

Kwa kipindi hiki, ni vyema kuanza na viti vikiwa vimepangwa katika nusu mduara vikielekea mbele. Bandika 'Ramani ya uhuru wa dini au imani' na bango-kitita ya 'Mawazo ya utekelezaji: Mbinu za Dharura' ukutani kabla ya kipindi kuanza.

'Mimi ni nani?'

"Zoezi la 'Washuhudiaji na waponyaji' na 'Mimi ni nani' lilizua hisia mseto. Kulikuwa na huzuni kutokana na kutambua ni mara ngapi tumekuwa washuhudiaji tu, ikiwemo kwenyemitandaoya kijamii. Hata hivyo, kujifunza mbinu madhubuti tunazoweza kutumia kuleta tumaini kubwa kuhusu jinsi tunavyoweza kubadilika na kuwa wachochezi wa mabadiliko wanaotenda. Kulikuwa na dhamira thabiti ya kutumia mbinu hizo katika kundi."

UKOHA NGWOBIA, MWEZESHAJI, NIGERIA

Mpango wa kina wa kipindi

1. Zoezi la ufunguzi: Makundi ya kujadili hadithi za wanamabadiliko Dakika 20

ZOEZI LA KIKUNDI KIDOGO

MAELEZO
Hadithi tatu zitasomwa kisha kujadiliwa katika vikundi vidogo.

LENGO
Kuanzisha mchakato wa Sehemu ya 2 ya mafunzo na kuanza kipindi kwa mtazamo chanya kwa kuchukua msukumo kutoka kwa hatua za mabadiliko zilizochukuliwa na wengine.

NYENZO

- Slaidi za PowerPoint 1-10 au nakala za slaidi zilizochapishwa.

JINSI YA KUANZA ZOEZI DAKIKA 2
Karibisha kila mmoja kwenye kipindi kisha ueleze yafuatayo:

- Katika vipindi vilivyopita, tumeelewa haki za binadamu, haki ya uhuru wa dini au imani, na ukiukwaji wa haki hiyo. Pia tumetengeneza ramani ya ukiukwaji wa uhuru wa dini au imani katika jamii yetu.
- Kuanzia sasa tutazingatia hatua za kuchukua! Katika kipindi hiki na kijacho, tutagundua mbinu mbalimbali zinazoweza kutumiwa kutetea haki za binadamu na kufikiria jinsi tunavyoweza kuzitumia. Katika vipindi viwili vya mwisho, tutazingatia kutengeneza mipango ya utekelezaji.
- Tutaanza kwa kusikiliza hadithi tatu za watu wanaofanya mabadiliko kwa uhuru wa dini au imani katika jamii zao.

JINSI YA KUENDESHA ZOEZI DAKIKA 16

- Soma hadithi tatu za 'wanamabadiliko' kutoka kurasa za 124-125, ukitumia slaidi 3-10 za PowerPoint au nakala zilizochapishwa.
- Waombe washiriki wajiunge kwenye vikundi ya watu watatu na kujadili: Ni hadithi gani iliyokugusa au kukupa msukumo zaidi na kwa nini?

JINSI YA KUHITIMISHA ZOEZI DAKIKA 2
Hitimisha kwa kusema kwamba, hata kama hali zilizo katika hadithi hizo zinaweza kuwa tofauti sana na zetu, na hata kama hatua ambazo watu walichukua si mambo yanayoweza kuwa muhimu kwetu kufanya, tunatumaini kwamba wanamabadiliko hawa wabunifu na wenye ujasiri wanaweza kutupa msukumo wa kuamini kuwa mabadiliko yanawezekana na yanastahili kupiganiwa. Kuamini kwamba kila mtu anaweza kufanya jambo, hata liwe dogo kiasi gani, ili kuleta tofauti.

2. Zoezi la kutafakari: Washuhudiaji na waponyaji Dakika 25

ZOEZI LA PAMOJA

MAELEZO
Washiriki watafakari nyakati walizoingilia kati kusimamisha ukiukwaji wa haki (hata ikiwa ni mdogo) na nyakati walipokaa kimya, wakijadili sababu zinazosababisha mtu kuchukua hatua au kutofanya chochote.

LENGO

Zoezi hili linanuia:

- Kuwasaidia washiriki kutambua kwamba kila mmoja wetu, kwa wakati fulani, amewahi kuwa mshuhudiaji (kwa kukaa kimya tunapoona ukosefu wa haki) na pia mponyaji (kwa kusimama kidete kulinda haki zetu au za wengine), hata kwa njia ndogo.
- Kuwasaidia washiriki kubaini maamuzi na hatua za makusudi wanazoweza kuchukua ili kuwa waponyaji wenye mchango mkubwa zaidi katika kukabiliana na ukiukwaji wa haki.

NYENZO

- Karatasi moja ya A4 kwa kila mshiriki.
- Kalamu za kawaida za kutosha kwa kila mshiriki kuwa na moja au mbili.
- Bango-kitita/ubaoni na kalamu za alama.

JINSI YA KUANZA ZOEZI DAKIKA 2

Mpe kila mshiriki karatasi tupu ya A4 na uwaombe waikunje mara mbili. Kisha, waambie waandike neno 'Mshuhudiaji' juu ya nusu moja na neno 'Mponyaji' juu ya nusu nyingine.

Eleza yafuatayo:

- Tutafanya zoezi ambalo litatusaidia kutafakari kuhusu uzoefu wetu wa kuleta mabadiliko.
- Mshuhudiaji ni mtu anayebaki kimya na kutofanya lolote anapoona dhuluma ikifanywa – kwa mfano, unyanyasaji au ubaguzi.
- Mponyaji ni mtu anayesimama kidete, anasema au kuchukua hatua ili kusaidia mtu au watu walioathiriwa na ukiukwaji wa haki.
- Sisitiza kwamba sote tumewahi kucheza nafasi zote mbili nyakati tofauti maishani mwetu.

JINSI YA KUENDESHA ZOEZI DAKIKA 20

- **KUANDIKA NA KUCHORA** (DAKIKA 5)
  Mwombe kila mshiriki aandike au achore mfano wa wakati ambapo aliigiza mojawapo ya hizi nafasi kwenye karatasi yake. Mfano unaweza kuwa hali ya kila siku, kama vile wakati walipomuita mtu wa kusaidia walipoona mwanafunzi mwenzao akinyanyaswa, au wakati waliposimama kidete na kusema wazi pale ambapo mwanafamilia au mfanyakazi mwenzao alitendewa vibaya au wakati walipokuwa mshuhudiaji na hawakuchukua hatua, kwa sababu yoyote ile.

- **MJADALA WA PAMOJA** (DAKIKA 15)
  Anza kwa kusisitiza kwamba kila mtu, kwa wakati fulani, amewahi kuwa mshuhudiaji na pia mponyaji kisha waombe washiriki wawili au watatu wajitolee kushiriki mfano wa wakati walipokuwa mshuhudiaji au mponyaji. Usijadili matukio yao moja kwa moja, kwani lengo la zoezi si kuchanganua matukio, bali kuthibitisha uzoefu wa kila mtu.
  Kisha, uliza kundi maswali yafuatayo:
  – Zoezi hili limekufanya uhisi vipi?
  – Kwa nini wakati mwingine ulichukua hatua na wakati mwingine hukufanya hivyo? Nini kilifanya iwe tofauti?

MJADALA WA PAMOJA

– Ni mambo gani yanaweza kukusaidia kuhamasika kutoka kuwa mshuhudiaji hadi kuwa mtu anayesimama kutetea haki zake na haki za wengine?

Jaribu kuchochea majibu yafuatayo kutoka kwa washiriki kuhusu swali la mwisho, au uwahimize kutoa majibu haya kwa kuuliza maswali yanayohusiana na hoja hizi:

– Tunakuwa na uwezekano mkubwa wa kuchukua hatua tunapokuwa na uhusiano au tunapomwonea mwathiriwa huruma.

– Tunakuwa tunajiamini zaidi wa kuchukua hatua tunapokuwa na mtu mwingine, hasa kama sehemu ya kundi lililoandaliwa.

– Tunakuwa tunajiamini zaidi kuchukua hatua ikiwa tuna ujuzi kuhusu mada husika na 'mfumo' – kujua kanuni ni zipi na ni nani wa kumlalamikia au kumwomba msaada.

– Tunajiamini zaidi ikiwa tumejiandaa – ikiwa tumefikiria hali hiyo na kupanga mapema jinsi tunavyotaka kuchukua hatua, au ikiwa tumewahi kufanya hivyo hapo awali. Mazoezi ya

JINSI YA KUHITIMISHA ZOEZI DAKIKA 3

Hitimisha mjadala kwa kusisitiza mambo yafuatayo huku ukiwaonyesha slaidi ya 11 kwenye PowerPoint:

- Tunaweza kufanya maamuzi ya makusudi kuwa waponyaji badala ya washuhudiaji, kwa mfano kwa kujenga mahusiano na watu wanaoathiriwa na ukiukwaji wa haki, kujiunga na vikundi vilivyoandaliwa, kutafuta taarifa tunazohitaji, na kupanga jinsi tunavyotaka kuchukua hatua kwa pamoja.
- Hatutaweza kila wakati kuchukua hatua – wakati mwingine haitakuwa salama au yenye manufaa kufanya hivyo! Lakini tutakuwa na uwezekano mkubwa wa kuchukua hatua na kuwa na ufanisi zaidi tukijenga mahusiano, na tukifanya kazi kwa pamoja, n.k.
- Elekeza washiriki kwenye ramani ya uhuru wa dini au imani ya mji wetu iliyo kwenye bango-kitita. Waombe wafikirie kimya kimya ni tatizo gani kati ya yale yaliyoorodheshwa wangependa kuwa waponyaji wake. (Wape muda mfupi wa kutafakari, lakini usihimize majibu kwa sauti.)
- Katika vipindi vilivyobaki, tutafikiria JINSI ya kuondokea kuwa washuhudiaji hadi kuwa waponyaji kuhusiana na matatizo haya.

3. Zoezi la uchoraji: Mimi ni nani? Dakika 15

ZOEZI LA KILA MTU

ZINGATIA

Zoezi hili ni la kufurahisha na lina ujumbe muhimu, lakini si la lazima katika mchakato wa kipindi. Unaweza kuamua kuliondoa na kutumia muda zaidi kwa mazoezi mengine.

MAELEZO NA LENGO

Washiriki wanatambua 'wapi' wanaweza kuleta mabadiliko kwa kuchora mitandao yao ya kibinafsi na kitaaluma.

NYENZO

- Bango-kitita, kalamu.

JINSI YA KUANZA ZOEZI DAKIKA 1
Wape kila mshiriki bango-kitita na kalamu ya rangi.

Elezea yafuatayo:
Sisi sote ni sehemu ya jamii ambamo tuna mahusiano mengi na tunatekeleza majukumu tofauti – katika familia zetu, maeneo yetu ya kazi au jumuiya za kidini, pamoja na mitandao yetu ya marafiki na watu tunaofahamiana nao.

JINSI YA KUENDESHA ZOEZI DAKIKA 10
Elezea yafuatayo:
Sasa tutajaribu kuchora mitandao yetu ya kibinafsi. Chora picha yako katikati ya karatasi, kisha chora mitandao yako katika sehemu tofauti za karatasi.

Hii inaweza kuwa:
- Familia na marafiki.
- Mahali pa kazi na wafanyakazi wenzako / shule na wanafunzi wenzako.
- Jumuiya yako ya kidini na vikundi vingine vya kijamii unavyoshiriki – labda kupitia uraibu kama vile timu ya michezo au kikundi cha wanawake. Vikundi hivyo vinaweza kuwa rasmi au visivyo rasmi.
- Mtandao wako wa mitandao ya kijamii.

Kwa kila kikundi au mtandao ambao unautambua, fikiria ni jukumu gani unaweza kuwa nalo ili kuendeleza uhuru wa dini au imani ndani au kupitia mazingira hayo. Unayo dakika 10 kwa ajili ya hili.

JINSI YA KUHITIMISHA ZOEZI DAKIKA 4
Waombe washiriki wote wasimame katika duara na kuinua michoro yao. Toa maoni kuhusu jinsi picha zilivyo za kina na zinavyoonyesha nafasi mbalimbali tunazoshikilia maishani.

Sisistiza hoja zifuatazo:
- Katika kila mazingira tuliyoyatambua, tunaweza kuwa washuhudiaji au waponyaji wa dhati. Tunaweza kuwa nyenzo muhimu katika kuhamasisha uhuru wa dini au imani ndani na kupitia mitandao hii.
- Katika kila jambo utakalosikia na kufanya katika kipindi kilichosalia cha kozi hii, tafadhali fikiria maswali haya matatu. (Onyesha slaidi ya 12 ya PowerPoint au andika maswali haya kwenye bango-kitita.)
  - Naweza kufanya nini?
    Je, ninaweza kuchukua hatua katika nafasi yangu kama mzazi, mtoto, rafiki au jirani? Naweza kufanya nini kupitia jukumu langu kazini au maisha yangu binafsi – kwa mfano, katika jumuiya yangu ya kidini?
  - Tunaweza kufanya nini tukijipanga na kushirikiana?
    Je, jumuiya yangu ya kidini, kikundi cha vijana au mahali pa kazi kinaweza kuchukua hatua fulani, kwa mfano?
  - Tunaweza kuwahamasisha watu/taasisi gani kuchukua hatua?
    Kuna mambo ambayo hatuwezi kufanya sisi wenyewe, lakini wengine wanaweza. Labda jumuiya nyingine ya kidini au mwalimu mkuu wa shule ya mtaa anaweza kuchukua hatua. Tunaweza kuhimiza nani kuchukua hatua?

4. Uwasilishaji: Utangulizi kwa mbinu Dakika 10

WASILISHO

MAELEZO NA LENGO

Wasilisho hili linakusudia kuongeza uelewa wa njia za vitendo ambazo washiriki wanaweza kutumia kukuza haki za binadamu. Linatambulisha aina nne za mbinu ambazo watu wanaweza kutumia ili kukuza haki za binadamu.

NYENZO

- Nakala ya mwongozo inapatikana kwenye ukurasa wa 121 wa Kiongozi hiki.
- Nakala hii inalingana na slaidi za 13-24 za PowerPoint ya kipindi na imejumuishwa kwenye maelezo ya msemaji kwa slaidi hizo.
- Toleo la mwongozo huu linapatikana katika mfumo wa kompyuta la Word ambalo linaweza kuhaririwa.

MAANDALIZI YA AWALI

Jiandae kulingana na mwongozo uliotolewa kwenye ukurasa wa 15, 'Jinsi ya kujiandaa kwa kila kipindi'. Soma na rekebisha nakala na slaidi za PowerPoint (au tengeneza bango-kitita kwa hoja kuu zilizo kwenye slaidi). Fanya mazoezi ya kuwasilisha mada pamoja na slaidi/bango-kitita.

KIDOKEZO! Waombe washiriki wahifadhi maswali/maoni yao hadi mwisho wa Uwasilishaji wako.

5. Zoezi la Majadiliano: Kuzungumzia mbinu za dharura Dakika 45

ZOEZI LA KIKUNDI

MAELEZO NA LENGO

Hili ni zoezi la mjadala wa kikundi ambapo washiriki wanajifunza kuhusu mbinu za dharura kwa kuchunguza mifano halisi ya jinsi watu wanavyozitumia kukabiliana na changamoto zinazohusiana na uhuru wa dini au imani. Washiriki watafakari kuhusu mbinu hizo na kubuni mawazo ya kuzitumia katika jamii zao ili kukuza uhuru wa dini au imani, wakikuza maarifa na ujuzi wa kuchukua hatua.

NYENZO

- Chapisho la mabango yote ya 'Mbinu za dharura'.
- Karatasi za kunata na kalamu.
- Bango-kitita yenye kichwa 'Mawazo ya utekelezaji: Mbinu za dharura'.

JINSI YA KUANZA ZOEZI DAKIKA 4

Toa hoja zifuatazo:

- Katika sehemu iliyosalia ya kipindi hiki, tutazingatia mbinu za dharura na kufikiria ikiwa tunaweza kuzitumia kushughulikia changamoto zinazohusiana na uhuru wa dini au imani katika jamii zetu. Tutazichambua mbinu nyingine katika kipindi kijacho.
- Kupitia zoezi hili, tutajifunza kuhusu mbinu za dharura na kubuni mawazo mengi kadri iwezekanavyo kuhusu hatua za kuchukua katika jamii yetu. Tukifikiria – ninaweza kufanya nini, tunaweza kufanya nini, tunaweza kuwahamasisha wengine wafanye nini.

- Lakini kabla ya kuanza, tukumbuke nini kinachohusisha 'dharura' ya uhuru wa dini au imani. Mbinu za dharura hutumiwa pale ambapo ukiukwaji wa haki za binadamu unafanyika au uko karibu kutokea kwa mtu fulani mahali fulani. Kwa hiyo, ni aina gani za ukiukwaji wa uhuru wa dini au imani tunajaribu kushughulikia kwa kutumia mbinu hizi?
  Unyanyasaji, kwa mfano unyanyasaji mitaani wa wanawake wa jamii ndogo
  Matamshi ya chuki (mtandaoni au ana kwa ana):
  - Uhalifu wa chuki kama vile uharibifu wa mali au shambulio
  - Mashambulizi dhidi ya maeneo ya ibada
  - Vurugu za kijamii
  - Kukamatwa kiholela

JINSI YA KUENDESHA ZOEZI DAKIKA 40

- **MJADALA KATIKA MAKUNDI** (DAKIKA 20)
  - Gawa washiriki katika makundi matatu. Kuna mbinu tatu za dharura: Kuzuia – Kusimamisha na kuokoa – na Kuomba msaada/kutoa onyo. Eleza kuwa kila kundi litazingatia mbinu moja kati ya hizi.
  - Gawa kila kundi karatasi za kunata na kalamu, bango linaloeleza mbinu husika pamoja na mabango ya hadithi yanayohusiana, na karatasi ya maswali ya majadiliano kwa mbinu yao maalum.
  - Toa maagizo yafuatayo kwa makundi: Someni maandishi kwenye mabango. Kisha jadilini maswali yaliyo kwenye karatasi ya maswali. Katika mjadala wenu, mtabuni mawazo ya kutumia mbinu hii – andikeni mawazo yenu ya utekelezaji kwenye karatasi za kunata. Mna dakika 20 kwa ajili ya majadiliano.

- **MAONI YA PAMOJA** (DAKIKA 20)
  Toa hadi dakika 5 kwa kila kundi kuwasilisha mbinu waliyoangazia na mawazo yao ya utekelezaji. Bandika mawazo yao ya utekelezaji kwenye bango-kitita yenye kichwa Mawazo ya Utekelezaji: Hatua za Dharura.
  Baada ya kuwasilisha, fungua mjadala kwa maswali yafuatayo:
  - Baada ya kusikiliza makundi mengine, je, kuna mtu yeyote mwenye mawazo zaidi kuhusu namna ya kushughulikia dharura?
  - Ilikuwa ngumu kufikiria mawazo mapya?
  - Ni mawazo yapi mliyopenda zaidi?

JINSI YA KUHITIMISHA ZOEZI DAKIKA 1

Himiza kundi kwa kupongeza mawazo yoyote waliyotoa, ukitambua kuwa si rahisi kila mara kubuni mawazo mapya – hasa yanayohusiana na mbinu za dharura, ambapo kuchukua hatua kunaweza kuwa hatari au lenye changamoto.

6. Maoni ya hitimisho Dakika 5

GUMZO FUPI

Hitimisha kipindi kwa kushiriki maoni yafuatayo, ukionyesha slaidi za 26-28:

- Mapema katika kipindi hiki, tulijadili njia za kuhamasika kutoka kuwa washuhudiaji hadi kuwa waponyaji. Tulizungumzia kuhusu kujenga mahusiano, kushirikiana, kutafuta taarifa, pamoja na kupanga na kujiandaa.

- Kuhusiana na mbinu za dharura, hii inahusisha kuuliza aina ya maswali tuliyojadili hivi punde. Kwa mfano:
  - Kutambua ni nani anaweza kuathirika na dharura zinazohusiana na uhuru wa dini au imani, wapi na lini.
  - Kufikiria jinsi tunavyoweza kuitikia dharura hizi kabla hazijatokea. Kwa mfano: Je, ninataka kuchukua hatua gani kibinafsi ninapoona hotuba ya

  chuki kwenye mitandao ya kijamii au unyanyasaji mitaani? Au ninataka kuunda mwitikio wa pamoja, ulioandaliwa vyema, kama sehemu ya kundi linalopanga, kujiandaa na kuchukua hatua kwa pamoja?
  - Kuhakikisha kuwa tunazo taarifa zote na mawasiliano yanayohitajika ili kuweza kuitikia ipasavyo.
  - Na bila shaka, kutathmini hatari ili kuhakikisha tunabaki salama na hatuzidishi tatizo.

- Inawezekana kwamba mbinu za dharura si zile tunazotaka kutumia. Kwa mfano, huenda tukawa katika nafasi bora zaidi ya kuhamasisha jamii au kufanya kampeni za mabadiliko. Hakuna mtu anayeweza au anayepaswa kujaribu kufanya kila kitu!
- Katika kipindi kijacho, tutajifunza na kubuni mawazo ya hatua kuhusu mbinu za mabadiliko, mbinu za kujenga na mbinu za uponyaji. Tunakusudia kukusanya mawazo mengi ya utekelezaji iwezekanavyo!
- Kisha, katika vipindi viwili vya mwisho vya kozi, tutaanza kuchambua mambo kwa undani – tukifikiria ni matatizo yapi tunataka kuyashughulikia hasa, na ni mawazo yapi ya hatua yatakayokuwa yenye ufanisi na yanayoweza kutekelezeka kwetu.
- Hitimisha kipindi kwa kuwashukuru wote kwa ushiriki wao makini.

Vyanzo

Washuhudiaji na waponya: Imetolewa katika Human Rights Education Handbook, Kristi Rudelius-Palmer, Kituo cha Chuo Kikuu cha Minnesota cha Nyenzo za Haki za Binadamu. https://ihs.smc.global/wp-content/uploads/documents/Human_rights_education_handbook.pdf

Utangulizi wa mbinu/Kuzungumzia mbinu za dharura: Uwasilishaji wa asili na mazoezi yaliyojengwa kwa kuzingatia mchakato wa mbinu za mradi wa New Tactics in Human Rights. www.newtactics.org

Mwongozo wa uwasilishaji

Mbinu za kuhamasisha haki za binadamu

Nakala hii ya uwasilishaji wa kipindi cha 6 inaonyeshwa kwenye slaidi za 13-24 za PowerPoint ya kipindi.

UTANGULIZI

Katika kipindi hiki na vile vilivyotangulia, tumesikia hadithi kuhusu watu mbalimbali wanaofanya juhudi tofauti ili kuboresha hali ya uhuru wa dini au imani katika jamii yao. Pia, tumekumbushana matatizo yanayohusiana na uhuru wa dini au imani katika jamii yetu. (*bango-kitita yenye mada ya uhuru wa dini au imani katika mji wetu*).

Sasa tunakwenda kujifunza kuhusu mbinu mbalimbali zinazoweza kutumika kuhamasisha na kulinda haki za binadamu katika ngazi ya jamii. Pia tutafikiria jinsi tunavyoweza kutumia mbinu hizi kushughulikia matatizo tuliyotambua katika jamii yetu.



Kwa hivyo, tunaposema mbinu tunamaanisha nini? Mbinu zinafafanuliwa kama 'mfululizo wa hatua zilizopangwa ili kufanikisha lengo fulani.'

Kuna aina nne tofauti za mbinu katika kazi ya haki za binadamu. Ili kuelewa aina hizi nne za mbinu, tunaweza kutumia moto kama sitiari ya kuwakilisha ukiukaji wa haki za binadamu. Hapa hatuzungumzii moto mzuri wa kuota joto, bali moto hatari usiodhibitika. Kama ilivyo kwa ukiukaji wa haki za binadamu, moto huathiri watu – huleta msongo wa mawazo, hujeruhi na hata kuua watu, na huharibu mali pamoja na ardhi.

Basi tunazuiaje moto? Tunafanya mambo manne:

1. MBINU ZA DHARURA

Mbinu za dharura zinahusu kuzuia moto kabla haujaanza, kuzima moto, na kuwaokoa watu.

Utafanya nini ukimwona mtoto akicheza na kiberiti? Bila shaka, utazima cheche za moto na kuchukua viberiti hivyo! Utajaribu kuzuia moto usianze. Ikiwa umechelewa na moto mdogo tayari umewaka, huenda utajaribu kuuzima mwenyewe kwa kutumia kizima moto au ndoo ya maji. Utafanya kila uwezalo kulinda watu na mali ili kuzuia moto usisambae. Na ikiwa moto ni mkubwa mno kushindwa nao peke yako, utaita kikosi cha zimamoto na kuwaonya watu waondoke eneo hilo.

Mbinu za dharura katika haki za binadamu zinafanana kabisa na hili! Tunazitumia kukabiliana na ukiukaji wa haki za binadamu unaokaribia kutokea au ambao tayari unafanyika kwa watu fulani, mahali fulani. Hii inaweza kumaanisha kuingilia moja kwa moja ili kuzuia au kusitisha ukiukaji na kuwaokoa wahanga, au inaweza kumaanisha kuita msaada na kuwaonya wale walio hatarini.



Basi, ni ukiukaji gani wa uhuru wa dini au imani tunaoweza kutumia mbinu za dharura kuukabili? Unyanyasaji, hotuba za chuki, mashambulizi, uharibifu wa mali, mashambulizi kwenye maeneo ya ibada, ghasia za kijamii na kukamatwa kiholela ni mifano ya ukiukaji unaowalenga watu au makundi fulani, katika maeneo na nyakati maalum.

Ingawa mbinu za dharura hutumika kukabiliana na matukio ya papo hapo kama haya, zinahitaji maandalizi – kujua nini cha kufanya. Kama vile watu hujifunza namba ya kikosi cha zimamoto au jinsi ya kutumia kizima moto, nasi tunaweza kujifunza mbinu za kuzuia, kusitisha na kuita msaada wakati ukiukwaji wa haki za binadamu unapotokea.

2. MBINU ZA MABADILIKO



Moto huwaka na kusambaa kwa sababu fulani – kwa mfano, nyaya za umeme zilizowekwa visivyo. Mbinu za mabadiliko zinahusu kubadili hali zinazosababisha moto kuwaka – kwa mfano, kuhakikisha kuwa kuna kanuni za ujenzi zinazohakikisha usalama wa nyaya za umeme.

Ukiukaji wa haki za binadamu hutokea kwa sababu fulani pia – kwa mfano, kwa sababu jamii haina sheria zinazohitajika kulinda watu au kwa sababu wale wanaopaswa kuhakikisha sheria hizo zinafuatwa hawafanyi hivyo. Kwa maneno mengine, jamii 'imeunganishwa' visivyo.

Ukiukwaji mwingi wa haki za binadamu unaweza tu kutatuliwa kwa kuwashawishi watu kubadili sheria au jinsi mambo yanafanywa. Tunaweza kufanya hivyo kwa njia nne tofauti:

- kwa kuendesha kampeni na maandamano ili kuonyesha ukubwa wa tatizo,
- kwa kuwashawishi wale wenye mamlaka ya kufanya mabadiliko kwamba wanapaswa kuchukua hatua – tutaweza kuita hii utetezi,
- kwa kutoa motisha kwa watu kubadili tabia zao,
- au kwa kukataa kwa amani sheria mbaya au mila potofu ili kuonyesha kuwa hatuzikubali.

Hizi ndizo mbinu za mabadiliko. Kawaida hulenga matatizo ya muda mrefu na ya kimuundo katika jamii – matatizo yanayowaathiri watu wengi katika maeneo mengi.

3. MBINU ZA KUJENGA

Njia nyingine ya kusaidia kuzuia moto ni kwa kujenga uelewa wa umma na kubadili mitazamo, kwa mfano, kwa kuhamasisha watu kuhusu hatari za kutupa mabaki ya sigara kwenye ardhi kavu. Tunaweza pia kuimarisha ushiriki wa jamii – kwa kushirikisha watu wengi zaidi katika shughuli za kujitolea za kuzima moto. Aidha, tunaweza kujenga ujuzi – kwa kuhakikisha kuwa watu wanajua jinsi ya kutumia kizima moto.

Katika haki za binadamu, mbinu za kujenga zinahusu kazi ya muda mrefu ya kujenga utamaduni wa kuheshimu haki za binadamu.Hii inamaanisha kufanya kazi kuelekea jamii ambayo kila mtu anaelewa haki zake na za wengine, anaona heshima kwa haki za binadamu kama jambo la kawaida na sahihi, anajua la kufanya ikiwa haki zinakiukwa na anajua JINSI ya kuheshimu na kutetea haki zake na za watu wengine.

Kujenga jamii ya aina hii kunahusisha mambo manne:

- Kujenga uelewa kuhusu umuhimu wa haki za binadamu, ukiukwaji unaotokea na madhara yake.
- Kujenga ushiriki – kuhakikisha kuwa watu wengi zaidi wanajitolea kuchukua hatua za kutetea haki za binadamu.
- Kujenga ujuzi – ili watu wajue jinsi ya kutetea haki za binadamu.
- Na kujenga mitandao ya watu na mashirika yanayofanya kazi katika maeneo tofauti lakini kwa lengo moja kwa njia iliyoratibiwa.

Hizi ni mbinu za muda mrefu zinazounda mazingira muafaka kwa mabadiliko. Zinajenga msingi imara wa kutumia mbinu nyingine zote.

4. MBINU ZA UPONYAJI



Hatimaye, tunazo mbinu za uponyaji. Kama moto unavyoharibu watu, mali na jamii, ukiukwaji wa haki za binadamu pia unaleta madhara makubwa. Mbinu za uponyaji zinahusu kile tunachofanya ili kuwasaidia watu baada ya ukiukaji wa haki za binadamu kutokea.

Sehemu ya kazi hii ni kuhakikisha kuwa waathiriwa wanapata msaada wa kimatibabu, kimwili na kisaikolojia ili waweze kupona. Lakini pia ni suala la heshima na haki:

- kuhakikisha kuwa matukio yanarekodiwa ili yasiweze kufutwa au kupuuzwa.
- kuwapa watu nafasi ya kueleza na kuenzi yaliyowapata.
- kuhakikisha kuwa wahusika wanapata haki na fidia.

HITIMISHO

Njia zote hizi za kazi ni muhimu katika kutetea haki za binadamu. Zinakamilishana, zinaingiliana na zinaweza kutumiwa kwa wakati mmoja.

Hakuna mtu mmoja au shirika moja linaloweza kutumia mbinu zote – tunayo majukumu, ujuzi na fursa tofauti zinazoathiri uchaguzi wetu wa mbinu. Lililo muhimu ni kwamba kila mtu anaweza kufanya jambo fulani, na kwamba kwa kushirikiana kupitia mitandao ya watu na mashirika yanayolenga mwelekeo mmoja, tunaweza kuleta mabadiliko.

Sote tunaweza kuchangia kuzima moto wa ukiukaji wa haki za binadamu na kujenga jamii inayoheshimu haki za binadamu majumbani mwetu, katika jamii zetu, na ndani ya serikali zetu.

Shukurani
Mwongozo huu limechangiwa na linatumia toleo lililorekebishwa la mfumo wa mbinu uliotengenezwa na mradi wa New Tactics in Human Rights, unaosimamiwa na Kituo cha Waathiriwa wa Mateso. www.newtactics.org

Hadithi ya wanamabadiliko

Hadithi zifuatazo zinasomwa wakati wa utangulizi wa zoezi la 'Makundi ya kujadili hadithi ya wanamabadiliko' katika kipindi cha 6. Zinaonyeshwa kupitia slaidi za 3-10 za uwasilishaji wa PowerPoint wa kipindi hiki.

Hadithi ya Rahul, India

HADITHI

Rahul anaishi Bhagalpur, mashariki mwa India. Takriban asilimia 80 ya wakazi wa jiji hili ni Wahindu, huku asilimia 18 wakiwa Waislamu. Jiji hili lina historia ya machafuko, na mwaka 1989, zaidi ya Waislamu 1000 waliripotiwa kuuawa katika ghasia zilizosababisha watu 50,000 kupoteza makazi yao.

Rahul, ambaye ni Mhindu, anahusika na kituo cha amani cha kidini katika jiji hili. Kituo hiki hufanya kazi ya kujenga mahusiano na kuimarisha uaminifu kati ya jamii mbalimbali, kwa mfano, kupitia kamati za amani, kuandaa tamasha la kitamaduni kila mwaka, na kuwaunganisha viongozi wa kidini. Kazi hii ya muda mrefu ya kujenga amani huweka msingi wa kuchukua hatua za dharura pale hali inapozidi kuwa mbaya – jambo ambalo hutokea mara kwa mara.

Machafuko huwa ya kawaida hasa wakati wa kampeni za uchaguzi. Mwaka 2019, mgombea wa uchaguzi kutoka kundi la kitaifa la Wahindu aliongoza maandamano katika eneo la Waislamu na kutumia lugha ya chuki ili kuchochea ghasia. Vijana wa Kiislamu waliporudisha majibu kwa hasira, mgombea huyo alianzisha ghasia zilizoharibu maduka na nyumba. Kulikuwa na hatari kubwa ya machafuko kusambaa katika maeneo mengine na kuwa mabaya zaidi. Rahul na wenzake walitambua jinsi hali hii ilivyokuwa hatari.

Katika siku zilizofuata, Rahul na wenzake waliandaa mikutano ya jamii katika vitongoji vya Waislamu na Wahindu vilivyokuwa katika hatari kubwa ya kushuhudia ghasia. Katika mikutano hiyo, makundi ya wajitolea wa amani yaliundwa, na wajitolea hao walienda kutoka nyumba hadi nyumba katika vitongoji vyao.

Rahul anasema, "Ilikuwa muhimu wanaume na wanawake waende pamoja wawili wawili, ili kuwe na mtu ambaye angeweza kuzungumza kwa uhuru na yeyote aliyefungua mlango."

Wajitolea waligawa vipeperushi, wakazungumza na kusikiliza majirani zao, wakisisitiza kuwa ghasia zingezidisha matatizo kwa kila mtu, bila kujali dini. Kwa bahati nzuri, mikutano ya jamii na wajitolea hao ilisaidia kutuliza hali jijini.

Chanzo
Kituo cha Utafiti wa Jamii na Usekulari, India

Usihukumu kitabu kwa jalada lake – Maktaba ya Binadamu™, Denmark

HADITHI

Katika miaka ya katikati ya 1990, marafiki wanne walianzisha shirika la vijana ili kupambana na vurugu mijini. Wanachama wake waliongezeka, na mwandaaji wa tamasha la muziki nchini Denmark akawaomba waje na wazo la tukio litakalohamasisha mazungumzo kati ya wageni wa tamasha. Hapo ndipo walipobuni wazo la maktaba ya binadamu, ambapo wageni wanaweza "kukopa" vitabu vya binadamu – watu walioko tayari kushiriki mazungumzo ya heshima kuhusu utambulisho na uzoefu wao wa maisha.

Kwa kawaida, vitabu vya binadamu ni watu kutoka katika jamii ya eneo husika wanaojitolea kuruhusu hadithi zao kuwa sehemu ya uzoefu wa kujifunza kwa wengine. Mara nyingi, wanaojitolea ni watu ambao kipengele fulani cha utambulisho wao kinahusishwa na ubaguzi au unyanyapaa – kwa mfano, dini yao, imani, kabila, mwelekeo wa kijinsia, ulemavu, au hali ya kuwa na virusi vya UKIMWI. Hii husaidia kupunguza dhana potofu zisizo sahihi. Shirika la Maktaba ya Binadamu™ sasa lina shughuli katika zaidi ya nchi 85.

Chanzo
Shirika la Maktaba ya Binadamu www.humanlibrary.org

Mamlaka yenye ushawishi wa kuchukua hatua, Kyrgyzstan

HADITHI

Baada ya mapinduzi ya mwaka 2010, genge dogo la wahuni wasiotaka kuvumilia imani nyingine lilianza kuvamia na kupora maeneo ya ibada ya madhehebu ya Kiprotestanti na Kiothodoksi. Mashambulizi haya yaliendelea kwa takriban miezi sita. Licha ya malalamiko mengi, hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa na Ofisi ya Mwendesha Mashtaka, Tume ya Serikali ya Masuala ya Kidini, wala Wizara ya Mambo ya Ndani. Hata hivyo, mamlaka ziliwashauri waathiriwa wajitatulie tatizo hilo wenyewe.

Wakiwa wamekata tamaa, viongozi wa kidini waliungana na kuwasiliana na gazeti moja la kitaifa ili kufichua matukio haya na kutochukuliwa hatua na mamlaka husika. Habari zilimfikia Rais, ambaye alichukua suala hilo moja kwa moja chini ya usimamizi wake. Ndani ya siku nne, wahusika wote wa genge hilo walikamatwa.

Chanzo
Nellya Shakirova, Mchungaji, United Methodist Church in Bishkek.

KIPINDI CHA 7

Kuzungumza kuhusu mbinu

Muhtasari wa kipindi

Uchunguzi wa mbinu za kuendeleza haki za binadamu ulioanza katika kipindi cha 6 unaendelea katika kipindi cha 7. Vipindi hivi viwili vimeunganishwa – vina malengo ya pamoja ya kujifunza na mchakato mmoja wa kujifunza. Tafadhali angalia mpango wa kipindi cha 6 kwa malengo ya kujifunza ya kipindi hiki. Kutegemeana na jinsi kundi lako linavyojadili kwa upana, kipindi hiki kinaweza kuchukua muda mfupi kuliko masaa mawili yaliyopangwa.

Yaliyomo katika kipindi na muda

Ukaribisho na utangulizi Kuwakumbusha washiriki kuhusu aina nne za mbinu zilizowasilishwa katika kipindi kilichopita.	Dakika 5
Mjadala wa kikundi: Kuzungumza kuhusa mbinu, sehemu ya 1 Washiriki wanajadili mbinu za mabadiliko, kujenga na uponyaji na kubuni njia za kuzitumia katika muktadha wao.	Dakika 50-65
Zoezi la kuchangamsha: Utosini hadi unyayoni Zoezi la mwili ambapo washiriki wanaiga harakati za mwezeshaji.	Dakika 5
Mjadala wa pamoja: Kuzungumza kuhusa mbinu, sehemu ya 2 Mjadala wa pamoja kuhusu mawazo ya utekelezaji yaliyotokana na kazi ya vikundi.	Dakika 20-40
Zoezi la kufunga: Vielelezo vya hisia Washiriki waonyesha jinsi wanavyojihisi kuhusu walichojifunza kwa kutumia mionekano ya kisanii.	Dakika 5
JUMLA YA MUDAU	**Mpaka masaa 2**

Jiandae

Jiandae kwa kipindi kwa mujibu wa mwongozo uliopo ukurasa wa 15, 'Jinsi ya kujiandaa kwa kila kipindi'. Kumbuka – unawafahamu vizuri wanafunzi wako! Unakaribishwa kurekebisha na kubadilisha vipengele vyovyote vya kipindi ili vikidhi mahitaji ya kundi lako.

NYENZO ZA KIPINDI HIKI

Mbali na nyenzo za kawaida kwa kila kipindi zilizoorodheshwa ukurasa wa 16, utahitaji nyenzo zifuatazo ili kuendesha kipindi hiki:

- Nakala zilizochapishwa za mbinu/hadithi za 'Mabadiliko', 'Kujenga' na 'Uponyaji'.
- Karatasi tatu za bango-kitita zilizoandaliwa mapema zenye vichwa vya habari 'Mawazo ya Utekelezaji: Aina ya Mbinu'– moja kwa kila aina ifuatayo ya mbinu: Mbinu za Mabadiliko, Mbinu za Kujenga, Mbinu za Uponyaji.
- Bango-kitita yenye kichwa 'Mawazo ya Hatua: Mbinu za Dharura' kutoka kipindi cha 6.
- Bango-kitita zenye kichwa 'Ramani ya uhuru wa dini au imani ya mji wetu' kutoka kipindi cha 5.
- Karatasi nyingi za kubandika na kalamu.

NYENZO ANDAMIZI za kipindi hiki zinaweza kupatikana hapa.

ANDAA UKUMBI

Kabla ya kipindi, panga viti katika nusu-mduara vikielekea mbele.

Weka mabango ya mbinu na hadithi za mabadiliko, kujenga, na uponyaji kwenye meza tatu tofauti ambako washiriki wataweza kukaa (kila aina ya bango iwe kwenye meza yake). Weka bango-kitita yenye maandishi 'Mawazo ya Utekelezaji' inayolingana na mbinu hizo kwenye meza pamoja na mabango, pamoja na karatasi za kunata na kalamu.

Bandika bango-kitita za 'Ramani ya uhuru wa dini au imani' (kutoka kipindi cha 5) na mabango ya mbinu za dharura (kutoka kipindi cha 6) kwenye kuta.

'Kuzungumza kuhusa mbinu'

"Kilikuwa kipindi murwa zaidi. Shughuli zilisaidia washiriki kugundua njia mbalimbali za kukabiliana na ukiukwaji wa haki za binadamu. Mabango yaliwasaidia kuelewa dhana ya mbinu na kuwaza kuhusu hatua wanayoweza kuchukua katika kuendeleza haki za binadamu katika jamii. Washiriki tofauti waliweza kujiona wakitumia mbinu mbalimbali."

HAMMAM HADDAD, MWEZESHAJI, JORDAN

Mpango wa kina wa kipindi

1. Ukaribisho na utangulizi   Dakika 5

GUMZO FUPI

LENGO

Kuwakumbusha washiriki kuhusu aina nne za mbinu za kushughulikia ukiukwaji wa haki za binadamu ambazo zilijadiliwa katika kipindi kilichopita.

NYENZO

Slaidi ya PowerPoint ya kipindi au bango la muhtasari wa mbinu (inapatikana ukurasa wa 2 katika waraka wa mabango ya mbinu).

NINI CHA KUSEMA

Karibisha kila mmoja kwenye kipindi. Eleza hoja zifuatazo kwa kurejelea slaidi ya 3 ya PowerPoint au bango la muhtasari wa mbinu:

Kwenye kipindi kilichopita, tulijifunza kuhusu mbinu mbalimbali zinazoweza kutumika kushughulikia ukiukwaji wa haki za binadamu. Je, mnakumbuka tulivyotumia mfano wa moto kuwakilisha ukiukwaji wa haki za binadamu na tukazungumzia njia tofauti za kukabiliana na moto?

- Tunazuia moto kusambaa na kuuzima, tunaita msaada na kuwaonya watu. Hizi ni mbinu za dharura.
- Tunapigania sheria bora za usalama wa moto na kupiga marufuku bidhaa hatari kupitia kampeni na utetezi. Hizi ni mbinu za mabadiliko.
- Tunajenga uelewa wa umma, ushirikishwaji na ujuzi ili watu wajue jinsi ya kuzuia na kuzima moto. Hizi ni mbinu za kujenga.
- Tunawatunza waathiriwa wa moto, tunakumbuka waliopoteza maisha, na kutafuta haki na fidia kwa waathiriwa na familia zao. Hizi ni mbinu za uponyaji.

Mbinu za dharura, mabadiliko, kujenga na uponyaji ndizo aina nne za mbinu zinazoweza kutumika kushughulikia ukiukwaji wa haki za binadamu.

Katika kipindi kilichopita, tulijadili mbinu za dharura na tukafikiria mawazo ya hatua za kutumia mbinu hizi kushughulikia matatizo kama vile matamshi ya chuki au unyanyasaji katika jamii yetu.

Katika kipindi hiki, tutaendeleza mjadala huu kwa kuangalia aina tatu zilizobaki za mbinu: mbinu za mabadiliko, mbinu za kujenga, na mbinu za uponyaji.

2. Mjadala wa kikundi: Kuzungumza kuhusa mbinu Dakika 50-65

ZOEZI LA KIKUNDI

MAELEZO

Makundi yanazunguka kati ya meza, yakichunguza aina 3 za mbinu moja baada ya nyingine. Wanasoma hadithi kuhusu watu wanaotumia mbinu hizo na kubuni mawazo ya utekelezaji.

LENGO

Kuimarisha na kuendeleza uelewa wa mbinu za kuhamasisha haki za binadamu na kutumia mafunzo haya katika muktadha wao, kwa kubuni mawazo ya utekelezaji.

NYENZO

- Slaidi ya 4 ya PowerPoint (maelekezo ya majadiliano ya kikundi) au bango-kitita iliyo na maelekezo.
- Nakala iliyochapishwa ya mabango ya hadithi kuhusu mbinu za Mabadiliko, Kujenga, na Uponyaji.
- Bango-kitita zenye kichwa "Mawazo ya Utekelezaji: Aina ya Mbinu" (moja kwa kila aina ya mbinu tatu).
- Karatasi za kunata na kalamu.

MAANDALIZI YA AWALI

Weka mabango ya mbinu/hadithi na bango-kitita za mawazo ya utekelezaji kwenye meza tatu (moja kwa kila aina ya mbinu, kwa mfano, mbinu za kujenga), kama ilivyoelezwa katika sehemu ya 'andaa ukumbi' hapo juu.

JINSI YA KUANZA ZOEZI DAKIKA 5

Onyesha slaidi ya 4 (au bango-kitita iliyo na maelekezo) kwa muda wote wa zoezi

Eleza yafuatayo:

- Tunaenda kufanya zoezi la kuchangia wa mawazo kwa vikundi. Tutajadili aina tatu za mbinu – mbinu za mabadiliko, mbinu za kujenga, na mbinu za uponyaji – katika vikundi vitatu. Kila kikundi kitachukua dakika 20 kusoma mabango na kubuni mawazo kwa ajili ya aina moja ya mbinu. Baada ya hapo, vikundi vitabadilishana na kutumia dakika 20 kujadili aina nyingine ya mbinu, kisha vitabadilishana tena kwa mjadala wa mwisho.

- Soma na utafakari: Ukifika kwenye mabango yenu, tumia dakika chache kusoma na kutafakari yaliyomo, pamoja na mawazo ya hatua yaliyoachwa na vikundi vya awali kwenye vidokezo vya karatasi za kubandika.

- Uchangiaji wa mawazo: Ukizingatia matatizo tuliyotambua kwenye ramani ya uhuru wa dini au imani ya mji wetu (onyesha bango-kitita ya ramani ya uhuru wa dini au imani), jadilini mawazo mengi iwezekanavyo kuhusu jinsi mbinu hizi zinavyoweza kutumika kukabiliana na matatizo hayo.

- Andika mawazo yenu kwenye vidokezo vya karatasi za kunata na uzibandike kwenye karatasi ya 'mawazo ya utekelezaji iliyo karibu na mabango. Tafadhali andikeni kwa uwazi ili wengine waweze kuyasoma! Katika hatua hii, si lazima mawazo yawe ya uhalisia – kuwa mbunifu kadri inavyowezekana!

- Kumbuka kufikiria hatua tunazoweza kuchukua kama watu binafsi katika maisha yetu ya kila siku na hatua tunazoweza kuchukua kama vikundi au mashirika – labda kupitia jumuiya zetu za kidini, sehemu zetu za kazi, vikundi vya vijana, au kwa kukusanya kundi jipya la watu kwa ajili ya hatua fulani.

JINSI YA KUENDESHA ZOEZI DAKIKA 45-60

Gawanya washiriki katika makundi matatu. Yaeleze makundi ni seti gani ya mabango wanapaswa kuanza nayo kisha waache waanze kufanya kazi. Yaambie makundi wakati wa kuhamia kwenye kundi linalofuata la mabango – kila baada ya dakika 20. Wakati wa kazi ya makundi, tembea kati ya makundi ili kufuatilia maendeleo yao.

(Zoezi hili litaendelea kwa mjadala wa pamoja baada ya kichangamshi.)

3. Zoezi la kuchangamsha: Utosini hadi unyayoni Dakika 5

ZOEZI LA PAMOJA

MAELEZO

Hii ni shughuli ya kuchangamsha mwili ambapo washiriki wanarudia kile ambacho mwezeshaji anasema na kufanya. Inaweza kurekebishwa kwa njia mbalimbali kulingana na mahitaji.

LENGO

Kuongeza viwango vya nguvu.

JINSI YA KUANZA ZOEZI

Waambie washiriki kwamba sasa ni wakati wa kuongeza nguvu zetu ili tuendelee kuwa wabunifu! Waombe wote wasimame na kuhakikisha kuna nafasi ya kutosha kati yao na mtu mwingine. Waeleze kwamba kwa dakika chache zijazo, wanapaswa kurudia kile utakachosema na kufanya, kwa kurudia maneno yako na kunakili harakati zako..

JINSI YA KUENDESHA ZOEZI

Taja sehemu zifuatazo za mwili kwa sauti huku ukiweka mikono yako kwenye sehemu husika:Kichwa, mdomo, mabega, viwiko, nyonga, magoti, vidole vya miguu.

Anza kwa kutamka maneno haya polepole huku ukifanya harakati kwa utulivu. Kisha, rudia mchakato huo kwa kuongeza kasi na nishati katika harakati zako kila wakati.

4. Maoni ya pamoja: Kuzungumza kuhusu mbinu Dakika 20-40

MJADALA WA PAMOJA

Huu ni mwendelezo wa zoezi la mjadala wa kikundi kuhusu 'Kuzungumza kuhusu mbinu'.

JINSI YA KUENDELEA NA ZOEZI

Chukua bango-kitita yenye mawazo matatu ya hatua ('Action ideas') kutoka kwenye meza, pamoja na bango-kitita yenye mawazo ya utekelezaji wa dharura kutoka kwenye kipindi kilichopita. Bandika karatasi hizo nne kwenye ukuta kwa nafasi inayoruhusu kila moja kuonekana wazi.

Waombe washiriki wakusanyike karibu na karatasi hizo na kuzisoma kwa makini. Baada ya dakika chache, waombe wachague wazo moja la hatua wanaloona ni wazo zuri ambalo linaweza 'kufanya kazi' katika muktadha wao. Wanapaswa kuchukua karatasi ndogo ya kunata yenye wazo hilo kutoka kwenye bango-kitita kisha wakae chini (katika mjadala wa pamoja).

Mpe kila mshiriki nafasi ya kushiriki kwa kueleza wazo alilochagua na sababu ya kulichagua. Kisha waulize wengine ambao wanafikiri hilo ni wazo zuri kuinua mikono yao. Chagua mmoja au wawili kati yao waeleze kwa nini wanafikiri ni wazo bora.

Ikiwa kuna muda baada ya kila mshiriki kushiriki, waulize ikiwa kuna mawazo mengine ya hatua waliyopenda lakini hayakuchaguliwa na yeyote.

Kusanya karatasi ndogo zote za kunata zilizo na mawazo ambayo washiriki wamechagua na zibandike kwenye bango-kitita mpya yenye kichwa 'Mawazo yetu pendwa ya utekelezaji.

JINSI YA KUHITIMISHA ZOEZI

Washiriki hutumia nyuso na miili yao kuunda vielelezo vya hisia vinavyoonyesha wanavyojihisi kuhusu yale waliyojifunza katika vipindi vya kuzungumza kuhusu mbinu za. Zoezi hili linaweza kuachwa ikiwa muda hautoshi.

5. Zoezi la kufunga: Vielelezo vya hisia Dakika 5

ZOEZI LA PAMOJA

MAELEZO NA LENGO

Washiriki wanatumia nyuso na miili yao kutengeneza vielelezo/maumbo ya kuonesha hisia ili kuonyesha namna wanavyojisikia jinsi walivyojifunza katika kipindi cha mbinu. Unaweza kuruka zoezi hili kama hauna muda.

JINSI YA KUENDESHA ZOEZI

Waombe washiriki wote wasimame. Waambie wafikirie neno moja linaloeleza jinsi wanavyojihisi kuhusu yale waliyojifunza katika vipindi vya kuzungumza kuhusu mbinu za. Kisha, waambie watumie nyuso na miili yao kuunda kielelezo cha hisia kinachoakisi hisia hiyo.

Baada ya kila mmoja kutengeneza kielelezo chake cha hisia, tembea kuzunguka duara ukiwaomba washiriki waseme neno walilokuwa wakifikiria.

JINSI YA KUHITIMISHA ZOEZI NA KIPINDI

Baada ya kila mshiriki kuzungumza, thibitisha hisia zote, iwe ni chanya au hasi, kama vile kuhisi kusongwa na wingi wa taarifa mpya au kulemewa na jukumu la kuhamasisha uhuru wa dini au imani.

Tambua kuwa kikao hiki kimejumuisha maarifa mengi na kwamba tumechunguza mbinu mbalimbali. Eleza kuwa si mkakati mzuri wala hali halisi kwa mtu mmoja au shirika moja kujaribu kufanya kila kitu peke yake. Badala yake, kinachohitajika ni wadau tofauti wanaotekeleza hatua zinazokamilishana.

Lengo la kuchunguza mbinu hizi zote ni kutambua mambo ambayo yanawezekana na ni ya kimkakati kwa SISI kuyatekeleza, kulingana na nafasi yetu na muktadha wetu. Katika vipindi viwili vya mwisho, tutachagua changamoto muhimu na mawazo ya hatua tunayoweza kutumia katika uundaji wa mipango ya utekelezaji.

Hakuna mtu anayeweza kufanya kila kitu—lakini kila mmoja wetu anaweza kuchangia kwa njia fulani, na kwa pamoja, mchango wetu unaweza kuleta mabadiliko makubwa.

Chanzo

Kuzungumza kuhusu mbinu: Zoezi la asili lililotokana na marekebisho ya muundo wa mbinu uliotengenezwa na New Tactics in Human Rights Project. www.newtactics.org

KIPINDI CHA 8

Safari ya mabadaliko yetu

Muhtasari wa kipindi

Vipindi vya 8 na 9 'vimeunganishwa'—vikishirikisha malengo ya pamoja ya kujifunza na mchakato mmoja wa kujifunza. Katika vipindi hivi, washiriki hutumia maarifa na mawazo ya hatua waliyobuni katika vipindi viwili vilivyopita ili kuandaa mpango wa utekelezaji katika mfumo wa safari ya mabadiliko inayoonekana.

Washiriki wanatambua matatizo wanayotaka kushughulikia na kuongozwa katika mchakato wa kuyafanya yawe dhahiri zaidi—kutengeneza malengo, kutambua wahusika wengine wanaohusika na jinsi ya kushirikiana nao, kuchagua mbinu na hatua, kuandaa jumbe, na kutathmini hatari.

Kwa kuzingatia muda uliopo, lengo si kuunda mpango kamili wa utekelezaji, bali kujifunza na kufanya mazoezi ya ujuzi wa kupanga hatua. Mipango inayoundwa inaweza kuwa mipango halisi ambayo washiriki wanakusudia kutekeleza au mipango ya mazoezi inayowapa ujuzi wa kutekeleza mchakato wowote wa mabadiliko watakaoshiriki.

Malengo ya mafunzo

Kipindi hiki kinazingatia kukuza ujuzi wa kupanga hatua. Kufikia mwisho wa vipindi vya 8 na 9, washiriki wataweza:

- kuandaa mipango rahisi ya utekelezaji wa kukuza uhuru wa dini au imani katika jamii.
- kutaja hatua mahususi wanazoweza kuchukua binafsi ili kuhamasisha uhuru wa dini au imani na haki nyinginezo.
- kueleza dhamira yao ya kuchukua hatua ili kukuza uhuru wa dini au imani na haki nyinginezo.

Pale inapowezekana, washiriki wataweza:

- kutekeleza mipango yao ya utekelezaji baada ya mafunzo.

ZINGATIA

Haki zetu za binadamu zina uhusiano wa karibu. Mara nyingi, ukiukwaji wa uhuru wa dini au imani huambatana na ukiukwaji wa haki nyingine—kama vile haki za wanawake, haki za elimu, ajira, au uhuru wa kujieleza. Hii inamaanisha kuwa ili kukuza uhuru wa dini au imani, huenda ikahitajika pia kuzingatia haki nyingine.

Hakikisha unasisitiza hili washiriki wanapochagua matatizo na kuandaa mipango yao ya utekelezaji katika kipindi hiki na kinachofuata.

Yaliyomo katika kipindi na muda

Zoezi la ufunguzi: Nisifie Linawakumbusha washiriki umuhimu wa mchango wa kila mtu katika kundi na katika kuleta mabadiliko.	Dakika 5
Zoezi la mjadala: Tatizo ni nini? Participants identify a small number of problems to develop action plans for.	Dakika 52
Kichangamshi: Fanya mabadiliko Ni la haraka, la kufurahisha na la kimwili – washiriki huanza kwa kuchuchumaa na kunong'ona kisha kuruka na kupaza sauti wakisema 'leta mabadiliko'.	Dakika 5
Uwasilishaji: Safari ya mabadiliko yetu Maelezo muhimu kuhusu mchakato wa kuandaa mpango wa utekelezaji kwa kutumia taswira ya safari.	Dakika 10
Zoezi la kikundi: Safari ya mabadiliko yetu Washiriki wanaandaa mpango wa utekelezaji wa kuona kwa kutumia mchakato walioujifunza.	Dakika 45
Maoni ya hitimisho	Dakika 3
JUMLA YA MUDA	**Saa 2**

Jiandae

Jiandae kwa kipindi kwa kufuata mwongozo uliopo ukurasa wa 15, 'Jinsi ya kuandaa kila kipindi'. Kumbuka – unawajua washiriki wako! Unakaribishwa kurekebisha na kubadili vipengele vyovyote vya kipindi ili viendane na mahitaji ya kundi lako.

NYENZO ZA KIPINDI HIKI

Mbali na nyenzo za kawaida kwa kila kipindi zilizoorodheshwa kwenye ukurasa wa 16, utahitaji nyenzo zifuatazo kwa ajili ya kipindi hiki:

- Nakala moja ya kipeperushi ya 'Safari ya mabadiliko yetu' kwa kila mshiriki.
- 'Ramani ya uhuru wa dini au imani' ya mji wetu kwenye bango kitita, iliyotengenezwa katika kipindi cha 5.
- Karatasi kubwa tano za bango kitita zenye 'Mawazo ya Ute kelezaji' kutoka vipindi vya 6 7.
- Mabango yote ya mbinu za utekelezaji.

NYENZO ANDAMIZI za kipindi hiki zinaweza kupatikana hapa.

ANDAA UKUMBI

Kwa kipindi hiki, ni wazo zuri kuanza kwa kupanga viti katika mduara ili kuhimiza majadiliano na ushirikiano. Kwa zoezi la kikundi la 'Safari ya mabadiliko yetu', ni vyema kuwa na meza kubwa na viti kwa kila kikundi ili kurahisisha kazi ya pamoja.

Kabla ya kipindi kuanza, weka bango-kitita tupu, kalamu, na nakala za 'Safari ya mabadiliko yetu' mezani. Bandika Ramani ya uhuru wa dini au imani, bango-kitita za Mawazo ya Utekelezaji, pamoja na mabango ya mbinu za utekelezaji, ukutani kama nyenzo za rejea.



'Safari ya mabadiliko yetu'

"Kipindi cha kufurahisha! Washiriki walifurahia kuandaa ramani za safari yao ya mabadiliko. Wote walikuwa na mawazo thabiti kuhusu wanachotaka kufanya ili kuleta mabadiliko baada ya kozi kumalizika."
HIDAYA DUDE, MWEZESHAJI, TANZANIA

"Shughuli katika vipindi vya upangaji wa hatua zinawasaidia washiriki kunoa ujuzi wao – watakuwa na ufanisi zaidi kama wawezeshaji wa mabadiliko."
HAMMAM HADDAD, MWEZESHAJI, JORDAN

"Washiriki waliamua kuunda kikundi ambacho kitaendelea kushirikiana kuendeleza Uhuru wa Dini au Imani jijini kupitia utetezi, uhamasishaji na ushawishi wa jamii."
UKOHA NGWOBIA, MWEZESHAJI, NIGERIA

Mpango wa kina wa kipindi

1. Zoezi la ufunguzi: Nisifie   Dakika 5

ZOEZI LA PAMOJA

MAELEZO
Washiriki wanazunguka duara wakimsifia mtu aliye kushoto mwao.

LENGO
Kuhakikisha kila mshiriki anatambua sifa za kipekee na ujuzi ambao kila mtu analeta katika kundi, na kusisitiza kuwa mchango wa kila mtu utakuwa muhimu katika mchakato wa kuandaa mipango ya utekelezaji.

JINSI YA KUANZA ZOEZI
Kaa katika mduara. Karibisha kila mtu kwenye kipindi na waambie kuwa tutaanza kwa kutoa sifa kwa wenzao!

JINSI YA KUENDESHA ZOEZI
Kila mtu amtazame mtu aliye upande wake wa kushoto na kufikiria jambo moja kubwa ambalo mtu huyo analileta kwenye kundi – kwa mfano mawazo mazuri, uzoefu au ucheshi.

Zungukeni duara, kila mtu akimgeukia mtu aliye upande wake wa kushoto na kusema neno moja au mawili yanayoonyesha kile mtu huyo analeta kwenye kundi.

JINSI YA KUHITIMISHA ZOEZI
Waambie washiriki kujipigia makofi kwa kuwa watu wazuri mno! Toa hoja hizi muhimu:

- Kila mmoja wetu ana sifa za kipekee – tunakamilishana na mchango wa kila mtu ni muhimu.
- Kujenga jamii zinazoenzi haki za binadamu ni sawa – tunakuwa na ufanisi zaidi tunaposhirikiana. Mchango wa kila mtu, hata ukiwa mdogo, ni muhimu kwa sababu kwa pamoja tunaweza kuleta mabadiliko.
- Katika kipindi hiki na kinachofuata, tutaunda mipango ya utekelezaji – hebu tuhakikishe kila mtu anapata fursa ya kushiriki mchango wake wa kipekee!

2. Zoezi la mjadala: Tatizo ni nini?   Dakika 52

ZOEZI LA PAMOJA

MAELEZO NA LENGO
Katika zoezi hili, washiriki wanachagua matatizo mahususi ambayo wangependa kuunda mipango ya utekelezaji kuyashughulikia. Mbinu inayotumiwa inahakikisha kila mshiriki anashiriki katika mchakato huu.

NYENZO

- Bango-kitita za 'Mawazo ya Utekelezaji kutoka kwenye kipindi kilichopita.
- Bango-kitita ya Ramani ya uhuru wa dini au imani ya mji wetu.
- Bango-kitita na kalamu.

MAANDALIZI YA AWALI

Amua ni vikundi vingapi ya mipango ya utekelezaji utakuwa navyo katika zoezi la 'Safari ya mabadiliko yetu' (angalia ukurasa 137). Unahitaji washiriki 4-8 kwa kila kikundi. Kwa kuwa muda wa kuripoti matokeo katika kipindi kijacho ni mfupi, jaribu kuweka idadi ya vikundi visivyozidi vitatu.

JINSI YA KUANZA ZOEZI DAKIKA 2

Waombe washiriki wakusanyike karibu na bango-kitita za 'Ramani ya uhuru wa dini au imani' na 'Mawazo ya utekelezaji', kisha eleza yafuatayo:

Lengo la mafunzo haya lilikuwa ni kutusaidia kuwa wawezeshaji wa mabadiliko katika jamii zetu. Katika vipindi hivi viwili vya mwisho, tutaandaa mipango ya utekelezaji ambayo vikundi vinaweza kutumia kushughulikia tatizo fulani katika jamii yetu. Swali ni: tutashughulikia matatizo gani?

Tulitambua matatizo yanayohusiana na uhuru wa dini au imani katika zoezi la 'Ramani ya uhuru wa dini au imani ya mji wetu'. Kutokana na hayo, tulibuni mawazo ya hatua na tukachagua mawazo tunayoyapenda zaidi. Kila wazo linahusiana na tatizo fulani ambalo tunaliona kuwa muhimu.

Katika zoezi hili, tutachagua matatizo ya uhuru wa dini au imani ambayo tutatengeneza mipango ya utekelezaji kuyashughulikia, tukichagua kutoka miongoni mwa matatizo tuliyotambua. Bila shaka, kuna matatizo mengine mengi ya haki za binadamu yanayohitaji kushughulikiwa. Leo tunajikita katika uhuru wa dini au imani, lakini ujuzi mtakaopata unaweza kutumika kuandaa mpango wa utekelezaji kwa tatizo lolote katika jamii.

JINSI YA KUENDESHA ZOEZI 50 MIN

- **FIKIRI** (DAKIKA 5)
  Waombe washiriki watazame bango-kitita za 'Mawazo ya utekelezaji, hasa sehemu ya 'Mawazo yetu pendwa ya utekelezaji', kisha wawazie kimya kimya kuhusu maswali haya:
  – Matatizo gani mawazo yetu ya hatua yanajaribu kushughulikia?
  – Ni matatizo yapi yaliyo ya muhimu zaidi kushughulikiwa?
  – Ni matatizo yapi tunaweza kuyatatua kwa ufanisi?

- **KUWA PAMOJA** (DAKIKA 10)
  Waombe washiriki waingie katika vikundi vya watu wawili wawili kisha waeleze kazi ifuatayo:
  Katika jozi zenu, chagueni tatizo moja mnalodhani tunapaswa kuandaa mpango wa utekelezaji kulitatua leo. Chagueni kwa kuzingatia umuhimu wake na uwezo wetu wa kuleta mabadiliko. Hakikisheni mnalielezea tatizo kwa njia mahususi na dhahiri. Kwa mfano, badala ya kusema tatizo ni 'kutovumiliana', mnaweza kusema:
  – Watoto wa kutoka jamii za watu wachache wananyanyaswa shuleni, au
  – Viongozi wa kidini au kisiasa wa eneo letu, au vyombo vya habari, vinatumia lugha ya chuki.
  Badala ya kusema 'wanawake kutoka jamii ya watu wachache (au wote) wako hatarini', mnaweza kusema:
  – Viwango vya juu vya kuacha shule kwa wasichana wa jamii fulani,
  – Unyanyasaji mitaani, hasa dhidi ya wanawake kutoka jamii ya watu wachache, au
  – Ndoa za mapema na za kulazimishwa.
  Na badala ya kusema 'ubaguzi wa serikali', mnaweza kusema:
  – Polisi wa eneo hawachunguzi ipasavyo uhalifu dhidi ya watu kutoka jamii za watu wachache au
  – Jamii X haipewi kibali cha kujenga mahali pa ibada.

KIDOKEZO! Wianisha mifano hii na mazingira yako!

- **SHIRIKISHA** (DAKIKA 10)
  Omba kila jozi ya washiriki iseme kwa sentensi moja tatizo walilochagua. Andika matatizo haya kwenye orodha upande wa kushoto wa bango-kitita au ubaoni.Acha nafasi upande wa kulia ambapo watu wataweka alama ya X kwa matatizo wanayotaka kupigia kura.

- **PIGA KURA NA CHAGUA** (DAKIKA 20)
  Waombe kila mshiriki aweke alama ya X kwenye bango-kitita kando ya MATATIZO MAWILI wanayodhani kuwa kundi linapaswa kuandaa mipango ya utekelezaji kuyatatua. Jadilini matokeo katika kundi na kwa pamoja amueni juu ya kiwango cha juu cha matatizo matatu ya kuandikia mipango ya utekelezaji, (chini ya matatu ikiwa kundi lako ni dogo kuliko 12 kwani unahitaji kiwango cha chini cha washiriki wanne kwa kila tatizo).
  Sisitizeni kwamba hata kama tatizo ulilowekea alama ya 'X' halijachaguliwa, unaweza kutumia ujuzi wa kupanga mipango ya utekelezaji tunaojifunza leo kufanya kazi na tatizo ulilochagua baadaye.

- **GAWA KATIKA MAKUNDI** (DAKIKA 5)
  Waombe washiriki wasimame katika duara. Zunguka duara ukiwahesabu washiriki kuanzia moja hadi idadi ya vikundi ya mipango ya utekelezaji mtakayokuwa nayo (kwa mfano, kuanzia 1 hadi 3 ikiwa mtakuwa na vikundi vitatu).
  Gawa kila kikundi tatizo moja na waambie washiriki kwamba kikundi chao kitaandaa mpango wa utekelezaji kwa tatizo hilo baadaye katika kipindi.
  Ikiwa mshiriki yeyote anapendelea sana kuwa katika kikundi tofauti na alilopangiwa (labda kwa sababu ana ujuzi wa tatizo fulani), angalia ikiwa kuna mtu yuko tayari kubadilishana naye.

3. Kichangamshi: Fanya mabadiliko Dakika 5

ZOEZI LA PAMOJA

MAELEZO NA LENGO
Zoezi la mwili la kuongeza viwango vya nguvu.

JINSI YA KUENDESHA ZOEZI
Waombe washiriki wasimame katika duara na wainame chini kadiri wanavyoweza (kulingana na uwezo wa kila mmoja). Waombe wote wanong'oneze maneno "Fanya mabadiliko: M-A-B-A-D-I-L-I-K-O!" kwa pamoja. Waombe warudie maneno haya tena na tena, kila mara kwa sauti kubwa kidogo na wakinyanyuka kidogo. Kiasi cha sauti kinaongezeka taratibu na kundi linanyanyuka polepole hadi mwishowe wote wanaruka juu kadiri wawezavyo wakipaza sauti: "Fanya mabadiliko: M-A-B-A-D-I-L-I-K-O!"

KIDOKEZO! Onyesha kwa vitendo – kuwa mwenye sauti na uchangamfu zaidi kadri mchezo unavyoendelea!

4. Uwasilishaji: Safari ya mabadiliko yetu Dakika 10

WASILISHO

MAELEZO NA LENGO
Uwasilishaji huu unalenga kujenga ujuzi wa upangaji wa hatua. Unatumia taswira ya kupanga safari ili kuanzisha mchakato wa upangaji wa hatua na zana ya upangaji wa hatua ambayo washiriki watatumia katika zoezi litakalofuata.

NYENZO

- Nakala ya mwongozo inapatikana kwenye ukurasa wa 140 wa Kiongozi hiki.
- Nakala hii inawiana na slaidi za 3-24 za kipindi cha PowerPoint na imejumuishwa katika maelezo ya msemaji kwa slaidi hizi.
- Toleo la mwongozo huu linapatikana katika mfumo wa kompyuta la Word ambalo linaweza kuhaririwa.

MAANDALIZI YA AWALI
Andaa kulingana na mwongozo uliotolewa kwenye ukurasa wa 15, 'Jinsi ya kujiandaa kwa kila kipindi'. Soma na urekebishe nakala na slaidi za PowerPoint (au bango-kitita kwa hoja muhimu kwenye slaidi) na fanya mazoezi ya kuwasilisha pamoja na slaidi/bango-kitita.

KIDOKEZO! Waombe watu wahifadhi maswali/maoni mpaka mwisho wa wasilisho.

5. Zoezi la kikundi: Safari ya mabadiliko yetu Dakika 45

ZOEZI LA KIKUNDI

MAELEZO NA LENGO
Zoezi hili linaendelea katika sehemu iliyosalia ya kipindi hiki na mwanzoni mwa kipindi kijacho. Katika zoezi hili, vikundi vinatayarisha mipango ya utekelezaji kwa kutumia nyenzo ya upangaji wa hatua iliyoelezwa katika slaidi iliyotangulia. Kulingana na aina ya kikundi, mipango hii inaweza kuwa mipango halisi inayokusudiwa kutekelezwa na kikundi, au inaweza kuwa mipango ya mafunzo inayoundwa kwa madhumuni ya kujifunza ujuzi wa upangaji wa hatua.

Vikundi vinachora na kuandika mipango yao ya utekelezaji kama ‘safari’ inayoonekana kwenye bango kitita.

NYENZO

- Kijitabu kimoja cha 'Safari ya mabadiliko yetu' kwa kila mshiriki.
- Bango-kitita, kalamu za kuandikia kwenye bango-kitita, na kalamu za kawaida.

MAANDALIZI YA AWALI
Bandika pamoja pande fupi za bango-kitita ili kutengeneza karatasi ndefu. Andaa moja kwa kila kundi.

JINSI YA KUANZA ZOEZI DAKIKA 5
Onyesha tena slaidi ya 24 na eleza yafuatayo:
Katika kikao cha awali, tulichagua matatizo na tukajigawa katika vikundi. Sasa kila kikundi kitajaribu kuandaa mpango wa utekelezaji ili kushughulikia tatizo lao, kwa kutumia mfano wa 'Safari ya mabadiliko yetu" ambao tulisikia katika uwasilishaji.

Mipango hii ya utekelezaji inaweza kuwa mipango halisi tunayotaka kutekeleza baada ya mafunzo, au inaweza kuwa mazoezi ya kutusaidia kukuza ujuzi wa kupanga mipango ya utekelezaji ambayo tutaweza kutumia baadaye.

Katika meza za vikundi, mtapata bango-kitita ambapo mtachora na kuandika safari yenu ya mabadiliko. Pia mtapata nakala za ‘mfumo wa Safari Yetu ya Mabadiliko’ ili kuwasaidia na pia kama kipeperushi cha kubeba nyumbani.

Jukumu lenu ni kuunda mpango wa utekelezaji wa kushughulikia tatizo la kikundi chenu bango-kitita, kwa kutumia vipengele mbalimbali vya mfano wa safari ya mabadiliko. Mna muda wa kikao hiki na sehemu ya kwanza ya kikao kijacho kufanya hivi – jumla ya zaidi ya saa moja.

Onyesha slaidi ya 25 huku ukieleza yafuatayo:

Hatua za kuandaa mpango ni kama zifuatazo:
- Amueni wanamabadiliko ni kina nani: Ni kikundi gani cha watu au taasisi itakayotekeleza mpango huu?
- Andikeni tatizo kuu ambalo kundi lenu limepewa kushughulikia.
- Tambueni mitazamo, tabia au kanuni mahususi mnazotaka kubadilisha.

- Tengenezeni lengo linaloakisi tatizo lenu.
- Elezeni mitazamo, tabia na kanuni mnazotamani kuziendeleza.
- Ongezeni watu wengine wanaohusika – wale wanaoathirika, mashirika au mamlaka zilizoko kwenye tatizo au zenye uwezo wa kuleta mabadiliko.
- Chagueni na ongezeni mbinu na shughuli kuu zinazohitajika ili kufanikisha lengo.
- Bainisheni hatua chache muhimu za utekelezaji wa shughuli hizo.
- Tambueni ujumbe wenu kwa watu mbalimbali waliohusika – Hoja gani zitawashawishi?
- Na hatimaye, fikirieni hatari mnazoweza kukutana nazo njiani.

Hamna ulazima wa kufuata mpangilio huu, lakini utasaidia!

Sisitiza yafuatayo:
Inawezekana kutumia muda mrefu kutafakari kila swali, lakini lengo la zoezi hili ni kuunda 'mwonekano' wa mpango – picha kubwa ambayo tunaweza kuiboresha baadaye tukiamua kuutekeleza.

Lenga kutumia takribani dakika 8 kwa kila sehemu! Kumbuka, huu ni ubunifu wa haraka wa mpango, kwa hivyo andikeni mawazo yenu ya papo hapo badala ya kutumia muda mwingi kuyapanga kwa ufasaha – sentensi moja fupi au nukta chache zinatosha.

Na msisahau mawazo ya hatua za utekelezaji tuliyoandika kwenye bango-kitita! Huenda mkaweza kutumia moja au mawili kwenye mpango wenu.

JINSI YA KUENDESHA ZOEZI DAKIKA 40
Watume washiriki kwenye vikundi vyao waanze kazi. Tembelea kila kikundi ukihakikisha wanaelewa wanachopaswa kufanya.

Zingatia muda! Wakumbushe kusonga mbele baada ya kila dakika 10. Fuatilia mijadala yao, uhakikishe wanabaki kwenye mada na kuwapa mwongozo inapobidi.

Wahimize na uwape vidokezo wanapohitaji msaada. Ikiwa kundi limeshindwa swali fulani, waelekeze waendelee na hatua nyingine na warejee swali hilo baadaye.

6. Maoni ya hitimisho Dakika 3

GUMZO FUPI

Muda unapoisha, wapongeze wanakundi wote kwa kazi yao ngumu na uwajulishe kuwa wataendelea na mpango wao wa safari ya mabadiliko katika kipindi kijacho. Wahimize waendelee kutafakari mpango wao hadi kipindi kinachofuata na waandike mawazo yoyote mapya watakayopata.

Mwongozo wa uwasilishaji

Safari ya mabadiliko yetu – zana inayoonekana ya kuandaa mpango wa utekelezaji

Nakala hii ya uwasilishaji wa kipindi cha 8 inaonyeshwa kwenye slaidi za 3-24 za PowerPoint ya kipindi.

MPANGO WA UTEKELEZAJI NI NINI NA KWA NINI NI MUHIMU?

Basi, mpango wa utekelezaji ni nini na kwa nini ni muhimu? Mpango wa utekelezaji ni mpango wa JINSI tunavyotaka kufika kutoka pale tulipo hadi pale tunapotaka kuwa.

Ikiwa tunasafiri kwa safari ndefu, ni wazo zuri kuwa na ramani na mpango wa jinsi tutakavyosafiri. Labda tutatembea hadi kituo cha basi, kisha tupande basi, halafu garimoshi, na hatimaye tukodishe gari ili kufika mwisho wa safari yetu! Bila ramani na mpango, huenda tusiwahi kufika tunakotaka, au inaweza kutuchukua muda mrefu zaidi kufika.

Mpango wa utekelezaji ni kama ramani na mpango wa safari – unaonyesha hatua tunazopanga kuchukua ili kufanikisha lengo letu, na hutusaidia kuwa na mkakati na makusudi.

Sote tunatengeneza mipango ya utekelezaji. Wakati mwingine ni rahisi sana, karibu ya kiasili, na tunayahifadhi vichwani mwetu. Lakini kwa changamoto ngumu, kama mambo ambayo hatujawahi kuyafanya au kazi tunazofanya kwa vikundi, tunahitaji kupanga kwa makini zaidi na kuyaandika mipango yetu ili kila mtu aweze kuyakumbuka.

Katika sehemu iliyobaki ya uwasilishaji huu, tutajifunza kutumia zana rahisi ya kutazama inayoitwa 'Safari ya mabadiliko yetu' ili kuunda mpango wa utekelezaji.

WASAFIRI



Tunapotengeneza mpango wa utekelezaji kwa safari ya kuleta mabadiliko, swali la kwanza ni 'sisi ni nani?'

Ni akina nani wasafiri wanaoelekea kwenye safari ya mabadiliko? Kama vile wasafiri wengine wanapaswa kutembea huku wengine wanaweza kuendesha gari au kupanda ndege, sisi kama watu binafsi, vikundi au mashirika tuna fursa, nguvu, udhaifu na hatari tofauti. Kuanzia kwa kuuliza 'sisi ni nani?' hutusaidia kuzingatia mambo haya.

Tubuni safari ya mabadiliko ya kufikirika na tuseme kwamba sisi ni marafiki wachanga kutoka jamii tofauti za kidini katika mji wetu.

SEHEMU YETU YA KUANZIA



Tunapopanga safari, jambo la kwanza tunalohitaji kujua ni tunapoanzia. Safari ya mabadiliko huanza na tatizo, na tunaanza kwa kulielezea.Kadiri tunavyolielezea tatizo letu kwa usahihi zaidi, ndivyo inavyokuwa rahisi kubaini jinsi ya kuleta mabadiliko.

Kwa hiyo badala ya kusema kwamba tatizo ni 'kutovumiliana', tunaweza kusema 'Watoto hawana marafiki kutoka jamii nyingine za kidini.' Hili ni tatizo ambalo ni matokeo ya kutovumiliana, lakini pia ni chanzo cha kuendelea kwa hali hiyo.



Matatizo kama haya yana vichocheo mbalimbali vinavyochangia kuwepo kwake. Vichocheo hivi vinaweza kuwa:

- mitazamo yenye matatizo walio nayo watu,
- tabia zenye matatizo – mambo ambayo watu wanafanya.
- sheria, kanuni au sera zenye matatizo.

Kwa pamoja, mitazamo, tabia na sheria hizi ndizo zinazosababisha tatizo. Sasa, kuhusiana na tatizo tulilobaini, ni mitazamo, tabia au sheria gani mahsusi tunazotaka kubadilisha?



Kuhusiana na mfano wetu, tunaweza kusema 'Wazazi wana mitazamo hasi kuhusu watoto wao kuwa na marafiki kutoka jamii nyingine au 'Shule inanyamazia unyanyasaji kati ya watoto wa jamii tofauti za kidini' au 'Kiongozi wa kidini wa mtaa anasema urafiki kati ya watoto wa jamii tofauti hauruhusiwi' Hizi ni mielekeo, tabia na sheria zinazochangia tatizo letu.

MAHALI TUNAKOTAKA KUFIKA

Tunaposafiri kwa safari ya kuleta mabadiliko, ni muhimu kujua tunakotaka kufika! Kufafanua lengo letu ni jambo gumu. Sote tunataka kufikia amani, haki na kutokuwepo kwa ubaguzi! Lakini tunapaswa kuwa wazi na halisi kuhusu kile tunachoweza kufanikisha ndani ya muda fulani.



Kwa mfano, lengo letu linaweza kuwa kwamba 'Watoto wawe na marafiki kutoka jamii nyingine za kidini.' Na kwa lengo hilo, tunaweza kufikiria mitazamo, tabia au sheria mahsusi tunazotaka kuona zikichukua nafasi ya zile za zamani zenye matatizo.

Kwa mfano: 'Wazazi wanawahimiza watoto wao kuwa na marafiki kutoka jamii nyingine za kidini', au 'Shule inapambana kikamilifu na unyanyasaji wa kidini', au 'Viongozi wa kidini wanahimiza urafiki kati ya jamii.'



Kama unavyoona, tatizo letu na lengo letu ni kama picha zinazoakisi moja nyingine. Tatizo linaelezea mwanzo wa safari ya mabadiliko yetu. Mchakato wa mabadiliko huanza wapi, na tunataka utupeleke wapi?

WATU TUNAOKUTANA NAO NJIANI



Katika safari ndefu, tunaweza kukutana na watu wengi – wasafiri wenza wanaoelekea upande wetu, wakaguzi wa tiketi wanaoangalia maendeleo yetu, au watu wanaoweka vizuizi barabarani kutuzuia au kutuelekeza njia nyingine. Sasa basi, katika safari ya mabadiliko yetu, ni akina nani tutakaokutana nao njiani?



Kutakuwa na:

- watu walioathiriwa na tatizo (watoto katika kisa chetu).
- watu wenye mamlaka ya kufanya jambo kuhusu tatizo (baraza la shule na wafanyakazi, wazazi na viongozi wa kidini, kwa mfano).



Huenda pia kukawa na:

- wasafiri wenza, watu wanaoshiriki lengo letu na wanaoweza kutusaidia njiani. Katika mfano wetu, washirika wetu huenda wakawa baraza la jumuiya za dini mbalimbali.
- au watu wanaopinga lengo letu na wanaojaribu kutuzuia. Pengine ni ushawishi wa mitandao ya kijamii asiyevumilia katika jamii yetu.



Tunapoandika mpango wa utekelezaji, ni vyema kufikiria watu, mashirika na taasisi hizi ni nani, ili tuweze kuwakumbuka tunapochagua mbinu zetu na kupanga hatua zetu.

Nani anaweza kusaidia kuleta mabadiliko pamoja nasi? Tunahitaji kumshawishi nani – na kuhusu nini? Na ni nani anayeweza kujaribu kuzua mabadiliko?

KUCHAGUA NJIA



Kwa kawaida, kuna njia nyingi tofauti za kutoka A hadi B – njia tofauti na aina mbalimbali za usafiri. Kwa hivyo, tutachagua njia ipi?

Njia yetu inaamuliwa na mbinu tunazotumia. Kumbuka, kuna mbinu 15 tofauti za kuchagua – kutoka kuhamasisha, kufanya ushawishi, hadi kuandika ripoti za ukiukwaji. Tayari tumebuni mawazo mengi ya hatua kwa kutumia mbinu hizi! Hapa ndipo unaweza kuzitumia!



Katika mfano wetu, je, tutaelekeza juhudi katika kubadilisha mtazamo wa watoto kwa kuunda timu ya imani mbalimbali ya mpira wa miguu, au katika kurekodi matukio ya unyanyasaji na kutumia hayo kushawishi baraza la shule kuchukua hatua? Au katika kuunda motisha kwa walimu kuhimiza mahusiano chanya kwa kuanzisha tuzo kwa mwalimu anayehimiza utofauti na kuhakikisha heshima darasani? Au katika kuwashawishi viongozi wa kidini kuhimiza urafiki kati ya waumini wa dini tofauti? Au mchanganyiko wa haya yote?

Kuna mambo mengi sana tunayoweza kufanya. Hatutaweza kufanya yote, lakini huenda tukahitaji kufanya zaidi ya jambo moja ili kufanikiwa. Kwa mfano, hakutakuwa na haja kuanzisha timu ya mpira ikiwa viongozi wakuu wa kidini wataikemea na hakuna atakayethubutu kushiriki. Mipango madhubuti ya utekelezaji kwa kawaida huwa na mbinu chache tofauti lakini zinazokamilishana.

HATUA ZA SAFARI



Baada ya kuamua mbinu gani tutatumia, tunafikiria JINSI ya kuzitumia. Ni hatua gani mahususi tunazopaswa kuchukua na kwa mpangilio upi? Nani atafanya nini na lini kwa kila mbinu tuliyochagua? Tutaandaa na kutangaza vipi timu ya mpira wa miguu au kufanya utafiti? Ni nani atakayezungumza na viongozi gani wa kiimani?

UJUMBE



Na tunapozungumza na watu, tunapaswa kufikiria kuhusu kile tunachotaka kusema. Ni aina gani ya taarifa au hoja zitakazowashawishi washirika watarajiwa wa kuungana nasi au kuwashawishi watu kubadili mitazamo yao au tabia zao? Ni nini kitakachowashawishi wenye mamlaka kuchukua hatua? Na je, kuna njia za kuwasilisha ujumbe wetu ili tuepuke upinzani?

Kwa mfano, wazazi wanaweza kuhitaji kusikia kuhusu manufaa ya kujenga mahusiano kati ya jamii kwa ajili ya mustakabali wa watoto wao, pamoja na taarifa za kiutendaji zinazowahakikishia kuwa watoto wao watakuwa salama na watatunzwa vyema katika timu ya mpira wa miguu.

Baraza la mahusiano ya dini katika jamii linaweza kupendezwa kusikia jinsi tutakavyohusisha watu wazima kutoka jamii mbalimbali katika kuongoza timu ya mpira wa miguu.

Na bodi ya shule inaweza kutiwa moyo kusikia jinsi sera dhidi ya unyanyasaji inaweza kutumika kuinua hadhi ya shule.

VIKWAZO NA UHATARISHI



Katika safari ndefu na ngumu, wasafiri wanaweza kukumbana na vikwazo, hatari na dhoruba wanazopaswa kuepuka au kushinda ili kufika wanakotaka. Mchakato wowote wa mabadiliko huambatana na vikwazo na hatari. Inasaidia iwapo tutapanga mapema, tuchague njia salama kadri inavyowezekana, na kuwa na mipango ya kushughulikia hali mbalimbali zitakazojitokeza.

Kwa hivyo, ni vikwazo na hatari gani tunaweza kukumbana navyo ikiwa tutachukua hatua tulizozipanga? Je, kuna hatua zozote zilizo na hatari kubwa mno, na je, kuna njia za kupunguza hatari hizo?

Kwa mfano: Katika muktadha fulani, kuhamasisha timu ya mpira ya madhehebu tofauti kupitia redio ya jamii kunaweza kuvuta makini isiyotakikana kutoka kwa makundi yasiyovumilia tofauti za kidini, ambayo yanaweza kuibua upinzani. Huenda ikawa bora kuanza kimya kimya na kujenga uungwaji mkono wa jamii.

HITIMISHO

Sasa tumepitia mchakato wa kuandaa mpango wa utekelezaji. Katika safari ya mabadiliko yetu, tumetambua:

- Mahali tunapoanzia – tatizo.
- Mahali tunapolenga kufika – lengo.
- Watu tutakaokutana nao njiani – marafiki, wapinzani na wale tunaotaka kuwaathiri kwa namna fulani.
- Njia – mbinu tutakazotumia na hatua mahususi tunazohitaji kuchukua ili kusonga mbele.
- Tumefikiria pia kuhusu ujumbe wetu na hatari tunazoweza kukumbana nazo njiani.

Mchakato huu unaweza kutumika kuandaa mpango rahisi au wa kina wa utekelezaji kwa mbinu yoyote unayotaka kutumia.

Sasa ni wakati wako kujaribu – tengeneza mpango wako mwenyewe wa safari ya mabadiliko kwa tatizo unalotaka kutatua!

KIPINDI CHA 9

Safari ya mabadiliko yetu (inaendelea)

Muhtasari wa kipindi

Mchakato wa kuandaa mpango wa utekelezaji ulioanza katika kipindi cha 8 unaendelea katika kipindi cha 9. Hiki ni kipindi cha mwisho cha mafunzo na kinahitimishwa kwa zoezi la tathmini na sherehe.

Vipindi vya 8 na 9 vimeunganishwa – vikiwa na malengo ya pamoja ya kujifunza na mchakato mmoja wa kujifunza. Tafadhali angalia mpango wa kipindi cha 8 kwa malengo ya kujifunza ya kipindi hiki.

Yaliyomo katika kipindi na muda

Kipindi cha 9 kimepangwa kuchukua takriban saa 2 na dakika 30. Hata hivyo, urefu wake na muda wa vipengele mbalimbali unategemea idadi ya vikundi vinavyohitaji kufanya mrejesho kwenye mjadala wa pamoja. Ikiwa kuna zaidi ya vikundi vitatu, utahitaji muda mrefu zaidi. Ikiwa kuna chini ya vikundi vitatu, unaweza kutumia muda wa chini ya saa 2 na dakika 30.

Dakika 30 za mwisho zinajumuisha zoezi la tathmini na sherehe.

Zoezi la kikundi: Safari ya mabadiliko yetu (inaendelea) Washiriki wanaendelea kuandaa mipango ya utekelezaji waliyoanza katika kipindi cha 8.	Dakika 30 minimum
Mjadala wa pamoja: Safari ya mabadiliko yetu – uwasilishaji na maoni Vikundi vinawasilisha na kujadili mipango yao ya utekelezaji	Dakika 10-20 kwa kila kikundi
Kichangamshi: Muonekano wa kisanii wa wanamabadiliko Vikundi vinatumia miili yao kuunda sanamu ya kibinadamu kwa ushirikiano inayoakisi mpango wao wa utekelezaji.	Dakika 5
Mjadala wa pamoja: Tunaelekea wapi kutoka hapa? Washiriki wanajadili hatua wanazotaka kuchukua binafsi na kwa pamoja baada ya kozi.	Dakika 25 minimum
Zoezi la tathmini: Kichwa, moyo, mikono Washiriki wanatafakari kuhusu mafunzo wanayopata kutoka kwenye mafunzo.	Dakika 20
Sherehe Kusherehekea maarifa, mitazamo, ujuzi na mahusiano yaliyoibuliwa wakati wa mafunzo.	Dakika 10
JUMLA YA MUDA	**Saa 2 Dakika 30**

Jiandae

Jiandae kwa kipindi kulingana na mwongozo uliopo ukurasa wa 15, 'Jinsi ya kujiandaa kwa kila kipindi'. Kumbuka – unawajua washiriki wako! Unakaribishwa kurekebisha na kubadilisha vipengele vyovyote vya kipindi ili kiendane na mahitaji ya kundi lako.

AMUA KUHUSU MUDA WA KIPINDI

Kwa kipindi hiki, unapaswa kuamua ni muda gani utatenga kwa kazi za vikundi na mjadala wa pamoja. Muda unaopatikana kwa haya unategemea idadi ya vikundi vinavyohitaji kuwasilisha mipango yao ya utekelezaji

NYENZO ZA KIPINDI HIKI

Mbali na nyenzo za kawaida kwa kila kipindi zilizoainishwa katika ukurasa wa 16, utahitaji nyenzo zifuatazo ili kuendesha kipindi hiki kulingana na mpango wa kipindi:

- Bango-kitita ya 'Safari ya mabadiliko yetu' kutoka kipindi cha 8.
- 'Ramani ya uhuru wa dini au imani ya mji wetu' – bango-kitita zilizotayarishwa katika kipindi cha 5.
- Bango-kitita za 'Mawazo ya Utekelezaji' kutoka vipindi vya 6-7.
- Mabango yote ya mbinu.

NYENZO ANDAMIZI za kipindi hiki zinaweza kupatikana hapa.

ANDAA UKUMBI

Kipindi hiki kitaanza kwa kutumia mgawanyo wa vikundi kama ulivyokuwa mwishoni mwa kipindi cha 8. Panga meza na viti kwa mpangilio huo.

Weka bango-kitita ya kila kundi kutoka kwenye zoezi la 'Safari ya mabadiliko yetu' katika kipindi kilichopita kwenye meza zao, pamoja na kalamu na vibandiko vya kunata.

'Bandika 'ramani ya uhuru wa dini au imani', bango-kitita za 'Mawazo ya Utekelezaji, na mabango ya mbinu ukutani kama nyenzo za marejeo.

'Kichwa, mikono, moyo'

Mpango wa kina wa kipindi

KUMBUKA:
Unapaswa kuamua muda wa kazi za vikundi na mjadala wa pamoja!

1. Zoezi la kikundi: Safari ya mabadiliko yetu (inaendelea)
si chini ya dakika 30

ZOEZI LA KIKUNDI

NYENZO

Bango-kitita za 'Safari ya mabadiliko yetu' zilizotengenezwa na makundi katika kipindi kilichopita, makapeni, kalamu za kawaida, na vibandiko vya kunata.

JINSI YA KUANZA ZOEZI
Wakaribishe tena wote kwenye kipindi cha mwisho cha mafunzo. Watie moyo kwa kupongeza kazi nzuri wanayofanya.

Waombe washiriki warejee kwenye vikundi vyao vya upangaji wa hatua za utekelezaji kutoka kipindi kilichopita ili kuendelea na kazi yao kuhusu ''Safari ya mabadiliko yetu'. Wahimize wanakundi kuelekeza juhudi zao kwenye mbinu na hatua za utekelezaji ikiwa bado hawajafanya hivyo. Waeleze muda waliopewa kwa kazi hii.

2. Mjadala wa pamoja: Safari ya mabadiliko yetu – uwasilishaji na maoni
Dakika 15 – 20 / kundi

MJADALA WA PAMOJA

MAELEZO
Hii ni hatua ya mwisho ya zoezi la 'Safari ya mabadiliko yetu', ambapo makundi yanawasilisha mipango yao ya utekelezaji na kupokea maoni.

ZINGATIA

Ikiwa mna kundi dogo sana na wote wameshirikiana kuandaa mpango mmoja, ruka hatua ya uwasilishaji na fanyeni mjadala wa hitimisho kwa kutumia maswali yaliy-oorodheshwa chini ya sehemu ya 'Jinsi ya kuendesha zoezi'.

JINSI YA KUANZA ZOEZI DAKIKA 1
Eleza kwamba kila kundi litakuwa na dakika 5 kuwasilisha 'safari ya mabadiliko yetu' kwa kikao cha pamoja, kisha mjadala ufuate kuhusu mpango wao.

Eleza kwa uwazi kwamba lengo la mjadala huu ni kusaidiana, kutiana moyo na kusaidiana kukuza mawazo yetu kwa pamoja. Huu si ushindani wa kuona nani ana mpango bora wa utekelezaji – hakuna hata mmoja wetu aliyepata muda wa kuandaa mpango mkamilifu!

JINSI YA KUENDESHA ZOEZI
Karibisha kila kikundi kwa zamu ili kiwasilishe (kwa dakika 5) na kupokea maoni (si zaidi ya dakika 15).
Tumia maswali yafuatayo kuongoza mjadala wa mrejesho:

- Unapenda nini kuhusu mpango huu wa utekelezaji?
- Je, una mapendekezo yoyote ya jinsi ya kuufanya mpango huu kuwa bora zaidi? Kwa mfano, watu wa ziada tunaoweza kushirikiana nao au mbinu nyingine zinazoweza kutumika.
- Je, kuna mbinu/hatua zozote ambazo hazitakuwa na ufanisi, hazitekelezeki, au zina hatari kubwa?

- Je, unadhani mbinu/hatua zilizopangwa zitasababisha kufanikisha malengo ya kubadili mitazamo, tabia na sheria au kupiga hatua kuelekea lengo hilo?

Weka nidhamu kali katika utunzaji wa muda, ili kuhakikisha kila kikundi kinapata nafasi sawa ya kuwasilisha na kupokea maoni.

JINSI YA KUHITIMISHA ZOEZI DAKIKA 2
Wapongeze washiriki kwa kazi yao bora na ushiriki wao. Sisitiza kuwa, iwe watautumia mpango wao wa utekelezaji au la, wamejifunza ujuzi mwingi wa upangaji wa hatua za utekelezaji ambao wanaweza kutumia katika michakato mbalimbali ya mabadiliko watakayohusika nayo siku zijazo.

3. Zoezi la kuchangamsha: Muonekano wa kisanii wa wanamabadiliko Dakika 5

KIDOKEZO! Ikiwa kikundi kinaonyesha uchovu baada ya zoezi la awali, ingiza zoezi hili la kuimarisha nguvu mapema – kabla ya uwasilishaji unaofuata.

LENGO
Kuchangamsha hali katika kikao hiki kinachohitaji umakini mkubwa.

JINSI YA KUENDESHA ZOEZI
Toa maelekezo haya kwa washiriki na fuata mchakato ufuatao:
Katika kikundi chenu cha upangaji wa hatua, tengenezeni muonekano wa kisanii wa kibinadamu kwa kushirikiana, kwa kutumia miili yenu, ili kuwakilisha mpango wenu wa utekelezaji. Mna dakika 4. Wakati muda utakapokwisha, nitapiga makofi – na kila mtu anapaswa kuganda katika nafasi yake. Kisha, tutatazama mwonekano ya kisanii ya kila kundi na kupiga makofi kwa pamoja!

4. Mjadala wa Pamoja: Tunaenda wapi kutoka hapa? Si chini ya dakika 25

MJADALA WA PAMOJA

MAELEZO
Mjadala huu wa pamoja unahitimisha mafunzo. Unalenga katika kile ambacho washiriki wanataka kufanya ili kuendeleza uhuru wa dini au imani baada ya mafunzo kuisha.

JINSI YA KUANZA ZOEZI
Eleza yafuatayo:
Tunakamilisha mafunzo yetu pamoja. Mafunzo haya imejikita katika haki ya binadamu ya uhuru wa dini au imani.

Tumetafakari kuhusu utambulisho wetu, kuhusu upendeleo na changamoto tunazokumbana nazo. Tumeelewa haki za binadamu, uhuru wa dini au imani, na ukiukaji wa haki hiyo. Tumeelewa mbinu mbalimbali zinazoweza kutumiwa kuendeleza haki za binadamu, na tumefanya mazoezi ya kuunda 'safari za mabadiliko' – mipango yetu ya utekelezaji.

Sasa, tunataka kUenda wapi kutoka hapa – kama watu binafsi na kama kundi? Tunataka kusonga mbele vipi katika kuwa wanamabadiliko?

JINSI YA KUENDESHA ZOEZI
Waombe washiriki watafakari maswali yafuatayo katika muda wa wazi wa kushirikiana na kujadili:

- Je, kuna mambo tunayotaka kubadilisha katika maisha yetu ya kila siku kutokana na kile tulichojifunza?
- Je, tunataka kama kundi kuendelea kufanya kazi juu ya baadhi ya mawazo/mipango yetu ya utekelezaji na kuitekeleza pamoja? Ni mipango/mawazo yapi? Ni nani angependa kushiriki? Ikiwa ndivyo, hatua yetu inayofuata inapaswa kuwa ipi?

- Je, tunaweza kuendeleza baadhi ya mawazo yetu ya utekelezaji kupitia njia nyingine tunazoshiriki moja kwa moja – kama vile jumuiya zetu za kidini, maeneo yetu ya kazi, au vikundi vya wanawake?
- Je, kuna mashirika au vikundi ambavyo hatuhusiani navyo moja kwa moja, lakini tunaweza kusema navyo na kuhamasisha kuchukua hatua? Ni nani na ni hatua gani?

Andika maelezo ya mjadala kuhusu kila swali kwenye bango-kitita nne, zenye vichwa vifuatavyo:

- Mambo ninayotaka kufanya.
- Mambo tunayotaka kufanya katika kikundi hiki.
- Mambo tunayotaka kufanya kama sehemu ya vikundi/mashirika mengine.
- Mambo tunayotaka kuwahimiza wengine kufanya.

Usihangaike ikiwa kutakuwa na baadhi ya mambo yanayojirudia kati ya bango-kitita – lengo si kuainisha kila kitu kwa usahihi, bali ni kutafakari njia tofauti tunazoweza kutumia kuchukua hatua zinazofuata.

Katika mjadala, eleza kwamba tafiti zinaonyesha kuwa mabadiliko hufanikiwa kwa urahisi zaidi kupitia mitandao mipana ya watu binafsi, vikundi na mashirika yanayoshirikiana kuelekea lengo moja, huku kila mmoja akichukua hatua tofauti zinazosaidiana kwa namna iliyoratibiwa.

5. Zoezi la tathimini: Kichwa, moyo, mikono Dakika 20

ZOEZI LA KILA MTU

Zoezi hili rahisi la tathmini ya kibinafsi linawasaidia washiriki kutafakari kile wanachojifunza kutoka kwenye mafunzo haya.

NYENZO

- Chapisho moja la 'Kichwa-Moyo-Mikono' kwa kila mshiriki.
- Kalamu moja kwa kila mshiriki.

JINSI YA KUANZA ZOEZI DAKIKA 2

Mpe kila mshiriki nakala yenye 'Kichwa-Moyo-Mikono'.

Eleza kwamba watafanya zoezi la tathmini ili kutafakari kile wanachojifunza kutoka kwenye kozi hii. Eleza wazi ikiwa karatasi hizo zitakusanywa kwa madhumuni ya kutathmini kozi au ikiwa washiriki watachukua zao kama kumbukumbu. Ni muhimu kuhakikisha watu hawaandiki tafakari za faragha ikiwa karatasi zitakusanywa!

JINSI YA KUENDESHA ZOEZI DAKIKA 18

Waombe washiriki watafakari kwa utulivu yafuatayo:

- Fikiria kile ulichopata kwa upande wa maarifa na mawazo. Andika mawazo yako katika sehemu ya kichwa.
- Fikiria kuhusu hisia zako, mambo uliyogundua kuhusu wewe mwenyewe au mitazamo mipya uliyojenga. Andika haya katika sehemu ya moyo.
- Fikiria kuhusu mawazo uliyo nayo ya kuchukua hatua au kufanya mambo kwa njia tofauti. Andika haya katika sehemu ya mkono.
- Hakikisha unatoa maelezo ya kina kadri uwezavyo. Wape dakika 8 za kutafakari na kuandika.

Kulingana na ukubwa wa kundi lako, ama waombe washiriki wote washiriki kwa kusema angalau jambo moja waliloandika kwa mzunguko au wajadili kwa makundi ya wawili wawili ili kushirikishana na kutafakari. (Dakika 10)

(Toleo mbadala: Chora kichwa, moyo na mkono kwenye karatasi tatu tofauti za bango-kitita. Waombe washiriki wajibu maswali yaliyo hapo juu kwenye vibandiko vya kunata na wavibandike kwenye bango-kitita. Jadili matokeo katika kikao cha pamoja.)

6. Sherehe! Dakika 10

Wakati wa mafunzo haya, washiriki wamefahamiana zaidi na wametumia muda na nguvu zao katika mchakato huu. Sasa ni wakati wa kusema asante na kusherehekea mawazo mapya, uelewa, ujuzi, na mahusiano waliyojenga katika mafunzo haya! Andaa hafla fupi ya kusema hongera na asante. Unaweza kuimba wimbo, kusema maneno machache ya shukrani, kuomba, kufurahia vitafunwa pamoja au kucheza dansi.

Cheti kinapatikana kwa kuchapishwa na kutolewa kwa washiriki iwapo unataka.

'Wanamabadiliko wa Jamii'

> "Kuwa mwanamabadiliko ni safari ambayo kila mtu anapaswa kuianza."
> **MSHIRIKI**, NIGERIA

SEHEMU YA C

Nyenzo za rejea

Ahadi muhimu za haki za binadamu zinazohusiana na uhuru wa dini au imani

Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu (UDHR), Kifungu cha 18

Kila mtu ana haki ya uhuru wa mawazo, dhamiri na dini; haki hii inajumuisha uhuru wa kubadili dini au imani yake, na uhuru wa kudhihirisha dini au imani yake, peke yake au kwa kushirikiana na wengine, kwa faragha au hadharani, katika mafundisho, vitendo, ibada na utekelezaji wa imani.

Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa (ICCPR), Kifungu cha 18

1. Kila mtu ana haki ya uhuru wa mawazo, dhamiri na dini. Haki hii inajumuisha uhuru wa kuwa na au kuchagua dini au imani yake, na uhuru wa kudhihirisha dini au imani yake, peke yake au kwa kushirikiana na wengine, kwa faragha au hadharani, kupitia ibada, utekelezaji, mafundisho na maadhimisho.
2. Hakuna mtu anayepaswa kulazimishwa kwa njia yoyote inayoweza kuathiri uhuru wake wa kuwa na au kuchagua dini au imani yake.
3. Uhuru wa kudhihirisha dini au imani unaweza kuzuiwa tu kwa masharti yaliyowekwa kisheria na ambayo ni muhimu kwa ajili ya kulinda usalama wa umma, utulivu wa jamii, afya, maadili, au haki na uhuru wa msingi wa wengine.
4. Nchi Wanachama wa mkataba huu zinajitolea kuheshimu uhuru wa wazazi na, inapohitajika, walezi wa kisheria kuhakikisha kuwa elimu ya kidini na maadili ya watoto wao inalingana na imani zao.

Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto (CRC), Kifungu cha 14

1. Nchi wanachama zitaheshimu haki ya mtoto ya uhuru wa mawazo, dhamiri na dini.
2. Nchi wanachama zitaheshimu haki na majukumu ya wazazi na, inapohitajika, walezi wa kisheria, kuwaongoza watoto katika utekelezaji wa haki hii kwa namna inayozingatia maendeleo yao.
3. Uhuru wa kudhihirisha dini au imani unaweza kuzuiwa tu kwa masharti yaliyowekwa kisheria na ambayo ni muhimu kwa ajili ya kulinda usalama wa umma, utulivu wa jamii, afya, maadili, au haki na uhuru wa msingi wa wengine.

ZINGATIA

Maazimio ya haki za binadamu ni ahadi za kimataifa zenye mshikamano wa kisiasa, ilhali mikataba, makubaliano na itifaki ni ahadi zinazofungamanishwa kisheria chini ya sheria za kimataifa. Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu, ingawa si mkataba wa kisheria, limekubalika kwa upana kiasi kwamba sasa linachukuliwa kuwa sehemu ya sheria ya kimataifa ya desturi.

Tazama pia

Maoni ya Jumla Na. 22 ya Kamati ya Haki za Binadamu, ambayo inatoa mwongozo wa kitaalamu juu ya tafsiri ya Kifungu cha 18 cha ICCPR.
https://www.equalrightstrust.org/ertdocumentbank/general%20comment%2022.pdf

Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu Kuondoa Aina Zote za Kutovumiliana na Ubaguzi kwa Msingi wa Dini au Imani.
https://www.ohchr.org/en/professionalinterest/pages/religionorbelief.aspx

Mpango wa Rabat wa Utekelezaji kuhusu Kuzuia Mhimili wa Chuki ya Kitaifa, Kimbari, au Kidini inayochochea Ubaguzi, Uadui au Vurugu.
https://www.ohchr.org/EN/Issues/FreedomOpinion/Articles19-20/Pages/Index.aspx

Unaweza pia kupata hapa mkusanyiko kamili wa viwango vya kimataifa vya haki za binadamu vinavyohusiana na uhuru wa dini au imani, kutoka Ofisi ya Kamishna Mkuu wa Haki za Binadamu wa Umoja wa Mataifa:
https://www.ohchr.org/EN/Issues/FreedomReligion/Pages/Standards.aspx

Taarifa kuhusu kazi ya Mwandishi Maalum wa Umoja wa Mataifa kuhusu uhuru wa dini au Imani:
https://www.ohchr.org/EN/Issues/FreedomReligion/Pages/FreedomReligionIndex.aspx

Jifunze zaidi

Tazama filamu fupi nane za Jukwaa la Kujifunza Uhuru wa Dini au Imani kuhusu maana ya uhuru wa dini au imani na hali ambazo unaweza kuwa na mipaka.
https://www.forb-learning.org/films/films-on-forb/

FILAMU

Tafuta taarifa kuhusu uhuru wa dini au imani katika nchi yako

Ushauri wa jumla wa kuchagua vyanzo vya taarifa

Ni vyema kusoma kuhusu hali ya uhuru wa dini au imani na haki za binadamu kwa ujumla katika nchi yako kabla ya kuongoza Kozi ya Wanamabadiliko wa Jamii. Hii itakusaidia kuhakikisha kuwa masuala ya kisheria katika ngazi ya kitaifa na uzoefu wa makundi mbalimbali nchini yanajumuishwa kwenye mafunzo na mijadala.

Tafuta vyanzo vya kitaifa vya taarifa, kama vile mashirika huru yasiyo ya kiserikali (NGOs), na kisha ulinganishe na taarifa kutoka kwa vyanzo vya kimataifa vinavyoaminika. Unapotafuta taarifa, kumbuka kuwa haiwezekani kuelewa hali ya kundi moja pekee bila kuelewa muktadha mpana, ikiwa ni pamoja na jinsi makundi mengine ya imani yanavyoathirika. Hakuna nchi ambako haki za kundi moja pekee la kidini ndizo zinavunjwa – makundi mengi huathirika kwa viwango tofauti na kwa njia mbalimbali. Hii haimaanishi upuuze vyanzo vinavyoangazia kundi moja, bali hakikisha unasoma kutoka kwa vyanzo zaidi ya kimoja kuhusu makundi mbalimbali.

FIKIRIA KWA MAKINI!

Unaposoma taarifa, fahamu hatari ya propaganda na upendeleo. Baadhi ya serikali huzuia ufuatiliaji na uandishi wa ripoti za haki za binadamu kwa kutumia taarifa potofu, vitisho, na shuruti. Kwa hivyo, taarifa kutoka kwa serikali kuhusu hali ya haki za binadamu nchini mwao zinaweza kuwa si za kuaminika.

Mara nyingine, taarifa zinazotolewa na serikali za kigeni au wadau wa kidini na jamii zinaweza kuwa na upendeleo au kupotosha. Wakati mwingine, kuna upendeleo wa kisiasa wa makusudi. Mara nyingi, mtazamo potofu wa hali nzima hutokana na kulenga kundi moja pekee. Tumia vyanzo mbalimbali, hakiki ukweli wa taarifa zako, na fikiri kwa umakini!

Vyanzo vya kimataifa vya taarifa

Hapa kuna vyanzo muhimu vya taarifa. Vinjari ili kupata sehemu zinazohusiana na nchi yako.

Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani – Ripoti ya kila mwaka kuhusu hali ya uhuru wa dini au imani karibu katika kila nchi duniani.
www.state.gov/international-religious-freedom-reports

Tume ya Marekani ya Kimataifa kuhusu Uhuru wa Kidini (USCIRF) – Ripoti ya kila mwaka kuhusu hali ya uhuru wa dini au imani katika nchi zenye ukiukwaji mkubwa wa haki hii.
www.uscirf.gov/annual-reports

Kituo cha Utafiti cha Pew – Takwimu kuhusu vizuizi vya kiserikali na uhasama wa kijamii unaohusiana na dini duniani kote.
https://www.pewresearch.org/topic/religion/religious-freedom-restrictions/

Kundi la Haki za Wachache Duniani – Orodha ya taarifa za nchi kuhusu jamii za wachache wa kidini na asili.
https://minorityrights.org/directory

Ripoti za Mtaalamu Maalum wa Umoja wa Mataifa kuhusu Uhuru wa Dini au Imani – Ripoti za mada maalum na ziara za nchi mbalimbali.
https://www.ohchr.org/en/issues/freedomreligion/pages/freedomreligionindex.aspx

Forum 18 - Ufuatiliaji na uchambuzi wa ukiukwaji wa uhuru wa dini au imani katika Asia ya Kati, Caucasus Kusini, Urusi, Belarus, Crimea na Uturuki.
www.forum18.org

Ripoti za uhalifu wa chuki katika ukanda wa OSCE – Ripoti zinazoangazia uhalifu wa chuki, ikiwemo ule unaotokana na utambulisho wa kidini katika Ulaya, Caucasus, Asia ya Kati na Amerika Kaskazini.
OSCE - ODIHR | Hate Crime Reporting

RIPOTI ZINAZOLENGA MAKUNDI FULANI YA KIDINI

Anti-Semitism Worldwide – Ripoti za kila mwaka kutoka Kituo cha Kantor kuhusu chuki dhidi ya Wayahudi.
https://cst.tau.ac.il/annual-reports-on-worldwide-antisemitism/

Ripoti ya UN kuhusu Kukabiliana na Ubaguzi na Chuki Dhidi ya Waislamu – Ripoti ya Mtaalamu Maalum wa Umoja wa Mataifa kuhusu Uhuru wa Dini au Imani, 2021.
https://www.ohchr.org/en/documents/ahrc4630-countering-islamophobiaanti-muslim-hatred-eliminate-discrimination-and

Freedom of Thought Report – Ripoti ya kila mwaka kutoka Humanists International.
https://fot.humanists.international/

Ubaguzi dhidi ya Wafuasi wa Ahmadiyya Duniani – Ripoti kwa Umoja wa Mataifa kutoka Kamati ya Kimataifa ya Haki za Binadamu, Shirika lisilo la Kiserikali linalotetea haki za waislamu wa Dhehebu la Ahmadiyya.
https://ihs.smc.global/wp-content/uploads/documents/Report-Persecution-of-Ahmadis-Worldwide.pdf

Ubaguzi dhidi ya Jehovah's Witnesses Duniani – Ripoti kutoka USCIRF
https://www.uscirf.gov/publication/issue-update-global-persecution-jehovahs-witnesses

World Watch List – Ripoti ya kila mwaka kuhusu mateso ya Wakristo kutoka Open Doors.
https://www.opendoorsuk.org/persecution/world-watch-list/

NYENZO KUHUSU DEMOKRASIA NA HAKI ZA BINADAMU KWA UJUMLA, IKIWEMO UHURU WA DINI AU IMANI KWA VIWANGO TOFAUTI

Hufuatilia hali ya demokrasia, ikiwemo uhuru wa dini au imani, katika nchi zote duniani. Chagua nchi yako kwenye ramani shirikishi ili kuchunguza data.
https://www.idea.int/democracytracker/

CIVICUS Hufuatilia vizuizi vya haki za kiraia, ikiwemo uhuru wa kujieleza, kukusanyika na kushirikiana – haki ambazo zinahusiana kwa karibu na uhuru wa dini au imani.
https://monitor.civicus.org/

Freedom House – Upimaji na ripoti kuhusu upatikanaji wa haki za kisiasa na uhuru wa kiraia katika nchi na maeneo 210. Bofya nchi yako ili kupata taarifa maalum.
https://freedomhouse.org/explore-the-map

Human Rights Watch huandaa ripoti ya kila mwaka kuhusu hali ya haki za binadamu katika zaidi ya nchi 100. (Ili kupata ripoti ya hivi karibuni, badilisha "2021" kwenye kiungo na mwaka wa sasa.)
https://www.hrw.org/previous-world-reports

Wasifu wa nchi za Amnesty International unaangazia uhuru wa dini au imani kwa viwango tofauti.
www.amnesty.org/en/countries/

Endelea kujifunza: Nyenzo za ziada na kozi za mtandaoni

Jifunze kuhusu uhuru wa dini au imani

Jukwaa la Kujifunza uhuru wa dini au imani na wanachama wa NORFORB wanatoa nyenzo na kozi mbalimbali za kukusaidia kuimarisha uelewa wako.
forb-learning.org

Nyenzo Zinajumuisha:

- filamu mbalimbali zinazotambulisha uhuru wa dini au imani, upatikanaji wa haki, uelewa wa dini, na zana za uchanganuzi wa muktadha.
- kozi ya mtandaoni inayopatikana kwa mahitaji kuhusu uhuru wa dini au imani.
- kozi ya mtandaoni inayopatikana kwa mahitaji kuhusu uhuru wa dini au imani na jinsia.
- kozi ya mtandaoni inayopatikana kwa mahitaji kuhusu kukabili hotuba za chuki.
- na ripoti kuhusu masuala mbalimbali kama vile uhuru wa dini au imani na jinsia, na uhuru wa dini au imani na nafasi ya kiraia inayopungua

JUKWAA LA KUJIFUNZA KUHUSU FORB
forb-learning.org

FORB Learning Platform

Boresha ujuzi wako wa uwezeshaji wa uhuru wa dini au imani

Mbali na Mafunzo ya Wanamabadiliko wa Jamii, Jukwaa la Kujifunza kuhusu Uhuru wa Dini au Imani pia linatoa

- Kifurushi cha Uwezeshaji cha uhuru wa dini au imani – Kifurushi cha mazoezi kwa yeyote anayehusika na utoaji wa elimu ya haki za binadamu kuhusu uhuru wa dini au imani.
- Mafunzo ya mtandaoni ya wiki 10 kwa wakufunzi/wawezeshaji, wa – mafunzo haya yanaendeshwa kwa mwongozo wa mwezeshaji na inahitaji takribani saa 6 za kazi kwa wiki. (Nafasi ni chache).
- Fursa za kujenga mtandao – jiunge na mtandao wetu wa wawezeshaji na wakufunzi wa uhuru wa dini au imani ili upate taarifa za hivi punde kuhusu nyenzo na kozi mpya, na pia kushiriki katika hafla za mtandao.

Jifunze zaidi kuhusu mbinu na jinsi ya kuzitumia

Hapa unaweza kupata viungo vya nyenzo mbalimbali za bure za kujifunza na kozi za mtandaoni kutoka kwa watoa huduma wengine.

MBINU ZA DHARURA: KUZUIA, KUSIMAMISHA, KUITA MSAADA NA KUTOA ONYO
Mbinu za dharura hutumiwa kukabiliana na vitisho vya haraka kwa haki za binadamu. Nyenzo zifuatazo zinaweza kusaidia katika kutumia mbinu hizi.

KOZI ZA MTANDAONI

KUELEWA NA KUKABILIANA NA MATAMSHI YA CHUKI MTANDAONI
Kozi inayotolewa na FacingFacts, mpango wa elimu wenye lengo la kukabiliana na uhalifu wa chuki na matamshi ya chuki barani Ulaya. Mengi ya mafunzo haya yanafaa katika mazingira mbalimbali. Pia, angalia kozi zingine zinazotolewa, kwa mfano, 'Kuelewa na kutambua uhalifu wa chuki dhidi ya Wayahudi'.

MSAADA WA MCHAKATO WA AMANI NA KUZUIA VURUGU ZA UCHAGUZI
Kozi za mtandaoni kutoka taasisi ya Marekani.

NYENZO

UDHALILISHAJI MITAANI

Udhalilishaji mitaani unawaathiri wanawake wote. Wanawake wa jamii za wachache wanaweza kuwa katika hatari zaidi ya kunyanyaswa kwa chuki au unyanyasaji wa kingono. Pata mawazo na mikakati ya jinsi ya kukabiliana na hali hii kama mwathiriwa au shahidi hapa:

MBINU ZA MABADILIKO: KAMPENI, UTETEZI, MOTISHA NA UKAIDI

Utetezi na kampeni ni mbinu muhimu za kuleta mabadiliko. Pata mwongozo kuhusu kutumia mbinu hizi kupitia nyenzo na kozi zifuatazo.es.

KOZI ZA MTANDAONI

MSINGI WA UTETEZI

Kozi ya mtandaoni inayopatikana wakati wowote, inayotolewa na Tearfund. Jisajili kwa kufungua akaunti kupitia kiungo kilicho hapa chini na tafuta ‘Advocacy Essentials’ katika orodha ya kozi.

CHUO CHA UTETEZI CHA ACT

Kozi ya mtandaoni inayopatikana wakati wowote inayotolewa na ACT Alliance. Unda wasifu kwenye Fabo.org ili ufikie kozi hii.

NYENZO

KIFURUSHI CHA ZANA ZA UTETEZI – KUWA MABADILIKO UNAYOTAKA KUONA

Kimeandaliwa na Africa Platform for Social Protection and the Commonwealth Foundation.

KIFURUSHI CHA ZANA ZA UETETZI – MWONGOZO WA MSINGI

Kimeandaliwa na Tearfund.

UTETEZI: MWONGOZO KWA MASHIRIKA MADOGO NA DAYASPORA

Kimeandaliwa na INTRAC.

GAME ON – MWONGOZO WA VITENDO KATIKA KAMPENI

Kimeandaliwa na Wigwam na finep.

MBINU ZA KUJENGA: UHAMASISHAJI, USHIRIKISHO, UJUZI NA MITANDAO

Mbinu za kujenga hutumiwa kuunda msingi wa muda mrefu wa mabadiliko, kwa njia ya uelewa wa umma na mitandao ya watu waliohusika ambao wamewezeshwa kwa ujuzi unaohitajika kutumia kila aina ya mbinu.

KOZI ZA MTANDAONI

TUMIA PODCASTS, VIDEO NA KUKAA SALAMA MTANDAONI

Tembelea tovuti ya Advocacy Assembly ili kupata kozi fupi za bure za mtandaoni zitakazokusaidia kukuza ujuzi wa vitendo.

MAZUNGUMZO YA KIDINI

KAIICID inatoa kozi kadhaa za mtandaoni kuhusu mbinu za mazungumzo ya kidini.

KUJENGA AMANI NA ZAIDI

Kozi za mtandaoni zilizohifadhiwa na taasisi ya Marekani.
https://www.usip.org/academy/catalog/religious-engagement-peacebuilding-common-ground-approach
https://www.usip.org/academy/catalog/introduction-religion-and-peacebuilding

ISHI UNACHOAMINI

Warsha kwa viongozi na watu wenye ushawishi wanaotaka kujifunza jinsi ya kukuza ujumuishaji, uanuwai, na uhuru wa imani katika mazingira ya kazi na jamii zao.

NYENZO

KIFURUSHI CHA WIKI YA SHUGHULI ZA KIDINI

Mwongozo wa vitendo wa kuandaa shughuli za kijamii zinazohusisha mazungumzo ya kidini, uliochapishwa na Mtandao wa Kidini wa Uingereza.

KIFURUSHI CHA IMANI KWA HAKI

Moduli za elimu ya haki za binadamu zinazochunguza uhusiano kati ya dini, imani, na haki za binadamu kulingana na ahadi 18 za mfumo wa Faith for Rights.

KIFURUSHI CHA MATAMSHI YA CHUKI MTANDAONI KWA WALIMU NA WAFANYAKAZI WA VIJANA

Kifurushi cha mtandaoni cha Selma kinatoa nyenzo zinazoweza kubadilishwa kulingana na mahitaji ya walimu na wale wanaofanya kazi na watoto na vijana kuhusu suala la matamshi ya chuki mtandaoni.

KOZI YA MAFUNZO YA MTANDAONI YA WALIMU KUHUSU KUHAMASISHA UJUMUISHO

Kozi mseto inayowafundisha walimu jinsi ya kukuza ujumuisho na jamii shirikishi katika mazingira ya darasani. Inatolewa na Hardwired Global kwa lugha ya Kiingereza na Kiarabu.
Email: info@hardwiredglobal.org

NYENZO ZA KITHEOLOJIA KUTOKA DINI KWA AJILI YA AMANI

Dini za Ibrahimu za Kiyahudi, Kikristo na Kiislamu Katika Kuunga Mkono Uraia; Uhuru wa Mawazo, Dhamiri na Dini au Imani; Na Ulinzi wa Jamii Zilizo Hatarini.

MBINU ZA UPONYAJI: KUTUNZA KUMBUKUMBU, KUKUMBUKA, KUTAFUTA HAKI NA FIDIA, KUTOA MSAADA WA KIFEDHA NA KISAIKOLOJIA

Mbinu za uponyaji hutumika kuwahudumia na kutafuta haki kwa watu na jamii zilizoathiriwa na ukiukwaji wa haki.

KOZI ZA MTANDAONI

KUTUNZA KUMBUKUMBU ZA UKIUKWAJI WA HAKI ZA BINADAMU

Tembelea tovuti ya Advocacy Assembly upate kozi fupi za bure zitakazokusaidia kuboresha ujuzi wako wa kurekodi ukiukwaji wa haki za binadamu. Kozi zinajumuisha:

- Kutunza kumbukumbu na kuripoti ukiukwaji wa haki za binadamu kwa kutumia ushuhuda.
- Kunasa, kuhifadhi na kushiriki ushahidi wa video.

MSAADA WA KIJAMII NA KISAIKOLOJIA(CBPS)

Kozi ya mtandaoni inayopatikana kwa mahitaji yenye moduli tatu za CBPS itakusaidia kujifunza misingi yake. Imetayarishwa na Kanisa la Sweden (kwa ajili ya Act Alliance).

Orodha ya mazoezi

Mazoezi ya jumla

Zoezi	Lengo	Ukurasa
Kamilisha sentensi	Utambulisho wa washiriki – kuangazia motisha zao za kushiriki	35
Kubadilishana mawazo	Utambulisho wa washiriki – kuangazia mambo wanayoshabihiana	36
Pitisha kapu	Zoezi la kanuni za msingi	36
Nisifie	Inasisitiza mchango wa washiriki unaokamilishana katika kikundi.	135
Eleza kila kitu	Zoezi la ufunguzi linalokumbusha washiriki mafunzo ya vipindi vilivyopita	49
Mtandao wa mazuri	Kuangazia mazuri katika jamii zetu	99
Kila mtu abadilishane viti	Kichangamshi kinachoangazia mambo ya kufanana	71
Tembea kisha simama	Kichangamshi	103
Utosini hadi unyayoni	Kichangamshi	130
Fanya mabadiliko	Kichangamshi	137
Muonekano wa kisanii wa mwanamabadiliko	Kichangamshi	147
Vielelezo vya hisia	Zoezi la kufunga linaloangazia hisia za washiriki kuhusu waliyojifunza	131
Kichwa, moyo, mikono	Zoezi la tathmini	148

Mazoezi ya kuchunguza kwa mapana haki za binadamu, ubaguzi na utambulisho wa kijamii

Zoezi	Lengo	Ukurasa
Supu ya maisha na matunzio ya haki za binadamu	Mazoezi mawili yanayosaidia washiriki kuunganisha mahitaji yao na Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu	37, 38
Chungu cha bahati	Kuangazia upendeleo, unyanyasaji na faida za mshikamano	68
Hatua moja mbele	Kuwasaidia washiriki kutambua hali ya unyanyasaji wa kiuchumi na ubaguzi wa kimfumo	69
Utambulisho wetu kijamii	Kuwasaidia washiriki kuona mambo ya kufanana kati yao na watu wa dini/imani nyingine	72

Mazoezi ya kuchunguza hususani uhuru wa dini au imani

Zoezi	Lengo	Ukurasa
Hapo zamani za kale	Kuwasaidia washiriki kutafakari iwapo wanathamini mambo yanayolindwa na uhuru wa dini au imani	50
Uhuru wa dini au imani katika siku yangu	Kuwasaidia washiriki kuelewa jinsi wanavyotumia haki yao ya uhuru wa dini au imani katika maisha ya kila siku	52
Maigizo mafupi ya dakika mbili ya uhuru wa dini	Kuendeleza ujuzi wa kutambua ukiukwaji wa uhuru wa dini au imani	82
Ramani ya uhuru wa dini au imani ya mji wetu	Zoezi la sehemu mbili linalosaidia washiriki kuunda uchanganuzi wa muktadha wa uhuru wa dini au imani	101, 104

Mazoezi yanayolenga njia za kuhamasisha haki za binadamu na kupanga hatua

Zoezi	Lengo	Ukurasa
Makundi ya kujadili hadithi za wanamabadiliko	Kuhamasisha na kuweka muktadha wa mijadala kuhusu hatua za kuchukua	114
Washuhudiaji na waponyaji	Kuwasaidia washiriki kutambua mambo yanayowawezesha kuchukua hatua badala ya kuwa washuhudiaji tu	114
Mimi ni nani?	Kuwasaidia washiriki kutambua vichocheo vya kuwasaidia kuchukua hatua	116
Kuzungumzia mbinu za dharura	Zoezi la mjadala linalohusiana na uwasilishjai la mbinu katika kipindi cha 6	118
Kuzungumza kuhusu mbinu	Kuchangia mawazo kuhusu njia za kuhamasisha haki za binadamu	129
Tatizo na nini?	Kuwasaidia washiriki kuchagua changamoto za kuandaa mipango ya utekelezaji	135
Safari ya mabadiliko yetu	Zoezi la kupanga hatua kwa njia ya picha	138, 146
Tunaelekea wapi kutoka hapa?	Kuwasaidia washiriki kubaini hatua zinazofuata	147

Watu wengi wanahofia ukiukwaji wa haki ya uhuru wa dini au imani katika nchi yao na mvutano kati ya dini tofauti katika jamii zao, lakini hawajui jinsi ya kuleta mabadiliko.

Kozi ya Wanamabadiliko wa Jamii ni mfululizo wa warsha tisa, kila moja ikiwa ya saa mbili, iliyoundwa kuwapa nguvu makundi ya watu wazima na vijana katika ngazi ya jamii ili kujifunza na kushiriki katika kukuza uhuru wa dini au imani kwa wote ndani ya jamii zao.

Katika mwongozo huu wa wawezeshaji pamoja na nyenzo zinazoambatana, watapata mipango ya vipindi, nakala za mwongozo, slaidi za PowerPoint, hadithi, mabango na kadi za michezo – kila kitu unachohitaji ili kuendesha mafunzo haya. Tunatumai kwamba nyenzo hizi zitakusaidia kuanzisha mchakato wa mabadiliko katika eneo lako.

forb-learning.org

THE LOCAL
CHANGEMAKERS
COURSE

Nordic Ecumenical Network on Freedom of Religion or Belief
NORFORB

FORB Learning Platform

Mwongozo huu umeandaliwa na The Freedom of Religion au Belief Learning Platform, mradi wa NORFORB
© SMC Faith in Development 2022, www.smc.global, kwa niaba ya mtandao wa NORFORB.
Mwandishi: Katherine Cash | Msanifu michoro na aikoni: KSB Design/Kristina Schollin-Borg & Eva-Marie Wadman.
Michoro: Toby Newsome | Michoro ya Powerpoint: Gry Zierau
ISBN: 978-91-85141-40-1 | Mawasiliano: info@forb-learning.org | Tovuti: www.forb-learning.org
Mfasiri/Mhakiki wa kiswahili: Shisia Ali Abubakar na Furaha Dimitrios Caloupis